**27 APRILI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Saba - Tarehe 27 Aprili, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. KIJA L. NTEMI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mjumbe wa Kamati.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa *Engineer* Chacha Mwita Wambura, Mbunge wa Geita Mjini, sasa aulize swali lake.

**MHE. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa swali langu Na. 153 liweze kupata majibu ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Mheshimiwa Mbunge, swali lako ni Na. 191, ninaomba urudie.

**MHE. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa swali langu Na. 191 liweze kupata majibu ya Serikali.

Na. 191

### Kuunda Ajira na Kukuza Uchumi wa Vijana

**MHE. CHACHA M. WAMBURA** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa kuunda ajira na kukuza uchumi wa vijana kupitia miradi ya uzalishaji na ujasiriamali ili kupunguza utegemezi wa sekta ya madini – Geita?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, ninapenda kujibu swali zuri la Mheshimiwa *Engineer* Chacha Mwita Wambura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mkakati wa kuunda ajira na kukuza uchumi wa vijana kwa kuwawezesha kushiriki katika miradi ya uzalishaji na ujasiriamali, sambamba na kupunguza utegemezi wa sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mradi wa Mageuzi katika Sekta ya Madini kwa Maendeleo Jumuishi na Endelevu *(MBT),* vijana 5,983 wamewezeshwa kwa kupatiwa leseni, mafunzo na mitaji, huku wachimbaji wadogo 658 wakipatiwa mafunzo kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi katika mikoa ya kimadini ya Geita, Mbogwe na Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inatekeleza mikakati jumuishi ikiwemo uratibu wa utekelezaji wa Sera ya Ajira ya Mwaka 2008 pamoja na sera nyingine za kisekta. Vilevile, utekelezaji wa programu za kuwawezesha vijana kama *BBT* na *BBT-LIFE,* pamoja na utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kupitia Halmashauri na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inaendelea kukuza ujuzi wa vijana, kuratibu fursa za ajira ndani na nje ya nchi, na kuhakikisha masuala ya ajira yanajumuishwa katika mipango ya maendeleo, hatua zinazolenga kukuza fursa za ajira na kuimarisha uchumi wa vijana kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa *Engineer* Chacha Mwita Wambura, swali la nyongeza.

**MHE. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, tunajua kwamba uchumi wa Geita unategemea sana sekta ya madini na nia ni kuhakikisha kwamba tunapata miradi mbadala ambayo tutakuwa hatutegemei madini tu. Kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambapo uchaguzi ulifanyika mwaka 2025 ilionesha kwamba tunaenda kupata miradi ambayo itaenda kukuza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa ajili ya uhakika kwamba vijana wanapata ajira na wanaenda kukua kiuchumi. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga hii miradi ili hao vijana wa Geita waweze kupata sehemu ya kufanya kazi na kupata ajira? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali zuri la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Chacha Wambura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuanzisha miradi mikubwa ya kimkakati ili kuzalisha ajira na fursa mbalimbali kwa vijana wa Mkoa wa Geita. Ninataka nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge, Serikali iko tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ningependa pia kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba uanzishwaji wa miradi mikubwa na ya kimkakati unategemea bajeti ya Serikali iliyotengwa. Hivyo basi, Mheshimiwa Mbunge ushauri wake umepokelewa na utafanyiwa kazi kadiri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Catherine Joachim, swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu ya swali la Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama hauna swali la nyongeza ninaomba usiwashe kisemeo, kwa sababu ninakuona hapa. Ninashukuru sana.

Tunaendelea na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, sasa aulize swali lake.

Na. 192

**Kutenga Fedha ya Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya Samani na Ufuatiliaji wa Miradi**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kutenga sehemu ndogo ya fedha za Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya samani za ofisi na ufuatiliaji wa miradi ya Mfuko huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Jimbo la Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo huchangia shughuli na miradi ya maendeleo inayobuniwa na kuibuliwa na wananchi kupitia mpango wa fursa na vikwazo na kuidhinishwa na halmashauri. Katika kutekeleza azma hii, mwaka 2009 Bunge lako lilipitisha Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo Sura ya 96 ambayo imeanzisha Mfuko pamoja na Kamati ya kuchochea maendeleo ya jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 8 na 19 cha Sheria hiyo kinabainisha aina ya miradi inayoweza kugharamiwa chini ya sheria hii. Miradi hiyo ni pamoja na miradi ya kijamii ambayo ni lazima iwe na manufaa kwa sehemu kubwa ya wakazi wa jimbo husika. Miradi ya maendeleo, inaweza kujumuisha gharama za utafiti, upangaji, usanifu au mchango wa kitaalamu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi; miradi ya miundombinu na huduma za jamii mfano ujenzi wa shule, zahanati, barabara ndogo, miradi ya maji, na miradi ya kilimo cha pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hiyo inaruhusu kutumia fedha za Mfuko wa Jimbo kwa ufuatiliaji wa miradi, lakini siyo kwa matumizi ya samani au gharama za kawaida za ofisi. Kwa msingi huo, halmashauri zinaweza kutumia fedha za Mfuko wa Jimbo kutekeleza jukumu la ufuatiliaji wa miradi, lakini siyo kwa matumizi ya samani. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nifahamu je, ni kiasi gani kinachoruhusiwa kutumika kwa ajili ya ufuatiliaji wa samani hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi kumekuwa na changamoto, unavyokwenda kuwaambia halmashauri kwamba waweze kutoa kiasi cha fedha kwa ajili ya samani za ofisi kwenye Mfuko wa Jimbo zinakuwa hazitoki. Je, Serikali haioni kuwa kuna sababu sasa ya kuipa hadhi Ofisi ya Mbunge kwa kuhakikisha kwamba inatoa fedha maalumu kabisa kwa ajili ya samani (viti, pamoja na meza) ambapo wakati wageni au watu wanaokuja kuleta changamoto zao pale wanaweza hata kukaa katika viti hivyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Jimbo ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria Sura 96 na Vifungu vile cha 8 na 19 kimeeleza vizuri kwamba

shughuli zipi zinatakiwa kutekelezwa kwa Mfuko wa Jimbo. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mchungahela, kwanza tunafahamu kwamba Mfuko huu unatekeleza shughuli za miradi ambayo iko ndani ya halmashauri iliyoibuliwa na wananchi na inaruhusiwa kutumia sehemu kidogo ya fedha hizo kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wastani wa asilimia mbili hadi tano ya fedha ile inaweza ikatumika kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ambayo imedhaminiwa na Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, Mfuko wa Jimbo hauruhusiwi kutumika kwenye samani za ofisi za Waheshimiwa Wabunge. Tunavyo vyanzo vingine ambavyo vinaweza vikatumika kuboresha Ofisi za Waheshimiwa Wabunge, na tunatambua umuhimu wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mchungahela, ikiwa kuna uhitaji wa samani katika ofisi ya Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine, tutaona utaratibu mzuri ambao Serikali imeuweka kwa ajili ya kuhakikisha Waheshimiwa Wabunge wana ofisi nzuri kwa matumizi yao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ibrahim Shayo, swali la nyongeza.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Moshi Mjini kuna madaraja mawili; daraja la kwanza lipo Kata ya Ng'ambo na daraja la pili lipo Kata ya Mji Mpya. Madaraja yale kutokana na mvua hizi, ni mabovu sana. Je, ni lini Serikali itakwenda kuyarekebisha madaraja haya ili wananchi wale wawe salama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Shayo, Mbunge wa Moshi Mjini kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na madaraja na kuyatengeneza mara kwa mara. Ninafahamu Mheshimiwa Mbunge ana changamoto ya Daraja la Kata ya Ng'ambo ambalo limekatika siku chache zilizopita na kuathiri mawasiliano kutoka kata hiyo kwenda kata za jirani. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii itafuatilia kuhakikisha kwamba tunafanya matengenezo mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kumwelekeza Meneja wa *TARURA*, Wilaya ya Moshi na Mkoa wa Kilimanjaro wafike eneo la *site* wafanye tathmini mapema iwezekanavyo ili tupate fedha za dharura kwa ajili ya kurekebisha hali hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 193

**Kumaliza Tatizo la Matundu ya Vyoo Nchini**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kumaliza tatizo la matundu ya vyoo katika halmashauri nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya upungufu wa vyoo katika baadhi ya shule za msingi na sekondari nchini. Kwa mujibu wa takwimu za sensa ya elimu msingi ya mwaka 2025 uwiano wa matundu ya vyoo kwa wanafunzi wa shule za msingi ni 1:46 (wavulana) na 1:42 (wasichana) na sekondari uwiano ni 1:27 (wavulana) na 1:25 (wasichana).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha na kujenga matundu ya vyoo kila mwaka, ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya shilingi bilioni 12.87 zilitumika kujenga matundu 6,283. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 hadi Aprili, 2026 kiasi cha shilingi bilioni 5.42 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo 6,283.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha katika bajeti kila mwaka ili kutatua changamoto za matundu ya vyoo nchini, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, Mheshimiwa Waziri ameshafanya tathmini ya kujua ukubwa wa tatizo la matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari kwa nchi nzima na kupanga mkakati wake? Ninataka nijue, ni sahihi katika karne ya sasa Wabunge wa Tanzania, kuendelea kujadili na kuuliza maswali kila mwaka ya matundu ya vyoo, meza na viti na watoto kukaa nchini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumhakikishia Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara kwamba Serikali inatambua umuhimu wa shule zetu zote kuwa na matundu ya vyoo yanayotosheleza na yenye viwango na ubora unaotakiwa katika kuhakikisha kwamba watoto wetu wanasoma katika mazingira bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kila mwaka tumekuwa tukifanya tathmini ya matundu ya vyoo yaliyopo, upungufu na kuweka mikakati katika kila bajeti kutenga fedha kupitia mapato ya ndani ya halmashauri na pia kupitia Serikali Kuu kwa ajili ya kujenga matundu ya vyoo. Kwa hiyo, tuna tathmini ya kila mwaka, tunajua kiasi gani tunayo, kiasi gani tunahitaji na Serikali imeendelea kutenga fedha na kujenga ili kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni dhamira ya Serikali kwamba tuondokane na changamoto ya matundu ya vyoo kabisa na ndiyo maana tumeendelea kutenga fedha kila mwaka. Kwa mujimu wa taarifa za Benki ya Dunia ambayo *assessment* imefanyika hivi karibuni, tunahitaji kwa ujumla katika shule yenye wanafunzi 400 tunahitaji wastani wa matundu ya vyoo 12 (sita ya watoto wa kike na sita ya watoto wa kiume) na sisi kwa kiasi kikubwa baadhi ya shule tumeshazidi kiwango hicho. Kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha tunaboresha kwenye yale maeneo mengine ambayo yana uhitaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuhakikisha tunajenga matundu ya vyoo, lakini zoezi hili ni endelevu kwa sababu tutaendelea kujenga shule, *population* ya watoto itaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hakuna siku tutasema tumemaliza, hatujengi vyoo kabisa, kwa sababu *population* ipo na shule zitaendelea kujengwa na zitahitaji kujenga vyoo. Kwa hiyo, ni zoezi endelevu. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba zile shule ambazo zina upungufu tunaondokana na changamoto hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maelezo ya Serikali yanaonesha kwamba wana dhamira ya dhati ya kumaliza tatizo la matundu ya vyoo na kwa sababu shule zilizopo vijijini ndio ambazo zina tatizo kubwa la upungufu wa

matundu ya vyoo, je, Serikali ipo tayari itakapoanza kumaliza tatizo hili, kuanza na shule za vijijini hasa katika Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Kilindi, Korogwe Vijijini na Lushoto? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba tunatoa kipaumbele kwenye maeneo ambayo yana shule zenye upungufu mkubwa zaidi wa vyoo zikiwemo halmashauri za vijijini hasa Halmashauri ya Lushoto katika Mkoa wa Tanga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninatambua Serikali yetu ni namna gani ambavyo inajenga shule kwenye maeneo mbalimbali *primary schools* na sekondari, lakini tunapozungumzia mkakati maalumu wa kujenga matundu ya vyoo ni pamoja na shule zile chakavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *crisis* hii ni kubwa kwenye halmashauri zetu. Waziri alikuja na mpango wa kuhakikisha wanaandika andiko kwa ajili ya *maintenance* kwenye shule chakavu. Serikali haioni kwamba ni wakati mwafaka sasa hili tatizo la matundu ya choo kukawa kuna mkakati mahususi ili tumalize tatizo hili kwenye nchi yetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, wazo la Mheshimiwa Mbunge ni zuri na tunalipokea. Kama ambavyo iliwasilishwa kwenye bajeti yetu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ule mpango mkakati ambao umewasilishwa Ofisi ya Mipango kupitia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni *inclusive* na miundombinu yote ambayo inatakiwa kwenye shule. Kwa hiyo, vyoo pia vitakuwa sehemu ya miundombinu ambayo itaboreshwa. Pia suala la kuwa na

mpango mkakati ni wazo zuri, tunalichukua kuhakikisha kwamba, tunaboresha vyoo katika nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali inapojenga vyoo katika shule za msingi na sekondari, ina mpango gani wa kutenga eneo maalum linaloweza kuwapa faragha watoto wa kike, kwa mfano wanapoweza kubadilisha taulo za kike? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika michoro yetu ya ujenzi wa miundombinu hiyo ambayo imeendelea kutolewa katika shule zetu, eneo maalum limeendelea kupewa kipaumbele na ziko baadhi ya shule wameanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia nafasi hii kuwakumbusha Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kwamba, pale tunapojenga miundombinu hiyo katika shule ambazo zina watoto wa kike, ni muhimu kuwa na eneo maalum kwa ajili ya huduma hiyo muhimu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, Mbunge wa Igalula, sasa auliuze swali lake.

Na. 194

**Kuongeza Shule za Msingi na Sekondari, Jimbo la Igalula**

**MHE. JUMA M. KAWAMBA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Shule za Msingi na Sekondari, pamoja na miundombinu katika Shule zilizopo Jimbo la Igalula?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Mustapha Kawamba, Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya vipaumbele vya Serikali katika sekta ya elimu msingi na sekondari ni pamoja na ujenzi wa madarasa, shule za msingi na sekondari katika maeneo mbalimbali yenye vigezo stahiki kote nchini. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 – 2025/2026 Serikali imetoa shilingi bilioni 4.23 katika jimbo la Igalula, kwa ajili ya ujenzi wa shule mbili za msingi za Mnadani na Izumba Migusa, shule nne za sekondari za Venant Daud, Mmale, Magulyati na Uyui *Modern* na madarasa 33 katika shule 17 za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi bilioni 1.25 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Msingi Mzumba na madarasa 54, ya msingi 40 na ya sekondari 14, pamoja na matundu ya vyoo 10 katika shule mbili za sekondari. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule za msingi na sekondari na kuongeza miundombinu katika shule zilizopo kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Mheshimiwa Juma Mustafa, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Igalula linapatikana maeneo ya kijijini ndani ya Mkoa wa Tabora, lakini tuna shule shikizi takribani 35 ambazo zimejengwa kwa nguvu za

wananchi. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuleta fedha kwa ajili ya kumalizia shule hizi ndani ya Jimbo la Igalula?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Serikali ina mkakati gani wa kutuletea fedha kwa ajili ya kumalizia na kujenga shule za sekondari zifuatazo; Shule ya Sekondari Ipululu iliyopo Kata ya Igalula, Shule ya Sekondari Malakaseko iliyopo Kata ya Goweko, Shule ya Sekondari Itona iliyopo Kata ya Loya na Shule ya Sekondari ya Uyui *Modern School?* Hii ni shule ya amali iliyopo katika Kata ya Goweko, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, ninawapongeza sana wananchi wa Jimbo la Igalula kwa kuanza ujenzi wa shule za msingi shikizi 35. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua juhudi hizo za wananchi na itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kwenda kumalizia ujenzi wa shule hizi kwa awamu ili ziweze kutoa huduma ya elimu kwa watoto wetu. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunazitambua shule hizi na tunaendelea na taratibu za kupata fedha, ili kuendelea kuzikamilisha kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la pili, tunafahamu ziko shule ambazo zimejengwa, lakini hazijakamilika ikiwemo hii Shule ya *Igalula Modern* na nyingine zote ambazo Mheshimiwa Mbunge umezitaja. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mpango ambao tunaendeleanao, ukiwemo mpango wa kuanza naye *double cohort* ya Januari, 2028, yako maeneo ambayo tumeshayafanyia tathmini. Tutapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha shule ambazo zipo, lakini yako maeneo ambayo tutajenga shule nyingine kwa hiyo, katika kipindi hicho tutahakikisha tunatoa kipaumbele katika shule ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, Serikali imejipangaje kwa nchi nzima kukamilisha nyumba za walimu ambazo hazijakamilika, madarasa ambayo hayajakamilika na maabara ambazo hazijakamilika kwa nchi nzima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, tunazo nyumba za walimu, maabara, madarasa na baadhi ya miundombinu ya elimu ambayo shughuli za ujenzi zimeanza na zinaendelea katika hatua mbalimbali lakini hazijakamilishwa. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Cecilia Paresso kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa kukamilisha miundombinu hiyo, na tayari kwenye bajeti zetu hata bajeti ijayo ya 2026/2027 tumetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu hiyo. Pia tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha miundombinu hiyo inakamilika na kutoa huduma ambayo inatakiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kata ya *Seed Farm*, Manispaa ya Songea, haina sekondari ya kata. Je, ni lini Serikali itajenga sekondari ya kata katika kata hiyo ya *Seed Farm*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Songea Mjini, kaka yangu Ndumbaro, amefuatilia mara kadhaa suala la ujenzi wa shule ya sekondari katika Kata ya *Seed Farm*, Manispaa ya Songea. Ninaomba nimhakikishie tu kwamba, tuko hatua za mwisho. Tulikubaliana na wataalamu wafanye tathmini ya vigezo na

baada ya hapo tuhakikishe tunapeleka fedha, kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutahakikisha baada ya kupokea vigezo hivyo na kufanya tathmini, tutatoa kipaumbele kinachotakiwa kupitia mapato ya ndani ya Manispaa ya Songea na Serikali Kuu, ili tuweze kujenga shule hiyo ikiwa vigezo vitakuwa vimefikiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Makete bado tuna uhitaji wa sekondari, hususan kwenye Kata ya Mlondwe, ambayo hata Mheshimiwa Waziri anaifahamu; kama wilaya na kama halmashauri tumeandaa eneo. Ni lini Serikali itatoa fedha kwenye kipaumbele hiki cha wananchi wa Wilaya ya Makete ili Shule ya Sekondari Mlondwe ijengwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete, kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kujenga shule za sekondari katika kata ambazo hazina sekondari, kama Kata ya Bulongwa na hivyo tutahakikisha tunaweka vipaumbele. Jambo la msingi tunafanya tathmini ya vigezo, tukijiridhisha tutahakikisha tunapeleka shule kwa ajili ya kusogeza huduma za elimu karibu na wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Neema Majule, swali la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuuliza, je, Serikali ipo tayari kubaini yale maeneo ya shule ya msingi ambayo ni makubwa, ambayo yana uwezo wa

kujengwa sekondari palepale ili kuendana na huu mpango wa elimu jumuishi, yaani shule ya msingi na palepale sekondari?

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani; kwa mfano hapa Dodoma, Shule ya Ipagala 'A' ina eneo kubwa sana ambalo hapo hapo ingeweza kujengwa sekondari, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Dkt. Neema ni ya msingi, na Serikali tayari imeanza. Yako maeneo ambayo yana shule za msingi zenye maeneo makubwa, maeneo hayo pia, yametumika kujenga shule za sekondari. Kwa hiyo, zoezi hili tutaendelea kulifanya. Tutapita pia, kwenye Shule ya Msingi ya Ipagala 'A', kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ili tuweze kuona kama kuna uhitaji wa ujenzi wa shule ya sekondari na kama eneo linatosha, basi Serikali itaendelea kuyafanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haiderali Gulamali, swali la nyongeza.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba, pale Ilongero shule zetu zina uchakavu mkubwa sana, zinatakiwa ukarabati katika kata mbalimbali. Tuliwasilisha maombi yetu kwa maandishi ofisini kwa Mheshimiwa Waziri. Tunaomba majibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninawapongeza wananchi wa Jimbo la Ilongero pamoja na Mheshimiwa Mbunge kwa kuwasilisha orodha ya shule ambazo ni chakavu na zinahitaji ukarabati. Ninaomba nimhakikishie kwamba, Serikali inaandaa mpango mkakati mahususi ambao utaainisha shule zote chakavu ambazo tayari, *of course* tumeainisha, lakini tunatafuta fedha kwa ajili ya kuona namna ambavyo tutakwenda kuzikarabati shule zile kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie kwamba katika vipaumbele ambavyo vipo kwenye sekta ya elimu ni pamoja na kwenda kuondokana na shule chakavu na kongwe. Tunaendelea na taratibu za kupata fedha, ili tuje kukarabati. Tutahakikisha kwamba shule za Jimbo la Ilongero pia zitapata kipaumbele.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Tabora Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 195

**Ujenzi wa Soko la Kisasa la Machinga, Tabora Mjini**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la Kisasa la Machinga katika Jimbo la Tabora Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Soko la Machinga katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora upo katika Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2025 - 2030) wa Halmashauri hiyo. Ujenzi huo umepangwa kuanza katika Mwaka wa Fedha 2027/2028.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2026/2027 Halmashauri imetenga shilingi milioni 150 kupitia mapato ya ndani, ili kuanza maandalizi ya nyaraka za miradi ya kimkakati ikiwemo soko hilo. Nyaraka zitakazoondaliwa na upembuzi yakinifu wa miradi huo utafanyika. Baada ya halmashauri kukamilisha

maandalizi na upembuzi yakinifu wa mradi huo, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, itafanya mapitio ya maandiko dhana kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Tabora katika utekelezaji wa ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninatoa masikitiko yangu kwa majibu ya Serikali kuhusiana na suala zima la Soko la Machinga katika Jimbo la Tabora Mjini. Suala hili siyo la leo na wala siyo la Mkataba wa 2025 - 2030. Suala hili limefuatiliwa na wameona ni namna gani wafanyabiashara wadogo wadogo kwenye Jimbo la Tabora Mjini wanavyofanya biashara kwenye mazingira ambayo siyo rafiki kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Serikali inasema kwamba, ndiyo kwanza wanakwenda kufanya upembuzi yakinifu. Hawawatendei haki wafanyabiashara wadogo wadogo wa Jimbo la Tabora Mjini kwa sababu, tayari Serikali iliahidi humu Bungeni ujenzi wa Soko la Machinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kufahamu hapa, na wananchi wa Tabora wapo kwenye runinga wasikie, ni lini Soko la Machinga, Jimbo la Tabora Mjini, litaanza ujenzi wake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Uchumi wa wananchi wa Tabora unategemea kilimo pamoja na biashara ndogo ndogo. Wafanyabiashara hawa hawana mazingira rafiki kwa biashara zao. Serikali iliahidi katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba, watajenga Soko la Machinga haraka iwezekanavyo. Ninataka kufahamu, baada ya uchaguzi, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko na siyo upembuzi yakinifu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Naibu Spika, jambo la kwanza, ninawapongeza Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, kwanza kwa dhamira yao ya kujenga Soko la Machinga. Ikumbukwe kwamba, maandalizi ya *design,* michoro na eneo la ujenzi ni jukumu la Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tuliwaelekeza na wameandaa mpango mkakati wa miaka mitano ambao una miradi kadhaa, ikiwemo Soko la Machinga la Manispaa ya Tabora, na tunafuatilia kwa karibu kuona wanakamilisha usanifu na michoro na kuiwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, ili sisi tuipitie na kuridhia na ujenzi uweze kuanza mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Manispaa ya Tabora, wamepanga kwenye mipango yao kuanza mwaka wa fedha 2027/2028, lakini kwa sababu ya uhitaji wa soko hilo, tutawaelekeza waweze kuanza mapema zaidi mwaka huu wa fedha, ili kuweza kufikisha huduma hizi muhimu kwa wananchi wa Tabora. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mwaifunga, Serikali hii inatambua umuhimu na ndiyo maana tumewaelekeza na wataleta maandiko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko tayari hata wakileta leo kufanya tathmini kwa ajili ya kuanza hatua mbalimbali za ujenzi, kwanza, kupitia mapato ya ndani ya manispaa. Pili, halmashauri tayari imetenga, katika mwaka ujao wa fedha, shilingi milioni 150 kwa ajili ya soko hilo. Kwa hiyo, ninamhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge, tutasimamia suala hilo na tutahakikisha kwamba soko hilo la Machinga linajengwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawaona mko wengi, naomba maswali mafupi. Mheshimiwa Bahati Ndingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Mkakati uliopo kwenye ilani yetu ni kutujengea soko kubwa la Kimataifa la zao la mpunga ndani ya Jimbo la Mbarali. Lini mkakati huo utaanza ili wakulima wa Mbarali waweze kupata soko la uhakika la zao lao la mpunga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, uko mpango wa Serikali wa kujenga masoko ya kimkakati katika maeneo mbalimbali, ikiwemo katika Jimbo la Mbarali. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mipango mikakati iko katika hatua mbalimbali; kwanza mingine iko kwenye maandiko ngazi ya halmashauri, mingine iko ngazi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na mingine iko ngazi ya Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, tutahakikisha pia, tunafuatilia hatua za utekelezaji wa soko hilo ili liweze kujengwa katika eneo ambalo limepangwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amosy Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mji wa Sikonge ni miongoni mwa miji mikongwe sana katika Taifa letu, lakini umekuwa hauna soko kwa muda wote huu, na kwa vile katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi wameahidi kujengewa soko hilo, je, Serikali ni lini sasa itaanza ujenzi wa soko hilo katika Mji wa Sikonge?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia nafasi hii kuwakumbusha Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kwamba, katika mipango yao ya kila mwaka ni muhimu kuainisha vipaumbele ambavyo ni mahitaji ya juu ya jamii katika maeneo yao, yakiwemo masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Halmashauri ya Sikonge ni halmashauri kongwe na inahitaji kuwa na soko zuri ambalo litakidhi mahitaji ya wananchi wa Sikonge. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Maganga, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, namwelekeza Mkurugenzi wa

Halmashauri ya Sikonge kwanza wafanye tathmini ya gharama zinazohitajika katika ujenzi wa soko hilo, waainishe eneo, na pia, waanze kutenga fedha za mapato ya ndani kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikihitajika Serikali Kuu kuunga mkono, tutaunga mkono wakileta andiko hilo. Lengo ni kuhakikisha kwamba, soko hilo linajengwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tinnar Chenge, swali la nyongeza.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Bariadi ni Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu, na kwa kuwa, mji huu unakua kwa haraka sana, je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga soko kwa maana ya Machinga *Complex* kwa ajili ya wajasiriamali wa Mkoa wa Simiyu?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkipiga makofi kabla Mbunge hajauliza swali, Mheshimiwa Waziri hawezi kusikia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Tinnar ninaomba urudie swali lako.

Waheshimiwa Wabunge tuwe wavumilivu. Tupige makofi baada ya majibu.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Bariadi ni Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu, na kwa kuwa mji huu unakua kwa kasi sana; je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga soko, kwa maana ya Machinga *Complex*, kwa ajili ya wajasiriamali wa Mkoa wa Simiyu?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Swali ni fupi na la Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Bariadi kwanza ni miongoni mwa halmashauri ambazo ziko kwenye Mpango wa *TACTIC*. Ninafahamu kwamba, soko la pale Mjini Bariadi limeingizwa kwenye Mpango wa *TACTIC* na hatua zimeanza kutekelezwa. Kwa hiyo, pale litajengwa soko la kisasa sana kwa ajili ya

Halmashauri ya Mji wa Bariadi ambapo ni Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumepokea ombi la Mheshimiwa Mbunge la kuhitaji kujenga Machinga *Complex*. Tutafanya tathmini na kuona uwezekano wa kufanya hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Jimbo la Nanyumbu halina soko. Mahali ambapo soko lipo ni viwanja vya watu binafsi. Sasa ninaomba kuuliza, ni lini Serikali itatuletea fedha, ili tujengewe soko la kisasa, kama lilivyoainishwa katika mchoro ambao tumeuleta Wizarani na usanifu na kila kitu kimefanyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba, halmashauri zetu, na hususan maeneo ya miji, tunakuwa na masoko yanayokidhi mahitaji. Ninatumia nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itafuatilia kupitia Halmashauri ya Nanyumbu kuona watafute kwanza eneo kwa sababu, eneo linalotumika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, siyo eneo la Serikali. Ni muhimu halmashauri wapate eneo lao na tuweke mipango endelevu ya kujenga soko kwa ajili ya huduma za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulifuatilie suala hili. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nanyumbu tunamwelekeza aanze mchakato huo mapema iwezekanavyo ili Serikali iweze kuona namna ya kushirikiana na mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa soko hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fagason Nkingwa, swali la nyongeza.

**MHE. FAGASON A. NKINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niulize swali dogo la nyongeza. Jimbo langu la Mbogwe lina kata 17, lakini zipo kata tatu ambazo hazina masoko ya kisasa nazo ni Kata ya Masumbwe, Nyakafulu na Lulembela. Je, ni lini Serikali ina mpango wa kuja kuweka soko la kisasa katika kata hizi tatu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, zipo Kata ambazo zina idadi kubwa ya wananchi na zina uhitaji wa masoko kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mbogwe amezitaja. Ninaomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaendelea kwa awamu na tunafahamu safari ni hatua, kata hizo zinahitaji masoko. Tutaendelea kutenga fedha ili kuhakikisha kwamba tunajenga masoko hayo kwa awamu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 196

**Ujenzi wa Barabara ya Hedaru – Mamba Vunta**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza: -

Je, lini barabara ya Hedaru - Mamba Vunta yenye Km 42.44 itaboreshwa ili kuokoa uchumi wa Wananchi wa Kata ya Mamba Vunta?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa

Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikihudumia Barabara ya Hedaru - Vunta - Myamba yenye urefu wa kilometa 42.44 (Hedaru - Mamba Vunta) kwa vipindi tofauti kwa kuijenga na kuifanyia matengenezo mbalimbali tangu mwaka 2020/2021 hadi 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu zenye kona hatarishi 13 zilizoko katika mlima wa Kidenge zilifanyiwa matengenezo makubwa. Matengenezo hayo ni kujengwa kwa kiwango cha zege kwa kilomita 2.04, kujenga makalavati 18, drifti nane, daraja moja, ujenzi wa mifereji mita 1,800, kuchonga barabara kilometa 40, kuweka changarawe kilomita 15 na ujenzi wa kingo kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa barabara kwa jumla ya shilingi bilioni 2.73.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali imeweka katika mipango yake bajeti ya shilingi milioni 102 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya kawaida katika barabara ili kuhakikisha inaendelea kupitika wakati wote, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alipokuja Same tarehe 30 Septemba, 2025 alisema maneno haya, “kwa kuwa najua barabara za kule mlimani Tarafa ya Mamba mvua zinaponyesha mnashindwa kusafirisha tangawizi, tunakwenda kuzijenga barabara hizo kwa zege na lami.”

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni baada ya Rais kutoa ahadi hii, ni vyema sasa wakati sisi wananchi tunasubiri ujenzi mkubwa wa lami na zege, ikajengwa barabara hii yote

kutoka Hedaru – Vunta mpaka Mamba kwa kiwango cha changarawe ili barabara hii iweze kupitika kwa miezi yote 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Hapa ninapoongea, niliposimama, barabara ile sehemu ya Kata ya Mpinji haipitiki kabisa. Kwa hiyo, malori mengi yapo pale yanatafuta njia ya kupeleka tangawizi tambarare. Je, Serikali haioni ni vema sasa ikafanya jambo la dharura tu kwenda kutengeneza ile barabara pale Mpinji ili kuboresha uchumi wa wananchi wangu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie mama yangu, Mheshimiwa, Anne Kilango Malecela kwamba Serikali inaitambua sana barabara hiyo na ndiyo maana katika kila mwaka wa fedha imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ujenzi na kuhakikisha kwamba inapitika, kwa sababu ni barabara muhimu ya shughuli za kiuchumi na za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kipaumbele namba moja. Tunafahamu Rais ameelekeza, na Serikali tupo kwenye taratibu za kuandaa fedha kwa awamu kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa maelekezo hayo. Kwa hiyo wananchi wa Jimbo la Same Mashariki na Mheshimiwa Mbunge wawe na uhakika kwamba Serikali itatekeleza ahadi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Same, pamoja na Mkoa wa Kilimanjaro, wafike mara moja kwenye hilo eneo ambalo lina changamoto na halipitiki kwa sasa ili tuweze kuona namna ya kulitengeneza kwa dharura ili wananchi waweze kupitisha mizigo yao na kuendelea na shughuli zao za kiuchumi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Morris Makoi, swali la nyongeza.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Ninaomba niungane na Mheshimiwa Mbunge wa Same, Mheshimiwa Anne Kilango. Mheshimiwa Rais alipokuja Kilimanjaro alitoa ahadi ya kumalizia ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, barabara ya Rau Madukani - Materuni Shimbwe yenye kilometa 9.7. Ninaomba kauli ya Waziri ni lini Serikali itamalizia sehemu iliyobaki, kwa sababu sehemu hiyo inasaidia sana utalii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu hiyo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema. Kama nilivyosema, ninarejea kwamba ahadi za Rais ni kipaumbele namba moja katika utekelezaji wa miradi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba barabara hiyo ya kilometa tisa ipo kwenye mpango hivi sasa, na tutaendelea kuhakikisha tunatafuta fedha mapema iwezekanavyo kwa awamu kuendelea kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili iweze kutoa huduma ambayo inahitajika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, *TARURA* imekuwa ikijenga barabara kwa kiwango cha lami kwa baadhi ya *centre,* lakini katika Halmashauri ya Shinyanga, Jimbo la Solwa hakuna Kata ambayo ina barabara ya kiwango cha lami, ni lini Serikali itatujengea angalau kwenye Makao Makuu ya Halmashauri barabara kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mpango wetu wa barabara za vijijini na mijini tunazo barabara za udongo, barabara za changarawe na barabara za lami, na tumeweka kipaumbele kuendelea kuongeza barabara za lami, hususan maeneo ya miji ili kuendelea kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie kwamba tunapoendelea na bajeti zetu, tutatoa kipaumbele kwenye eneo la Jimbo hilo la Solwa na hizo barabara za Kata zile ambazo zinawezekana kujengwa kwa awamu, tutaanza ujenzi kwa awamu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Barabara ya Kapanga - Bujombe - Kalia inayounganisha na Wilaya ya Uvinza Mkoa Kigoma, ina hali mbaya baada ya mvua kunyesha na Serikali iliahidi kutoa fedha za kuiunganisha hiyo barabara kwa shilingi bilioni 1.5. Ni lini Serikali itatoa fedha hizo ili iweze kujenga hiyo barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, zipo barabara ambazo zimeathiriwa sana na mvua ambazo zinaendelea kunyesha kote nchini, ikiwepo barabara ambayo Mheshimiwa Kakoso ameisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumetoa taarifa kadhaa kwa Wabunge, tayari Serikali katika kipindi cha miezi hii miwili iliyopita imepeleka katika Majimbo yetu zaidi ya shilingi bilioni 21.4 kwa ajili ya kufanya shughuli za dharura za kutengeneza barabara ili ziweze kupitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tunaendelea na tathmini za mwisho kwa sababu bado kuna maeneo mvua zinaendelea kunyesha. Kwa hiyo, tunafanya tathmini za mwisho za gharama za fedha zinazohitajika kwa ajili ya kwenda kufanya marekebisho na matengenezo ya barabara hizo, na mpaka wiki mbili zilizopita tulikuwa tuna takribani shilingi bilioni 98 zinahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kakoso, mara baada ya kukamilisha tathmini hiyo, tutaanza kupeleka fedha za dharura kwa ajili ya kurekebisha barabara hizo na tutahakikisha pia barabara hiyo inapelekewa hiyo shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya matengenezo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa, Mbunge wa Bukoba Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 197

**Upanuzi wa Kituo cha Umeme Kibeta**

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha upanuzi wa Kituo cha umeme Kibeta?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini kwa niaba ya Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa *Eng.* Johnston Johansen Mutasingwa, Mbunge wa Bukoba Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea na upanuzi wa Kituo cha Kupooza Umeme cha

Kibeta kwa kuongeza uwezo wa transfoma iliyokuwepo kutoka *MVA 20* na kufunga transfoma yenye uwezo wa miundombinu ya Gridi ya Taifa ambapo utekelezaji wake umefikia 95% na unatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu wa 2026. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Johnston Johansen Mutasingwa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda niishukuru Serikali kwa majibu mazuri iliyoyatoa na sasa naona changamoto ya umeme kupungua au *low voltage* katika Jimbo letu la Bukoba Mjini linaenda kutoweka. Sasa ninapenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Je, ni lini Serikali sasa itamlipa huyu mkandarasi ili aweze kumaliza hiyo kazi kwa wakati na kama Serikali ilivyoahidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, katika Jimbo letu la Bukoba Mjini tuna Kata kama nane ambazo zinapakana na Jimbo la Bukoba Vijijini ambazo ni Ijuganyondo, Tendagulo, Kibeta, Kashai hasa maeneo ya Rwomwe, Ijuganyondo, Kahororo na Buhembe. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi hawa umeme wa *REA* kwa shilingi 27,000 ili waweze na wenyewe kupata huduma ya umeme kwa uhakika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba kumpongeza *Engineer* Mutasingwa, Mbunge wa Bukoba Mjini kwa jinsi ambavyo amekuwa mtetezi wa dhati wa mahitaji ya msingi ya wapigakura wake wa Jimbo la Bukoba Mjini. *Engineer* huyu kwa kweli anapenda wapigakura wake wajue kwamba hawakukosea kumleta katika Bunge lako Tukufu, maana ni mtetezi wa kweli wa mahitaji ya watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la msingi, ni lini huu mradi utakamilishwa wa kuongeza hiyo transfoma ya kuongeza umeme ambao umeshatekelezwa kwa 65%,

ninapenda kukuhakikishia kwamba, kwa kuwa *IPT* imeshapelekwa Wizara ya Fedha, mkandarasi huyu atalipwa na mradi huu unakwenda kukamilika ndani ya muda uliopangwa ambao ni kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu Kata na Vijiji alivyovitaja anavyoviombea vipewe umeme wa *REA*, hizi bila shaka ni vile vijiji vinavyopakana na Miji, tunaviita *Peri-urban areas* ambavyo kuna siku Waziri amesimama hapa katika Bunge lako Tukufu akatoa ufafanuzi kwamba vijiji hivyo vinavyopakana na miji yenye hadhi ya vijiji, vyote vitakwenda kupatiwa umeme wa *REA* kwa bei ya shilingi 27,000. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Mji Njombe ni eneo linalokua kiuwekezaji, lakini haliwezi kuendelea na kupata wawekezaji wengi kama hatuna *substation*. Ni lini Serikali itajenga *substation* kubwa itakayovutia uwekezaji Njombe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Nishati, imeshafanya tathmini ya mahitaji ya umeme katika nchi nzima na ni katika azma hiyo Serikali imeweza kufikisha umeme katika vijiji vyote vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na maeneo yote yanayohitaji kuongezewa nguvu ya umeme, transfoma, na vituo vya kupoza umeme. Pia vinazingatia ikiwa ni pamoja na eneo lake. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba Serikali ipo kazini kuhakikisha kwamba atafikishiwa umeme wanaouhitaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhael Lufungija, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii. Jimbo la Ulyankulu ni miongoni mwa majimbo yenye shida kubwa ya kukatikakatika kwa umeme mara kwa mara, na wakati huo huo umeme tunaupata kutoka

Mkoani Tabora zaidi ya kilometa 90, na tunayo miradi mingi ya uwekezaji ikiwepo migodi ya madini, vituo vya afya sita na sekondari...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa umezima, washa kisemeo.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itatujengea *switching station* kwa ajili ya kuweka uimara ya ukatikaji wa umeme katikaJimbo la Ulyankulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge pia kwa maswali hayo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba mpango wa Serikali wa kusambaza umeme toshelevu katika maeneo yote ya nchi yetu unaendelea. Baada ya ukamilishaji wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, sasa hivi shida ya nchi yetu siyo umeme tena, ni ujenzi wa miundombinu ya kufikisha umeme kwa walengwa wote ikiwepo migodi, sehemu za kutoa huduma za afya kama elimu na maeneo yote ya matumizi ya jamii na hasa maeneo ya biashara ambayo inaiingizia Taifa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, awe na subira, utekelezaji wa miradi yote inaendelea sambamba na sawia katika nchi nzima ikiwepo eneo lake.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, sasa aulize swali lake.

**27 APRILI, 2026**

Na. 198

**Bei Elekezi ya Makato ya Huduma za *Mobile Money* Nchini**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali haitoi bei elekezi kwa makato ya huduma za *Mobile Money* ili kuwapunguzia gharama wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu Swali Na. 198 la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa huduma za miamala ya fedha kwa mitandao ya simu zinapatikana kwa gharama nafuu. Hatua hizi zimejikita katika kupunguza gharama za miamala ya kielektroniki, kuimarisha miundombinu ya mifumo ya malipo na kuweka mazingira rafiki ya kisera na kikanuni ili kuchochea matumizi ya huduma za kifedha za kidijitali na kupunguza gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zifuatazo zimechukuliwa kwa kipindi cha mwaka 2024 na 2025: -

(i) Mwezi Aprili, 2024 Benki Kuu ya Tanzania iliweka kikomo cha juu cha gharama ya muamala kwa Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Papo na Mfumo wa *Tanzania Automated Clearing House (TACH)* kwa miamala kati ya benki na benki, ambapo gharama ya juu kwa muamala mmoja ni shilingi 2,000.

(ii) Mwezi Aprili, 2025, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kupunguza gharama za miamala ya kutuma fedha kidijitali, ikijumuisha miamala ya kuhamisha fedha kutoka simu kwenda akaunti za benki na kutoka benki kwenda simu kupitia mfumo wa malipo madogo na ya haraka. Gharama za miamala

zimepunguzwa na kuwekwa ukomo wa shilingi 5,000 kwa miamala yote inayozidi shilingi 500,000, kwa miamala isiyozidi shilingi 500,000, mwongozo wa ukomo wa gharama kwa kiwango tofauti umeainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutoa leseni kwa watoa huduma mbalimbali ili kuhakikisha ushindani katika sekta ya mifumo ya malipo ya kielektroniki. Hadi kufikia mwezi Machi, 2026, watoa huduma 113 walikuwa wameshapata leseni ya kutoa huduma za mifumo ya malipo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kushirikiana na watoa huduma wa mifumo ya malipo ya kielektroniki katika kufanya tathmini ya gharama za miamala na kuchukua hatua zinazofaa za kupunguza gharama ziada, bila ya kuathiri uthabiti na usalama wa mfumo wa malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya ziada tu ni kwamba, kwa ujumla bado Serikali inaendelea kutumia Sera ya Soko Huria na kuhimiza ushindani wa haki unaozingatia haki ya mlaji na uwazi wa kupatikana taarifa za bei kupitia Benki yetu Kuu, ambayo pia inatoa mwongozo wa bei na tozo mbalimbali.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa hatua ambazo inazichukua katika kuhakikisha kwamba utumiaji wa huduma za kidijitali kwenye utumiaji wa fedha unakuwa na unafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu mimi lililenga kwenye huduma ya simu kwa simu, sikuwa na tatizo kati ya benki na simu, simu na benki, lakini ni mtu kwa mtu. Simu moja kwenda simu nyingine. Ukituma unakatwa fedha, ukipokea unakatwa fedha; mwananchi hana unafuu. Swali langu ni kwa nini kusiwepo na bei elekezi kutoka Benki Kuu kuweka kikomo kama ilivyoweka kikomo kwenye huduma za benki na simu? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ni kwa nini Serikali isifikirie kuondoa angalau upande mmoja, kwamba ukituma unaweza ukakatwa, lakini wakati wa kupokea, wapokee bure, ili fedha ziweze zikazunguka na kuwasaidia wananchi wetu kuwaondolea mzigo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, ninamshukuru sana Mheshimiwa Tarimba Abbas, kwenye swali lake na ni kweli kulikuwa na sehemu muhimu hii ambayo ameitaja ya huduma ya fedha za moja kwa moja, mtu na mtu. Kwenye hili ndiyo nilisema kwamba sera yetu hasa ilikuwa ni kuendelea kuwa na soko huria, lakini kwa kujali masilahi ya mlaji. Kwa sasa hivi hakukuwa na bei kwenye ukomo wa bei, lakini Benki Kuu imeendelea kufuatilia kwa ukaribu gharama ambazo zinatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu imeendelea kutoa mwongozo; na imetoa mwongozo wa ada hizi ambazo zinatozwa na kampuni za simu kwenye huduma za *mobile service*, imetoa mwongozo mwaka 2024, imesisitiza kuwepo kwa uwazi na *disclosure*. Kwa hiyo, kila mtoa huduma za malipo ya fedha analazimika kuweka bei ambazo atazi-*charge* ambazo tunazitumia kwenye huduma za kutuma na kutolea pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Benki Kuu imeweka kiwango cha ulinganisho, kimeweka kwenye *portal,* na pia imeweka na kiwango cha ulinganisho, wenyewe wanaita *plus comparator* ambayo inasaidia watumaji na watoaji wa huduma kuweza kuona zile *charge* zenyewe. Kwa hiyo, kwenye ukomo hakujawekwa, lakini kumetolewa mwongozo wa namna ya kuweka *chargers* mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Tarimba lile la kuondoa upande mmoja, tulichukuwe, lakini kwa sasa hivi bado mtumaji na mtoaji vilevile wanachajiwa kwa sababu wote wawili wanapata huduma.

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa majibu ya swali la Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, Mbunge wa Singida Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 199

**Kukamilika kwa Mradi wa Maji Katika Mitaa 38 ya Manispaa ya Singida**

**MHE. YAGI M. KIARATU** aliuliza: -

Je, lini mradi wa maji unaotekelezwa katika mitaa 38 ya Manispaa ya Singida utakamilika ili wananchi wapate huduma ya majisafi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Injinia Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji wa mitaa 88 katika Manispaa ya Singida ni miongoni mwa Mradi wa Maji wa Miji 28 unaotekelezwa na Serikali kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 17.7. Kazi zilizopangwa kutekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu 12, ujenzi wa matanki tisa yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 4.1, ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 58.7 sanjari na ujenzi wa kituo cha uendeshaji wa mitambo *(pump station)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu mingine unaendelea sambamba na utafiti wa maji chini ya ardhi ili kuweza kupata visima vitakavyoweza kukidhi mahitaji ya mradi huu ambayo ni lita za maji milioni 22.3 kwa siku. Aidha, visima vitatu tayari vimechimbwa na vina uwezo wa uzalishaji wa maji

zaidi ya lita milioni 4.9 kwa siku. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha visima vyote vinavyohitajika vinachimbwa na mradi kuendelea na utekelezaji ambapo unatarajiwa, kwa mujibu wa mkataba, utakamalika ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yagi, swali la nyongeza.

**MHE. YAGI M. KIARATU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitaishukuru Serikali kutokana na historia ya upatikanaji wa majisafi na salama kwa Mji wa Singida. Hata hivyo, bado lipo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mji wa Singida wananchi wanahitaji lita milioni 24 kwa siku ilhali upatikanaji ni lita milioni 11 kwa siku; utaona ni chini ya 50% ya mahitaji ya wananchi. Mradi huu wa miji 28 anaousemea Mheshimiwa Naibu Waziri ni mradi ambao umechelewa sana. Mkataba ulisainiwa Juni, 2022 lakini mradi ukaanza Aprili, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuamini mpaka leo bado wanachimba visima, hakuna matanki yaliyojengwa wala mitandao haijatandazwa. Hii inawasababishia wananchi adha ya maji, na hivi ninavyoongea, kuna mgawo mkali wa maji katika mji wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Viko vijiji 12 na mitaa kumi ambayo haijawahi kupata maji ya bomba tangu vijiji hivyo vimeanzishwa. Vijiji hivyo ni Uhamaka, Mwampafa, Isomia, Mwachichi, Unyamikumbi A, Unyamikumbi B, Ikhade, Ugauga A, Ugauga B, Ikenga, Isasida A, Isasida B, Unyambwa A, Unyambwa B, Mtamaa A, Mtamaa B, Kimai, Mtaa wa Mtisi, Mwinyutuka na vijiji vingine. Wananchi hawa hawajawahi kufungua bomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba *commitment* ya Waziri, na ikibidi, akikubali, basi tutafute muda tuongozane mimi na yeye akaone hali halisi huko ndani. Wananchi wanachangia maji na wanyama katika enzi hizi ambazo Rais ana nia nzuri ya kuwatua wanawake ndoo kichwani…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, umeeleweka.

**MHE. YAGI M. KIARATU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba majibu ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, Mbunge mahiri kabisa kutoka Jimbo la Singida Mjini na kwa namna ambavyo anafuatilia kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba ni kweli tunayo mitaa ambayo bado haina maji, lakini pia tunavyo vijiji kwa sababu jimbo lake lina vijiji na mitaa, katika mitaa 53, mitaa 40 ina maji, mitaa mitatu ina maji ambayo kidogo hayatoshelezi, lakini mitaa 10 ndiyo mitaa ambayo haina maji kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vijiji 19, tunavyo vijiji saba ambavyo vina maji ya kutosha, pia tuna vijiji takribani vitatu ambavyo maji yake hayatoshi. Vijiji vingine vilivyobaki tunakiri kama Serikali, kwamba bado maji hayajafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi, Serikali mpaka sasa imeshafanya kazi kubwa sana kwa sababu hadi sasa Jimbo la Singida Mjini upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama umefikia zaidi ya 76%. Tunatambua kuwa bado kuna kazi kubwa ambayo tunaendelea kuifanya, lakini kwenye suala la mradi huu wa miji 28, dhamira ya Serikali siyo kuchelewesha miradi, bali kukamilisha miradi ili itoe matokeo, na wananchi wapate huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mradi huu wa Singida ni kwamba visima ambavyo vilikuwa vinachimbwa, *scenario* hii ni sawa na kule Chunya, kwamba wanachimba, lakini visima vinamomonyokea ndani kiasi kwamba wanachimba, lakini bado kunakuwa na changamoto ya kukiendeleza kwa sababu udongo unarudi ndani. Mkandarasi alipata shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tumeamua kumtumia mkandarasi aliyechimba Nzunguni, Zuzu, na Nala, sasa tunamhamishia ili aende na vifaa vyake akachimbe katika Mradi wa Miji 28 Singida Mjini ambapo mpaka sasa tumeshachimba visima vitatu. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imejidhatiti na iko makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kutengeneza mradi ambao hautakuwa na matokeo, na hatuwezi kutengeneza mradi ambao baada ya muda mfupi unakuwa umebaki kama *white elephant*. Kwa hiyo, tuko makini kufuatilia ili utakapokamilika, utoe matokeo yaliyokusudiwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho, niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo lake la Singida Mjini ili kujionea hali halisi ya maendeleo ya miradi mbalimbali ndani ya jimbo lake.

**NAIBU SPIKA:** Asante. Mheshimiwa Nancy Nyalusi, swali fupi la nyongeza.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, lini Serikali itamalizia mradi wa maji katika Kata ya Wambingetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua kata hiyo iko katika jimbo lipi?

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kilolo, Wilaya ya Kilolo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Nancy, kwa kuendelea kuwasemea akina mama, hasa katika kumtua mama ndoo kichwani; na hiyo ni dhamira ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Tunaendelea kuhakikisha kwamba sera yetu ya maji inahakikisha kwamba watu wapate huduma ya majisafi na salama. Vijiji vyake hasa katika kata ambayo ameitaja katika

Jimbo la Kilolo tumeiweka kwenye mpango wa bajeti wa mwaka 2026/2027 ili iende ikatekelezwe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujua, nini mpango wa Serikali kupeleka fedha za mradi wa maji wa Mafizi ambao sasa hivi umefikia 98%, lakini mkandarasi hajalipwa hata senti tano? Halikadhalika Mradi wa Maji wa Nyani ambao umefikia 75%, lakini miradi hiyo yote wakandarasi hawajalipwa, kwa mfano Nyani wamefanya hadi *mobilization* ya vifaa; je, Serikali ina mpango gani wa kulipa fedha ili kazi hiyo ikamalike na wananchi wapate maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba miradi yote ambayo imefikia katika hatua nzuri za utekelezaji, tunasukuma kwa nguvu kubwa sana upelekaji wa fedha ili miradi hiyo ianze kutoa matokeo. Ni dhamira ya Serikali pia kwamba pale ambapo tutakamaliza miradi ambayo imefikia katika hatua nzuri, tunakuja katika miradi ambayo iko katika hatua za katikati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba tunayo *commitment* ya Serikali katika miradi mingi nchini ambapo tutakuwa tunapeleka fedha kwa awamu kwa vipaumbele vya kimkakati. Lengo ni kwamba Watanzania waendelee kupata huduma ya majisafi na salama. Tunatambua kwamba Serikali ina dhamira ya kuikamilisha miradi hii yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe hofu kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo kwa kuendelea kuwasemea wananchi wake na sisi Wizara ya Maji tutaendelea kushirikiana naye ili kuhakikisha kwamba miradi hiyo inakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ningependa kujua ni lini mradi wa Mugango – Kiabakari – Butiama kwa vijiji kumi ambavyo vinne ni vya Kata ya Biregi, viwili ni vya Kata ya Mtuguri, kimoja Kata ya Isaba, na kimoja Kata ya Busengwe vitaanza kupata maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imewekeza fedha zaidi ya shilingi bilioni 70 ndani ya Mugango – Kiabakari – Butiama ambapo tayari mradi huo ulishaanza kutoa huduma ya majisafi na salama. Mimi pia nilifanya ziara na Mheshimiwa Mbunge, tukashirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tukabaini kwamba ni kweli kuna maeneo bado ambayo bado yana changamoto. Sasa, tunachokifanya kupitia mradi huo, tunafanya upanuzi ili uende kwenye kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amezisema. Sasa mpango wa Serikali, tumeweka kwenye bajeti ili kuhakikisha sasa tunaenda kufanya *extension* ya mradi huu ili uweze kufika katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyahitaji.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 200

**Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria – Mji wa Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza: -

Je, lini Mradi wa Maji Ziwa Victoria utakamilika na kutoa huduma ya Maji kwa Mitaa yote 81 ndani ya Mji wa Tarime?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa Maji wa Miji 28 wa Rorya - Tarime uliopo mkoani Mara kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 134. Kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huu ni pamoja na ujenzi wa dakio *(intake)* katika Ziwa Victoria lenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 29 kwa siku; ujenzi wa mtambo wa kutibu maji, *(treatment plant)*, wenye uwezo wa kutibu maji lita milioni 28 kwa siku; ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 110; ujenzi wa matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita milioni kumi; sanjari na ujenzi wa kituo kimoja cha kusukuma maji, *(booster station)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu umefikia wastani wa 16% na unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 kulingana na upatikanaji wa fedha, ambapo unalenga kunufaisha zaidi ya wananchi 460,000 waishio katika Wilaya za Rorya na Tarime, ikiwemo mitaa 81 iliyopo kwenye kata nane za Tarime Mjini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Mradi huu ulitarajiwa kukamilika Novemba, 2025, wakafanya *extension* kuja Septemba, 2026. Nimeuliza takribani mara 40. Bunge lililopita niliuliza takribani mara 26 na Bunge hili takribani mara 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, kwa kuwa Mji wa Tarime una mitaa 81 una kata nane. Kata nne tu ndizo zinapata kama takribani 45% za maji; kata nne nyingine hazipati kabisa maji; na zile kata zina mitaa, lakini zina taswira kama ya vijiji. Ninataka kujua ni kwa nini sasa Serikali iweke mpango wa dharura wakati tukisubiri mradi huu ambao unachukua muda mrefu sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ione kuwa kuna haja ya kuchimba visima kwenye kata hizi, ili hii mitaa ambayo haina maji kabisa, hasa kwenye taasisi za shule na vituo vya afya waweze

kupata maji wakati tukisubiria huu mradi wa Ziwa Victoria kama vile ambavyo wenzenu wa umeme wanafanya wanapeleka *REA* kwenye mitaa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mradi huu wakati unapita, kuna wananchi ambao ardhi zao zimechukuliwa kwa ajili ya kupisha mradi huu lakini mpaka sasa wananchi hawa hawajajua hatma yao lini watalipwa fidia zao. Ninataka nijue ni mkakati gani Serikali ilionao wa haraka kuhakikisha kwamba wanawalipa wale wananchi fidia waliopisha mradi huu ili kuendelea kupata baraka wakati wanajenga mradi huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Esther Matiko kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya ya kuwasemea wana Tarime Mjini. Pia ninakiri, ukiachana na Bunge lililopita ndani ya kipindi hiki cha Bunge, nimejibu hili swali la Mheshimiwa Esther Matiko zaidi ya mara 10, ninatambua kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba mradi huu una maslahi makubwa sana kwa Majimbo ya Tarime Mjini, Tarime Vijijini, na Rorya; na Waheshimiwa Wabunge wote, akiwemo Mheshimiwa Waitara pamoja na Mheshimiwa Chege wamekuwa wakiuongelea mradi huu. Sisi kama Serikali tumesikia sauti ya Wanatarime, tumesikia sauti ya wananchi wake na sisi tutahakikisha kwamba tunaongeza *speed* ya kupeleka fedha ili mradi huu uende kwa kasi zaidi ili uweze kutoa matokeo kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na fidia, labda niseme hivi, kuhusu fidia ya wananchi tulikubaliana na wananchi wake. Sehemu ambapo bomba linapita Serikali haitalipa fidia, tulikubaliana na kwa maandishi. Maeneo ambayo tunalipa fidia ni eneo la chanzo cha maji, eneo la *booster station* na eneo la mtambo wa kutibu maji; na katika eneo hilo tayari tumeshalipa zaidi ya milioni 36. Orodha tunayo, Mheshimiwa Mbunge akiomba tutampatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunatambua kwamba tuna zaidi ya wananchi 20 ambao wameshalipwa. Eneo ambapo bomba linapita hatulipi fidia ya ardhi, tunalipa fidia ya uharibifu wa mazao. Tayari tumeshafanya tathmini, tunahitaji shilingi milioni 40 na tayari malipo yanaendelea. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tuko makini kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata haki yao kulingana na jinsi ambavyo wamejitolea ili mradi huu uweze kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hivi vijiji katika kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amesema, kata hizi changamoto yake kubwa ni kwamba, visima vinapochimbwa katika hizi kata baada ya kuweka pampu, maji yanakauka. Pia tatizo kubwa la Tarime Mjini vyanzo vya maji ni shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu kwamba umuhimu wa wananchi katika kata hizi tano ikiwemo Nyandoto, Nankende. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi kata tumemwelekeza *MD* aweze kufanya tathmini, iwapo katika kata nyingine kuna mradi ambao una maji ya kutosha, tufanye *extension* kwenda katika hizo kata ambazo zina changamoto ya maji wakati tukiwa tunasubiri utekelezaji wa mradi mkubwa wa Ziwa Victoria wa shilingi bilioni 134 ambao ni uwekezaji mkubwa sana wa Serikali ya Awamu ya Sita. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kelemasimba ambao upo Kata ya Dalai, na Mradi wa Ovada wa Kata ya Ovada, na Mradi wa Maji wa Kubunko ulioko Kata ya Makorongo, miradi hii imekuwa ya muda mrefu, ina takribani zaidi ya miaka miwili haijakamilika. Je, kuna mkakati gani wa haraka wa kukamilisha miradi hii ili wananchi wangu wa Wilaya ya Chemba waweze kupata maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge ambaye pia anatoa ushauri na taarifa, na anawasemea wananchi wa Chemba. Sisi Serikali, dhamira yetu ni kuhakikisha kwamba miradi inakamilika. Nimtoe hofu, tutaongeza *speed* ya kupeleka fedha katika kata hizo ili mkandarasi aweze kukamilisha miradi hiyo na wananchi wake waweze kupata huduma ya majisafi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Regina Malima, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi. Ni jambo la kushangaza kuwa wananchi wa Kisiwa cha Ukerewe kinachozungukwa na Ziwa Victoria hawana majisafi na salama, ikiwemo Kijiji cha Busagami Kata ya Namilembe. Nini kauli ya Serikali juu ya hali hii, na ni hatua gani za haraka zitachukuliwa kuhakikisha wananchi wa kisiwa hiki wanapata huduma ya majisafi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu kwamba kiu ya Mheshimiwa Mbunge ni kuhakikisha wananchi wake wa Ukerewe wanapata huduma ya majisafi na salama kwa 100%, lakini mpaka sasa upatikanaji wa maji ndani ya Kisiwa cha Ukerewe ni zaidi ya 65%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaamini kwamba kiu yake ni kwamba tuongeze ili wananchi wengi zaidi wakiwemo katika Kijiji ambacho Mheshimiwa amekitaja, nikuhakikishie Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza, tayari wanafanya tathmini ya kujua ukubwa wa tatizo ili waweze kufanya usanifu na tuweze ku-*establish* gharama za kwenda kutekeleza miradi ambayo itatatua changamoto ya maji katika Jimbo la Ukerewe. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Paschal Chinyele, swali la nyongeza.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Wakazi wa Mitaa ya Kata za Chang'ombe, Nkuhungu, Mnadani pamoja na Nala, wanakabiliwa na uhaba mkubwa sana wa maji. Hii ni kutokana na kuzidiwa kwa Mfumo wa Maji wa Mzakwe. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa miradi ya maji ya Nzuguni, Nala pamoja na Zuzu ili kuepusha uhaba huo wa maji? Katika kata hizi, vipo vituo vya afya kama Chang'ombe pamoja na Zuzu, lakini havina maji. Ni lini Serikali itashughulikia tatizo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Inyasi, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Jiji la Dodoma ambapo nikiri kabisa kwamba hata ofisini kwetu ameshakuja mara kadhaa, ili kuendelea kuwasemea wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini, wakiwemo Wabunge wanaoishi katika Jiji la Dodoma. Mheshimiwa Chinyele, kwenye suala la miradi yetu, tunao mradi wa Nzuguni, Serikali imewekeza zaidi ya shilingi 9,000,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nzuguni *One* ambapo mradi huo umefikia 98% bado tu kidogo ukamilike. Pia tuna Nzuguni *Two* ambao unaendelea. Tuna mradi wa Nala ambao pia Serikali imewekeza shilingi 4,000,000,000, tunao Mradi wa Zuzu ambao tumeweka shilingi 7,000,000,000 ambapo kwa ujumla wake huo, mahitaji ya Jiji la Dodoma ni lita 160,000,000 mpaka sasa uzalishaji wetu ni lita 80,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii mitatu yote itakapokamilika tutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita 80,000,000 mpaka lita 120,000,000. Maana yake ni kwamba tutakuwa tumefikia zaidi ya 80% ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea na michakato ya miradi hii, na ipo katika hatua nzuri kabisa. Miradi hii itakapokamilika wananchi wa Jiji la Dodoma pamoja na Jimbo la Mtumba itakuwa ina uhakika

wa kupata majisafi na salama, wakiwemo Wabunge wanaoishi katika Jiji hili la Dodoma.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge, naona muda wetu umekimbia, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala, Mbunge wa Kwimba sasa aulize swali lake.

Na. 201

**Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Mazao Hungumalwa**

**MHE. COSMAS M. BULALA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao katika Kijiji cha Hungumalwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha miundombinu ya uhifadhi wa chakula nchini, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali ilikamilisha ujenzi wa ghala 28 katika Mkoa wa Ruvuma yenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 28,000. Lengo ni kuhakikisha upotevu wa mazao ili kuimarisha usalama wa chakula nchini unapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na utaratibu wa kufanya tathmini kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa ghala katika Wilaya mbalimbali ili kubaini mahitaji halisi ya ghala. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara itafanya tathmini katika Wilaya ya Kwimba ili kubaini mahitaji halisi ya ghala kwa kuzingatia hali ya uzalishaji na mahitaji katika maeneo husika na itafanya maamuzi stahiki juu ya suala hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cosmas, swali la nyongeza.

**MHE. COSMAS M. BULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Hungumalwa Jimbo la Kwimba ni kitovu cha biashara ya ukusanyaji, usafirishaji na usambazaji wa mazao kwenye Mkoa wa Mwanza ambao unategemewa na wilaya jirani za Kishapu, Shinyanga Vijijini, Misungwi, Magu na Shinyanga Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini hasa tathmini hiyo itafanyika na kukamilika; na kwa sababu tayari wananchi wa Kijiji cha Hungumalwa wameshatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa ghala ili utekelezaji wa mradi huo uanze?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Wiki iliyopita kumetokea janga katika Vijiji vya Buyogo na Mwang'ombe kwenye Kata ya Hungumalwa ambapo mvua kali ya mawe imenyesha na kuharibu mazao kama mtama, viazi pamoja na mpunga uliopo mashambani. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura kwenda kusaidia wananchi walioathirika na mafuriko haya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Cosmas Bulala, Mbunge wa Jimbo la Kwimba, kwanza, kwa maswali yake ya msingi, na pili, kwa ufuatiliaji ambao amekuwa akiufanya muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja, tunatambua umuhimu wa Mji wa Hungumalwa na tunatambua biashara kubwa inayofanyika pale na nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mwaka wa fedha huu tunaokwenda kuuanza, Serikali itafanya tathmini katika eneo hilo. Baada ya tathmini, tutatafuta fedha ambayo nimhakikishie kwamba tutajenga ghala ambalo litawasaidia wananchi wake katika eneo la Hungumalwa ambao wapo katika Jimbo la Kwimba. Kwa hilo, nina uhakika nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto ambayo imetokana na mvua, nimwambie tu kwamba Wizara ya Kilimo tutashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu ambao ndio wana jukumu kubwa la kuratibu maafa na wakati wanafanya ule uratibu, kila

Wizara ina jukumu lake. Kwa hiyo, tukishamaliza jukumu hilo ninaamini Serikali chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan itapeleka msaada katika eneo hilo kwa wananchi ambao wamekutwa na maafa hayo, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Athumin Mapalilo, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMIN O. MAPALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Wanawake wa Mkoa wa Mtwara hujihusisha zaidi na kilimo cha kunde, njugu na karanga, je, Serikali ina mpango gani wa kuingiza mazao haya katika Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ili tuwe na uhakika wa soko? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimpongeze vilevile Mheshimiwa Mbunge kwa swali la msingi. Ni kweli stakabathi za ghala imekuwa na faida kubwa kwa wananchi, na tumekuwa tukiingiza zao moja baada ya linguine, maana yake hatuwezi kuingiza mazao yote kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaangalia vilevile na ukubwa wa biashara ya hayo mazao, lakini na upatikanaji wake kwa urahisi, na biashara ya soko husika. Kwa hiyo, tutalifanyia tathmini zao la kunde ili tufanye haraka iwezekanavyo kuingiza katika Mfumo wa Stakabadhi ya Ghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili maana yake tunafanya sisi Wizara ya Kilimo tukishirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ambao ndiyo wasimamizi wa Bodi ya *WRRB* wale wasimamizi wa stakabadhi ya ghala.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Enock Zadock Koola, Mbunge wa Vunjo, sasa aulize swali lake.

Na. 202

**Kuanzisha Kituo cha Kukodi Vifaa vya Kilimo**

**MHE. ENOCK Z. KOOLA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanzisha Kituo cha kukodi vifaa vya kilimo katika Wilaya ya Moshi Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inaendelea kutekeleza mpango wa uanzishaji wa vituo 1,000 vya kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima katika ngazi ya Kata ifikapo mwaka 2030, lengo likiwa ni kusogeza na kuwawezesha wakulima, kupata huduma za zana za kilimo kwa wakati na gharama nafuu ili kuongeza uzalishaji na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza hilo, Wizara imeanzisha vituo 79 katika Halmashauri mbalimbali nchini, ikiwemo Halmashauri ya Moshi ambapo jumla ya matrekta madogo ya mkono *(Power tiller)* 29 na zana zake zimepelekwa ili kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kufungua vituo vya zana za kilimo nchini ikiwemo Wilaya ya Moshi vijijini kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Enock Zadock, swali la nyongeza.

**MHE. ENOCK Z. KOOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na kwa kuwa Halmashauri ya Moshi imeshawekwa kwenye awamu ya kwanza, ningependa kujua kauli ya Serikali kuhusu hivi vituo viko wapi na vitajengwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa maeneo ya Jimbo la Vunjo, kuna sehemu kubwa ya tambarare yenye mashamba makubwa ya kilimo cha mpunga; je, Serikali ipo tayari

kupeleka matrekta makubwa yanayokidhi mahitaji na kuongeza tija? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimthibitishie tu Mbunge wa Jimbo la Vunjo, Mheshimiwa Enock Koola kwamba moja, ametaka kujua kauli ya Serikali, kuhusu hayo matrekta yako wapi? Wizara ya Kilimo tunapeleka matrekta katika Halmashauri ya Wilaya na wao wanatuainishia maeneo ambayo sisi tunapeleka kile kituo na hususan yale maeneo ambayo vituo hivi vinapaswa kwenda ni yale maeneo ambayo kuna uzalishaji mkubwa, ndiyo maeneo hayo ambapo tumekuwa tukiweka kama ambavyo iko katika eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika kipindi hiki cha mwanzo, unakuta mengi yamewekwa katika halmashauri za wilaya katika hatua za mwanzo, wakati huo wakitafuta maeneo ambapo yatakwenda kupelekwa kwa ajili ya kutoa hiyo huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali iko tayari kupeleka matrekta makubwa katika maeneo hayo kwa ajili ya kuwasaidia wananchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali iliweza kutoa matrekta na hata Halmashauri yangu ya Mji wa Tunduma niliyaona, je, ni upi utaratibu uliowekwa kwa ajili ya matumizi ya matrekta haya kwa watu wetu huko wilayani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Neema, dada yangu. Utaratibu ni kwamba, lengo la Serikali kwanza ni kuanzisha vituo 1,000 nchi nzima ambavyo vitafika katika halmashauri zote nchini. Moja ya lengo letu ni kupeleka karibu takribani trekta 10,000 kusambaza

katika hivyo vituo. Lengo kubwa la Serikali ni kumpunguzia mkulima gharama ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, matrekta yale yakishakwenda katika yale maeneo, wananchi watakuwa wanakodi kwa bei nafuu, kwa sababu tunaamini kwamba wananchi wengi wanalima chini ya ekari tano. Mtu mwenye ekari tano, ekari moja hahitaji kununua trekta, isipokuwa anahitaji huduma ya trekta, ambayo sasa anaweza kuipata kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama hii, yaani tunasema mfumo huu ni uendelevu wa mfumo wa ruzuku wa kumsaidia mwananchi kupunguza gharama. Kwa hiyo, hilo ndilo lengo la Serikali na tunaendelea kulifanya hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lililopita Serikali ilikubali ombi letu la kuboresha kituo cha Kilimo cha *KATRIN* pale Ifakara kwa kuleta pia zana za kilimo ikiwemo matrekta ili wananchi waweze kuyakodi kwa bei nafuu. Je, mpango huu na mkakati huu umefikia wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Vilevile, ninampongeza kaka yangu Mheshimiwa Asenga kwa kufuatilia jambo hili kwa ajili ya jimbo lake na hususan katika eneo la Ifakara na anajua tumeshalizungumza hili kabla na nimeshampa mpango wa Serikali. Hata hivyo, kwa sababu wananchi wake wanahitaji kusikia hili, ni kwamba hili lipo katika mwaka wa fedha unaokuja kutekelezeka. Tutaongeza hivyo vifaa na wananchi watapata hivyo vifaa na vitawasaidia.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwetu na majibu kutoka kwa upande wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nilete matangazo ya wageni, nitaanza na wageni waliopo kwenye Jukwaa la Spika asubuhi hii. Tunao wageni wa Mheshimiwa Spika kutoka Bunge la Malawi wakiongozwa na Mheshimiwa Illyas Abdulkarim (Mbunge) ambaye ni kiongozi wa msafara. *(Makofi)*

Wapo pia Mheshimiwa Grace Kwelepeta (Mbunge); Mheshimiwa Ishmael Rashid, (Mbunge); Deus Gumba (Mbunge); Mheshimiwa Emmanuel Jere (Mbunge); na Ndugu Harold Kwalimba Afisa Dawati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ni wawakilishi wa Tawi la *CPA* la Bunge la Malawi. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 12 wa Mheshimiwa Spika, ambao ni wa Taasisi ya *TUNAWEZA* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wengine waliokaa Jukwaa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, ambaye ni Waziri wa Madini. Wageni hao ni Mhandisi Yahya Samamba ambaye ni Katibu Mkuu; *IGP* (Mstaafu) Balozi Simon Sirro, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO);* na Dkt. Janet Lekashingo, Mwenyekiti wa Tume ya Madini. *(Makofi)*

Tunaye pia Dkt. George Mofulu, Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Jimolojia Tanzania *(TGC);* Ndugu Yokbeth Myumbilwa, Mwenyekiti Bodi ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania *(GST);* na Dkt. Abdulrahman Mwanga, Kamishna wa Madini. *(Makofi)*

Tunaye pia Mhandisi Theonestina Mwasha, Kamishna wa Tume ya Madini; Dkt. Theresia Numbi, Kamishna wa Tume ya Madini; Ndugu Augustine Ollal, Mkurugenzi wa Sera na Mipango; na Dkt. Venance Mwasse, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)*. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Mariam Mgaya, Katibu Mtendaji Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia; Mhandisi Ramadhani Lwamo, Katibu

Mtendaji Tume ya Madini; na Mhandisi Ally Maganga, Mratibu Kituo cha Jimolojia Tanzania. *(Makofi)*

Tunaye Mhandisi Ally Samaje, Mtendaji Mkuu Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania; na Ndugu Ali Said Ali, Mtendaji Mkuu wa *STAMIGOLD*. *(Makofi)*

Wapo pia, Mheshimiwa Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma; Mheshimiwa Jabir Shekimweri, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma; Alhaj Adam Kimbisa, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma; Ndugu Pili Mbanga, Katibu wa CCM Mkoa wa Dodoma; na Ndugu Charles Mamba, Mwenyekiti ya CCM Wilaya ya Dodoma. *(Makofi)*

Tunaye pia, Ndugu Sofia Kibaba, Katibu wa CCM Wilaya ya Dodoma; Ndugu Aman Mulagizi, Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya ya Dodoma; Ndugu Fadhili Chibago, Mwenyekiti wa Bodi *DUWASA* na Naibu Meya Mstaafu Jiji la Dodoma; na Mheshimiwa Alimwoni Chaula, Meya wa Jiji la Dodoma. *(Makofi)*

Tunaye pia Padri Joby Tharayil, Mwakilishi wa *TEC* Jimbo Kuu Katoliki Dodoma; Mchungaji Elia Makhata, Mwenyekiti *CPCT* Dodoma; Askofu Joseph Mtolela, Mwenyekiti *CCT* Dodoma; na Askofu Dkt. Damas Kasheegu, Mwenyekiti wa Umoja wa Madhehebu Dodoma. *(Makofi)*

Yupo pia, Chifu Yasin Bilinje *IV,* Mwenyekiti wa Machifu wa Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ni Maafisa Madini Wakazi *(RMO's)*, na Baraza la Madiwani wa Jiji la Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini, ambao ni wapiga kura wake kutoka Longido Mkoani Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, kutoka Jijini Dar es Salaam na Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, wapigakura wake kutoka Mkoani Mara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 11 wa Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, wapiga kura wake kutoka Rorya Mkoani Mara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 37 wa Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Wanafunzi na Walimu wa Shule *MJ Islamic* kutoka Jimbo la Mwera Zanzibar. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, Viongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wachimba Madini Tanzania. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao viongozi sita, hao ni Viongozi wa *Ng'imba Mining Company Limited* kutoka Kahama Mkoani Shinyanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 129 na Walimu saba wa Shule ya Awali na Msingi Misericordia ya Jijini Dodoma. Karibuni sana hapa Bungeni, Ahsante. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamwita Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Waziri wa Madini awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua bajeti ya Wizara ya Madini, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida na maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba hotuba yangu yenye kurasa 137 iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa kwenye Ofisi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuendelea kuijalia nchi yetu amani na baraka na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki huu Mkutano wa Tatu. Tunamwomba aendelee kutujaalia rehma, hekma, busara na umoja katika kujadili hotuba za Wizara mbalimbali ikiwemo Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa nia ya kuendeleza Taifa letu na kuboresha ustawi wa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wenye maono mapana, mahiri, weledi na dhamira thabiti ya kuwaletea

Watanzania maendeleo jumuishi. Kwa wakati wote Mheshimiwa Rais ameendelea kuhimiza uwajibikaji, amani, utawala bora, umoja na mshikamano wa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuimarisha na kulinda Muungano, kusimamia masuala ya mazingira na usimamizi bora wa rasirimali zetu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuiongoza Zanzibar vizuri. Hakika kiongozi huyu amekuwa nguzo imara katika kudumisha Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kupitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuendelea vyema kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee ninaomba nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Sekta ya Madini. Ni ahadi yangu kwake na kwa Bunge lako Tukufu pamoja na Watanzania wote kwamba nitaendelea kuitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na kwa uwezo wangu wote ili kuendeleza sekta hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu inayotoa mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za Serikali ambayo imeonesha mafanikio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026, utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 pamoja na mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni kutokana na uzoefu na umahiri wako katika shughuli za Bunge, tunaamini utafanya kazi hii vyema kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa ninampongeza sana Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kuteuliwa na kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya na umahiri mkubwa alionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue fursa hii niwapongeze sana Mheshimiwa *CPA* Subira Khamis Mgalu, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na Mheshimiwa *CPA* Simon Songe Lusengekile, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kuteuliwa kuiongoza Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninawapongeza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kuteuliwa kutekeleza majukumu ya Kamati. Wizara inaishukuru Kamati kwa ushauri wake makini ambao imekuwa ikiutoa katika kuhakikisha kuwa sekta hii inakuwa na tija kwa Taifa na kuwanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninaishukuru Kamati kwa kujadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na kuyapitisha kwa kauli moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Kumi na Tatu kwa kuwa sehemu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaomba ushirikiano wao katika kuendeleza sekta hii muhimu katika kujenga uchumi imara na maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa

kuongoza Wizara mbalimbali. Pia, ninawapongeza viongozi wote waandamizi wa Serikali walioaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nyadhifa mbalimbali. Ninawatakia utendaji mwema katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Mtumba kwa kuniamini na kunichagua. Ninaamini mtaendelea kushirikiana nami katika kutekeleza majukumu yangu kama mwakilishi wenu katika Bunge hili Tukufu. Ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote na kwa kipaji nilichojaliwa na Mwenyezi Mungu katika kuleta maendeleo ya jimbo na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, kwa kuteuliwa tena na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwa Naibu Waziri wa Madini. Aidha, ninamshukuru kwa dhati kabisa kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Hakika amekuwa ni msaada mkubwa kwangu katika kuhakikisha sekta hii inatimiza malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumshukuru Mhandisi Yahya Ismail Samamba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini kwa kuratibu na kusimamia utendaji wa Wizara. Pia, ninampongeza Ndugu Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu kwa kuendelea kumpatia ushirikiano Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninamshukuru Dkt. AbdulRahman Shabani Mwanga, Kamishna wa Madini kwa kutekeleza majukumu yake vizuri. Halikadhalika, nichukue fursa hii kuishukuru Menejimenti ya Wizara pamoja na wafanyakazi wote kwa ushirikiano na utendaji kazi mzuri katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Wenyeviti wa Bodi kwa ushauri na utendaji kazi wa ufanisi katika kusimamia Sekta ya Madini. Viongozi hao ni Dkt. Janeth Lekashingo, Mwenyekiti wa Tume ya Madini; Bi. Yokbeth Myumbilwa, Mwenyekiti wa Bodi ya

*GST*; *IGP* Mstaafu Mheshimiwa Balozi Simon Sirro, Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO*, Mheshimiwa Balozi Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya *TEITI*, Makamishna wa Tume ya Madini; na Wajumbe wa Bodi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini; Mhandisi Ramadhani Lwamo (Katibu Mtendaji, Tume ya Madini), Mhandisi Ally Samaje (Mtendaji Mkuu, *GST*), Dkt. Venance Mwasse (Mkurugenzi Mkuu, *STAMICO*), Bi. Mariam Mgaya (Katibu Mtendaji, *TEITI*) na Mhandisi Ally Maganga (Mratibu wa Kituo cha Jemolojia Tanzania) kwa kuzisimamia kwa makini na weledi taasisi wanazoziongoza. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Maafisa Madini Wakazi *(RMO's)* na Maafisa Migodi Wakazi *(MRO's)* kwa utekelezaji fanisi wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa naishukuru kwa moyo wa dhati familia yangu, mke wangu mpendwa Jacquelyne Moses Lupasa na watoto wangu Atarah na Allan kwa kunipa ushirikiano mkubwa na utulivu katika kusimamia majukumu yangu ya Ubunge na Uwaziri na kukubali kubeba baadhi ya majukumu ya familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa niungane na Watanzania wenzangu kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama. Pia, nitoe pole kwa wananchi wa Dar es Salaam kwa kuondokewa na Mheshimiwa Halima Idd Nassor, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Halikadhalika, nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo la Isimani kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi. Mwenyezi Mungu awarehemu Marehemu na awape faraja familia na wananchi waliokuwa wakiongozwa nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote kutokana na vifo, majeraha, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu kufuatia majanga mbalimbali

yaliyosababishwa na mvua nyingi, ajali za barabarani, majini, moto na migodini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini. Kwa mujibu wa utafiti wa Taasisi ya *Fraser* ya Canada iliyofanyika mwaka 2025 Tanzania ilishika nafasi ya nne Afrika na ya 34 duniani katika kiashiria cha kuvutia uwekezaji *(Investment Attractiveness Index)*. Aidha, Tanzania ilipata alama 68.04 mwaka 2025 ikilinganishwa na alama 62.75 katika mwaka 2024. Vilevile, Tanzania ipo nafasi ya 15 duniani kwa hazina ya rasilimali madini ikiwa na alama 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 2025, Sekta ya Madini imeendelea kuongoza kwa kuvutia uwekezaji wa mtaji wa nje ambapo mwaka 2024 mtaji wa uwekezaji ulifikia dola bilioni 9.79 kutoka dola bilioni 9.15 mwaka kwa 2023 na dola bilioni 8.64 mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili ni matunda ya uhamasishaji wa uwekezaji, mazingira wezeshi kwa wawekezaji yaliyochochea upanuzi wa miradi iliyopo, uwekezaji wa fedha inayozalishwa ndani ya sekta na uunganishaji wa mitaji ndani ya sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imepiga hatua kubwa na ya kihistoria katika kuendeleza Madini Muhimu na Madini Mkakati kwa kuingia makubaliano ya kutekeleza miradi ya *niobium*, nikeli, kinywe na dhahabu katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Mathalani, tarehe 24 Machi, 2026, Serikali ilisaini mkataba wa kuendeleza uchimbaji wa madini ya *niobium* wa *Panda Hill* uliopo Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *Panda Hill* unatarajiwa kuwa ni miongoni mwa miradi mikubwa Afrika na kuiweka Tanzania katika nafasi ya wazalishaji wakubwa wanne duniani. Mradi huu utazalisha ajira 1,600 za moja kwa moja na ajira 1,336 zisizo za moja kwa moja. Ununuzi wa ndani wa takribani dola za Marekani bilioni 1.77 pamoja na uwajibikaji kwa jamii *CSR*. Aidha,

Serikali inatarajia kupata mapato ya takribani shilingi trilioni mbili kutokana na mrabaha, kodi, tozo, gawio za hisa la Serikali za 16% zisizohafifishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa salamu za shukrani, pongezi, pole na baadhi ya mafanikio ya Sekta ya Madini, sasa ninaomba nijielekeze katika maeneo mahsusi ya hotuba yangu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa biashara ya madini duniani umeendelea kubadilika kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na mahitaji ya soko. Mathalani, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, bei ya dhahabu iliongezeka hadi kufikia wastani wa dola 4,190.47 kwa wakia kutoka dola 2,655.80 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Ongezeko hili limechangiwa na mahitaji makubwa ya dhahabu kama hifadhi salama ya thamani ya fedha duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, bei ya almasi ilishuka kwa asilimia tano nukta tatu tisa kutoka wastani wa Dola za Marekani 168.95 kwa karati katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025 na kufikia wastani wa Dola za Marekani 159.84 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2025/2026. Kushuka huko kwa bei kumetokana na uwepo wa almasi ya viwandani *(synthetic diamond)* zilizosababisha kupungua kwa uhitaji wa almasi asilia hususan katika masoko makubwa duniani yakiwemo ya China na Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, bei ya makaa ya mawe imeshuka na kufikia wastani wa dola za Marekani 26.69 kwa tani katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, ikilinganishwa na wastani wa bei ya Dola za Marekani 40.75 kwa tani kwa kipindi kama hicho mwaka 2024/2025 sawa na upungufu wa 34.50%. Upungufu huu wa bei unatokana na kupungua kwa mahitaji ya makaa ya mawe katika Soko la Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa biashara ya madini ya *Tanzanite* umeendelea kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa masoko ya uhakika kutokana na vikwazo vya kibiashara duniani na uwepo wa vito vya kutengeneza viwandani. Aidha,

hali hiyo imesababisha kushuka kwa bei kutoka wastani wa Dola za Marekani 2,433 kwa kilogramu katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 na kufikia Dola za Marekani 2,270.44 kwa kilogramu katika kipindi kama hicho mwaka 2025/2026 sawa na asilimia sita nukta saba mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mahitaji ya madini mkakati na muhimu kama *lithium, cobalt, nickel* na *rare earth elements*, yameendelea kuongezeka kutokana na matumizi yake katika teknolojia za kisasa na nishati safi. Hii inaipa Tanzania fursa ya kuongeza thamani ya madini haya ndani ya nchi ili kukuza mapato, ajira na michango katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 224.98 kwa Wizara ya Madini ambapo shilingi bilioni 100.38 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha shilingi bilioni 76.11 za matumizi mengineyo na bilioni 24.27 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa wizara na taasisi zake. Aidha, shilingi bilioni 124.60 zilitengwa kwa ajili miradi ya maendeleo ikijumuisha shilingi bilioni 71.51 fedha za ndani na shilingi bilioni 53 fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 82.90 ambapo shilingi bilioni 10.48 ni za maendeleo zikiwa ni fedha za ndani na shilingi bilioni 72.43 za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 54.76 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 17.66 kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2025/2026; moja, kuimarisha ukusanyaji maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ilipangiwa kukusanya maduhuli ya shilingi trilioni 1.41 kutoka vyanzo mbalimbali. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.20 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina na shilingi bilioni 205 zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2026 shilingi trilioni 1.03 sawa na 114.94% ya lengo la makusanyo ya kipindi husika zilikusanywa na kuwasilishwa Hazina. Aidha, ili kuongeza maduhuli ya Serikali, Wizara imejipanga kuimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, masoko ya madini, vituo vya ununuzi wa madini na mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2026, biashara ya madini yenye thamani ya shilingi trilioni 4.9 imefanyika kwa kupitia masoko na vituo vya ununuzi wa madini ikilinganishwa na shilingi trilioni 2.82 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini nchini unaofanywa na baadhi ya wachimbaji wa wafanyabiashara wa madini wasio waaminifu. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali imefanikiwa kukamata madini ya aina mbalimbali yenye thamani ya shilingi bilioni 3.31 katika matukio 55 kwenye baadhi ya mikoa ya kimadini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, madini yaliyokamatwa yalitaifishwa na Serikali na watuhumiwa walifikishwa kwenye vyombo vya sheria. Ni rai yangu kwa wachimbaji na wafanyabiashara wote wa madini kuzingatia sheria za nchi kuhusiana na biashara ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato ya fedha za kigeni yatokanayo na mauzo ya madini nje ya nchi yamekuwa yakiimarika mwaka hadi mwaka. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi ilikuwa Dola za Marekani milioni 5.4 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 4.1 mwaka 2024, sawa na ongezeko la 31.1%.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mwaka 2025 thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi yalichangia 52.57% ya mauzo yote ya bidhaa za asili na zisizo za asili yaliyouzwa nje ikilinganishwa na 45.17% mwaka 2024. Vilevile, kwa upande wa mauzo ya bidhaa zisizo za asili pekee, sekta ya madini ilichangia 63.73%

mwaka 2025 ikilinganishwa na mchango wa 56.99% mwaka 2024. Pia, thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 3,419 kwa mwaka 2024 na kufikia Dola za Marekani milioni 4,753 mwaka 2025 sawa na ongezeko la 39.0%.

(b) Kuongeza Mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa sekta ya madini katika pato la Taifa umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka. Mchango huo uliongezeka kufikia asilimia tisa nukta moja mwaka 2023 na kufikia 10.1% mwaka 2024. Aidha, katika kipindi cha robo tatu ya mwaka 2025 yaani Januari mpaka Septemba wastani wa mchango wa sekta umefikia 11.9%. Mwenendo huu umechangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji kwenye sekta ya madini.

(c) Kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini muhimu na madini mkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni 454 za madini muhimu na madini mkakati yakiwemo madini ya kinywe, ambayo ni leseni 271, *nickel* 136, *cobalt* leseni 2, *lithium* leseni 6, *heavy mineral sands* leseni 11 na *rare earth elements* leseni 28. Utoaji wa leseni hizi unaendelea kuweka msingi thabiti wa kukuza uwekezaji katika utafutaji na uendelezaji wa madini muhimu na madini mkakati hapa nchini.

(d) Kuhamasisha uwekezaji na uongezaji thamani madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta ya madini, Wizara imeendelea kutangaza fursa na kutoa elimu kwa umma kupitia ziara za viongozi, vyombo vya habari na mikutano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Aidha, Wizara ilishiriki katika mikutano, makongamano na maonesho ya Kimataifa nane ikiwemo, *Future Minerals Forum* – Saudi Arabia, *Mining Indaba* – Afrika Kusini, *ZIMEC* - Zambia, Mikutano ya *ADPA* na Maonesho ya 69 ya vito Bangkok - Thailand.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ndani ya nchi, Wizara iliandaa na kushiriki maonesho matano yakiwemo Maonesho ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini, Geita, Maonesho ya Saba Saba Dar es Salaam na Maonesho ya Biashara Zanzibar. Jitihada hizi zimeongeza mwamko wa uwekezaji na kuimarisha taswira ya Tanzania Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania na wadau wameendelea kuelimishwa na kufahamishwa kuhusu uwepo wa fursa za uwekezaji katika sekta ya madini ikiwemo sheria, kanuni na miongozo inayosimamia sekta. Aidha, elimu imeendelea kutolewa kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo ni pamoja na jarida la mtandaoni la madini na uchumi, programu maalumu za urushwaji wa vipindi mubashara vilivyoelezea masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya madini. Vyombo hivyo ni pamoja na *TBC*, *Clouds media*, *Crown media*, *ITV*, *Kiss FM*, Azam *media*, Wasafi *media*, *VOA*, *BBC*, *DW*, *TRT*, Radio France, *ZBC* na *Morning Star*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha uandaaji wa mkakati wa uongezaji thamani madini. Mkakati huo unatoa mwelekeo kwa Serikali wa kubadilisha sekta ya madini kutoka kwenye uuzaji wa madini ghafi na kuelekea kuuza madini yaliyoongezewa thamani ndani ya nchi. Lengo kuu ni kutumia rasilimali ya madini kama njia ya kufungamanisha sekta ya madini na sekta nyinginezo za kiuchumi ikiwemo viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mkakati huu utachochea ongezeko la thamani ya madini yetu na kuongeza viwanda vitakavyosababisha upatikanaji wa ajira, pato la Taifa, ubunifu, kuongeza ujuzi na kuimarisha ushindani wa bidhaa zitokanazo na madini katika masoko ya ndani na nje ya nchi kupitia mnyororo imara wa uongezaji thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za uongezaji thamani madini hapa nchini kupitia viwanda sita vya kusafisha dhahabu vilivyopo mkoani Dodoma kimoja, Shinyanga kimoja, Geita viwili kikiwemo kiwanda cha *GGR*, Dar es Salaam kimoja na Mwanza kimoja. Aidha, Wizara

inaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuyeyusha madini ya shaba, nikeli, bati na chumvi katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Kagera, Mbeya, Lindi na Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Wizara inaendelea kushirikiana na wamiliki wa viwanda vya kusafisha dhahabu ili kupata ithibati ya *LBMA* kwa ajili ya kuwezesha viwanda hivyo kutambulika katika masoko ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuimarisha shughuli za uongezaji thamani madini ya vito na metali hapa nchini kwa kuendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa jengo pacha la ghorofa nane katika Kituo cha Jemolojia Tanzania, pale Arusha ili kuongeza uwezo wa kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini.

(e) Kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Soko la Bidhaa Tanzania *(TMX)* iliendesha mnada mmoja wa ndani wa madini ya vito uliofanyika kielektroniki, Jijini Arusha mwezi Novemba, 2025. Katika mnada huo, madini yenye thamani ya shilingi 231,000,000 yalinunuliwa. Hata hivyo, Wizara inaendelea kuhamasisha na kuongeza mwamko wa ushiriki wa wadau katika minada ya madini ya vito.

(f) Kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za kina za madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini *(GST)* imefanya utafiti wa jiofizikia kwa kutumia ndege nyuki katika maeneo ya Geita, Manyara na Lindi ambapo taarifa muhimu za kina za jiolojia zilibainishwa katika maeneo hayo. Sambamba na hilo, umefanyika pia utafiti wa kina wa jiofizikia *(High Resolution Airborne Geophysical Survey)* katika maeneo ya leseni za *STAMICO* zilizoko Mkoa wa Lindi, hatua inayolenga kuongeza uelewa wa kina kuhusu rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti huo uliofanyika umewezesha Serikali kubaini uwezekano wa matumizi ya ndege

nyuki kutumika katika upatikanaji wa taarifa za kina za jiofizikia kwenye leseni ndogo za uchimbaji wa madini. Hivyo, hatua hii itasaidia kutumia teknolojia ya ndege nyuki katika kupata taarifa za kina za jiofizikia kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *GST* imekamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia katika vitalu viwili vya kimkakati vilivyoko Kusini - Magharibi mwa nchi, vyenye ukubwa wa takribani kilometa za mraba 176,676 sawa na 18% ya eneo lote la nchi yetu ya Tanzania. Utekelezaji wa utafiti huu unatarajiwa kuongeza upatikanaji wa taarifa za kina za jiofizikia kutoka 16% ya sasa hadi kufikia 34%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kutokuwepo kwa taarifa za kina za jiofizikia kwenye baadhi ya maeneo ya nchi, Wizara imeendelea kuhamasisha kampuni mbalimbali kufanya utafiti za kina kwenye maeneo ya leseni zao kama hatua za awali za utafutaji madini. Mathalani, hivi karibuni Kampuni ya Barrick imefanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa kutumia helikopta katika maeneo ya Msalala, Nzega, Igunga, Mbogwe na Nyang'hwale kwa ajili ya kubaini uwepo wa maeneo mapya yenye madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *GST* imeendelea na ujenzi wa mfumo wa usimamizi na usambazaji wa taarifa za jiosayansi na rasilimali za madini ambapo hadi kufikia Machi, 2026 ujenzi wa mfumo huo umekamilika kwa 45%. Aidha, kukamilika kwa mfumo huo kutaimarisha usimamizi na upatikanaji wa taarifa za miamba na madini yaliyopo nchini. *(Makofi)*

(g) Kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya leseni 8,878 za uchimbaji mdogo zimetolewa na Wizara kupitia Tume ya Madini. Aidha, *STAMICO* inaendelea kusaidia wachimbaji wadogo kwa kutoa huduma za kitaalamu katika utafiti, uchimbaji, uchenjuaji na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi husika, jumla ya wachimbaji 451 wamepatiwa mafunzo kupitia vituo vya mfano

vya Lwamgasa, Katente na Itumbi. Wizara kupitia *STAMICO* imetoa huduma ya uchorongaji katika maeneo mbalimbali, ambapo jumla ya meta 3,896 zilichorongwa kwa ajili ya utafutaji wa dhahabu. Kwa upande wa wazalishaji chumvi wadogo, ujenzi wa jengo la kiwanda cha kusafisha chumvi kilichopo Nangurukuru Wilaya ya Kilwa umekamilika, na hatua inayofuata sasa ni kukamilisha usimikaji wa mitambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Tume ya Madini imefanya ufuatiliaji wa kutambua maeneo ya kugawia wachimbaji wadogo ambapo hadi sasa jumla ya maeneo 99 yamependekezwa kwa ajili ya uchambuzi. Aidha, maeneo mawili yametengwa kwenye mikoa ya kimadini ya Mbogwe ambako ni Msasa, leseni 35 zimetolewa na Lindi - *Ntaka Hill*, leseni 69 zimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu na kuwezesha ushiriki wa wachimbaji wadogo katika warsha, makongamano, mikutano na majukwaa ya Kitaifa na Kimataifa kwa ajili ya kujifunza teknolojia mbalimbali na kutafuta fursa za kibiashara. Mathalani, chini ya uratibu wa *FEMATA*, jumla ya wachimbaji 31 walifanya ziara ya mafunzo nchini Uturuki kuanzia tarehe 3 hadi 4 Septemba, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Tume ya Madini imesaini Hati ya Makubaliano na Benki ya *CRDB* kwa ajili ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini. Aidha, kikundi cha Wachimbaji wadogo cha Songwe *Gold Family* – Saza mkoani Songwe kinatarajiwa kupata mkopo wa shilingi bilioni 50 kutoka Benki ya *CRDB* ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa makubaliano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuzishukuru benki za *CRDB*, *NMB*, *NBC*, AZANIA, *Stanbic* na *KCB* kwa kuendelea kuwakopesha wachimbaji wadogo. Hivyo, ninaomba kutoa wito kwa benki nyingine nchini kuendelea kuwaamini na kuwakopesha wachimbaji wadogo.

(h) Kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara na Taasisi zake zimejaza nafasi 147 kwa utaratibu wa uhamisho 55 na ajira mpya 92. Aidha, kupitia uhamisho huo, Wizara imepata watumishi 24: Tume ya Madini 17, *TEITI* nane na *GST* sita. Vilevile, kwa upande wa ajira mpya Wizara imepata watumishi tisa, *STAMICO* mmoja, Tume ya Madini 66, *GST* 12 na *TGC* wanne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, kwa upande wa mafunzo kwa watumishi, Wizara na Taasisi zake zimewawezesha watumishi 455 kupata mafunzo. Kati ya hao watumishi 347 walipata mafunzo ya muda mfupi na 108 ya muda mrefu katika masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa, taasisi zilizo chini yake zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuzipatia vitendea kazi. Tume ya Madini imewezeshwa vifaa vya masoko na TEHAMA, *STAMICO* imewezeshwa kupata leseni mbili za utafiti wa madini ya nikeli na adimu, *GST* imewezeshwa upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya utafiti wa madini ikiwemo magari manne, *TGC* imewezeshwa kuboresha miundombinu ya kutolea mafunzo, huduma za uzalishaji wa bidhaa kwa lengo la kukuza shughuli na uongezaji thamani madini nchini na *TEITI* imewezeshwa kwa kupewa jengo kwa ajili ya ofisi lililopo mji wa Serikali Mtumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imeendelea na taratibu za kuidhinishwa kwa *TGC* kuwa taasisi inayojitegemea. Hatua hii itaiwezesha *TGC* kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maeneo mengine ya Wizara katika mwaka wa fedha 2025/2026.

(a) *Mining Vision* 2030, Madini ni Maisha na Utajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha andiko la *Mining Vision* 2030 linalozingatia nguzo tano ambazo ni kuwa na taarifa za jiosayansi, kuimarisha mfumo wa kisheria na kitaasisi, kuimarisha ufungamanishaji wa sekta ya madini na sekta nyingine za kiuchumi, kukuza uchimbaji mdogo wa madini, na kuimarisha usimamizi wa mazingira. Kwa kuzingatia nguzo hizo, sekta ya madini itafikia malengo na matarajio ya dira 2050.

(b) Programu ya *Mining for a Brighter Tomorrow* – MBT.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa *MBT* ambao ni wa miaka mitano kuanzia mwaka 2025/2026 hadi 2029/2030. Mpango huo unalenga kuongeza ushiriki wa vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalumu katika mnyororo wa thamani kwenye sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, malengo mahsusi ya mpango wa *MBT* ni pamoja na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya sekta, kujenga uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za mnyororo wa thamani wa madini, na kuimarisha ujumuishi na manufaa yatokanayo na sekta ya madini kwa vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza malengo ya Mpango wa *MBT*, Wizara imetoa jumla ya leseni 273 za uchimbaji wa madini kwa vikundi 183 katika mikoa mbalimbali ikiwemo Mara, Kagera, Shinyanga, Morogoro, Dodoma na Njombe. Aidha, Wizara ilitoa elimu kuhusu usalama wa afya, utunzaji wa mazingira na usimamizi wa rasilimali fedha kwa wanufaika wa leseni zilizotolewa. Vilevile, Wizara imeendelea kuratibu shughuli za makundi hayo kupitia miradi mbalimbali ya uchimbaji na biashara ya madini ikiwemo mradi wa Nyamongo kwa kushirikiana na mgodi wa dhahabu wa *North* Mara katika Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, mpango huu unatekelezwa katika maeneo ya Mirerani Mkoa wa Manyara, Mbogwe na Nyang'hwale Mkoa wa Geita. Wizara pia

imeendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa *MBT*.

(c) Kuwajengea uwezo wataalamu kwenye maeneo muhimu kwenye sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi mahitaji ya wataalamu na uwepo wa teknolojia mahsusi katika mnyororo wa thamani wa madini nchini, Wizara imekamilisha taratibu za kuwapeleka wataalamu masomoni ndani na nje ya nchi katika fani mbalimbali zikiwemo ukadiriaji wa mashapo *(resource estimation)* modeli za kifedha *(financial modelling),* ukaguzi na usimamizi wa rasilimali madini, uthaminishaji wa madini, ukataji wa madini ya vito, utengenezaji wa bidhaa za usonara na uongezaji thamani madini. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepanga kuwajengea uwezo jumla ya watumishi nane katika maeneo ya ukadiriaji mashapo, modeli za kifedha na ukaguzi wa fedha.

(d) Kuboresha Usimamizi wa shughuli za madini kidigitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imeendelea na taratibu za kuanzisha mfumo wa usimamizi wa sekta ya madini kidijitali utakaojulikana kama *Mineral Sector Management Information System*. Mfumo huu unalenga kuimarisha usimamizi, uratibu na upatikanaji wa taarifa za sekta ya madini kwa kutumia teknolojia ya kidijitali, sambamba na jitihada za Serikali za kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za awali zimeanza kutekelezwa ikiwa ni pamoja na mfumo wa uchambuzi wa mahitaji ya mfumo, kubainisha wadau watakaohusika katika utekelezaji wa mfumo huo na maandalizi ya nyaraka muhimu zinazohitajika.

(e) Mpango mkakati wa madini muhimu na madini mkakati *(Critical and Strategic Minerals Strategy)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imekamilisha uandaaji wa mpango mkakati

wa madini muhimu na madini mkakati. Utekelezaji wake utaanza kutumika mara baada ya kuidhinishwa kwa orodha ya Madini Muhimu na Madini Mkakati. Mkakati huo ni moja ya nyenzo za kutekeleza Sera ya Madini iliyohuishwa pamoja na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa muda mrefu, ili kufikia malengo ya Dira 2050.

(f) Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura 123 na Kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi rejewa, Serikali imefanya marekebisho ya kanuni za wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii za mwaka 2025 kwa kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 563 la tarehe 12 Septemba, 2025 pamoja na Tangazo la Serikali Na. 692 la Desemba 19, 2025. Kanuni hizo ni Kanuni ya sita ili kuboresha muundo wa kamati ya wataalamu kwa lengo la kuongeza ufanisi. Kuongeza Kanuni ndogo ya saba, Kanuni ndogo ya tatu iliyolenga kupunguza gharama za utendaji wa kamati ya wataalamu na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya nane na tisa za kuweka ukomo wa muda wa kuwasilisha mipango, kanuni ya 15 imefutwa na kutungwa Kanuni mpya inayofafanua zaidi majukumu ya wamiliki wa leseni za madini ikiwemo kuwasilisha taarifa za fedha na miradi. Kanuni ndogo ya 16(6) inayohusu usimamizi, ufuatiliaji na ukaguzi wa utekelezaji wa mipango ya wajibu wa wenye leseni kwenye jamii na yenyewe imeongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi rejea, Wizara imetunga kanuni mpya; Kanuni za Leseni Ndogo ya Uchenjuaji wa Madini za Mwaka 2025 na kutangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 572 la tarehe 12 Septemba, 2025. Kanuni hizi zitaboresha shughuli za Sekta ya Madini kwa kuwatambua na kutoa leseni kwa wachenjuaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa shughuli za taasisi zilizo chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Wizara imeendelea kuzisimamia na kuziwezesha taasisi zake tano, ili ziendeleze kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kuzingatia sera,

sheria na miongozo inayosimamia Sekta ya Madini. Taasisi hizo ni Tume ya Madini, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania, Shirika la Madini la Taifa, Kituo cha Jemolojia Tanzania na Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, badhi ya majukumu yaliyotekelezwa na taasisi hizo ni utoaji na usimamizi wa leseni za madini, ukaguzi wa masuala ya afya na mazingira, kufanya utafiti wa jiosayansi na uboreshaji wa kanzidata ya Taifa ya taarifa za miamba na madini. Usimamizi wa vituo vya mfano vya wachimbaji wadogo wa madini, kusimamia utekelezaji wa miradi ya ubia, udahili na utoaji wa mafunzo kuhusu uongezaji wa thamani madini, uandaaji na uwekaji wazi wa ripoti ya ulinganifu wa mapato ya Serikali na mapato yaliyowasilishwa na kampuni za uzinduaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara imezingatia miongozo ifuatayo: -

(a) Mwongozo wa Kitaifa wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2026/2027;

(b) Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025;

(c) Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano;

(d) Mpango nne wa maendeleo ya Taifa wa miaka mitano;

(e) Maendeleo wa Muda Mrefu;

(f) Makubaliano ya Paris kuhusiana na mabadiliko ya Tabianchi;

(g) Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika;

(h) *Africa Mining Vision*;

(i) Sera ya Madini ya Mwaka 2009;

(j) Mpango Mkakati wa Wizara;

(k) Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030;

(l) Kifungu cha 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439; na

(m) Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine wa Kitaifa pamoja na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambayo yaliyotolewa kwa nyakati tofauti.

Mheshimwa Naibu Spika, Vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2026/2027, cha kwanza ni kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli. Katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa uchimbaji wa madini, ili uweze kunufaisha nchi na wawekezaji; kuimarisha na kusimamia masoko na vituo vya ununuzi wa madini nchini na kuendeleza mikakati ya kuimarisha usimamizi wa madini, ujenzi na viwanda, soko la Tanzanite na madini mengine ya vito hapa nchini, ili kuongeza mapato yatokanayo na madini hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ya kuimarisha utekelezaji wa Sheria ya Madini, ikiwemo kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini. Aidha, katika kuendelea kuimarisha udhibiti na kuzuia utoroshaji wa madini ya *Tanzanite*, Wizara kupitia Tume ya Madini, itakamilisha ununuzi wa kofia zenye kamera maalum, kwa ajili ya ukaguzi na itahakikisha wakaguzi na wathaminishaji wa madini hao wanatumia kofia hizo, ili kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mwenendo wa uzalishaji na biashara ya madini kwenye eneo tengefu la Mirerani.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ni kipaumbele ni kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa.

Katika kuongeza mchango wa wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo: -

(a) Kuhamasisha shughuli za utafiti wa madini na uanzishaji wa migodi mipya;

(b) Kuimarisha usimamizi wa migodi ya uchimbaji; kuboresha mfumo wa usimamizi wa madini ya ujenzi na ya viwandani;

(c) Kusimamia utekelezaji wa Sheria inayoitaka migodi mikubwa;

(d) Kuajiri, kununua huduma na bidhaa kutoka hapa nchini na kuhamasisha ushiriki wa Watanzania katika mnyororo wa uchumi wa madini na;

(e) kuendelea kuimarisha mazingira wezeshi ya kisera na kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itahakikisha kuwa wawekezaji waliopewa leseni za uchimbaji wa madini wanaanza uzalishaji mara baada ya kukamilisha taratibu za matakwa ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha tatu ni kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini muhimu na madini mkakati. Madini muhimu na madini mkakati ni madini ambayo yana mahitaji makubwa kwenye maendeleo ya uchumi na ulinzi wa Taifa. Madini hayo ni pamoja na *lithium*, *graphite*, *helium, nickel, cobalt, titanium*, *copper, aluminium, niobium* na *rare earth elements,* ambayo yanatumika kutengeneza vifaa vya teknolojia ya kisasa ikiwemo nishati safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza manufaa yatokanayo na madini muhimu na madini mkakati kwa uchumi wa Taifa, Wizara imepanga kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini hayo kwa kufanya yafuatayo: -

(a) Kuhamasisha uwekezaji katika utafutaji na uchimbaji wa madini muhimu na madini mkakati;

(b) Kufanya utafiti wa mahitaji ya madini mkakati ili kuyafikia masoko mbalimbali duniani;

(c) Kutoa leseni za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini muhimu na madini mkakati; na

(d) Kukamilisha na kutekeleza mkakati wa uendelezaji na uvunaji wa madini hayo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba, Watanzania wananufaika ipasavyo na uwepo wa rasilimali za madini muhimu na madini mkakati hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha nne ni kuhamasisha uwekezaji katika uongezaji thamani madini. Wizara itaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na madini. Kuendelea kutoa ushirikiano kwa wamiliki wa viwanda vya usafishaji wa madini ya dhahabu nchini, ili kupata ithibati ya *LBMA* na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Kituo cha Jemolojia, ili kiweze kutoa mafunzo na huduma kwenye mnyororo wa uongezaji thamani madini kwa ufanisi, ili kuhamasisha uwekezaji katika uongezaji thamani madini. Serikali imetenga eneo la Buzwagi lililopo Wilaya ya Kahama, kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani madini na viwanda vya uzalishaji bidhaa migodini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza kutangaza fursa za uwekezaji nchini, Wizara kwa kushirikiana na Chemba ya Migodi Tanzania *(Tanzania Chamber of Mines)* itafanya Mkutano wa Saba wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini. Mkutano huo unatarajiwa kufanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kuanzia tarehe 19 hadi 21 Novemba, 2026 Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkutano huu utakutanisha kwa pamoja makundi mbalimbali ya wataalamu wa masuala ya madini, wakurugenzi na watendaji wakuu wa kampuni za utafiti na uchimbaji wa madini, kampuni za utafiti na uchimbaji wa

madini, watoa huduma, wafanyabiashara na wawekezaji katika Sekta ya Madini kutoka ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito. Katika kutekeleza kipaumbele hiki Wizara itafanya yafuatayo: Kuimarisha uendeshaji wa viwanda vya kuongeza thamani madini nchini sambamba na uendelezaji wa minada na maonesho ya madini ya vito ya Arusha *(Arusha Gem Fair - AGF);* na minada ya madini ya vito ya Kimataifa ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara ya madini ya vito *(Gemstone Hub)*. Aidha, kuimarisha uendeshaji wa viwanda vya kuongeza thamani hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha sita ni kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za kina za madini. Katika utekelezaji wa shughuli hii, Wizara itafanya tafiti za kina za jiosayansi, ikiwemo jiofizikia *(High-resolution Airborne Geophysical Survey),* ili kuainisha uwepo wa madini mbalimbali yakiwemo madini muhimu na madini mkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kupitia *GST* itaendelea na ujenzi wa mfumo wa kusimamia taarifa za jiosayansi. Vilevile, Wizara itaendelea kushirikisha wadau wa ndani na nje ya nchi, ili kuongeza tafiti za madini katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuongeza wigo wa eneo la nje lililofanyiwa utafiti wa kina wa madini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba ni kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo. Wizara itaendelea na taratibu za kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuweka mazingira wezeshi yatakayowahamasisha kufanya uwekezaji, kuendelea kuhamasisha taasisi za fedha kutoa mikopo ya fedha na vifaa kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuandaa mpango wa kuwatambua na kuwaendeleza wachimbaji wadogo nchini kupitia mfuko wa dhamana kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, kuboresha utendaji wa vituo vya mfano, ili kuimarisha utoaji wa huduma na mafunzo kwa wachimbaji wadogo, kuimarisha huduma za uchorongaji kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuimarisha utekelezaji wa mipango ya kuwawezesha wachimbaji wadogo, ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija kwa kuwatengea maeneo na kuwawezesha kupata leseni kwenye maeneo yenye taarifa za msingi za kijiolojia, hasa kupitia Programu ya *MBT*, kuchukua hatua za ufutaji wa leseni za utafiti ambazo hazifanyiwi kazi na kuzirejesha Serikalini, ili kupangwa vyema na kugawiwa kwa wachimbaji wadogo. Kuhamasisha wachimbaji wadogo kushiriki mikutano, maonesho na makongamano mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kujifunza na kutangaza shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendesha makongamano kwenye mikoa ya kimadini, kwa ajili ya kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo na kwa wananchi kwa ujumla juu ya masuala ya sheria na kanuni mbalimbali za haki madini zikiwemo pia, sheria za *Local Content, CSR,* Haki Madini na Haki Ardhi. Pia, kuwahamasisha wachimbaji wadogo kushiriki kwenye minada na maonesho ya madini ya vito nchini, ili kupanua wigo wa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwawezesha wachimbaji wadogo waweze kunufaika na rasilimali madini, Serikali itaendelea kuitumia timu ya wataalamu wenye uzoefu na masuala ya fedha, madini na sheria, kwa ajili ya kutoa mapendekezo ya namna ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata mitaji na msaada wa kiufundi. Hatua hii itawawezesha wachimbaji hao kufanya uchimbaji wenye tija na kunufaika zaidi kiuchumi. Aidha, Wizara kupitia *STAMICO* itaendelea kuwalea na kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuwajengea vituo vya mfano katika maeneo yenye uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi iweze kuanzisha vituo vya kuuza na kukodisha vifaa na mashine mbalimbali za kufanyia shughuli za madini kwa lengo la kuwawezesha wachimbaji wadogo kutekeleza shughuli za madini kwa tija, ili kuongeza mchango wao kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha nane ni kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini. Ili kuzijengea uwezo taasisi, Wizara itafanya yafuatayo: -

(a) Kuiwezesha Tume ya Madini kupata rasilimali fedha na vifaa, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi; na

(b) Kuendelea kuimarisha *STAMICO,* ili ishiriki kikamilifu kwenye uwekezaji wa shughuli za madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuimarisha *GST,* ili iweze kufanya tafiti za jiosayansi kwa lengo la kubaini maeneo mapya yenye uwepo wa madini, kuimarisha *TGC,* ili iweze kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini ya vito na metali. Kuiwezesha *TEITI* kupata rasilimali mbalimbali, ikiwemo vifaa na vitendea kazi, ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ambayo yanatekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni kama ifuatavyo; *Mining Vision 2030,* Madini ni Maisha na Utajiri. Wizara ya Madini itaendelea na utekelezaji wa *Mining Vision 2030*, Madini ni Maisha na Utajiri, inayoweka matamanio ya kuwa na usimamizi thabiti na endelevu rasilimali madini, ili kukuza mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa. Vilevile kuboresha maisha ya Watanzania kupitia shughuli za madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara, kupitia *GST,* inatarajia kufanya tafiti za kina za jiosayansi ikiwemo utafiti wa kina wa jiofizikia *(High Resolution Airborne Geophysical Survey)*. Utafiti huo unatarajia kuongeza taarifa za kina za jiofizikia kutoka 16% ya sasa hadi kufikia 34%. Aidha, katika utekelezaji wa *Mining Vision 2030* Serikali itaendelea na jitihada za tafiti za kina ili angalau kufikia 50% ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizi zitaongeza uelewa wa jiolojia ya nchi yetu na hivyo kuvutia na kuboresha mazingira ya uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kuchochea ufungamanishaji na sekta nyingine za kiuchumi, hususan sekta za viwanda, kilimo, ujenzi, fedha na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nakushukuru wewe na Bunge lako Tukufu kwa kuiunga mkono Serikali katika kuhakikisha

utafiti wa kina wa madini unafanyika katika nchi yetu kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika,. Wizara ya Madini itaendelea kutekeleza Programu ya *Mining for a Brighter Tomorrow – MBT* kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2025/2026 hadi 2029/2030. Programu hii ni ya mageuzi katika Sekta ya Madini, ambayo imeanzishwa, kwa ajili ya kuboresha ushiriki wa wachimbaji wadogo ikiwemo wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum katika fursa zilizopo kwenye mnyororo wa thamani wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya *MBT* inatarajiwa kuongeza ushiriki wa vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum kwenye uchumi jumuishi kupitia Sera ya Madini na kuwawezesha kupata kipato na kuwaongezea fursa za ajira. Kuwajengea uwezo wataalam kwenye maeneo muhimu katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi mahitaji ya rasilimali watu katika shughuli za madini na uhitaji wa teknolojia mahsusi katika mnyororo wa thamani wa madini nchini, Wizara imetenga fedha za kuwajengea uwezo wataalam katika Sekta ya Madini kwa kuwasomesha ndani na nje ya nchi kupitia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu. Mafunzo hayo yatajikita katika fani za ukadiriaji wa mashapo *(resource estimation)*, modeli za kifedha *(financial modelling)* na ukaguzi wa fedha na rasilimali madini. Uthaminishaji wa madini na uongezaji thamani madini ikiwemo madini ya vito, madini muhimu na madini mkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea na hatua za ukamilishaji wa ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Sekta ya Madini Kidijitali utakaojulikana kama *Mineral Sector Management Information System*. Mfumo huu unalenga kuimarisha usimamizi, uratibu na upatikanaji wa Taarifa za Sekta ya Madini kwa kutumia teknolojia za kidijitali, sambamba na jitihada za Serikali za kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za umma. Mfumo huo utaunganishwa na mifumo mingine ya Serikali, ili kuongeza ufanisi katika usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za madini na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni Usimamizi wa Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi. Serikali itatekeleza mpango kazi wa mazingira wa Sekta ya Madini 2025/2030 ambao unazingatia Mpangokazi wa Taifa na Dira ya 2050. Lengo kuu la mpango huu ni kujumuisha kanuni za mazingira, jamii na utawala bora, katika upangaji, usimamizi, uangalizi na uthibiti wa sekta ya madini nchini, ili kuhakikisha kuwa maendeleo ya rasilimali madini yanachangia ukuaji wa uchumi endelevu bila kuathiri usalama wa mazingira na ustawi wa jamii. Aidha, Shughuli za usimamizi na utunzaji wa mazingira zitasimamiwa kwa kuzingatia Nguzo Namba tatu ya Dira 2050, Sheria ya Madini Sura 123 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zitakazotekelezwa na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027, ni kama ifuatavyo: -

(a) Tume ya Madini
   (i) Itafanya kazi ya Utoaji na Ufuatiliaji wa Leseni za Madini.

   (ii) Itafanya kazi ya kuimarisha usimamizi wa shughuli za madini na ukusanyaji wa mapato ya Serikalini.

(b) Kuimarisha ukaguzi wa afya, usalama mazingira na uzalishaji wa madini;

(c) Serikali itaendelea kuhakikisha wachimbaji wanafuata taratibu za uchimbaji salama ili kuepuka ajali zisizo za lazima ambazo zinaweza kuzuilika;

(d) Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini *(Local Content)* na wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii *(CSR);*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia ushirikishwaji wa Watanzania kwenye sekta ya madini, Tume ya Madini itaendelea kutekeleza na kuhakikisha kuwa kampuni zinazomiliki kampuni zinazomiliki leseni za madini, zinanunua bidhaa na huduma

zinazopatikana nchini. Aidha, Tume itaendelea kutangaza orodha ya huduma na bidhaa zinazotakiwa kutolewa na kampuni zinazomilikiwa na Watanzania kwa asilimia 100. Vilevile Tume itaendelea kusimamia wamiliki wa leseni za madini nchini kutimiza takwa la uwajibikaji kwa *CSR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni marufuku kwa mtu yeyote ambaye sio Mtanzania kusambaza bidhaa au huduma zilizotangazwa kufanywa na Watanzania kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuboresha mazingiraya utendaji kazi na kuwajengea uwezo watumishi. Taasisi ya Geolojia na Utafiti ya Madini Tanzania itafanya kazi zifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kufanya utafiti wa kisayansi na kuboresha kanzidata ya Taifa ya miamba na madini. *GST* itafanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege na ugani wa jiolojia na jiokemia katika *QDS* mbili *(QDS 239 na 240)* zilizopo Wilaya za Rufiji na Kilwa na kuchora ramani zake. Pia *GST* itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Mfumo wa Kanzidata ya Taifa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, *GST* itakusanya itahakiki na kutathmini uhalisia wa taarifa na takwimu za jiosayansi kutoka kwa wamiliki 40 wa leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini nchini na kuhuisha kanzidata rasilimali madini ya Taifa pamoja na kitabu cha madini. Pia itafanya kazi ya kuwajengea uwezo wa wachimbaji wadogo kwa kufanya utafiti wa jiosayansi katika eneo litakalotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo kwa kutumia vifaa vya kisasa ikiwemo ndege nyuki ili kupata taarifa za kina za jiofizikia lengo la kubaini sehemu zenye viashiria vya uwepo wa madini katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuboresha huduma za maabara. Katika kuboresha huduma za maabara *GST* itaendelea kufanya uchunguzi wa sampuli mbalimbali kwa kuzingatia vigezo vya ithibati. Aidha, *GST* itaendelea na ujenzi wa maabara mpya ya kisasa ya uchunguzi wa madini, *State of the Art Geoscientific Laboratory* katika eneo la Kizota - Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile *GST* itaendelea na ujenzi wa maabara za Kanda katika Mikoa ya Kimadini ya Chunya na Geita. *GST* pia itaendelea kufanya kazi ya ufuatiliaji na kuelimisha umma kuhusu majanga ya asili na jiolojia na kujengea uwezo watumishi wa *GST* kutokeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *STAMICO* itafanya kazi ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato kuwezesha shughuli za uchimbaji mdogo na kuimarisha vituo vya mfano, itaendeleza leseni za madini za shirika. Shirika limepanga kuendeleza na kufanya utafiti kwenye leseni moja ya dhahabu iliyoko Wilaya ya Bukombe Mkoa wa Geita, ambapo utafiti wake pamoja na taarifa ya upembuzi yakinifu utakamilika ifikapo Juni, 2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile shirika litaendelea na utafiti wa madini ya Kinywe katika leseni mbili zilizopo katika Wilaya ya Ruangwa na Nachingwea katika Mkoa wa Lindi pamoja na leseni tatu za madini ya shaba zilizopo Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Jemolojia Tanzania *(TGC)* kitendelea na kazi ya utoaji wa mafunzo ya uongezaji thamani madini, uzalishaji wa bidhaa za madini zinazoongezwa thamani, huduma za upimaji sampuli za madini ya vito na utafiti wa madini ya vito na metali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *TEITI* itaendelea na kazi ya kuandaa na kuweka wazi taarifa 17 ya *TEITI* ya mwaka wa fedha 2024/ 2025. *TEITI* itaandaa na kuweka wazi taarifa ya 17 ya mwaka wa fedha 2024/2025 ya ulinganishi wa malipo ya kodi na tozo kutoka kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato yaliyopelekwa Serikalini. Uandaaji wa taarifa hiyo ni utekelezaji wa vigezo vya uwazi na uwajibikaji vya mwaka 2023 ambapo nchi wanachama hutakiwa kuandaa na kuweka wazi taarifa husika kila mwaka. Pia itaweka wazi mikataba ya makampuni ya madini, mafuta na gesi asilia. Pia kuweka wazi orodha ya wamiliki wa hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hitimisha.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitazishukuru taasisi za fedha hususan mabenki kwa kuendelea kuwapa mikopo wadau wa sekta ya madini wakiwemo wachimbaji wakubwa, wa kati na wadogo. Vilevile, ninavishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kutuhakikishia usalama na kushirikiana nasi katika kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya shilingi 1,406,006,031,000, ninaomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha makadirio ya shilingi 174,983,580,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi 71,507,708,000 sawa na 40.87% ya bajeti yote ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, na shilingi 103,475,872,000 sawa na asilimia 59.13% ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 27,365,095,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 76,110,777,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini vimeambatishwa pamoja na hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Madini kwa kikoa cha *https://www.madini.go.tz. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**27 APRILI, 2026**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA ANTHONY PETER MAVUNDE (MB.), WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## A. UTANGULIZI

*1.* ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua bajeti ya Wizara ya Madini, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

*2.* ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kuijalia nchi yetu amani na baraka na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki Mkutano huu wa Tatu (3). Tunamuomba aendelee kutujalia rehema, hekima, busara na umoja katika kujadili hotuba za Wizara mbalimbali ikiwemo Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa nia ya kuendeleza Taifa letu na kuboresha ustawi na maendeleo ya Watanzania.

*3.* ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wenye maono mapana, mahiri, weledi na dhamira thabiti ya kuwaletea watanzania maendeleo jumuishi. Kwa wakati wote Mheshimiwa Rais ameendelea kuhimiza amani, uwajibikaji, utawala bora, umoja na mshikamano wa Kitaifa.

*4.* ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza na kumshukuru **Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuimarisha na kulinda muungano, kusimamia masuala ya mazingira na usimamizi bora wa rasilimali zetu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** nimpongeze pia **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuiongoza Zanzibar vizuri. Hakika kiongozi huyu amekuwa nguzo imara katika kudumisha muungano. Vilevile, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba** kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuendelea kuisimamia vyema Serikali.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Sekta ya Madini."Ni ahadi yangu kwake na kwa Bunge lako Tukufu pamoja na watanzania kwamba nitaendelea kuitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na kwa uwezo wangu wote ili kuendeleza sekta hii muhimu"

***7.*** ***Mheshimiwa Spika***, napongeza hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu inayotoa mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za Serikali ambayo imeonesha mafanikio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026, utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 pamoja na mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na uzoefu na umahiri wako katika shughuli za Bunge tunaamini utalifanya Bunge kuendelea kuwa chombo imara, madhubuti na chenye kuaminika.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kumpongeza **Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.)** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu. Aidha, niwapongeze Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kushirikiana nawe katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa weledi mkubwa. Ni matarajio yetu kuwa chini ya uongozi wako, Bunge litaendelea kufanya maamuzi sahihi na yenye manufaa kwa

maendeleo ya Taifa letu na kufanya liendelee kuheshimika ndani na nje ya nchi yetu.

***10. Mheshimiwa Spika,*** naomba niwapongeze sana **Mheshimiwa CPA. Subira Khamis Mgalu (Mb.)**, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na **Mheshimiwa CPA. Simon Songe Lusengekile (Mb.)**, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kuteuliwa kuiongoza Kamati hii. Aidha, nawapongeza wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kuteuliwa kutekeleza majukumu ya Kamati. Wizara inaishukuru Kamati kwa ushauri wake makini ambao imekuwa ikiutoa katika kuhakikisha kuwa sekta hii inakuwa na tija kwa Taifa na kuwanufaisha watanzania. Vilevile, ninaishukuru Kamati kwa kujadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na kuyapitisha kwa kauli moja.



**Picha Na. 1:** *Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini katika kutekeleza sehemu ya majukumu yake ikikagua mtambo wa uchenjuaji wa Madini ya Dhahabu katika Kituo cha Mfano cha Lwamgasa – Geita.*

***11. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la 13 kwa kuwa sehemu ya Bunge la

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niombe ushirikiano wao katika kuendeleza sekta hii muhimu katika kujenga uchumi imara na maendeleo endelevu ya Taifa letu.

***12. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Pia, niwapongeze viongozi wote waandamizi wa Serikali walioaminiwa na kuteuliwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nyadhifa mbalimbali, nawatakia utendaji mwema katika kutekeleza majukumu yao.

***13. Mheshimiwa Spika***, kwa heshima kubwa, nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Mtumba kwa kuniamini na kunichagua. Naamini mtaendelea kushirikiana nami katika kutekeleza majukumu yangu kama mwakilishi wenu katika Bunge hili Tukufu.
"Nawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote na kwa kipaji nilichojaliwa na Mwenyezi Mungu katika kuleta maendeleo ya jimbo na Taifa kwa ujumla"

***14. Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mb.)**, kwa kuteuliwa tena na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Naibu Waziri wa Madini. Aidha, namshukuru kwa dhati kabisa kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Hakika amekuwa ni msaada mkubwa kwangu katika kuhakikisha sekta hii inatimiza malengo yake.

***15. Mheshimiwa Spika,*** napenda kumshukuru **Eng. Yahya Ismail Samamba**, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini kwa kuratibu na kusimamia utendaji wa Wizara. Pia, nampongeza **Bw. Msafiri Lameck Mbibo**, Naibu Katibu Mkuu kwa kuendelea kumpatia ushirikiano Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini. Vilevile, nimshukuru **Dkt. AbdulRahman Shabani Mwanga**, Kamishna wa Madini kwa kutekeleza majukumu yake vizuri. Halikadhalika, nichukue fursa hii kuishukuru Menejimenti ya Wizara pamoja na wafanyakazi wote kwa ushirikiano na utendaji kazi mzuri katika kutekeleza majukumu yao.

***16. Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru Wenyeviti wa Bodi kwa ushauri na utendaji kazi kwa ufanisi katika kusimamia Sekta ya Madini. Viongozi hao ni: Dkt. Janeth Lekashingo, Mwenyekiti wa Tume ya Madini; Bi. Yokbeth Myumbilwa, Mwenyekiti wa Bodi ya GST; IGP Mstaafu Mheshimiwa Balozi Simon Sirro, Mwenyekiti wa Bodi ya STAMICO; Mheshimiwa Balozi Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya TEITI; Makamishna wa Tume ya Madini; na Wajumbe wa Bodi hizo.

***17. Mheshimiwa Spika,*** nawapongeza Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini: Eng. Ramadhani Lwamo (Katibu Mtendaji, Tume ya Madini); Eng. Ally Samaje (Mtendaji Mkuu, GST); Dkt. Venance Mwasse (Mkurugenzi Mkuu, STAMICO); Bi. Mariam Mgaya (Katibu Mtendaji, TEITI); na Eng. Ally Maganga (Mratibu wa Kituo cha Jemolojia Tanzania) kwa kuzisimamia kwa makini na weledi taasisi wanazoziongoza. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Maafisa Madini Wakazi (RMO's) na Maafisa Migodi Wakazi (MRO's) kwa utekelezaji fanisi wa majukumu yao.

***18. Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa naishukuru kwa moyo wa dhati familia yangu, mke wangu mpendwa Jacquelyne Moses Lupasa na watoto wangu Atarah na Allan kwa kunipa ushirikiano mkubwa na utulivu katika kusimamia majukumu yangu ya ubunge na uwaziri na kukubali kubeba baadhi ya majukumu ya familia.

***19. Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa niungane na watanzania wenzangu kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama. Aidha, nitoe pole kwa Wananchi wa Dar es Salaam kwa kuondokewa na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Vilevile, nitoe pole kwa Wananchi wa jimbo la Isimani kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi. Mwenyezi Mungu awarehemu marehemu na awape faraja familia na wananchi waliokuwa wakiongozwa nao.

***20. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watanzania wote

kutokana na vifo, majeraha, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu kufuatia majanga mbalimbali yaliyosababishwa na mvua nyingi, ajali za barabarani, majini, moto na migodini.

***21. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuendelea kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini ambapo nchi yetu imeendelea kung'ara kimataifa na kuongeza imani kwa wawekezaji wa madini duniani. Kulingana na utafiti uliofanywa na Taasisi ya *Fraser* ya nchini Canada ambayo inaaminika kimataifa katika kutathmini mwenendo wa masoko ya uwekezaji wa madini, Tanzania ilishika nafasi ya 4 Afrika na ya 34 duniani katika kiashiria cha kuvutia uwekezaji (Investment Attractiveness Index - IAI) uliofanyika mwaka 2025. Aidha, kwa mujibu wa taarifa hiyo, Tanzania ilipata alama 68.04 mwaka 2025 ikilinganishwa na alama 62.75 katika mwaka 2024. Vilevile, kwa upande wa hazina za rasilimali madini (mineral potential), Tanzania imeorodheshwa kuwa ya 15 duniani kwa kuwa na alama 75.

***22. Mheshimiwa Spika,*** kulingana na Ripoti ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 2025 (Tanzania Investment Report 2025), Sekta ya Madini imeendelea kuongoza katika thamani ya mtaji wa Uwekezaji Kutoka Nje (Foreign Direct Investment – FDI stock) katika mwaka 2024, ikiwa ni takriban robo tatu ya jumla ya mtaji wa uwekezaji katika sekta muhimu. Aidha, ripoti hiyo inaonesha kuwa kiwango cha mtaji kutoka nje katika Sekta ya Madini kiliongezeka hadi kufikia dola bilioni 9.79 mwaka 2024, kutoka dola bilioni 9.15 mwaka 2023 na dola bilioni 8.64 mwaka 2022. Ongezeko hilo limechangiwa na uhamasishaji na uwepo wa mazingira wezeshi kwa wawekezaji yaliyochochea upanuzi wa miradi iliyopo, uwekezaji wa faida inayopatikana na uunganishaji mitaji ndani ya sekta.

***23. Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kupiga hatua muhimu ya kihistoria katika kuendeleza Madini Muhimu na Madini Mkakati ambapo Serikali imeingia makubaliano ya kutekeleza miradi ya madini mbalimbali ikiwemo *niobium*, nikeli, kinywe na dhahabu katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Mathalani, tarehe 24 Machi 2026, kwa mara ya kwanza Tanzania iliweza kushuhudia kusainiwa kwa mkataba wa kuendeleza Madini

Muhimu na Madini Mkakati kwa kusaini mkataba wa kuendeleza mradi wa uchimbaji wa madini ya *niobium* wa Panda Hill uliopo Mkoa wa Mbeya.

***24.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu utakuwa ni mradi mkubwa na wa kipekee katika bara la Afrika ambao utaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wanne (4) duniani. Mkataba huo ni kati ya Serikali na Kampuni ya Panda Hill Tanzania Limited. Uwekezaji wa awali katika mradi huo unakadiriwa kuwa dola za Marekani milioni 442 na unatarajiwa kuzalisha ajira zipatazo 1,600 na ajira 6,336 zisizo rasmi. Aidha, Serikali inatarajia kupata mapato ya takribani shilingi trilioni 2 kutokana na mrabaha, kodi na tozo, gawio la hisa za Serikali asilimia 16 zisizohafifishwa na kukuza matumizi ya bidhaa na huduma za ndani (local content) pamoja na uwajibikaji kwa jamii (CSR), ambapo thamani ya manunuzi ya ndani inatarajiwa kufikia dola za Marekani bilioni 1.77.

***25.*** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi wa *niobium* utaiwezesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache duniani zinazochakata mbale na kuzalisha madini ya *niobium*. Aidha, madini hayo yana umuhimu mkubwa viwandani hususan katika kuongeza uimara wa chuma, matumizi ya teknolojia za kisasa ikiwemo vifaa vya elektroniki, magari ya umeme na injini za ndege.




**Picha Na. 2:** *Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini akisaini kwa niaba ya Serikali mkataba wa uchimbaji mkubwa wa madini ya Niobium utakaomilikiwa kwa ubia baina ya Serikali na Kampuni ya Panda Hill Tanzania Limited.*

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Awamu ya Sita chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeshuhudia mageuzi makubwa na mafanikio ya hali ya juu katika Sekta ya Madini. Mchango wa sekta hii kwenye Pato la Taifa umeendelea kuimarika na kukua mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2023 mchango ulikuwa asilimia 9.1 na mwaka 2024 ulikuwa asilimia 10.1. Aidha, hadi kufikia kipindi cha robo tatu ya mwaka 2025 (Januari –Septemba) wastani wa mchango wa sekta umefikia asilimia 11.9.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada za kuimarisha usimamizi wa rasilimali zetu zimewezesha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kuongezeka kutoka shilingi 753,175,680,203.96 Mwaka wa Fedha 2023/2024 hadi kufikia shilingi 2PM4VP437P5VXP32X1MM Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, hadi kufikia Machi 2026 shilingi 1,034,453,897,920.09 sawa na asilimia 114.94 ya lengo la makusanyo ya shilingi 900,000,000,000.00 kwa kipindi cha miezi tisa (9) zimekusanywa na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Mafanikio haya ni matokeo ya mikakati madhubuti ya Serikali ikiwemo kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta ya Madini, kudhibiti utoroshwaji wa madini, kuhamasisha uwekezaji kwenye shughuli za madini na kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa masoko na vituo vya ununuzi wa madini kutoka masoko 43 na vituo 114 mwaka 2024/2025 hadi kufikia masoko 44 na vituo 118 mwaka 2025/2026. Kupitia masoko na vituo hivyo ilifanyika biashara ya madini yenye thamani ya shilingi 2,819,220,651,824.38 kwa mwaka 2024/2025 na shilingi 4,903,477,353,887.03 hadi kufikia Machi 2026.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa salamu za shukrani, pongezi, pole na baadhi ya mafanikio ya Sekta ya Madini, naomba sasa nijielekeze katika maeneo mahsusi ya hotuba hii ambayo ni: Mwenendo wa Biashara ya Madini Duniani; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## B. MWENENDO WA BIASHARA YA MADINI DUNIANI

***30. Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa biashara ya madini duniani umeendelea kubadilika kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na mahitaji ya soko. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, bei ya madini ya dhahabu kwa wakia ilipanda hadi kufikia wastani wa dola za Marekani 4,190.47 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 2,655.80 katika kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kuongezeka kwa bei ya dhahabu kumetokana na sababu mbalimbali ikiwemo mahitaji makubwa ya madini hayo duniani kama njia ya kuhifadhi thamani ya fedha.

***31. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, bei ya madini ya almasi imeshuka na kufikia wastani wa dola za Marekani 159.84 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 168.95 kwa karati kwa kipindi kama hicho 2024/2025 sawa na upungufu wa asilimia 5.39. Mwenendo wa bei ya almasi duniani umeendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo: uwepo wa almasi ya viwandani (synthetic diamond) zilizosababisha kupungua kwa uhitaji wa almasi asilia hususani katika masoko makubwa duniani yakiwemo ya China na Marekani.

***32. Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa bei ya makaa ya mawe duniani umeendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo kupungua kwa mahitaji ya makaa ya mawe katika soko la dunia. Hali hiyo imesababisha kushuka kwa bei ya makaa ya mawe kufikia wastani wa dola za Marekani 26.69 kwa tani ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 40.75 kwa tani kwa kipindi kama hicho 2024/2025 sawa na upungufu wa asilimia 34.50.

***33. Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa biashara ya madini ya Tanzanite duniani umeendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo ukosefu wa masoko ya uhakika kutokana na vikwazo vya kibiashara duniani na uwepo wa vito vya kutengeneza viwandani. Hali hiyo imesababisha kushuka kwa bei ya madini ya Tanzanite kutoka wastani wa dola za Marekani 2,433.96 kwa kilogramu katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi

2025 na kufikia dola za Marekani 2,270.44 kwa kilogramu katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 sawa na upungufu wa asilimia 6.72.

***34.*** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa madini mkakati na madini muhimu yakiwemo *lithium, cobalt, nickel, copper, aluminium, zinc, graphite,* na *rare earth elements* (REE), uhitaji umeendelea kuongezeka duniani ikilinganishwa na upatikanaji wake. Hali hii inasababishwa na ongezeko la matumizi katika teknolojia mbalimbali za kisasa na nishati safi ikiwemo uzalishaji wa magari ya umeme, betri za kuhifadhi nishati, vifaa vya kuzalisha umeme wa jua na wa upepo, pamoja na vifaa vya kiteknolojia kama vile simu janja, darubini na kompyuta.

***35.*** ***Mheshimiwa Spika,*** hali hii inatoa fursa kubwa kwa Tanzania kuhakikisha madini haya yanaongezwa thamani ndani ya nchi ili kuongeza mapato, ajira, na mchango wake katika uchumi wa Taifa. Serikali imeendelea kuchukua hatua za kimkakati ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje katika Sekta ya Madini.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### (i) Makadirio ya Mapato na Matumizi

***36.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bunge lako Tukufu liliidhinisha bajeti ya jumla ya shilingi 224,984,150,000.00 kwa Wizara ya Madini. Kati ya fedha hizo, shilingi 100,379,362,000.00 ni bajeti ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi 76,110,777,000.00 ni za matumizi mengineyo na shilingi 24,268,585,000.00 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Aidha, shilingi 124,604,788,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi 71,507,708,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 53,097,080,000.00 ni fedha za nje.

***37.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,405,537,268,735.00. Kati ya

fedha hizo, shilingi 1,200,000,000,000.00 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 205,537,268,735.00 zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**(ii) Fedha Zilizopokelewa na Kutumika**

***38.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imepokea jumla ya shilingi 82,902,605,920.35. Kati ya fedha hizo shilingi 10,476,255,954.31 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambazo ni fedha za ndani na shilingi 72,426,349,966.04 kwa ajili ya matumizi ya kawaida zikijumuisha shilingi 54,763,814,101.03 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 17,662,535,865.01 kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

***39.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara ilipokea na kutumia fedha za maendeleo shilingi 10,476,255,954.31 ikiwa ni fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali ambazo ni: ujenzi wa jengo la ofisi ya Afisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Geita; ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Tume ya Madini; ujenzi wa maabara ya kisasa ya uchunguzi wa miamba na madini ya GST katika eneo la Kizota, Dodoma; ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya Wizara na Tume ya Madini; ununuzi wa vifaa vya kupimia madini kwenye masoko ya madini; ununuzi wa vifaa mbalimbali vya jiosayansi kwa ajili ya GST; kufanya ulinganishi wa mapato ya Serikali na malipo ya kampuni za uziduaji ili kuandaa Ripoti ya TEITI ya Mwaka 2023/2024; na kumlipa Mshauri Elekezi aliyefanya Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira (SEA) kwenye Ikolojia ya Mikumi - Selous.

**(iii) Utekelezaji wa Vipaumbelekwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

***40.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha Sekta ya Madini inaendelea kukua na kuwanufaisha watanzania ikiwa ni pamoja na kuendelea kuimarika kwa mchango wake kwenye Pato la Taifa, Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilijielekeza katika kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli; kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini

muhimu na madini mkakati; kuhamasisha uwekezaji na uongezaji thamani madini; kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za kina za madini; kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo; na kuzijengea uwezo Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini.

**(a) Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli**

***41.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilipangiwa kukusanya maduhuli ya shilingi 1,405,537,268,735.00 kutoka vyanzo mbalimbali. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,200,000,000,000.00 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina. Hadi kufikia Machi 2026 shilingi 1,034,453,897,920.09 sawa na asilimia 114.94 ya lengo la makusanyo ya shilingi 900,000,000,000.00 kwa kipindi cha miezi tisa (9) zimekusanywa na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 32 ikilinganishwa na shilingi 783,875,962,446.79 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, ili kuongeza maduhuli ya Serikali, Wizara imeimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, masoko ya madini, vituo vya ununuzi wa madini na mipaka ya nchi.

***42.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi zilizo chini ya Wizara zilipangiwa kukusanya na kutumia shilingi 205,537,268,735.00. Hadi kufikia Machi 2026 shilingi 61,850,652,766.87 zilikusanywa sawa na asilimia 40.12 ya lengo la makusanyo kwa kipindi rejewa. Lengo hilo halikufikiwa na STAMICO kutokana na kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa mikataba ya huduma ya uchorongaji; kushuka kwa bei ya makaa ya mawe kwenye soko la dunia; na Shirika kuchelewa kupokea mitambo ya kuzalisha nishati safi ya *Rafiki Briquettes* kutoka nje ya nchi. Aidha, kwa upande wa GST sababu zilikuwa ni kuharibika kwa vifaa vya maabara ikiwemo tanuru la kuchomea vyungu vya kuyeyushia sampuli za dhahabu (crucibles).

***43.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa kumekuwa na ongezeko la masoko na vituo vya ununuzi wa madini kutoka masoko 43 na vituo 114 Mwaka wa Fedha 2024/2025 hadi kufikia masoko 44 na vituo 118 Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kupitia

masoko na vituo hivyo, ilifanyika biashara ya madini yenye thamani ya shilingi 4,903,477,353,887.03 hadi kufikia Machi 2026 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ikilinganishwa na shilingi 2,819,220,651,824.38 kwa kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

***44. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini nchini unaofanywa na baadhi ya wachimbaji na wafanyabiashara wa madini wasio waaminifu. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali imefanikiwa kukamata madini ya aina mbalimbali yenye thamani ya shilingi 3,314,024,775.00 katika matukio 55 kwenye Mikoa ya kimadini ya Kahama, Mwanza, Geita, Dar es Salaam, Arusha, Songwe, Mbeya, Iringa, Mirerani, Mahenge, Chunya, Kagera, Manyara, Mbogwe na Morogoro. Aidha, madini yaliyokamatwa yalitaifishwa na Serikali na watuhumiwa walifikishwa kwenye vyombo vya Sheria. "Ni rai yangu kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa madini kuzingatia Sheria za Nchi kuhusiana na biashara ya madini"

***45. Mheshimiwa Spika,*** mapato ya fedha za kigeni yatokanayo na mauzo ya madini nje ya nchi yamekuwa yakiimarika mwaka hadi mwaka. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 5,401.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 4,119.9 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 31.1. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu na madini mengine. Aidha, mwaka 2025 thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi yalichangia asilimia 52.57 ya mauzo yote ya bidhaa za asili na zisizo za asili yaliyouzwa nje ikilinganishwa na asilimia 45.17 mwaka 2024. Vilevile, kwa upande wa mauzo ya bidhaa zisizo za asili pekee, Sekta ya Madini ilichangia asilimia 63.73 mwaka 2025 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 56.99 mwaka 2024. Pia, thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 3,419.6 mwaka 2024 na kufikia dola za Marekani milioni 4,753.9 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 39.0.

***46. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya vibali 8,635 vya usafirishaji madini nje ya nchi vilitolewa. Madini yaliyosafirishwa ni pamoja na dhahabu,

almasi, vito ghafi, vito vilivyokatwa na kusanifiwa, madini ya viwandani, madini ya bati, madini ya shaba na makaa ya mawe yenye jumla ya thamani ya shilingi 9,918,801,252,974.08. Aidha, katika kipindi rejewa, jumla ya vibali 195 vya kuingiza madini nchini vyenye thamani ya dola za Marekani 23,299,887.92 vilitolewa. Madini yaliyopata vibali vya kuingizwa nchini kwa kiwango kikubwa ni pamoja na *copper cathodes*, *loaded carbons* na *ferro-silicon manganese*.

**(b) Kuongeza Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa**

***47.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka. Mchango huo uliongezeka kutoka asilimia 9.1 mwaka 2023 na kufikia asilimia 10.1 mwaka 2024. Aidha, hadi kufikia kipindi cha robo tatu ya mwaka 2025 (Januari –Septemba) wastani wa mchango wa sekta umefikia asilimia 11.9. Mwenendo huu umechangiwa ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa usimamizi wa Sekta ya Madini, na kuongezeka kwa uwekezaji na uzalishaji.

**(c) Kuendeleza Mnyororo wa Thamani katika Madini Muhimu na Madini Mkakati**

***48.*** ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada mbalimbali zimeendelea kufanyika kuhakikisha Madini Muhimu na Madini Mkakati yananufaisha Taifa. Jitihada hizo ni pamoja na kufanya tafiti; kutangaza fursa za uwekezaji; na kutoa leseni za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na biashara ya madini muhimu na madini mkakati zilizopo nchini. Aidha, Wizara inaendelea na taratibu za kuidhinishwa orodha ya Madini Muhimu na Madini Mkakati Tanzania ili iweze kutumika katika usimamizi wa rasilimali za madini hayo.

***49.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni 454 za Madini Muhimu na Madini Mkakati yakiwemo madini ya kinywe (271), *nickel* (136), *cobalt* (2), *lithium* (6), *heavy mineral sands* (11) na *rare earth elements* (28). Utoaji wa leseni hizi unaendelea kuweka msingi thabiti wa kukuza uwekezaji katika utafutaji na uendelezaji

wa madini muhimu na madini mkakati nchini, sambamba na kuimarisha jitihada za Serikali za kukuza uchimbaji endelevu, kukuza uongezaji thamani wa madini, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali pamoja na mchango wa Sekta ya Madini katika maendeleo ya uchumi wa Taifa.

**(d) Kuhamasisha Uwekezaji na Uongezaji Thamani Madini**

***50. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha uwekezaji nchini, Wizara ilitangaza fursa za uwekezaji na kutoa elimu kwa Umma kupitia ziara mbalimbali za viongozi, vyombo vya habari na kwenye mikutano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Wizara ilishiriki kwenye mikutano, makongamano na maonesho ya kimataifa nane (8) ambayo ni: Mkutano wa *Future Minerals Forum* – Saudi Arabia; *Mining Indaba* – Afrika Kusini; Mkutano wa 13 wa Kimataifa wa Madini na Nishati - Zambia (Zambia International Mining and Energy Conference – ZIMEC); *Prospectors and Developers Association of Canada* (PDAC) – Canada; kushiriki mikutano ya Umoja wa Nchi za Afrika zinazozalisha Almasi (ADPA); *Africa Down Under* –Australia; *The International Conference on the Great Lakes Region* (ICGLR) – DRC na Uganda; na kwenye Maonesho ya 69 ya Vito na Usonara yaliyofanyika jijini Bangkok nchini Thailand.




**Picha Na. 3:** *Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini (katikati) katika picha ya pamoja na wawakilishi wa kampuni ya kimataifa ya uchimbaji madini ya dhahabu ya barrick baada ya Mkutano wa Kimataifa wa "African Mining Indaba". Upande wa kulia ni Bw. Msafiri Mbibo. Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Madini, wa pili kulia ni Mheshimiwa CPA. Simon Songe (Mb.),*

*Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na upande wa kushoto ni Dkt. Venance Mwasse, Mkurugenzi Mtendaji STAMICO.*

***51. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliandaa na kushiriki mikutano na maonesho ya ndani matano (5) ambayo ni: Maonesho ya 32 ya NaneNane Mkoani Dodoma; Maonesho ya nane (8) ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini yaliyofanyika mjini Geita; Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Sabasaba yaliyofanyika Dar es Salaam; Maonesho ya "*SAMIA CONNECT*" Jijini Arusha; na maonesho ya Kimataifa ya Biashara Zanzibar. Washiriki waliotembelea mabanda ya Wizara na taasisi zake walipata elimu kuhusu majukumu, sera, sheria na miongozo mbalimbali inayosimamia Sekta ya Madini pamoja na kufahamu fursa za uwekezaji zilizopo.

***52. Mheshimiwa Spika,*** kupitia mikutano hiyo kampuni mbalimbali zilionesha nia ya kuwekeza nchini na washiriki walipata nafasi ya kujifunza na kuongeza ujuzi kuhusu matumizi ya teknolojia za kisasa katika shughuli za madini, kujenga na kukuza diplomasia ya uchumi ambayo ni msingi wa ustawi wa biashara na uwekezaji baina ya nchi yetu na nchi nyingine.

***53. Mheshimiwa Spika,*** watanzania na wadau wameendelea kuelimishwa na kufahamishwa kuhusu uwepo wa fursa za uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini ikiwemo sheria, kanuni na miongozo inayosimamia sekta. Aidha, elimu imeendelea kutolewa kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwa ni pamoja na Jarida la Mtandaoni la Madini na Uchumi, programu maalumu za urushwaji wa vipindi mubashara vilivyoelezea masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Madini. Vyombo hivyo ni pamoja na *TBC, Clouds Media, Crown Media, ITV, Kiss FM, Azam Media, Wasafi Media, VOA, BBC, DW, TRT, Radio France, ZBC* na *Morning Star.*

***54. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha juhudi za kuelimisha umma na wadau kuhusu maendeleo ya Sekta ya Madini pamoja na fursa zilizopo katika uwekezaji na ushiriki wa wananchi. Ili kufikia azma hiyo, Wizara imeanzisha na kuendesha majukwaa maalum ya mawasiliano ya kidijitali yanayolenga kutoa elimu na taarifa sahihi kwa jamii. Miongoni mwa majukwaa

hayo ni mfululizo wa makala za video (Documentary) zinazojulikana kama "*Madini Diary*", zinazoangazia kwa kina shughuli mbalimbali za Sekta ya Madini, ubunifu wa teknolojia, mafanikio ya wadau na mchango wa sekta katika maendeleo ya Taifa.

***55.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeanzisha *podcast* ya "Madini Safari" ambayo hutumika kama jukwaa la majadiliano na wataalam, wachimbaji, wawekezaji na wadau wengine ili kutoa uelewa wa kina kuhusu maendeleo ya Sekta ya Madini nchini. Kupitia majukwaa hayo, Wizara imeendelea kuongeza uelewa kwa umma, kuhamasisha uwekezaji na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika kunufaika na rasilimali madini kwa maendeleo ya Taifa.

***56.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini zinaimarika na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa, Wizara ilifanya yafuatayo: kuendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini ya vito ambapo madini ghafi yenye uzito wa zaidi ya gramu mbili (2) yanatakiwa yaongezewe thamani ndani ya nchi kabla ya kusafirishwa nje ya nchi; kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha matumizi ya madini ya viwandani yanayotumika katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ambapo kwa sasa uzalishaji wa madini ya chokaa, jasi, udongo mwekundu unaotumika kutengeneza *clinker* kwa ajili ya kuzalisha saruji umeongezeka; kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa za madini; na kuendelea kutoa ushirikiano kwa wamiliki wa viwanda vya usafishaji wa madini ya dhahabu nchini ili kupata ithibati ya LBMA.

***57.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha uandaaji wa Mkakati wa Uongezaji Thamani Madini. Mkakati huo unatoa mwelekeo kwa Serikali wa kubadilisha Sekta ya Madini kutoka kwenye uuzaji wa madini ghafi na kuelekea kwenye kuuza madini yaliyoongezewa thamani ndani ya nchi. Lengo kuu ni kutumia rasilimali madini kama njia ya kufungamanisha Sekta ya Madini na Sekta nyingine za kiuchumi ikiwemo viwanda. Utekelezaji wa mkakati huo utachochea ongezeko la thamani ya madini yetu na kuongeza viwanda vitakavyosaidia upatikanaji wa ajira, Pato la

Taifa, ubunifu, kuongeza ujuzi na kuimarisha ushindani wa bidhaa zitokanazo na madini katika masoko ya ndani na nje ya nchi kupitia mnyororo imara wa uongezaji thamani.

***58.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia shughuli za uongezaji thamani madini nchini kupitia viwanda sita (6) vya kusafisha dhahabu (refinery) vilivyopo mikoa ya Dodoma (1), Shinyanga (1), Geita (2), Dar es Salaam (1) na Mwanza (1). Aidha, Wizara inaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuyeyusha madini ya Shaba, Nikeli, Bati na Chumvi katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Kagera, Mbeya, Lindi na Pwani. Sambamba na hilo, Wizara inaendelea kushirikiana na wamiliki wa viwanda vya kusafisha dhahabu ili kupata ithibati ya LBMA kwa ajili ya kuwezesha viwanda hivyo kutambulika katika masoko ya kimataifa.

***59.*** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha shughuli za uongezaji thamani madini ya vito na metali za thamani nchini kwa kuendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa jengo pacha la ghorofa 8 katika Kituo cha Jemolojia Tanzania ili kuongeza uwezo wa kutoa mafunzo. Ujenzi huo upo katika hatua ya ukamilishaji wa msingi (basement). Aidha, Wizara kupitia TGC inaendelea na taratibu za ununuzi wa viwanja viwili (2) kwa ajili ya upanuzi wa eneo la Kituo vyenye ukubwa wa mita za mraba 7,318 ambavyo vipo mkabala na eneo la ujenzi.

### (e) Kuimarisha Uendeshaji wa Minada na Maonesho ya Madini ya Vito

***60.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) iliendesha mnada mmoja (1) wa ndani wa madini ya vito uliofanyika kielektroniki Jijini Arusha Mwezi Novemba 2025. Katika mnada huo madini yenye thamani ya shilingi 231,250,000.00 yalinunuliwa. Wizara inaendelea kuhamasisha na kuongeza mwamko wa ushiriki wa wadau katika minada ya madini ya vito. Aidha, Wizara imeunda timu ndogo ya uhamasishaji na ufuatiliaji wa uzalishaji wa madini ya vito ikijumuisha maandalizi ya Mnada wa Kimataifa na Maonesho ya Madini ya Vito ya Arusha (Arusha Gem Fair) unaotarajiwa kufanyika mwezi Juni 2026.

**(f) Kuongeza Uwekezaji kwenye Tafiti za Kina za Madini**

***61. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia GST imefanya utafiti wa jiofizikia kwa kutumia ndege nyuki katika maeneo ya Geita, Manyara na Lindi ambapo taarifa muhimu za kina za jiolojia zilibainishwa katika maeneo hayo. Sambamba na hilo, umefanyika pia utafiti wa kina wa jiofizikia (High Resolution Airborne Geophysical Survey) katika maeneo ya leseni za STAMICO zilizoko Mkoa wa Lindi, hatua inayolenga kuongeza uelewa wa kina kuhusu rasilimali zilizopo. Utafiti huo uliofanyika umewezesha Serikali kubaini uwezekano wa matumizi ya ndege nyuki kutumika katika upatikanaji wa taarifa za kina za jiofizikia kwenye leseni ndogo za uchimbaji wa madini. Hivyo, hatua hii itasaidia kutumia teknolojia ya ndege nyuki katika kupata taarifa za kina za jiofizikia kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo.

***62. Mheshimiwa Spika,*** GST imekamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia katika vitalu viwili (2) vya kimkakati vilivyoko kusini-magharibi mwa nchi, vyenye ukubwa wa takribani kilomita za mraba 176,676.45 sawa na asilimia 18 ya eneo lote la nchi. Utekelezaji wa utafiti huu unatarajiwa kuongeza upatikanaji wa taarifa za kina za jiofizikia kutoka asilimia 16 ya sasa hadi kufikia asilimia 34.

***63. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kutokuwepo kwa taarifa za kina za jiofizikia kwenye baadhi ya maeneo ya nchi, Wizara imeendelea kuhamasisha kampuni mbalimbali kufanya tafiti za kina kwenye maeneo ya leseni zao kama hatua za awali za utafutaji madini. Mathalani, hivi karibuni kampuni ya Barrick imefanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa kutumia helikopta katika maeneo ya Msalala, Nzega, Igunga, Mbogwe na Nyang'hwale kwa ajili ya kubaini uwepo wa maeneo mapya yenye madini. Utafiti huo umelenga kubaini uwezekano wa maeneo mapya ya miradi ya uchimbaji wa dhahabu.




**Picha Na. 4:** *Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini akizindua mradi wa utafiti wa kina wa madini kwa kurusha helikopta unaotekelezwa na Kampuni ya Barrick.*

***64.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia GST imeendelea na ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi na Usambazaji wa Taarifa za Jiosayansi na Rasilimali za Madini ambapo hadi kufikia Machi 2026 ujenzi wa mfumo huo umefikia asilimia 45. Aidha, kukamilika kwa mfumo huo kutaimarisha usimamizi na upatikanaji wa taarifa za miamba na madini iliyopo nchini.

**(g) Kuwarasimisha na Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo**

***65.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya leseni 8,878 za uchimbaji mdogo zimetolewa na Wizara kupitia Tume ya Madini. Aidha, STAMICO inaendelea kusaidia wachimbaji wadogo kwa kutoa huduma za kitaalam katika utafiti, uchimbaji, uchenjuaji na utunzaji wa mazingira. Katika kipindi husika jumla ya wachimbaji 451 wamepatiwa mafunzo kupitia vituo vya mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi.

***66.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia STAMICO imetoa huduma ya uchorongaji katika maeneo mbalimbali, ambapo jumla ya mita 3,896.59 zilichorongwa. Kwa upande wa wazalishaji chumvi wadogo, ujenzi wa kiwanda cha kusafisha chumvi kilichopo Nangurukuru Wilaya ya Kilwa umekamilika, na hatua inayofuata ni kukamilisha usimikaji wa mitambo.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Madini imefanya ufuatiliaji wa kutambua maeneo ya kugawiwa kwa wachimbaji wadogo ambapo hadi sasa jumla ya maeneo 99 yamependekezwa kwa ajili ya uchambuzi. Aidha, maeneo mawili (2) yametengwa katika Mikoa ya kimadini ya Mbogwe - Msasa (Leseni 35 zimetolewa) na Lindi - Ntaka Hill (Leseni 69 zimetolewa).

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya wazalishaji chumvi 576 kutoka Mkoa wa Lindi na Mtwara, na wachimbaji wadogo 976 kutoka Mbogwe na Geita Mjini wamepewa mafunzo kuhusu utafiti, uchimbaji salama, uchenjuaji, afya, usalama na utunzaji wa mazingira migodini.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kuwezesha ushiriki wa wachimbaji wadogo katika warsha, makongamano, mikutano na majukwaa ya kitaifa na kimataifa kwa ajili ya kujifunza teknolojia mbalimbali pamoja na kutafuta fursa za biashara. Mathalani, chini ya uratibu wa FEMATA, jumla ya wachimbaji wadogo 31 walifanya ziara ya mafunzo nchini Uturuki kuanzia tarehe 3 hadi 14 Septemba 2025.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kupitia Tume ya Madini imesaini Hati ya Makubaliano na Benki ya CRDB kwa ajili ya upatikanaji wa mikopo kwa wachimbaji wadogo wa madini. Kama sehemu ya utekelezaji wa makubaliano hayo kikundi cha wachimbaji wadogo cha *Songwe Gold Family* – Saza mkoani Songwe kinatarajiwa kupata mkopo wa shilingi bilioni 50 kutoka benki ya CRDB. "Nitumie fursa hii kuzishukuru benki za CRDB, NMB, NBC, AZANIA na KCB kwa kuendelea kuwakopesha wachimbaji wadogo. Aidha, naomba kutoa wito kwa benki nyingine nchini kuendelea kuwaamini na kuwakopesha wachimbaji wadogo"




**Picha Na. 5:** *Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini akishuhudia utiaji saini wa makubaliano maalum ya kuwakopesha wachimbaji wadogo kati ya Tume ya Madini na Benki ya CRDB.*

**(h) Kuzijengea Uwezo Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ya Madini**

***71. Mheshimiwa Spika,*** Rasilimaliwatu ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha utendaji kazi unaimarika na malengo ya Wizara yanafikiwa. Hivyo, Wizara pamoja na Taasisi zake imeendelea kusimamia utendaji kazi na maslahi ya watumishi wake pamoja na kujaza nafasi zilizo wazi. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara na Taasisi zake imejaza nafasi 147 kwa utaratibu wa uhamisho (55) na ajira mpya (92). Aidha, kupitia uhamisho huo, Wizara imepata watumishi (24), Tume ya Madini (17), TEITI (8) na GST (6). Vilevile, kwa upande wa Ajira mpya Wizara imepata watumishi (9), STAMICO (1), Tume ya Madini (66), GST (12) na TGC (4). Pia, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini yake imeendelea kusimamia na kuhakikisha maslahi na stahiki za watumishi zinapatikana kwa wakati.

***72. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mafunzo kwa watumishi, Wizara na Taasisi zake zimewawezesha watumishi 455 kupata mafunzo. Kati ya hao watumishi 347 walipata mafunzo ya muda mfupi na 108 ya muda mrefu katika masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Madini.

***73. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa Taasisi zilizo chini yake zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuzipatia vitendea kazi. Tume ya Madini imewezeshwa vifaa vya masoko na TEHAMA; STAMICO imewezeshwa kupata leseni mbili za utafiti wa madini ya nikeli na adimu (REE); GST imewezeshwa upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya utafiti wa madini ikiwemo magari manne (4); TGC imewezeshwa kuboresha miundombinu ya kutolea mafunzo, huduma za uzalishaji wa bidhaa kwa lengo la kukuza shughuli za uongezaji thamani madini nchini; na TEITI imewezeshwa kwa kupewa jengo kwa ajili ya ofisi lililopo mji wa Serikali Mtumba.



**Picha Na. 6**: *Magari mapya manne (4) kwa ajili ya kuimarisha shughuli za utafiti GST.*

***74. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na taratibu za kuidhinishwa kwa TGC kuwa Taasisi inayojitegemea. Hatua hii itaiwezesha TGC kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**(iv) Utekelezaji wa Maeneo Mengine ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2025/2026**

***75. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imetekeleza majukumu yake mengine kama ifuatavyo:

**(i) *Mining Vision* 2030: Madini ni Maisha na Utajiri**

***76. Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia matarajio ya DIRA 2050, Wizara

imekamilisha Andiko la *Mining Vision 2030* lililozingatia nguzo tano (5) ambazo ni: kuwa na taarifa za jiosayansi; kuimarisha mfumo wa kisheria na kitaasisi; kuimarisha ufungamanishaji wa Sekta ya Madini na sekta nyingine za kiuchumi na uwekezaji; kukuza uchimbaji mdogo wa madini; na kuimarisha usimamizi wa mazingira.

**(ii) Programu ya *Mining for a Brighter Tomorrow* – MBT**

***77. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanza kutekeleza Mpango wa MBT ambao ni wa miaka mitano kuanzia mwaka 2025/2026 hadi 2029/2030. Mpango huo unalenga kuongeza ushiriki wa vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum katika mnyororo wa thamani kwenye Sekta ya Madini. Aidha, Malengo Mahsusi ya Mpango wa MBT ni pamoja na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya sekta, kujenga uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za mnyororo wa thamani wa madini, na kuimarisha ujumuishi na manufaa yatokanayo na Sekta ya Madini kwa vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum.

***78. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza malengo ya Mpango wa MBT, Wizara imetoa jumla ya leseni 273 za uchimbaji wa madini kwa vikundi 183 vyenye jumla ya wanavikundi 2,550 katika mikoa mbalimbali ikiwemo Mara, Kagera, Shinyanga, Morogoro, Dodoma na Njombe. Aidha, Wizara ilitoa elimu kuhusu usalama, afya, utunzaji wa mazingira na usimamizi wa rasilimali fedha kwa wanufaika wa leseni zilizotolewa. Vilevile, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa makundi hayo kupitia miradi mbalimbali ya uchimbaji na biashara ya madini ikiwemo mradi wa Nyamongo kwa kushirikiana na Mgodi wa dhahabu wa *North Mara* katika Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara. Sambamba na hilo, mpango huu unatekelezwa katika maeneo ya Mirerani Mkoa wa Manyara, Mbogwe na Nyang'hwale Mkoa wa Geita. Wizara pia imeendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa MBT.

**(iii) Kuwajengea Uwezo Wataalam kwenye Maeneo Muhimu katika Sekta ya Madini**

***79. Mheshimiwa Spika,*** ili kukidhi mahitaji ya wataalam na

uwepo wa teknolojia mahsusi katika mnyororo wa thamani wa madini nchini, Wizara imekamilisha taratibu za kuwapeleka wataalamu masomoni ndani na nje ya nchi katika fani mbalimbali zikiwemo: ukadiriaji wa mashapo (resource estimation); modeli za kifedha (financial modelling); ukaguzi na usimamizi wa rasilimali madini; uthaminishaji wa madini; ukataji wa madini ya vito; utengenezaji wa bidhaa za usonara na uongezaji thamani madini. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara imepanga kuwajengea uwezo jumla ya watumishi nane (8) katika maeneo ya ukadiriaji mashapo (resource estimation), modeli za kifedha (financial modelling) na ukaguzi wa fedha (financial auditing) migodini.

**(iv) Kuboresha Usimamizi wa Shughuli za Madini Kidijitali**

***80.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea na taratibu za kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Sekta ya Madini Kidijitali utakaojulikana kama "*Mineral Sector Management Information System - MSMIS*". Mfumo huu unalenga kuimarisha usimamizi, uratibu na upatikanaji wa taarifa za Sekta ya Madini kwa kutumia teknolojia za kidijitali, sambamba na jitihada za Serikali za kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za umma. Hatua za awali zimeanza kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi wa mahitaji ya mfumo, kubainisha wadau watakaohusika katika utekelezaji wa mfumo na maandalizi ya nyaraka muhimu zinazohitajika.

***81.***

***82.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mfumo huo, Wizara pamoja na Taasisi zake inatarajia kupata manufaa mbalimbali ikiwemo kuwepo kwa jukwaa la pamoja la kidijitali litakalorahisisha ukusanyaji, uchakataji, uhifadhi na usambazaji wa taarifa za Sekta ya Madini kwa ufanisi na kwa wakati. Aidha, mfumo utasaidia kuweka usimamizi thabiti wa taarifa zinazohusiana na utoaji wa leseni za uchimbaji madini, uzalishaji wa madini, biashara na masoko ya madini, na mapato yatokanayo na shughuli za madini. Vilevile, mfumo huo utaongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za madini kwa kuwezesha ufuatiliaji wa karibu wa shughuli za wadau wa Sekta ya Madini.

***83. Mheshimiwa Spika,*** manufaa mengine yatakayopatikana kutokana na uanzishwaji wa Mfumo wa MSMIS ni pamoja na kuiwezesha Serikali kufanya maamuzi sahihi ya kisera na kiutendaji kwa kuzingatia takwimu na taarifa sahihi zinazopatikana kwa wakati. Sambamba na hayo mfumo husika utapunguza utegemezi wa mifumo ya kianalojia, kurahisisha upatikanaji wa taarifa na kuboresha uratibu kati ya taasisi mbalimbali za Serikali zinazohusika na usimamizi wa Sekta ya Madini. Mfumo huo utaunganishwa na mifumo mingine ya Serikali ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa shughuli za madini na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**(v) Mpango Mkakati wa Madini Muhimu na Madini Mkakati (Critical and Strategic Minerals Strategy)**

***84. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imekamilisha Mpango Mkakati wa Madini Muhimu na Madini Mkakati. Utekelezaji wake utaanza kutumika mara baada ya kuidhinishwa kwa orodha ya Madini Muhimu na Madini Mkakati. Mkakati huo ni moja ya nyenzo za kutekeleza Sera ya Madini iliyohuishwa pamoja na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Muda Mrefu (LTPP 2050) ili kufikia malengo ya DIRA 2050.

**(vi) Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura 123 na Kanuni zake**

***85. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, Wizara imefanya marekebisho ya Kanuni za Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii za Mwaka 2025 na kutangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 692 la tarehe 19 Desemba, 2025. Baadhi ya marekebisho yaliyofanyika ni pamoja na kurekebisha kanuni ya 6 ili kuboresha muundo wa kamati ya wataalamu kwa lengo la kuongeza ufanisi.

***86. Mheshimiwa Spika,*** marekebisho mengine ni kuongeza kanuni ndogo ya 7(3) iliyolenga kupunguza gharama za utendaji wa kamati ya wataalamu na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa miradi kwa kuelekeza kila taasisi imgharamie mwakilishi wake. Kanuni za 8 na 9 zimeboreshwa kwa kuweka ukomo wa muda wa kuwasilisha mipango, kanuni ya 15 imefutwa na kutungwa kanuni

mpya inayofafanua vizuri zaidi majukumu ya wamiliki wa leseni za madini ikiwemo kuwasilisha taarifa za fedha na miradi. Pia, kanuni ndogo ya 16(6) inayohusu usimamizi, ufuatiliaji na ukaguzi wa utekelezaji wa mipango ya wajibu wa wenye leseni kwa jamii imeongezwa.

***87. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetunga Kanuni kuhusu marekebisho ya Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania katika shughuli za madini za mwaka 2025 na kutangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 563 la tarehe 12 Septemba, 2025. Lengo la marekebisho hayo ni kuimarisha na kuongeza ushiriki wa watanzania katika shughuli zote za mnyororo wa thamani wa Sekta ya Madini na kuongeza mamlaka ya Tume ya Madini ya kuidhinisha, kusimamia na kufuatilia mipango ya ubia kati ya watanzania na kampuni za kigeni ili kuhakikisha kuwa watanzania wanafaidika na mipango hiyo ya ubia. Pia, marekebisho hayo yanaipa mamlaka Tume ya Madini kutangaza kwa kadri itakavyoonekana inafaa bidhaa na huduma ambazo zinatakiwa kutolewa na watanzania au kampuni zinazomilikiwa na watanzania kwa asilimia 100.

***88. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, Wizara imetunga kanuni mpya, Kanuni za Leseni Ndogo ya Uchenjuaji wa Madini za Mwaka 2025 na kutangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 572 la tarehe 12/9/2025. Kanuni hizi zinazosimamia leseni ndogo za uchenjuaji wa madini zitaboresha shughuli za Sekta ya Madini kwa kuwatambua na kutoa leseni kwa wachenjuaji wadogo. Kanuni hizi zinazuia uchenjuaji holela uliokuwa unafanywa bila kuzingatia miongozo na taratibu za kiafya, usalama na utunzaji mazingira.

### (v) Utekelezaji wa Shughuli za Taasisi Zilizo Chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

***89. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuzisimamia na kuziwezesha taasisi zake tano (5) ili ziendelee kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kuzingatia Sera, Sheria na Miongozo inayosimamia Sekta ya Madini. Taasisi hizo ni Tume ya Madini; Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST); Shirika la Madini la Taifa (STAMICO); Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC); na Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali

Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI). Taarifa ya utekelezaji wa taasisi ni kama ifuatavyo:

**a. TUME YA MADINI**

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 Tume ya Madini imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

**(i) Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini**

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Tume ya Madini ilitoa jumla ya leseni 11,674 ikilinganishwa na lengo la kutoa leseni 11,463. Leseni zilizotolewa ni kama ifuatavyo: Leseni za Uchimbaji wa Kati wa Madini (MLs) - 21; Leseni za Utafutaji wa Madini (PLs) - 313; Leseni za Uchimbaji Mdogo (PMLs) –8,878; Leseni za Uchenjuaji wa Madini (PCLs) - 41; Leseni za Biashara Kubwa ya Madini (Dealer License - DLs) - 914 na Leseni za Biashara Ndogo ya Madini (Broker License -BLs) – 1,507.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, leseni 111 za utafutaji wa madini na leseni 35 za uchimbaji wa kati wa madini zilipewa hati za makosa kutokana na kutozingatia masharti ya leseni ikiwa ni pamoja na kutolipa ada za mwaka na kutoendeleza maeneo ya leseni. Aidha, leseni 53 za utafutaji madini na leseni 29 za uchimbaji wa kati wa madini zilifutwa baada ya wamiliki wake kushindwa kurekebisha makosa yao.

**(ii) Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Madini katika Uzalishaji na Biashara ya Madini**

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 madini yenye thamani ya shilingi 16,245,437,499,141.10 yalizalishwa na kuuzwa. Kutokana na thamani hiyo, Serikali iliweza kukusanya jumla ya shilingi 957,396,031,069.62. Kati ya fedha hizo shilingi 835,190,241,847.76 ni malipo ya mrabaha na shilingi 122;205,789,221.86 ni malipo ya ada ya ukaguzi. Uwiano wa uzalishaji kwa baadhi ya madini ni kama ifuatavyo: Dhahabu uzito wa kilo 51,819 yenye thamani ya shilingi 13,519,000,571,509.00;

makaa ya mawe tani 2,201,441 yenye thamani ya shilingi 699,950,878,624.00; madini ujenzi tani 30,215,970 yenye thamani ya shilingi 535,707,335,599.00; madini ya viwandani tani 12,269,218 yenye thamani ya shilingi 364,041,807,755.00; almasi karati 294,865 yenye thamani ya shilingi 109,315,499,461.00; na madini mengine mbalimbali yenye thamani ya shilingi 1,017,421,406,193.10.

***94.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi rejewa, Tume ya Madini kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za Serikali iliendelea kusimamia utendaji kazi wa masoko ya madini 44 na vituo vya ununuzi wa madini 118 ili kuhakikisha yanafanya kazi kwa ufanisi. Kupitia masoko na vituo vya ununuzi wa madini, Tume ya Madini ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 292,482,721,083.67 ikijumuisha shillingi 259,634,483,324.52 ikiwa ni mrabaha na shilingi 32,848,237,759.15 ada ya ukaguzi kutokana na mauzo ya madini yenye thamani ya shilingi 4,903,477,353,887.03.

**(iii) Ukaguzi wa Masuala ya Usalama, Afya na Mazingira**

***95.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, ukaguzi wa migodi kuhusu usalama, afya, mazingira na matumizi salama ya baruti ulifanyika. Ukaguzi huu ulihusisha migodi mikubwa sita (6), migodi ya kati 31 na migodi midogo 9,080 katika maeneo mbalimbali kwenye mikoa 30 ya kimadini nchini.

***96.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kaguzi hizo masuala mbalimbali yalibainika ikiwa ni pamoja na: kukosekana kwa mpango wa ufungaji mgodi uliohuishwa; kutotekelezwa kikamilifu kwa matakwa ya Sheria ya Baruti; kukosekana kwa taarifa za usanifu wa maeneo ya kuhifadhi miambataka pamoja na mabwawa ya topetaka; kukosekana kwa meneja mgodi aliyeteuliwa kwa mujibu wa utaratibu; maduara kutokuwa na miundombinu ya kiusalama; na vifaa kinga kutotumiwa ipasavyo. Wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu yaliyobainika ili kukidhi matakwa ya Sheria ya Madini Sura 123, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 pamoja na Sheria ya Baruti Sura 45.



**Picha Na. 7:** *Maafisa wakikagua masuala ya Usalama, Afya na Mazingira katika mgodi wa chini ya ardhi wa Polygold Co. LTD uliopo Musoma, Mara.*

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, ukaguzi ulifanyika katika maghala ya kuhifadhia baruti kwenye mikoa ya kimadini ya Kahama, Geita, Katavi, Kigoma, Manyara, Mirerani, Simiyu, Tanga, Mwanza, Mara, Tabora na Mbeya. Jumla ya maghala ya kuhifadhia baruti 678, bohari 145, Stoo 295 na masanduku 280 yalikaguliwa. Katika kaguzi hizo masuala mbalimbali yalibainika ikiwemo kukosekana kwa vipima joto ndani ya maghala, vinasa radi pamoja na uhifadhi wa baruti kuzidi uwezo wa maghala na wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya vibali 428 vya baruti vilitolewa. Kati ya vibali hivyo, vitano (5) ni vya kuuza baruti, 311 vya kuingiza baruti nchini, 81 vya kutoa baruti nchini kwenda nje ya nchi na 31 vya kusafirisha baruti kupitia nchini kwenda nchi nyingine. Vibali husika vilitolewa baada ya maombi kukidhi matakwa ya Sheria ya Baruti, Sura 45.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, maombi ya vibali 27 vya ujenzi wa hifadhi za baruti, kutengeneza, kuuza, kutunza na kutumia baruti yalipokelewa na kufanyiwa kazi katika mikoa ya kimadini 13. Kati ya maombi hayo, 21 yalikidhi vigezo na sita (6) hayakukidhi vigezo na wahusika walielekezwa kufanya marekebisho.

***100. Mheshimiwa Spika,*** maeneo manne (4) ya kuhifadhia miambataka yalikaguliwa kwa lengo la kuhakiki ubora na kutoa idhini ya matumizi katika Mikoa ya Geita, Kahama, Singida na Dodoma. Vilevile, mabwawa ya topetaka (TSF) 31 yalikaguliwa kwa lengo la kutoa idhini ya ujenzi au matumizi. Ukaguzi huo ulilenga kuangalia na kujiridhisha maeneo yaliyopendekezwa iwapo yanafaa kwa ajili ya ujenzi pamoja na kuangalia hatua za ujenzi kama zimekidhi matakwa ya taarifa ya usanifu iliyoidhinishwa. Katika kaguzi hizo masuala mbalimbali yalibainika ikiwemo kukosekana kwa visima vya kufuatilia uwepo wa nyufa zinazovujisha maji kutoka katika bwawa la topetaka (monitoring boreholes) na wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo.

***101. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya migodi saba (7) ya uchimbaji madini iliwasilisha maombi ya uidhinishaji wa mifumo ya kupandisha na kushusha watu na mizigo mgodini *(Hoisting Systems)* ambapo mifumo hiyo ilikaguliwa. Ukaguzi ulilenga kuhakikisha kama mifumo hiyo imekidhi vigezo stahiki ili iweze kupata idhini ya matumizi kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Migodi. Katika kaguzi hizo mapungufu kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na kutumia vifaa visivyo na ubora na wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo.

***102. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mitambo 52 ya kuchenjulia dhahabu ya *CIP/CIL; Vat Leaching* 509 na *Elution* 204 zilikaguliwa katika Mikoa ya Kimadini 25. Kaguzi hizi zililenga kuhakikisha miradi inakidhi matakwa ya sheria na taratibu ambazo zimeainishwa katika Sheria ya Madini Sura 123. Miongoni mwa masuala yaliyobainika ni pamoja na maeneo yenye marudio kutowekewa mifereji/kuta ya kuyazunguka kwa lengo la kuzuia utitirishaji wa maji kwenda kwenye mazingira. Wahusika walirekebisha mapungufu hayo kama walivyoelekezwa.

***103. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mipango ya ufungaji migodi minne (4) ilijadiliwa na Kamati ya Kitaifa ya Ufungaji Migodi. Kati ya mipango hiyo, hakuna mpango ulioidhinishwa kutokana na mapungufu mbalimbali yaliyobainika ikiwemo kukosekana kwa taarifa za utafiti wa

uimara wa miamba (Geotechnical studies), jiokemia, hydrolojia, pamoja na kukosekana kwa maoni ya wadau wa Kamati ya Wilaya ya Ufungaji Migodi (District Mine Closure Committee - DMCC) ili kuainisha miradi ya kiuchumi kwa jamii baada ya maisha ya mgodi. Wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo.

***104. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, elimu kuhusu masuala ya usalama, afya, mazingira pamoja na usimamizi na matumizi ya baruti ilitolewa kwa wachimbaji wadogo wa madini katika mikoa ya kimadini 23 ambapo jumla ya wachimbaji wadogo na wadau wa madini 18,621 walishiriki mafunzo hayo.

### (iv) Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini (Local Content) na Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (CSR)

***105. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya mipango 1,082 ya Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini iliwasilishwa kati ya mipango 750 iliyopangwa kuwasilishwa kwa kipindi husika. Aidha, Mipango 1,081 iliidhinishwa na mpango mmoja (1) haukuidhinishwa kutokana na kutokidhi matakwa ya kisheria. Kati ya mipango 1,082 iliyowasilishwa, 13 ilihusisha leseni za uchimbaji mkubwa (SML), 15 leseni za uchimbaji wa kati (ML), 11 leseni za uchimbaji mdogo (PML), 31 leseni za utafutaji (PL) na 1,012 ni watoa huduma mbalimbali kwa wamiliki wa leseni za madini. Katika kutekeleza matakwa ya Kanuni za *Local Content*, Tume ya Madini ilitangaza huduma na bidhaa 20 ambazo zinapaswa kutolewa na watanzania au kampuni zinazomilikiwa na watanzania.

***106. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2026, jumla ya ajira 20,421 zilizalishwa katika migodi mbalimbali. Kati ya ajira hizo, watanzania ni 19,695 na wageni 726. Aidha, kampuni za madini na watoa huduma zilinunua bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi 4,007,548,722,894.90 kutoka kampuni za Kitanzania sawa na asilimia 90.18 ya ununuzi wote wenye thamani ya shilingi 4,443,900,487,725.71. Vilevile, kupitia CSR miradi yenye thamani ya shilingi 16,173,999,085.52 ilitekelezwa katika Mikoa ya Kimadini ya Kahama, Mara, Geita, Songwe, Singida, Dar es

Salaam, Lindi, Mwanza na Shinyanga. Miradi hiyo ilihusisha masuala ya afya, kilimo, michezo, miundombinu ya barabara, mazingira na elimu.

**(v) Huduma za Maabara**

***107. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya sampuli 8,629 za wateja mbalimbali zilipokelewa na kuchunguzwa kupitia maabara ya Tume ya Madini. Kati ya sampuli hizo, 2,696 zilitoka migodi mikubwa ya dhahabu kwa ajili ya kuwezesha Serikali kukokotoa mapato stahiki na 5,933 zilitoka kwa wateja binafsi ili kuwasaidia kufanya maamuzi sahihi katika uzalishaji na biashara ya madini. Huduma iliyotolewa iliwezesha Serikali kukusanya shilingi 308,972,000.00.

**(vi) Ukaguzi wa Hesabu za Fedha na Kodi**

***108. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, ukaguzi ulifanyika katika migodi ya kati na mikubwa pamoja na miradi ya ujenzi wa barabara ambapo masuala mbalimbali yalibainika kutokana na kaguzi hizo ikiwa ni pamoja na hoja za mapunjo ya mrabaha na ada ya ukaguzi zenye jumla ya shilingi 2,459,084,728.94 ikijumuisha shilingi 1,843,925,731.91 ikiwa ni mapunjo ya mrabaha; shilingi 555,158,997.03 ni ada ya ukaguzi; na shilingi 60,000,000.00 ni adhabu kwa kukiuka Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania za Mwaka 2018.

***109. Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ukaguzi uliofanyika mwaka 2025/2026, jumla ya shilingi 2,699,419,438.66 zimekusanywa katika kipindi rejewa. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,968,667,252.96 ni mrabaha, shilingi 540,752,185.70 ni ada ya ukaguzi na shilingi 190,000,000.00 ni adhabu kwa ukiukwaji wa Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania.

**b. TAASISI YA JIOLOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA (GST)**

***110. Mheshimiwa Spika***, jukumu la Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania ni kufanya tafiti za jiosayansi kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. Kupitia tafiti hizo taarifa mbalimbali za jiosayansi za uwepo wa madini nchini huandaliwa ili

kuvutia uwekezaji katika utafutaji wa madini wa kina kwa lengo la kuanzisha migodi mipya.

***111. Mheshimiwa Spika,*** taarifa hizo za jiosayansi hutumika katika sekta nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, maji na ujenzi. Pia, GST ina jukumu la ufuatiliaji wa majanga ya asili ya jiolojia ikiwemo matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano na maporomoko ya ardhi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, GST imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

**(i) Tafiti za Jiosayansi na Uboreshaji wa Kanzidata ya Taifa ya Taarifa za Miamba na Madini**

***112. Mheshimiwa Spika,*** GST imekamilisha kuchora ramani mbili (2) za jiolojia na kuandaa ripoti zake baada ya kufanya ugani wa jiolojia katika QDS 221 na 222. QDS hizo zipo katika Wilaya za Kibiti na Rufiji katika Mkoa wa Pwani. Aidha, matokeo ya ugani huo yalionesha uwepo wa madini ya chokaa na miamba yenye ubora wa kuzalisha kokoto. Vilevile, GST ilifanya utafiti kuhusu kutambua umri wa miamba aina ya *granitoids* katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria. Taarifa kuhusu umri wa miamba itasaidia kubaini maeneo yenye madini na itachapishwa kwenye majarida yenye kutambulika.
"Natoa wito kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kutumia taarifa hizo kuweza kufanya uwekezaji katika maeneo husika"

***113. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, GST imetoa ushauri elekezi kwa wadau 49 waliowasilisha maombi katika nyanja za utafiti na uchenjuaji madini kwa Taasisi za Serikali na binafsi, kampuni za uchimbaji wa kati na mkubwa pamoja na wachimbaji wadogo. Aidha, ushauri wa kitalaam ikiwa ni pamoja na kubainisha mwelekeo wa mbale zinazobeba madini na namna bora ya uchenjuaji ulitolewa kwa wachimbaji wadogo 42 na utafiti kwa wachimbaji wakubwa wawili (2). Vilevile, ushauri ulitolewa kwenye maeneo ya ujenzi wa miundombinu hasa majengo kwa Taasisi nne (4) za Serikali na Taasisi binafsi moja (1).

***114. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika GST ilifanya utafiti

maalumu ili kubaini maeneo yenye nyufa hai (active fault zone) zinazoweza kuwa hatarishi kutokana na matetemeko katika Wilaya ya Hanang Mkoa wa Manyara. Matokeo ya utafiti huo yaliainisha maeneo yaliyo salama na kubainisha viashiria hatarishi kwa makazi. Taarifa hiyo iliwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Kitengo cha Maafa.

***115. Mheshimiwa Spika,*** GST inaendelea na ukamilishaji wa taratibu za ununuzi wa helikopta. Kwa sasa inafanya majadiliano na mzabuni aliyepatikana kabla ya kuingia kwenye mkataba wa ununuzi. Helikopta hii itasaidia kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia (High Resolution Airborne Geophysical Survey) katika maeneo mbalimbali nchini.

***116. Mheshimiwa Spika,*** GST imeendelea kujenga Mfumo wa Utunzaji na Usambazaji wa Taarifa za Jiosayansi na Rasilimali Madini ambapo hadi kufikia Machi 2026 ujenzi umefikia asilimia 45. Aidha, kukamilika kwa mfumo huo utaongeza usalama wa kanzidata ya taarifa za madini na utarahisisha utunzaji na usambazaji wa taarifa hizo kwa wadau.

**(ii) Uboreshaji wa Huduma za Maabara**

***117. Mheshimiwa Spika,*** maabara ya GST ni mojawapo ya maabara za jiosayansi inayofanya uchunguzi kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika kimataifa na ina Ithibati ya ubora (ISO 17025:2017). Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, GST imeanza ujenzi wa maabara ya kisasa (State-of-the-Art Laboratory) Mkoa wa Dodoma ambapo hadi sasa umefikia asilimia 8.5. Aidha, ujenzi wa maabara hiyo unatarajia kuongeza uwezo wake wa kufanya uchunguzi wa aina nyingi za madini ikiwemo ya kimkakati ambayo kwa sasa baadhi yanapelekwa nje ya nchi kufanyiwa uchunguzi.

***118. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, maabara ya GST imefanyiwa ukaguzi na Shirika linalodhibiti ubora wa huduma za maabara katika nchi zilizopo Kusini mwa Bara la Afrika (Southern African Development Community Accreditation Services - SADCAS) tarehe 24 Februari, 2026. Kupitia ukaguzi huo, maabara ya GST imekidhi vigezo vya kuendelea kuwa na Ithibati

ya uchunguzi wa madini. Hii inawezesha majibu yanayotolewa na maabara ya GST kuendelea kutambulika Kimataifa.

***119. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika jumla ya sampuli 16,612 zimefanyiwa uchunguzi wa jiokemia, *geotechnical*, majaribio ya uchenjuaji madini pamoja na utambuzi wa vito na madini yanayounda miamba (Petrographic Study) katika maabara ya GST.

***120. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, GST imefanya utafiti maalum wa udongo mfinyanzi (Ball Clay) katika Mkoa wa Dodoma Wilaya za Bahi, Mpwapwa, Chamwino na Dodoma Mjini. Utafiti huo ulilenga kubainisha maeneo yanayoweza kuwa na malighafi ya kutosha na kufaa kutengeneza vyungu vya kuyeyushia sampuli za miamba au udongo wenye madini ya metali hususan dhahabu. Lengo la utafiti huo ni kuiwezesha GST kupata maeneo yenye uhakika wa madini hayo na kuzalisha vyungu hivyo.

**(iii) Ufuatiliaji wa Majanga ya Asili ya Jiolojia na Uelimishaji wa Umma Kuhusu Namna Bora ya Kupunguza Athari za Majanga**

***121. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, GST kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Goethe cha Ujerumani ilifanya ufuatiliaji wa kina kuhusu mitetemo katika Mlima Oldoinyo Lengai ambapo vifaa 32 vya kupima mitetemo vilisimikwa katika eneo la mlima huo. Usimikaji wa vifaa hivyo utasaidia kutambua mwenendo wa mabadiliko yanayotokea.

**c. SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO)**

***122. Mheshimiwa Spika,*** STAMICO imepewa dhamana ya kuwekeza katika miradi ya kimkakati kwenye Sekta ya Madini kwa niaba ya Serikali. Aidha, Shirika limepewa jukumu la kuratibu uendelezaji wa wachimbaji wadogo nchini kwa kutoa ushauri wa kitaalamu. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, STAMICO imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

### (i) Uimarishaji wa Ukusanyaji wa Mapato

***123. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 STAMICO ilipanga kukusanya shilingi 201,883,018,735.00. Hadi kufikia Machi 2026, shilingi 60,043,431,896.00 zilikusanywa sawa na asilimia 40 ya lengo la makusanyo kwa kipindi rejewa. Lengo hilo halikufikiwa na STAMICO kutokana na kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa mikataba ya huduma ya uchorongaji; kushuka kwa bei ya makaa ya mawe kwenye soko la dunia; na Shirika kuchelewa kupokea mitambo ya kuzalisha nishati safi ya *Rafiki Briquettes* kutoka nje ya nchi.

- **Uzalishaji wa Makaa ya Mawe na Nishati Mbadala (Rafiki Briquettes)**

***124. Mheshimiwa Spika,*** STAMICO imeendelea na uzalishaji wa makaa ya mawe kupitia mradi wa Kiwira-Kabulo ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya tani 214,354 zimezalishwa. Kati ya kiasi hicho, tani 141,453 zimeuzwa na kuliingizia Shirika shilingi 6,207,291,139.00 na shilingi 1,626,764,661.62 zimelipwa kama mrabaha, ada ya ukaguzi, ada ya usafirishaji nje ya nchi (export fee) na ushuru wa huduma.

***125. Mheshimiwa Spika,*** Shirika kupitia mradi wa makaa ya mawe wa Kiwira - Kabulo umetekeleza shughuli za CSR ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 mradi huo umechangia shilingi 75,600,300.00 katika ujenzi wa madarasa matatu (3) katika Shule ya Msingi Kapeta, Wilaya ya Ileje – Mkoa wa Songwe.

***126. Mheshimiwa Spika,*** Shirika linaendelea na uzalishaji wa nishati safi ya Rafiki *Briquettes*. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Shirika limefanikiwa kuzalisha tani 1,530 za Rafiki *Briquettes* zenye thamani ya shilingi 1,460,738,800.00. Shirika limekamilisha usimikaji wa mitambo miwili (2) katika Mikoa ya Dodoma na Tabora. Kiwanda cha Tabora kilizinduliwa tarehe 21 Februari, 2026. Aidha, Kiwanda cha Dodoma kinatarajiwa kuzinduliwa mwezi Mei, 2026.



**Picha Na. 8:** *Kiwanda cha kuzalisha Nishati Safi ya Rafiki Briquettes Mkoani Tabora ambacho kilizinduliwa tarehe 21 Februari, 2026.*

***127. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa masoko, Shirika linaendelea kuitangaza nishati hiyo katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuweza kupata masoko zaidi. Juhudi hizo zimewezesha taasisi na maeneo mbalimbali kuanza kutumia nishati safi ya Rafiki *Briquette* ikiwa ni pamoja na Jeshi la Wananchi (JWTZ), Jeshi la Magereza, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Taasisi za Elimu (Shule na Vyuo), VETA, Soko la Samaki Feri, Soko la Kuchoma Nyama Kumbi la Moto na Zanzibar kupitia wakala wa Kikundi cha Maisha *Game*. Aidha, Shirika linauza bidhaa hiyo kupitia mawakala ambao wengi wao ni vikundi vya wanawake ikiwemo kikundi cha "Wanawake na Samia" waliopo kila Mkoa.

- **Shughuli za Uchorongaji**

***128. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Shirika limeendelea kufanya kandarasi katika migodi ya dhahabu ya GGM, Buckreef na Shanta (Singida na Chunya). Vilevile, Shirika limefanikiwa kupata kandarasi mpya kwa kampuni ya *Buhemba Resources* na kampuni ya GFX. Kandarasi hizi zimeiongezea Shirika shughuli za uchorongaji na uwezo wa ukusanyaji wa mapato. Jumla ya mita 86,037.64 zilichorongwa katika miradi hiyo. Kutokana na shughuli za uchorongaji huo, Shirika limekusanya jumla ya shilingi 38,374,171,624.00.

- **Uzalishaji wa Kokoto – Chigongwe**

***129. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya tani 5,475 za kokoto zimezalishwa na kuuzwa ambapo Shirika limepata mapato ya shilingi 346,399,600.00. Kutokana na mauzo hayo Shirika liliweza kulipa Serikalini shilingi 13,659,984.00 kama mrabaha na tozo mbalimbali.

**(ii) Uendelezaji wa Leseni za Shirika**

***130. Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kuendeleza leseni zake kwa kufanya utafiti lenyewe na kwa njia ya ubia. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Shirika limefanya utafiti wa madini ya dhahabu, kinywe, *lithium*, *phosphate* na bati (tin) katika leseni zake zilizopo kwenye Hifadhi ya Kigosi Wilaya ya Bukombe - Geita, Wilaya ya Ruangwa na Nachingwea - Lindi, Wilaya ya Bahi - Dodoma na Wilaya ya Kyerwa - Kagera.

***131. Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza leseni za shirika, kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Shirika limesaini mikataba miwili (2) ya ubia kuendeleza leseni za utafiti wa madini ya dhahabu na kinywe. Kwa madini ya dhahabu, Shirika limesaini mkataba na Kampuni ya *Plantcor Mining and Plant Hire* (PTY) Ltd ya nchini Afrika Kusini tarehe 24 Februari 2026 kwa kuendeleza leseni zilizopo Kigosi mkoani Geita. Kufuatia kusainiwa kwa mkataba wa ubia, taratibu za kutafuta wakandarasi wa utafiti wa kijiofizikia na kijiokemia zinaendelea. Kwa upande wa madini ya kinywe, Shirika limesaini Mkataba na Kampuni ya *Planet One Natural Resources Holdings PTE Limited* ya nchini Singapore tarehe 30 Machi 2026 wa kuendeleza leseni zake za utafiti zilizopo Mirerani, Manyara. Vilevile, Shirika limesaini Mkataba na kampuni ya *Costal Nickel* ya nchini China tarehe 12 Septemba 2025 wa kuchimba madini ya Nikeli katika eneo la Ntaka Lindi.




**Picha Na. 9:** *Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa (Mb.), Naibu Waziri wa Madini akishuhudia utiaji saini wa mkataba kati ya STAMICO na Kampuni ya "Plantcor Mining and Plant Hire (PTY) Ltd" kwa ajili ya uendelezaji wa leseni za shirika katika eneo la Kigosi.*

**(iii) Utekelezaji wa Miradi ya Ubia na Kampuni Tanzu**

- **Mgodi wa Dhahabu wa Biharamulo (Kampuni Tanzu ya STAMIGOLD)**

***132. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mgodi wa STAMIGOLD umezalisha dhahabu wakia 7,530.98 na wakia 486.00 za madini ya fedha na kupata shilingi 78,530,155,276.44. Aidha, kutokana na mauzo hayo, mgodi umelipa shilingi 3,337,531,599.25 kama mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma. Vilevile, mgodi umenunua mitambo ya uchimbaji yenye thamani ya shilingi 5,440,000,000.00 ambayo ni *Excavators* 2, *Tipper Trucks 6, Water Bowser* 1 na *Wheel Loader* 2.

***133. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, uchunguzi wa uimara wa miamba (geotechnical investigation*)* ulifanyika kwa ajili ya kubaini usalama wa mgodi wa chini ya ardhi. Vilevile, STAMIGOLD imekamilisha utafiti wa mashapo ulioanza mwaka 2022/2023. Pia, mgodi unaendelea kufanya uhakiki wa mashapo mengine kwenye leseni Na. SML157/2003 na PL 13075/2024 kwa kutumia teknolojia mbalimbali za utafiti. Lengo la uhakiki huo ni kuiwezesha STAMIGOLD kubaini mashapo mapya. Matokeo ya awali yanaonesha uwepo wa

wakia za dhahabu 196,990 ndani ya SML 157/2003 na viashiria vya uwepo wa wakia za dhahabu 105,000 kwenye leseni Na. PL 13075/2024. Hatua hii imelenga kuongeza uhai wa mgodi.

***134. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mgodi unatekeleza miradi ya wajibu wa mmiliki wa leseni kwa jamii (CSR) kiasi cha shilingi 94,960,465.00 Wilayani Biharamulo katika ujenzi wa bweni la Shule ya Msingi Iyengamulilo B' Kata ya Nyantakara; darasa moja (1) katika shule ya Msingi Midaho, Kata ya Lusahunga; darasa moja (1) katika Shule ya Msingi Kisuno, Kata ya Bisibo; na ujenzi wa matundu nane (8) ya vyoo katika Shule ya Msingi Mafukwe, Kata ya Kabindi.

- **Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza (Kampuni ya Ubia Mwanza Precious Metals Refinery)**

***135. Mheshimiwa Spika,*** kiwanda cha kusafisha dhahabu Mwanza kinamilikiwa na STAMICO kwa asilimia 25 na mbia asilimia 75. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kiwanda kimenunua dhahabu ghafi tani 1.960 yenye thamani ya shilingi 580,256,753,948.30 na kulipa Serikalini shilingi 24,660,912,042.80 ikiwa ni mrabaha na ushuru wa huduma. Aidha, kiwanda kimetoa huduma za usafishaji dhahabu jumla ya tani 6.217 kwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) pamoja na wateja wengine (dealers) kwa gharama ya shilingi 2,490,913,950.36. Kiwanda kimeendelea kupokea dhahabu inayonunuliwa na BoT kutoka kwa wachimbaji pamoja na wafanyabiashara wa madini kwa ajili ya kuisafisha kwa kiwango cha asilimia 99.99.

***136. Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha kiwanda kupata dhahabu ya kutosha, Shirika limefanya uhamasishaji kwa wachimbaji wadogo waweze kusafisha dhahabu kwenye Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza. Uhamasishaji huo ulihusu kuwapatia elimu ya manufaa yatokanayo na usafishaji dhahabu kwenye *refinery* ikiwa ni pamoja na kupata faida itokanayo na punguzo la mrabaha kwenye viwanda vya usafishaji dhahabu ndani ya nchi.

- **Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef (Kampuni ya Ubia ya Buckreef Gold Company)**

***137. Mheshimiwa Spika,*** mgodi wa dhahabu wa Buckreef uliopo mkoani Geita unamilikiwa kwa ubia kati ya STAMICO yenye hisa asilimia 45 na kampuni ya TRX Gold Tanzania yenye hisa asilimia 55. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mgodi umezalisha wakia za dhahabu 18,241.52 zenye thamani ya shilingi 194,232,491,026.87 na kulipa Serikalini shilingi 12,851,094,727.87 ikiwa ni mrabaha, ada ya ukaguzi, ushuru wa huduma na *HIV response levy*.

***138. Mheshimiwa Spika,*** mgodi wa Buckreef umetekeleza shughuli za CSR ambapo katika kipindi husika umetoa shilingi 172,196,260.18 katika kuboresha miundombinu na ujenzi wa nyumba za watumishi katika kituo cha afya Butundwe, ukarabati wa barabara ya kijiji cha Mnekezi na uchimbaji wa visima vya maji safi katika kijiji cha Lubanda na Lwamgasa Wilaya ya Geita.

- **Mgodi wa Nikeli – Ntaka (Kampuni ya Ubia Coastal Nickel Industry Limited)**

***139. Mheshimiwa Spika,*** mgodi wa uchimbaji madini ya nikeli uliopo Ntaka Mkoa wa Lindi unamilikiwa kwa ubia wa asilimia 15 kwenye mapato ghafi kwa STAMICO na *Coastal Nickel Industry Limited*. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, tani 4,973 za nikeli zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi 12,912,364,398 zimechimbwa. Shirika linatarajia kupata takriban shilingi 1,936,854,660.00 kama mapato yatokanayo na umiliki wake.

**(iv) Shughuli za Uchimbaji Mdogo na Uimarishaji wa Vituo vya Mfano**

***140. Mheshimiwa Spika,*** STAMICO inaendelea kuratibu shughuli za uchimbaji mdogo kwa kutoa huduma za kitaalam kwa Wachimbaji Wadogo katika nyanja za utafiti, uchimbaji, uchenjuaji madini pamoja na utunzaji wa mazingira. Aidha, jumla ya wachimbaji wadogo 451 wamepatiwa mafunzo kupitia vituo vya mfano. Vilevile, kupitia vituo hivyo huduma ya uchenjuaji mbale ya dhahabu kwa wateja 32 ilitolewa ambapo dhahabu ya

uzito wa gramu 106,029.18 yenye thamani ya shilingi 29,633,631,202.30 ilichenjuliwa na kuipatia Serikali mapato ya shilingi 2,163,255,077.77.

***141.*** ***Mheshimiwa Spika***, STAMICO imeendelea kutoa huduma ya uchorongaji kwa bei nafuu kwa wachimbaji wadogo ambapo katika kipindi rejewa, wachimbaji wadogo wamepata huduma hiyo katika maeneo ya Mbangala –Songwe, Sambaru – Singida, Mwagiwagi – Masumbwe, Kasimenti – Makongolosi, Kerende na Nyamongo –Tarime, Mnyolima - Mbeya, Melela – Morogoro, Kondoa –Dodoma, Isaula, Itumbi na Mapogoro – Chunya na Lwamgasa – Geita. Jumla ya mita 3,896.59 zimechorongwa katika maeneo hayo.

***142.*** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza wigo wa kuwahudumia wachimbaji wadogo, shirika limenunua vifaa wezeshi vya mitambo ya uchorongaji na mashine 10 za kupunguza ukubwa wa mawe ya mbale (crusher) kwa ajili ya vikundi maalum vya wanawake. Mashine hizo zimegawiwa kwa vikundi vya wanawake katika mikoa ya Iringa, Shinyanga, Dar es Salaam, Geita, Simiyu, Ruvuma na Mwanza. Aidha, jitihada zinaendelea kufanyika ili kupata mashine nyingine kwa vikundi vya wanawake katika mikoa mingine.

***143.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika zoezi la kuwaendeleza wazalishaji wadogo wa chumvi, Shirika linaendelea na ujenzi wa kiwanda cha kusafisha chumvi katika eneo la Nangurukuru kilichopo Wilaya ya Kilwa - mkoani Lindi. Aidha, hadi kufikia Machi 2026 ujenzi wa jengo la kiwanda umekamalika. Hatua inayoendelea ni usimikaji wa mitambo ya kusafisha chumvi.

## d. KITUO CHA JEMOLOJIA TANZANIA (TGC)

**(i)** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Jemolojia Tanzania kinatoa mafunzo ya uongezaji thamani madini ngazi ya astashahada na stashahada katika fani za utambuzi wa madini ya vito; uchongaji wa bidhaa za mapambo na urembo zinazotokana na miamba; ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za usonara. Aidha, TGC inatoa huduma za utambuzi wa madini ya vito kupitia maabara yake na utengenezaji wa bidhaa

zinazotokana na madini ya vito na miamba. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 TGC imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

**(ii) Utoaji wa Mafunzo na Huduma Nyingine**

***144. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya wanafunzi 93 walidahiliwa kati ya hao wanafunzi 35 ngazi ya Astashahada (*NTA Level* 4) na wanafunzi 58 ngazi ya Stashahada (*NTA Level* 5 na 6). Aidha, Kituo kilidahili wanafunzi 27 wa kozi za muda mfupi katika fani za ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito *(Lapidary),* usonara (*jewellery*) na sayansi ya madini ya vito (*Gemology)*. Kituo kilikusanya shilingi 88,743,077.00 ikiwa ni malipo ya ada na michango mingine inayotokana na mafunzo.

***145. Mheshimiwa Spika,*** ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko, TGC iliandaa mitaala miwili (2) katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ya mafunzo ya jemolojia na usonara (gemstone jewellery technology and gemstone technology - NTA Level 4, 5 and 6). Aidha, mitaala hiyo iliidhinishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) na kuanza kutumika katika Mwaka wa Masomo 2025/2026.

***146. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, *Sunset Gems Ltd* ilitoa mafunzo kwa watumishi na wanafunzi wa TGC kuhusu utumiaji wa mashine za kukata vito kutoka nchini Thailand ikiwa ni utekelezaji wa makubaliano ya pamoja (MOU). Pia, Taasisi ya *United African University of Rwanda* (UAUR) ya nchini Rwanda ilitoa mafunzo ya Jemolojia kwa watumishi na wanafunzi wa TGC.

***147. Mheshimiwa Spika,*** TGC imeendelea kutoa huduma mbalimbali kwa wadau ikiwa ni pamoja na kufanya utambuzi wa madini ya vito, ukataji wa madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za usonara. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya sampuli za madini ya vito 714 zilipokelewa na kutolewa taarifa za utambuzi. Aidha, huduma ya utengenezaji wa bidhaa za usonara 42 zilitolewa. Kutokana na huduma hizo, shilingi 20,856,000.00 zilipatikana.

### (iii) Uzalishaji wa Bidhaa

***148. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, TGC imeendelea kufanya shughuli za usanifu na uzalishaji wa bidhaa za madini ikiwa ni pamoja na kutengeneza bidhaa za usonara, kukata vito na uchongaji wa miamba ambapo vito 820 vilikatwa, bidhaa 959 za usonara na urembo za madini ya vito zilizalishwa, bidhaa 5,206 za mapambo na shanga (beads) 6,211 zilitengenezwa kwa kutumia miamba. Kutokana na uzalishaji huo Kituo kilikusanya jumla ya shilingi 73,816,413.14.

***149. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na soko la uhakika la bidhaa zinazozalishwa, TGC imefungua kituo cha mauzo na maonesho ya madini ya vito na bidhaa za usonara katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha – AICC. Vilevile, TGC imeendelea kuimarisha vituo vya mauzo vilivyopo katika eneo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro - KIA na katika Ofisi za TGC.



**Picha Na. 10:** *Kituo cha mauzo na maonesho ya madini ya vito na bidhaa za usonara kilichopo katika Ukumbi wa Mkutano wa AICC.*

## e. TAASISI YA UHAMASISHAJI UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA RASILIMALI MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA (TEITI)

***150. Mheshimiwa Spika,*** TEITI ina jukumu la kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia yanahakikiwa na kutumika kwa manufaa ya wananchi wote.

Aidha, TEITI ina jukumu la kuhakikisha kampuni zinazofanya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia inaweka wazi taarifa za shughuli zao kulingana na Sheria ya TEITA Sura 447. Vilevile, TEITI ina jukumu la kuwajengea uwezo wananchi katika kutumia takwimu zinazotokana na shughuli za uendeshaji wa makampuni ili kushiriki mijadala kuhusu manufaa ya uchimbaji madini, mafuta na gesi asilia. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, TEITI imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

**(i) Uandaaji na Uwekaji Wazi Ripoti ya 16 ya TEITI kwa Mwaka 2023/2024**

***151. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya TEITI inaendelea na ukamilishaji wa ripoti ya 16 inayoonesha ulinganishi wa malipo ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kampuni zilizochaguliwa kwa ajili ya zoezi la ulinganishi ni kampuni 37 zinazojihusisha na shughuli za madini, mafuta na gesi asilia. Aidha, ripoti hiyo itahusisha kampuni zilizolipa kodi na tozo mbalimbali Serikalini kuanzia shilingi bilioni mbili. Ripoti hii itawekwa wazi kwa umma ifikapo Juni, 2026.

**(ii) Uwekaji Wazi Mikataba ya Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia**

***152. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa TEITI imeweka wazi taarifa tatu (3) za mikataba ya kampuni za uchimbaji madini ambazo ni *Tembo Nickel Corporation Limited, Faru Graphite Corporation Limited* na *Williamson Diamond Limited*. Utekelezaji wa takwa hili ni kwa mujibu wa vigezo vya kimataifa vya uwazi na uwajibikaji (*EITI Standard, 2023*) pamoja na Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia, Sura 447. Aidha, TEITI inaendelea kushirikiana na wadau wengine wa mikataba ya madini, mafuta na gesi asilia katika kuhakikisha kuwa taarifa za mikataba yao inawekwa wazi kwa umma kwa mujibu wa sheria.

**(iii) Utoaji Elimu Kwa Umma Kuhusu Matumizi ya Takwimu za Ripoti ya TEITI**

***153. Mheshimiwa Spika,*** TEITI imeendelea kuelimisha Umma kuhusu matumizi ya takwimu zinazotolewa kwenye ripoti zake kupitia warsha, runinga (TBC, ITV, AZAM, Clouds na Channel Ten), redio, tovuti, mitandao ya kijamii na kwenye maonesho mbalimbali ikiwemo Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba na Maonesho ya Nane ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini. Aidha, TEITI ilifanya warsha katika Mkoa wa Mtwara ambapo washiriki wakiwemo Viongozi wa Halmashauri, Madiwani wa Mikoa ya Mtwara na Lindi na Viongozi wa Halmashauri walipewa elimu ya namna ya kutumia takwimu zinazotolewa na ripoti za TEITI.



**Picha Na. 11:** *Bi. Mariam Mgaya, Katibu Mtendaji wa TEITI (wa pili kulia) akiuelimisha Umma kuhusu majukumu ya TEITI kupitia kipindi cha "Morning Trumpet", Azam TV.*

**(iv) Ukamilishaji wa Mfumo wa Kielektroniki Utakaotumika Kuandaa Taarifa za TEITI**

***154. Mheshimiwa Spika,*** mfumo wa kielektroniki utakaotumika kuandaa taarifa za TEITI za kila mwaka ujulikanao kama "*Extractive Data Reporting Management Information System (EDR-MIS)*" umekamilika na kuwa tayari kutumika. Mfumo huu utatumika kukusanya na kuchakata takwimu mbalimbali kutoka katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia pamoja na Taasisi za Serikali ambazo zitawezesha kuandaa taarifa za TEITI. Matumizi ya mfumo huu utarahisisha uaandaji wa taarifa za TEITI.

### (v) Kufanya Tafiti Mbalimbali za Namna Wananchi Watakavyonufaika na Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia

***155. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, TEITI imekamilisha utafiti kuhusu utekelezaji wa sheria katika eneo la Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini (Local Content) na Wajibu wa Kampuni za Madini kwa Jamii (Corporate Social Responsibility) uliofanyika kwa kampuni za madini zenye leseni za uchimbaji wa kati na mkubwa katika mikoa ya Geita na Mara. Matokeo ya utafiti huo ni: kuwepo kwa maendeleo katika utekelezaji wa masuala ya *Local Content* na CSR; kutofautiana kwa mitazamo katika kupanga vipaumbele vya utekelezaji wa miradi ya CSR; uelewa na ushirikishwaji mdogo wa wadau; uwezo mdogo na kukosa uadilifu kwa baadhi ya wazabuni. Aidha, Wizara kupitia TEITI inaendelea kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyobainishwa kwenye taarifa ya utafiti. Vilevile, TEITI inaendelea na maandalizi ya kufanya tafiti kwa upande wa Sekta ya Uziduaji katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

## D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

***156. Mheshimiwa Spika,*** katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara imezingatia miongozo ifuatayo: Mwongozo wa Kitaifa wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2026/2027; Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031 (FYDP IV); DIRA 2050; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Muda Mrefu (LTPP 2050); Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi; Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; *Africa Mining Vision*; Sera ya Madini ya Mwaka 2009; Mpango Mkakati wa Wizara; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Kifungu cha 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439; Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine wa kitaifa pamoja na Maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambayo yaliyotolewa kwa nyakati tofauti.

## I. Vipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

***157. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara ya Madini itatekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli; kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini muhimu na madini mkakati; kuhamasisha uwekezaji katika uongezaji thamani madini; kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za kina za madini; kurasimisha na kuendeleza wachimbaji wadogo na kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya wizara ya madini.

### (i) Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli

***158. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa uchimbaji wa madini ili uweze kunufaisha nchi na wawekezaji; kuimarisha na kusimamia masoko na vituo vya ununuzi wa madini nchini; na kuendeleza mikakati ya kuimarisha usimamizi wa madini ujenzi na viwandani, soko la tanzanite na madini mengine ya vito hapa nchini ili kuongeza mapato yatokanayo na madini hayo.

***159. Mheshimiwa Spika***, Wizara inatarajia kununua magari kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ukusanyaji wa maduhuli. Hatua hii itachangia katika kusimamia ukusanyaji wa maduhuli, udhibiti wa utoroshwaji na biashara haramu ya madini pamoja na kufuatilia shughuli mbalimbali za madini.

***160. Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hayo, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ya kuimarisha utekelezaji wa Sheria ya Madini, ikiwemo kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini.

***161. Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuimarisha udhibiti na kuzuia utoroshaji wa madini ya tanzanite, katika mwaka ujao wa fedha Wizara kupitia Tume ya Madini, itakamilisha ununuzi wa kofia zenye kamera maalum kwa ajili ya ukaguzi na itahakikisha wakaguzi na wathaminishaji wa madini hayo wanavaa kofia ili kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mwenendo wa uzalishaji na biashara ya madini kwenye Eneo Tengefu la Mirerani.

### (ii) Kuongeza Mchango wa Sekta ya Madini Kwenye Pato la Taifa

***162. Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza mchango wa wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo: kuhamasisha shughuli za utafiti wa madini na uanzishaji wa migodi mipya, kuimarisha usimamizi wa migodi ya uchimbaji; kuboresha mfumo wa usimamizi wa madini ya ujenzi na ya viwandani; kusimamia utekelezaji wa Sheria inayoitaka migodi mikubwa kuajiri, kununua huduma na bidhaa kutoka hapa nchini na kuhamasisha ushiriki wa Watanzania katika mnyororo wa uchumi wa madini;na kuendelea kuimarisha mazingira wezeshi ya kisera na kisheria. Aidha, Wizara itahakikisha kuwa wawekezaji waliopewa leseni za uchimbaji wa madini wanaanza uzalishaji mara baada ya kukamilisha taratibu za matakwa ya kisheria.

### (iii) KuendelezaMnyororo wa Thamani Katika Madini Muhimu na Madini Mkakati

***163. Mheshimiwa Spika,*** madini muhimu na madini mkakati ni madini ambayo yana mahitaji makubwa kwenye maendeleo ya uchumi na ulinzi wa Taifa. Madini hayo ni pamoja na *lithium*, *graphite*, *helium, nickel, cobalt, titanium*, *copper, aluminium, niobium* na *rare earth elements* ambayo yanatumika kutengeneza vifaa vya teknolojia ya kisasa ikiwemo nishati safi.

***164. Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza manufaa yatokanayo na madini muhimu na madini mkakati kwa uchumi wa Taifa, Wizara imepanga kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini hayo kwa kufanya yafuatayo: kuhamasisha uwekezaji katika utafutaji na uchimbaji wa madini muhimu na madini mkakati; kufanya utafiti wa mahitaji ya madini mkakati ili kuyafikia masoko mbalimbali duniani; kutoa leseni za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini muhimu na madini mkakati; na kukamilisha na kutekeleza mkakati wa uendelezaji na uvunaji wa madini hayo nchini.

***"Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba watanzania wananufaika ipasavyo na uwepo wa rasilimali za madini muhimu na madini mkakati hapa nchini"***

**(iv) Kuhamasisha Uwekezaji katika Uongezaji Thamani Madini**

***165. Mheshimiwa Spika,*** ili kuhamasisha uwekezaji, Wizara itaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na madini; kuendelea kutoa ushirikiano kwa wamiliki wa viwanda vya usafishaji wa madini ya dhahabu nchini ili kupata ithibati ya LBMA; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Kituo cha Jemolojia Tanzania ili kiweze kutoa mafunzo na huduma kwenye mnyororo wa uongezaji thamani madini kwa ufanisi. Aidha, Wizara itaendelea kutangaza fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye mnyororo wa thamani wa madini nchini kupitia makongamano, maonesho, tovuti na vyombo vya habari.

***166. Mheshimiwa Spika,*** ili kuhamasisha uwekezaji katika uongezaji thamani madini, Serikali imetenga eneo la Buzwagi lililopo Wilaya ya Kahama kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani madini na viwanda vya uzalishaji bidhaa migodini.

***167. Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza kutangaza fursa za uwekezaji nchini, Wizara kwa kushirikiana na Chemba ya Migodi Tanzania (Tanzania Chamber of Mines) itafanya Mkutano wa saba (7) wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini. Mkutano huo unatarajiwa kufanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kuanzia tarehe 19 hadi 21 Novemba, 2026 Jijini Dar es Salaam. Mkutano huu utawakutanisha kwa pamoja makundi mbalimbali ya wataalamu wa masuala ya madini, Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa kampuni za utafiti na uchimbaji wa madini, kampuni za utafiti na uchimbaji wa madini, watoa huduma, wafanyabiashara na wawekezaji katika Sekta ya Madini kutoka ndani na nje ya nchi yetu.

**(v) Kuimarisha Uendeshaji wa Minada na Maonesho ya Madini ya Vito**

***168. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hiki Wizara itafanya yafuatayo: kuimarisha uendeshaji wa viwanda vya kuongeza thamani madini nchini sambamba na uendelezaji wa minada na maonesho ya madini ya vito ya Arusha (Arusha

Gem Fair - AGF) na Minada ya madini ya vito ya kimataifa ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara ya madini ya vito (Gemstone Hub). Aidha, Wizara itaendelea kuratibu utangazaji wa fursa za uwekezaji zilizopo kupitia makongamano, maonesho, tovuti na vyombo vya habari.

**(vi) Kuongeza Uwekezaji kwenye Tafiti za Kina za Madini**

***169. Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa shughuli hii, Wizara itafanya tafiti za kina za jiosayansi ikiwemo jiofizikia (High-resolution Airborne Geophysical Survey) ili kuainisha uwepo wa madini mbalimbali yakiwemo madini muhimu na madini mkakati. Aidha, Wizara kupitia GST itaendelea na ujenzi wa mfumo wa kusimamia taarifa za jiosayansi. Vilevile, Wizara itaendelea kushirikisha wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ili kushirikiana kufanya utafiti wa madini katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuongeza wigo wa utafiti wa kina wa madini nchini.

**(vii) Kuwarasimisha na Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo**

***170. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na taratibu za kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuweka mazingira wezeshi yatakayowahamasisha kufanya uwekezaji; kuendelea kuhamasisha taasisi za kifedha kutoa mikopo ya fedha na vifaa kwa wachimbaji wadogo; kuandaa Mpango wa kuwatambua na kuwaendeleza wachimbaji wadogo nchini kupitia Mfuko wa Dhamana kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha; kuboresha utendaji wa vituo vya mfano ili kuimarisha utoaji wa huduma na mafunzo kwa wachimbaji wadogo; na kuimarisha huduma za uchorongaji kwa wachimbaji wadogo.

***171. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuimarisha utekelezaji wa mipango ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija kwa kuwatengea maeneo na kuwawezesha kupata leseni kwenye maeneo yenye taarifa za msingi za jiolojia kupitia Programu ya MBT; kuchukua hatua za ufutaji wa leseni za utafiti ambazo hazifanyiwi kazi na kuzirejesha Serikalini ili kupangwa vyema na kugaiwa kwa wachimbaji wadogo; kuhamasisha wachimbaji wadogo kushiriki mikutano,

maonesho na makongamano mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kujifunza na kutangaza shughuli zao; kuendesha makongamano kwenye mikoa ya kimadini kwa ajili ya kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo na wananchi kwa ujumla kuhusu masuala ya sheria na kanuni mbalimbali za madini zikiwemo za *Local Content*, *CSR*, Haki Madini na Haki Ardhi; na kuhamasisha wachimbaji wadogo kushiriki kwenye minada na maonesho ya madini ya vito nchini ili kupanua wigo wa biashara.

***172. Mheshimiwa Spika***, ili kuwawezesha wachimbaji wadogo waweze kunufaika na rasilimali madini, Serikali itaendelea kuitumia Timu ya Wataalamu wenye uzoefu na masuala ya fedha, madini na sheria kwa ajili ya kutoa mapendekezo ya namna ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata mitaji na msaada wa kiufundi. Hatua hii itawawezesha wachimbaji hao kufanya uchimbaji wenye tija na kunufaika zaidi kiuchumi. Aidha, Wizara kupitia STAMICO itaendelea kuwalea na kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuwajengea vituo vya mfano katika maeneo yenye uchimbaji mdogo.

***173. Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuwahamasisha sekta binafsi iweze kuanzisha vituo vya kuuza na kukodisha vifaa na mashine mbalimbali za kufanyia shughuli za madini kwa lengo la kuwawezesha wachimbaji wadogo kutekeleza shughuli za madini kwa tija ili kuongeza mchango wao katika Pato la Taifa.

**(viii) Kuzijengea Uwezo Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ya Madini**

***174. Mheshimiwa Spika,*** ili kuzijengea uwezo taasisi, Wizara itafanya yafuatayo: kuiwezesha Tume ya Madini kupata rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi; kuendelea kuimarisha STAMICO ili ishiriki kikamilifu kwenye uwekezaji wa shughuli za madini.

***175. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuimarisha GST ili iweze kufanya tafiti za jiosayansi kwa lengo la kubaini maeneo mapya yenye uwepo wa madini; kuimarisha TGC ili iweze kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini ya vito na metali za thamani; na kuiwezesha TEITI kupata rasilimali mbalimbali ikiwemo vifaa na vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

## II. Maeneo Mengine Yatakayotekelezwa na Wizara katika Mwaka wa Fedha 2026/2027

***176. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itatekeleza maeneo mengine yatakayosaidia kuboresha zaidi ufanisi wa sekta. Utekelezaji huo umejikita zaidi katika kupata taarifa za jiosayansi kwa kufanya tafiti za kina ili kuendana na matarajio ya "***Mining Vision 2030***"; kuendelea na utekelezaji wa ***Programu ya Mining for a Brighter Tomorrow - MBT*** kwa ajili ya kuwainua wachimbaji ikiwemo wanawake, vijana na makundi yenye uhitaji maalum; kuwajengea uwezo Wataalamu kwenye maeneo muhimu katika Sekta ya Madini; kuboresha usimamizi wa shughuli za madini kidigitali (Mineral Trade Digitization); na usimamizi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

### (i) *Mining Vision* 2030: Madini ni Maisha na Utajiri

***177. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini itaendelea na utekelezaji wa "***Mining Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri***" inayoweka matamanio ya kuwa na usimamizi thabiti na endelevu wa rasilimali madini ili kukuza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; na kuboresha maisha ya watanzania kupitia shughuli za madini.

***178. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara kupitia GST inatarajia kufanya tafiti za kina za jiosayansi ikiwemo utafiti wa kina wa jiofizikia *(High Resolution Airborne Geophysical Survey)*. Utafiti huo unatarajia kuongeza taarifa za kina za jiofizikia kutoka asilimia 16 ya sasa hadi kufikia asilimia 34. Aidha, katika utekelezaji wa *Mining Vision 2030* Serikali itaendelea na jitihada za tafiti za kina ili angalau kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2030. Taarifa hizi zitaongeza uelewa wa jiolojia ya nchi yetu na hivyo kuvutia na kuboresha mazingira ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuchochea ufungamanishaji na sekta nyingine za kiuchumi hususan Sekta za Viwanda, Kilimo, Ujenzi, Fedha na nyingine zinazotoa huduma kwenye Sekta ya Madini.

"Mheshimiwa Spika, binafsi nikushukuru wewe na Bunge lako Tukufu kwa kuniunga mkono katika kuhakikisha utafiti wa kina wa madini unafanyika katika nchi yetu kwa kiasi kikubwa"

**(ii) Programu ya *Mining for a Brighter Tomorrow*– MBT**

***179. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini itaendelea kutekeleza Programu ya MBT kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2025 hadi 2030. Programu hii ni ya mageuzi katika Sekta ya Madini ambayo imeanzishwa kwa ajili ya kuboresha ushiriki wa wachimbaji wadogo ikiwemo wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum katika fursa zilizopo kwenye mnyororo wa thamani wa madini.

***180. Mheshimiwa Spika,*** Programu ya MBT inatarajiwa kuwa na matokeo yafuatayo: kuongeza ushiriki wa vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum kwenye Uchumi jumuishi kupitia Sekta ya Madini na kuwawezesha kupata kipato na kuwaongezea fursa za ajira.

**(iii) Kuwajengea Uwezo Wataalam kwenye Maeneo Muhimu katika Sekta ya Madini**

***181. Mheshimiwa Spika,*** ili kukidhi mahitaji ya rasilimali watu katika shughuli za madini na uhitaji wa teknolojia mahsusi katika mnyororo wa thamani wa madini nchini, Wizara imetenga fedha za kuwajengea uwezo wataalam katika Sekta ya Madini kwa kuwasomesha ndani na nje ya nchi kupitia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu. Mafunzo hayo yatajikita zaidi katika fani za ukadiriaji wa mashapo (resource estimation), modeli za kifedha (financial modelling), ukaguzi wa fedha na rasilimali madini, uthaminishaji wa madini na uongezaji thamani madini ikiwemo madini ya vito, madini muhimu na madini mkakati.

**(iv) Kuboresha Usimamizi wa Shughuli za Madini Kidijitali**

***182. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na hatua za ukamilishaji wa ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Sekta ya Madini Kidijitali utakaojulikana kama "*Mineral Sector Management Information System* (MSMIS)". Mfumo huu unalenga kuimarisha

usimamizi, uratibu na upatikanaji wa taarifa za Sekta ya Madini kwa kutumia teknolojia za kidijitali, sambamba na jitihada za Serikali za kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za umma. Mfumo huo utaunganishwa na mifumo mingine ya Serikali ili kuongeza ufanisi katika usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za madini na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**(v) Usimamizi wa Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi**

***183. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itaendelea kutekeleza yafuatayo: kufuatilia uzingatiwaji wa masuala ya usalama, afya na utunzaji wa mazingira katika maeneo ya migodi na mitambo ya uchenjuaji wa madini nchini; kuratibu tathmini ya kimkakati ya mazingira ya sekta na kupitia Mpango Kazi wa Mazingira wa Sekta ya Madini 2025 – 2030; kuendeleza kampeni za uhamasishaji na elimu kwa wachimbaji wa madini kuhusu masuala ya usalama, afya na utunzaji wa mazingira; kufuatilia uwekaji dhamana za urejeshaji wa mazingira na maandalizi ya mipango ya ufungaji migodi nchini; na kuendelea kusimamia Sekta ya Madini ipasavyo ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Shughuli za usimamizi na utunzaji wa mazingira zitasimamiwa kwa kuzingatia Nguzo Na. 3 ya DIRA 2050, Sheria ya Madini Sura 123 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191.

***184. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itatekeleza Mpango Kazi wa Mazingira wa Sekta ya Madini 2025 – 2030 (Mineral Sector Environmental Action Plan – MSEAP) ambao unazingatia Mpango Kazi wa Taifa wa Usimamizi wa Mazingira (National Environmental Action Plan - NEAP) na DIRA 2050. Lengo kuu la Mpango huu ni kujumuisha kanuni za Mazingira, Jamii na Utawala Bora (Environmental, Social and Governance - ESG) katika upangaji, usimamizi na uangalizi wa udhibiti wa Sekta ya Madini nchini, ili kuhakikisha kuwa maendeleo ya rasilimali madini yanachangia ukuaji wa uchumi endelevu bila kuathiri usalama wa mazingira na ustawi wa jamii.

## III. Kazi Zitakazotekelezwa na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

### (i) Tume ya Madini

***185. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Tume ya Madini imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

#### a) Utoaji na Ufuatiliaji wa Leseni za Madini

***186. Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha Sekta ya Madini inaendelea kuchangia katika Pato la Taifa ipasavyo, Tume ya Madini itaendelea kutoa leseni kwa ajili ya shughuli mbalimbali za madini na kufuatilia uendelezaji wa leseni hizo. Tume ya Madini itaendelea kusimamia Sheria ya Madini, ikiwemo kusimamisha au kufuta leseni kwa wamiliki ambao watakiuka masharti ya kisheria. Aidha, Tume ya Madini itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Vilevile, Tume ya Madini itaendelea kufanya uboreshaji wa huduma za utoaji wa leseni ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini.

#### b) Kuimarisha Usimamizi wa Shughuli za Madini na Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

***187. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini itaendelea kuimarisha usimamizi ili kuhakikisha kwamba migodi mikubwa na ya kati ambayo imepewa leseni inaanza uzalishaji; kuimarisha usimamizi katika masoko ya madini na vituo vya ununuzi wa madini nchini; kuendelea kudhibiti vitendo vya utoroshwaji wa madini nchini; kutanua wigo wa usimamizi wa uzalishaji wa madini ya ujenzi na madini ya viwandani; kuimarisha mifumo ya TEHAMA; kuendelea kufanya tafiti za kuibua vyanzo vipya vya mapato; na kuimarisha ukaguzi wa hesabu za fedha na kodi kwenye Sekta ya Madini ili kuhakikisha kuwa Serikali inapata mapato stahiki.

#### c) Kuimarisha Ukaguzi wa Afya, Usalama, Mazingira na Uzalishaji wa Madini

***188. Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kunakuwa na shughuli za uchimbaji madini endelevu, Tume ya Madini

itaendelea kufanya kaguzi za usalama, afya na mazingira katika migodi midogo, ya kati na mikubwa. Aidha, kaguzi hizo zitahusisha mabwawa ya kuhifadhia topetaka (TSF), sehemu ya kuhifadhia miambataka (*Waste Rock Dump* -WRD) na maghala ya kuhifadhia baruti. Vilevile, Tume ya Madini itaendelea kusimamia uwasilishaji na utekelezaji wa mipango ya uendelezaji na ufungaji migodi.

***"Serikali itaendelea kuchukua hatua stahiki kuhakikisha wachimbaji wanafuata taratibu za uchimbaji salama ili kuepuka ajali zisizo za lazima na ambazo zinaweza kuzuilika"***

**d) Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini (Local Content) na Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii (CSR)**

***189. Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia Ushirikishwaji wa watanzania katika Sekta ya Madini, Tume ya Madini itaendelea kutekeleza na kuhakikisha kuwa kampuni zinazomiliki leseni za madini zinanunua bidhaa na huduma zinazopatikana nchini.

***190. Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha Ushirikishwaji wa Watanzania kwenye Sekta ya Madini, Tume ya Madini itaendelea kutangaza orodha ya huduma na bidhaa zinazotakiwa kutolewa na kampuni zinazomilikiwa na Watanzania kwa asilimia 100. Aidha, Tume ya Madini itaendelea kusimamia wamiliki wa leseni za madini nchini kutimiza takwa la uwajibikaji kwa jamii (CSR).

***"Ni marufuku kwa mtu ambaye si Mtanzania kusambaza bidhaa au kutoa huduma zilizotangazwa kufanywa na Watanzania kwa asilimia mia moja"***

**e) Kuboresha Mazingira ya Utendaji Kazi na Kuwajengea Uwezo Watumishi**

***191. Mheshimiwa Spika,*** ili kujiimarisha katika utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Tume ya Madini imepanga kununua vitendea kazi na ujenzi wa majengo ya ofisi, ambapo itaendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi za Afisa Madini wakazi tatu (3) ambazo ni Mahenge, Rukwa

na Songwe; Ukarabati wa majengo ya Ofisi za Afisa Madini Wakazi Morogoro, Mtwara na Mbeya; ununuzi wa vitendea kazi vikiwemo magari (25), kompyuta (300), pikipiki (100) na vifaa vya masoko ya madini ikijumuisha XRF 40 na mizani 20; ununuzi wa vifaa vya ukaguzi wa migodi na mazingira; pamoja na ujenzi wa mfumo wa Kanzidata ya Madini.

***192. Mheshimiwa Spika,*** Ili kuhakikisha Tume ya Madini inatekeleza majukumu yake ipasavyo, itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu (70) na muda mfupi (170) katika kada mbalimbali kwa kuzingatia uhitaji uliopo. Aidha, Tume ya Madini itajaza nafasi kwa njia ya uhamisho (2) na ajira mpya (2).

**(ii) Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)**

***193. Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, GST imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

**a) Kufanya Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Kanzidata ya Taifa ya Taarifa za Miamba na Madini**

***194. Mheshimiwa Spika,*** GST itafanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege na ugani wa jiolojia na jiokemia katika QDS mbili (QDS 239 na 240) zilizopo Wilaya za Rufiji na Kilwa na kuchora ramani zake. QDS hizo ni miongoni mwa QDS 11 zilizobakia nchini bila kuchorewa ramani ya jiolojia ili kukamilisha asilimia 100 ya utafiti wa jiolojia ya utambuzi wa miamba kutoka asilimia
97 ya sasa na utafiti maalumu kwa ajili ya kutambua maeneo yenye Madini Muhimu na Madini Mkakati.

***195. Mheshimiwa Spika,*** GST itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Mfumo wa Kanzidata ya Taifa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kukamilika kwa mfumo huo kutaongeza usalama wa taarifa za jiosayansi na utarahisisha uhifadhi na usambazaji wake kwa wadau. Aidha, GST itachora ramani 25, kuhariri na kudurufu ramani 30 na kuchakata picha za satelaiti kwa ajili ya kuwezesha shughuli za ugani; na kuingiza taarifa/machapisho 500 katika mfumo wa digitali.

***196. Mheshimiwa Spika,*** GST itakusanya, itahakiki na kutathmini uhalisia wa taarifa na takwimu za jiosayansi kutoka kwa wamiliki wa leseni 40 za utafutaji na uchimbaji madini nchini; kuhuisha Kanzidata ya Rasilimali Madini ya Taifa pamoja na Kitabu cha Madini Yapatikanayo Tanzania; kukusanya na kuchakata taarifa za miamba choronge mita 1,000 kutoka kwa wamiliki wa leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini.

**b) Kuwajengea Uwezo Wachimbaji Wadogo**

***197. Mheshimiwa Spika,*** katika kuwajengea uwezo wachimbaji wadogo, GST inalenga kufanya utafiti wa jiosayansi katika eneo litakalotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo kwa kutumia vifaa vya kisasa ikiwemo ndege nyuki (drone) ili kupata taarifa za kina za jiofizikia kwa lengo la kubaini sehemu zenye viashiria vya uwepo wa madini katika eneo hilo. Aidha, GST itatoa mafunzo kuhusu kutambua ulalo, mwelekeo, tabia za mbale kwa uchenjuaji katika mikoa minne (4) ambayo ni Rukwa, Katavi, Kigoma na Kagera yenye shughuli hai za uchimbaji mdogo wa madini.

**c) Kuboresha Huduma za Maabara**

***198. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma za maabara, GST itaendelea kufanya uchunguzi wa sampuli mbalimbali kwa kuzingatia vigezo vya ithibati (accreditation). Aidha, GST itaendelea na ujenzi wa maabara mpya ya kisasa ya uchunguzi wa madini (State of the Art Geoscientific Laboratory) katika eneo la Kizota Dodoma. Vilevile, GST itaendelea na ujenzi wa maabara za kanda katika mikoa ya kimadini ya Chunya na Geita ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vyake kwa lengo la kusogeza karibu huduma kwa wananchi wanaojihusisha na shughuli za madini.

***199. Mheshimiwa Spika,*** GST itaendelea kutengeneza vyungu (crucibles and cupels) 250,000 kwa ajili ya kuwezesha uchunguzi wa sampuli za miamba na udongo hususani dhahabu. Aidha, GST itafanya uchunguzi wa sampuli 25,000 za udongo, miamba na madini na uandaaji wa sampuli rejea za ndani (internal certified reference materials) za dhahabu, shaba, fedha, zinki, chuma na *cobalt*.

**d) Ufuatiliaji na Kuelimisha Umma Kuhusu Majanga ya Asili ya Jiolojia**

***200. Mheshimiwa Spika,*** GST itakusanya na kuchakata taarifa kutoka vituo vinne (4) vya kudumu vya kunakili mienendo ya mitetemo vilivyopo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Geita na Mbeya. Aidha, GST itahuisha ramani inayoonesha vitovu vya matetemeko ya ardhi nchini. Sambamba, na hilo, GST itafanya matengenezo kinga ya vifaa vya kunakili mitetemo. Vilevile, GST itaendelea kutoa elimu kwa umma kwa njia ya machapisho, semina na vyombo vya habari kuhusu namna bora ya kujikinga na kupunguza athari za majanga ya asili ya jiolojia.

**e) Kuwajengea Uwezo Watumishi wa GST katika Kutekeleza Majukumu**

***201. Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uwezo wa Taasisi katika kutekeleza majukumu yake, GST itaboresha mifumo ya ndani ya uchakataji, uhifadhi, usambazaji wa taarifa, takwimu za jiosayansi na taarifa za uwepo wa madini. Aidha, GST itawajengea uwezo watumishi 30 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani mbalimbali ikiwemo masuala ya maabara.

***202. Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi, GST itaendelea na taratibu za ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo helikopta na ndege nyuki (drone) kwa lengo la kuongeza kasi ya kufanya utafiti wa kina wa madini nchini ikiwemo maeneo ya wachimbaji wadogo. Aidha, taasisi itanunua vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa sampuli za madini mbalimbali yakiwemo ya kimkakati, kukarabati majengo, kukamilisha ujenzi wa maabara kwenye kanda, kuboresha mikakati ya ukusanyaji mapato na usimamizi wa rasilimali watu na fedha.

**(iii) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)**

***203. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, STAMICO imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

**i. Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato**

***204. Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha mapato ya Shirika yanakua na kuimarika, Shirika limepanga kuongeza usimamizi kwenye uwekezaji uliopo katika miradi yake kama ifuatavyo:

**a) Uzalishaji wa Makaa ya Mawe na Nishati Safi ya Rafiki Briquettes**

***205. Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaendelea na uzalishaji wa makaa ya mawe katika eneo la Kabulo-Kiwira ambapo jumla ya tani 600,000 zimepangwa kuchimbwa. Aidha, Shirika linatarajia kukusanya shilingi 19,397,614,979.00 kutokana na uzalishaji huo utakaofanyika. Ili kufanikisha lengo hilo, Shirika limepanga kununua mitambo na vifaa mbalimbali vikiwemo *bull-dozer D8* (1), *longwall coal shearer* (2), *chain conveyor* (8), *hydraulic prop (1), underground and pit communication* (1) na *excavator* (1).

***206. Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaendelea na uzalishaji wa Nishati Safi ya *Rafiki Briquettes* kwa kutumia mitambo yake minne (4) ya Kisarawe, Kiwira, Chigongwe na Tabora na kuanza usimikaji wa mtambo mwingine katika Mkoa wa Geita. Kupitia mitambo hiyo, Shirika linatarajia kuzalisha jumla ya tani 25,470 za nishati safi zenye thamani ya shilingi 19,416,000,000.00.

**b) Kuimarisha Shughuli za Uchorongaji**

***207. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za uchorongaji kwa kutangaza huduma hizo na kutafuta kandarasi ndani na nje ya nchi pamoja na kununua mitambo mitatu (3) na vifaa vya uchorongaji. Shirika linakadiria kufanya uchorongaji wa mita 196,980 zenye thamani ya shilingi 89,823,450,000.00.

**c) Uzalishaji wa Kokoto - Chigongwe**

***208. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Shirika limepanga kuzalisha mita za ujazo 94,400 za kokoto katika mradi wa Chigongwe. Uzalishaji huo unatarajiwa kuliingizia Shirika mapato ya shilingi 3,350,400,000.00. Aidha, katika kuhakikisha

kunakuwa na soko la kokoto, Shirika limeendelea kufanya mazungumzo na kampuni mbalimbali kubwa za ujenzi katika miradi ya Serikali ikiwemo majengo, barabara, reli, viwanja vya mpira na viwanja vya ndege.

### ii. Kuwezesha Shughuli za Uchimbaji Mdogo na Kuimarisha Vituo vya Mfano

***209. Mheshimiwa Spika,*** STAMICO itaendelea kuwezesha wachimbaji wadogo kwa kufanya yafuatayo: kuendelea kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa vituo vya mfano vya Itumbi, Lwamgasa na Katente pamoja na mitambo 15 ya uchorongaji; kuendelea na uzalishaji katika mgodi wa mfano Lwamgasa; kuanza uzalishaji katika kiwanda cha chumvi kilichopo Mkoa wa Lindi; kukamilisha upanuzi wa Kituo cha mfano cha Katente; na kusimika mitambo miwili (2) ya uchenjuaji yenye uwezo wa kuchakata tani 120 za mbale ya dhahabu kwa siku kwa kila mtambo katika eneo la wachimbaji wadogo la Mwakitolyo - Shinyanga na Buhemba - Mara.

***210. Mheshimiwa Spika,*** Shirika limepanga kuzindua na kuanza kutumia mfumo wa usajili wa wachimbaji wadogo. Mfumo huu utawawezesha wachimbaji wadogo kupata taarifa za masoko, wasambazaji wa vifaa, malipo na kupata taarifa za kila siku za usajili wa wachimbaji wadogo wapya.

### iii. Kuendeleza Leseni za Madini za Shirika

***211. Mheshimiwa Spika,*** Shirika limepanga kuendelea na utafiti kwenye leseni moja (1) ya dhahabu iliyopo Wilaya ya Bukombe Mkoani Geita ambapo utafiti wake pamoja na taarifa ya upembuzi yakinifu utakamilika ifikapo Juni 2027. Vilevile, Shirika litaendelea na utafiti wa madini ya Kinywe katika leseni mbili (2) zilizopo Wilaya ya Ruangwa na Nachingwea, Mkoani Lindi pamoja na leseni tatu (3) za madini ya shaba zilizopo Katavi.

### iv. Miradi ya Ubia na Kampuni Tanzu

***212. Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaimarisha uendelezaji wa miradi ya ubia ambayo ni Mgodi wa Buckreef, Kiwanda cha

Kusafisha Dhahabu Mwanza, Mgodi wa Uchimbaji wa Madini ya Nikeli wa Ntaka pamoja na Kampuni tanzu ya STAMIGOLD ili kuongeza ufanisi na kuwezesha ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye miradi hiyo.

***213. Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaendelea kuiwezesha STAMIGOLD kufanya utafiti unaolenga kuongeza thamani ya matokeo ya utafiti wa awali pamoja na uhakiki wa uwepo wa mashapo katika leseni ya SML 157/2003 na PL 13075/2024 kwa lengo la kuongeza uhai wa mgodi huo.

**v. Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi**

***214. Mheshimiwa Spika,*** Shirika linatambua umuhimu wa kuwa na rasilimaliwatu pamoja na mazingira bora ya utendaji kazi. Shirika limepanga kuendelea kujaza nafasi wazi, kununua vitendea kazi na kuwaendeleza watumishi katika kada mbalimbali kwa kuzingatia uhitaji uliopo. Shirika linatarajia kujaza nafasi wazi 16 za watumishi kwa utaratibu wa uhamisho na ajira mpya. Aidha, watumishi 50 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi na wanne (4) ya muda mrefu. Vilevile, Shirika litaendelea kusimamia na kuhakikisha maslahi na stahiki za watumishi zinapatikana kwa wakati. Kadhalika, Shirika litajenga jengo la Makao Makuu lenye ghorofa 10 jijini Dodoma.

**(iv) Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)**

***215. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, TGC imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

**a) Utoaji Mafunzo ya Uongezaji Thamani Madini**

***216. Mheshimiwa Spika,*** TGC itaendelea kutoa mafunzo katika programu tatu (3) kwa ngazi ya Stashahada katika teknolojia za madini ya vito na usonara; kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za utambuzi wa madini ya vito, usonara, utengenezaji wa bidhaa za mapambo na urembo zinazotokana na miamba na vito na usanifu madini ya vito; na kufanya uhamasishaji kuhusu masuala ya uongezaji thamani madini ya vito katika shule za msingi na sekondari.

**b) Uzalishaji wa Bidhaa za Madini Zilizoongezwa Thamani**

***217.*** ***Mheshimiwa Spika,*** TGC imepanga kuzalisha na kuuza bidhaa za usonara na ukataji wa madini ya vito 1300, bidhaa za usonara 1400, bidhaa za miamba 7200, Shanga 7500. Bidhaa hizo zinatarajiwa kuwa na thamani ya shilingi 135,000,000.00

**c) Huduma za Upimaji wa Sampuli za Madini ya Vito**

***218.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuongeza ufanisi wa huduma za maabara TGC imepanga kuimarisha ufanisi wa maabara ambapo itaboresha huduma za upimaji wa madini ya vito hadi kufikia uwezo wa kupima sampuli 1200 kwa mwaka.

**d) Utafiti wa Madini ya Vito na Metali**

***219.*** ***Mheshimiwa Spika,*** TGC kwa kushirikiana na Taasisi ya Jemolojia ya Nchini Thailand (GIT) imepanga kufanya utafiti wa ubora na viwango vya madini ya Tanzanite. Tafiti hizi zitaongeza ubunifu na tija katika shughuli mbalimbali za uongezaji thamani kwa madini ya vito na metali.

**e) Kuwajengea Uwezo Watumishi na Kuboresha Mazingira ya Kazi**

***220.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuongeza idadi ya wakufunzi waliobobea katika fani za jemolojia, usonara na ukataji na ung'arishaji madini ya vito, TGC itawawezesha watumishi saba (7) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi. Lengo ni kuendelea kuwajengea uwezo katika maeneo yao ya utekelezaji wa majukumu. Aidha, TGC imepanga kununua mashine na vifaa mbalimbali kwa ajili ya karakana za mafunzo na uchakataji madini pamoja na ununuzi wa gari moja (1).

***221.*** ***Mheshimiwa Spika,*** TGC itaendelea na usimamizi wa ujenzi wa Jengo la ghorofa 8 (Twin Tower Building). Jengo hili litakuwa na miundombinu mbalimbali ikiwemo madarasa, karakana za uongezaji thamani madini, maabara ya kisasa ya madini ya vito na bidhaa za usonara, *mineral gallery*, ofisi, mabweni kwa ajili ya wanafunzi, kantini na maduka.

**(v) Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)**

***222. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, TEITI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

**a) Kuandaa na Kuweka Wazi Taarifa ya 17 ya TEITI ya Mwaka wa Fedha 2024/2025**

***223. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya TEITI itaandaa na kuweka wazi taarifa ya 17 ya TEITI ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 ya ulinganishi wa malipo ya kodi na tozo kutoka kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato yaliyopokelewa na Serikali. Uandaaji wa taarifa hiyo ni utekelezaji wa vigezo vya uwazi na uwajibikaji vya mwaka 2023 ambapo nchi wanachama wa EITI hutakiwa kuandaa na kuweka wazi taarifa husika kila mwaka. Vilevile, utekelezaji wa takwa hili ni kwa mujibu wa Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia, Sura 447.

**b) Kuweka Wazi Mikataba ya Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia**

***224. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya TEITI itaendelea kuweka wazi mikataba ambayo Serikali imeingia na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia hapa nchini ikiwa ni utekelezaji wa Sheria inayosimamia majukumu ya TEITI pamoja na utekelezaji wa Matakwa ya Kimataifa ya EITI.

**c) Kuweka Wazi Orodha ya Wamiliki wa Hisa katika Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia**

***225. Mheshimiwa Spika,*** TEITI itaendelea kuweka wazi majina ya wamiliki wa hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia (Beneficial ownership disclosure) kupitia ripoti zake za kila mwaka. Aidha, TEITI inakamilisha uandaaji wa rejista ya uwekaji wa majina ya wamiliki wa hisa ikiwa ni utekelezaji wa matakwa ya Kimataifa ya Uwazi na Uwajibikaji katika rasilimali madini, mafuta na gesi asilia (EITI Standard, 2023).

**d) Kutoa Elimu kwa Umma Kuhusu Matumizi ya Takwimu Zinazotolewa Kwenye Ripoti za TEITI**

***226.*** ***Mheshimiwa Spika,*** TEITI itaendelea kutoa elimu kwa umma kwa kuwafikia wadau ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi, kufanya warsha katika maeneo ambapo shughuli za uchimbaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia zinatekelezwa, na kufanya vipindi vya redio na runinga ili kutangaza majukumu ya taasisi na kuhamasisha matumizi ya takwimu zinazotolewa kwenye taarifa za TEITI. Lengo ni kuongeza uelewa kwa wananchi na wadau juu ya mapato na matumizi yatokanayo na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia.

**e) Kuwajengea Uwezo Watumishi**

***227.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuhakikisha TEITI inatekeleza majukumu yake ipasavyo, itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi wanne (4) na muda mfupi 12 katika kada mbalimbali kwa kuzingatia uhitaji uliopo.

**f) Kufanya Tafiti za Namna Wananchi Wanavyonufaika na Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia**

***228.*** ***Mheshimiwa Spika,*** TEITI itaendelea kufanya utafiti kuhusu utekelezaji wa sheria katika eneo la Ushirikishwaji wa Watanzania (Local Content) katika Sekta ya Uziduaji na Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (Corporate Social Responsibility - CSR) katika Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia. Aidha, TEITI itaendelea kufanya tafiti katika Sekta ya Uziduaji ili kuishauri Serikali namna bora ya kuboresha usimamizi wa Sekta ya Uziduaji.

**g) Utekelezaji wa Vigezo vya EITI Nchini**

***229.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2023 Tanzania ilifanyiwa tathmini ya utekelezaji wa vigezo vya EITI ambapo ilipata hadhi ya daraja la *moderate* kwa kiwango cha asilimia 77. Taasisi hii ya EITI ndio taasisi yenye jukumu la Kimataifa la kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Uziduaji kwa nchi wanachama ikiwemo Tanzania. Taasisi hiyo imepanga kufanya tathmini ya nne (4) kwa

TEITI Mwezi Januari, 2027. Aidha, tathmini hiyo itapima utekelezaji wa vigezo vya EITI. Ili kukamilisha tathmini hiyo, TEITI itafanya maandalizi husika.

## E. SHUKRANI

***230. Mheshimiwa Spika,*** natambua wazi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na juhudi kubwa za kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi yetu unaimarika. Kasi, juhudi na ubunifu mkubwa wa utendaji kazi anaoendelea nao **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** vinachochea kukua kwa maendeleo ya nchi yetu.

***231. Mheshimiwa Spika,*** kipekee nitumie fursa hii kumshukuru tena kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo anayotupatia katika Sekta ya Madini ambayo yanaifanya sekta hii kuendelea kukua kwa kasi na kuvutia wawekezaji kwa manufaa ya Taifa.

***232. Mheshimiwa Spika,*** nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa **Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa maelekezo na miongozo ambayo amekuwa akiitoa kwa Sekta ya Madini ili kuimarisha usimamizi na utendaji wa shughuli mbalimbali za sekta kwa manufaa ya Taifa.

***233. Mheshimiwa Spika,*** napenda pia nimshukuru **Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa usimamizi wake makini wa shughuli za kila siku za Serikali.

***234. Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru wadau wa Sekta ya Madini wakiwemo Chemba ya Migodi, FEMATA, TAWOMA, TAMIDA, CHAMMATA, WIMA, TWIMI, TAMISA na vyama vingine vya wachimbaji madini, watafutaji, wachimbaji, wamiliki wa mitambo ya uchenjuaji, uyeyushaji na usafishaji madini, wafanyabiashara wa madini na watoa huduma kwa kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi. Hii imerahisisha usimamizi wa Sekta ya Madini.

***235. Mheshimiwa Spika,*** nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitazishukuru taasisi za fedha hususan mabenki kwa kuendelea kuwapa mikopo wadau wa Sekta ya Madini wakiwemo wachimbaji wakubwa, wa kati na wadogo. Vilevile, nivishukuru Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kutuhakikishia usalama na kushirikiana nasi katika kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini kwenye maeneo yenye shughuli za madini bila kusahau vyombo vya habari kwa ushirikiano wanaotupatia katika kuitangaza Sekta ya Madini.

***236. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka migodi na watanzania wote kwa ujumla kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa wawekezaji katika maeneo yao. Hakika wamekuwa sehemu ya mafanikio ya Sekta ya Madini nchini.

## F. HITIMISHO

***237. Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya shilingi 1,406,006,031,000.00 naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha makadirio ya shilingi 174,983,580,000.00 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa mchanganuo ufuatao:

(i) shilingi 71,507,708,000.00 sawa na asilimia 40.87 ya bajeti yote ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

(ii) shilingi 103,475,872,000.00 sawa na asilimia 59.13 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 27,365,095,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi (PE) na shilingi 76,110,777,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ya Wizara na Taasisi zake.

***238. Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini vimeambatishwa pamoja na hotuba hii. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Madini kwa kikoa cha *https://www.madini.go.tz.*

***239. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuna tangazo la mgeni moja wa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ambaye ni Ndugu Bina, Rais wa Shirikisho la Wachimbaji Wadogo wa Madini *FEMATA*. Karibu sana. Karibu sana Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamwita Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini aweze kutoa maoni ya Kamati. Kwa niaba yake Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, karibu. *(Makofi)*

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi, maelezo ya awali. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuturuzuku uhai na afya njema na kutuwezesha Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya nchi kwa kutoa ushauri kwa Wizara ya Madini na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninakushukuru kwa kunipa nafasi niwasilishe taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Fungu Na. 100 Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 121(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ya Mwaka 2025 na imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo:

(a) Sehemu ya kwanza ni utangulizi na inaeleza kuhusu misingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake. Sehemu ya pili inaeleza kuhusu uchambuzi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Sehemu ya tatu ni uchambuzi kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Sehemu ya nne ni maoni na mapendekezo ya Kamati na sehemu ya tano ni hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitelekeza majukumu yake kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini wa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Kamati ilifanya yafuatayo:-

(a) Kupokea na kufanya uchambuzi wa randama ya Wizara Kanuni 118(1);

(b) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026, Kanuni ya 120(1);

(c) Kujadili utekelezaji wa bajeti ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na

(d) Kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Nabu Spika, matokeo ya uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Fungu Na. 100 yaani Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha, 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi na mawanda ya uchambuzi. Ibara ya 63 Kifungu cha 3(b) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inalipa Bunge madaraka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti. Kwa muktadha huo Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti kwa Kamati za kisekta kufanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi za Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia msingi wa uchambuzi, Kamati ilichambua taarifa za utekelezaji wa fungu Na. 100 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na kufanya ulinganisho na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa mujibu wa Kanuni Na. 120(2).

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Madini ilitengewa bajeti ya jumla ya shilingi 224,984,150,000. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 100.3 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 124.6 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilikuwa imepokea bilioni 74.3 sawa na 33% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, shilingi bilioni 64.1 sawa na 63.9% ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyokuwa imeidhinishwa na shilingi bilioni 10.2 sawa na asilimia nane ya bajeti ya maendeleo kama ambavyo imefafanuliwa na kielelezo namba moja cha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haijaridhishwa na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo

ambayo hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilikuwa imepokea asilimia nane tu ya bajeti ya maendeleo iliyokuwa imeidhinishwa. Upungufu huu wa bajeti unaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji na ukamilishaji wa miradi ya maendeleo ambayo ilipangwa kutekelezwa na Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kwamba mapokezi hafifu ya fedha za maendeleo yanatokana na kutokapatikana kwa mkopo wa shilingi bilioni 53.09 ambao ulikuwa unatoka Serikali *ya Spain*. Mkopo huu ulilengwa kutumiwa na Taasisi ya *GST* ili kutekeleza mradi wa utafiti wa madini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati kwa Serikali kuhakikisha kwamba inaweka kipaumbele kutenga fedha za ndani katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wizara hii na taasisi zake. Hali hii itasaidia bajeti ya maendeleo kutoathiriwa na changamoto za kukosekana au kuchelewa kwa fedha za washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo ya maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Madini iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya trilioni 1.4 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni pamoja na mapato mengineyo, ada za mwaka, ada za ukaguzi wa madini, mirabaha, ada za kijiolojia, adhabu na faini za malimbikizo mbalimbali ya ada, malipo ya huduma za maabara, *HIT Levy* pamoja na makusanyo ya maduhuli kutoka kwenye taasisi zake ambazo ni *STAMICO*, *GST* na *TGC*. Aidha, katika makadirio hayo ya makusanyo ya maduhuli kiasi cha shilingi trilioni 1.2 kilipangwa kuwasilishwa Hazina na kilichobaki ambacho ni shilingi bilioni 205 zilipangwa kutumiwa na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2026 makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 880.7 sawa na 109.5% ya malengo waliokuwa wamejiwekea ya miezi minane yaani Julai, 2025 hadi Februari, 2026. Mchanganuo wa mwenendo wa makusanyo kama yalivyofafanuliwa katika vielelezo namba mbili na namba tatu vilivyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wastani wa mwenendo wa makusanyo Fungu Na. 100 yaani Wizara ya Madini katika mwaka wa fedha 2025/2026, ni wa kuridhisha kwa kuwa hadi kufikia 2026 ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa umevuka lengo lililokuwa limekusudiwa. Kamati ilielezwa kwamba kuvuka kwa lengo hilo kulitokana na kuongezeka kwa ukusanyaji kutokana na vyanzo vyake ambavyo vimeainishwa katika kielelezo namba mbili cha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata ufafanuzi wa taasisi zilizo chini ya Wizara kutofikia lengo la ukusanyaji wa maduhuli kama ilivyoainishwa kwenye taarifa yetu ambayo imeingia katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Wizara kwa kuvuka lengo la ukusanyaji wa maduhuli hadi kufikia Februari, 2026. Aidha, ni ushauri wa Kamati kwa Serikali kuhakikisha kwamba taasisi zilizo chini ya Wizara zinafikia lengo la ukusanyaji wa maduhuli kwa kuwa sababu zilizochangia kutofikia malengo kwa kiasi kikubwa zimeshatatuliwa ikiwemo ujenzi wa *Kiwanda cha Rafiki Coal Briquette*, Mkoani Tabora. Kukamilika na kufungwa kwa mitambo ya *coal briquettes* Jijini Dodoma kufikia 80%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Madini ilitengewa jumla ya bilioni 103.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha hizo zilijumuisha bilioni 24.2 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara na bilioni 76.1 kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2026 jumla ya fedha matumizi ya kawaida zilizokuwa zimetolewa ni shilingi bilioni 64.1 sawa na 64% ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyokuwa imeidhinishwa. Kati ya fedha hizo bilioni 15.4 zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 48.7 kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* kama ambavyo inaonekana katika kielelezo namba nne cha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida kwa

Fungu Na.mba 100 yaani Wizara ya Madini na pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha ambazo zinasaidia Wizara na Watendaji wake kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Madini ilitengewa jumla ya fedha bilioni 124.6 ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 71.5 zilikuwa ni fedha ndani na shilingi bilioni 53.09 zilikuwa ni fedha za nje. Mwenendo wa mapokezi ya fedha za maendeleo unafafanuliwa katika kielelezo namba tano cha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haijaridhishwa na mapokezi ya fedha za maendeleo kwa Fungu Na. 100. Hadi kufikia Februari, 2026 jumla ya fedha zilizokuwa zimepokelewa ni asilimia nane tu ya bajeti ya maendeleo iliyokuwa imeidhinishwa. Mapokezi ya fedha ndani ni sawa na wastani wa 14% na kwa upande wa fedha nje hakuna fedha yoyote iliyokuwa imepokelewa. Hali hii inaleta mashaka kwenye utendaji wa Wizara hii ambayo kupitia taasisi zake imekuwa ni kinara katika ukusanyaji wa maduhuli na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ushauri wa Kamati kwa Serikali kuhakikisha kwamba inakuwa na vyanzo vya ndani ambavyo ni vya uhakika vitakavyoiwezesha Wizara kutekeleza miradi ya maendeleo iliyokusudiwa. Kutokupatikana kwa fedha za maendeleo kunaweza kuathiri mpango kazi na utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara ikizingatia mchango wa sekta ya madini katika kuongeza pato la Serikali kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 120(1), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kati ya Tarehe 12 - 18 Machi, 2026 katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Geita. Katika ziara hiyo Kamati ilifanya tathmini ya baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Tathmini iliyofanyika ilijumuisha uchambuzi wa mapokezi ya fedha, hali ya utekelezaji wa miradi husika na changamoto za utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa mustakabali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Na. 1119; Mradi wa Ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza mkaa mbadala wa kupikia Tabora. Mradi huu ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa na Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* kwa lengo la kutanua wigo wa matumizi ya makaa ya mawe kama nishati safi ya kupikia ijulikanayo kama *Rafiki Briquettes*.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za mradi huu ni takribani shilingi bilioni 3.03 ikihusisha gharama za ununuzi wa mtambo wenye uwezo wa kuzalisha mkaa mbadala tani 20 kwa saa, usafirishaji, ujenzi na ukarabati wa jengo ambalo lilitolewa na Chama cha Ushirika cha Wakulima wa Tumbaku Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kwamba malengo ya kuanzishwa kwa mradi huu kwa Mkoa wa Tabora ni kutoa suluhusho la kudumu la ukaushaji wa tumbaku ambao kwa kiasi kikubwa umeathiri na kuharibu mazingira kwa mkoa wa Tabora. Aidha, matarajio ya mradi huu ni kuongeza pato la Serikali kupitia kodi na tozo mbalimbali, na pia kutoa ajira kwa vijana na wanawake katika mnyororo wa usambazaji na uuzaji wa nishati hii safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa pongezi kwa juhudi zilizofanywa na *STAMICO* katika kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye matumizi ya nishati safi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na uzalishaji na usambazaji wa bidhaa hiyo ili iweze kuwafikia wahusika, ambao ni wakulima wa Tumbaku, kwa haraka na hivyo kutimiza lengo lililokuwa limekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa upanuzi wa Kituo cha Mfano cha Madini Katente na Bukombe, kimeanzishwa katika eneo la leseni ya uchimbaji mdogo Na. *PML04548MBG*

inayomilikiwa na *STAMICO*. Aidha, leseni hiyo awali ilikuwa inamilikiwa na Ushirika wa Wachimbaji Madini Katente *PML000194*.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za mradi huu zilikuwa shilingi bilioni 1.7 ikihusisha gharama za usimikaji wa mitambo na ununuzi wa vifaa mbalimbali vya uchenjuaji wa dhahabu kama ambavyo imebainishwa kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kuanzishwa kituo hiki ni kuwawezesha wachimbaji wadogo kuchenjua dhahabu kwa njia ya *CIP* ambayo ina ufanisi mkubwa zaidi ikilinganishwa na uchenjuaji wa kutumia *VAT leaching*. Pia kituo hiki kimeanzishwa ili kutoa elimu ya mafunzo kwa vitendo kwa wachimbaji wadogo juu ya namna ya kutumia njia za kisasa za uchenjuaji zenye tija kubwa katika uzalishaji wa dhahabu. Taarifa kuhusu kiasi cha dhahabu iliyochenjuliwa na thamani yake imeanishwa katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kituo hiki Serikali imeweza kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 3.9 ambayo inajumuisha mrabaha, ada ya ukaguzi, tozo za Halmashauri na *TRA* kama ambavyo imeoneshwa kwenye kilelezo namba sita cha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa mradi ambao unaendelea kuleta tija katika uchenjuaji dhahabu kwa wachimbaji wadogo. Ni rai ya Kamati kwa Serikali kupitia *STAMICO* kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wa maeneo ya Bukombe ndio wanakuwa wanufaika zaidi wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upanuzi wa Kituo cha Mfano cha Madini Lwamgasa, Geita. Kituo cha Lwamgasa kimeanzishwa kwenye eneo la uchimbaji mdogo lenye leseni *PML 0013603* na *PML 0013604* ambazo zinamilikiwa na Serikali ya Kijiji cha Lwamgasa kupitia Ushirika wa Wachimbaji Wadogo wa Madini Lwamgasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kituo cha Lwamgasa umegharimu shilingi 1,519,721,034 ikihusisha ujenzi wa kituo,

usimikaji wa mitambo na kazi nyingine mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanzishwa kwake mradi huu umeweza kuzalisha dhahabu zenye *gram* 210,824.34 zenye thamani ya jumla shilingi bilioni 44.9. Pia umeiwezesha Serikali kukusanya mapato shilingi 3,889,337,666.87, ambayo inajumuisha mrabaha, ada ya ukaguzi tozo ya halmashauri na *TRA*, kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba saba cha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, palipo na mafanikio, hapakosi changamoto. Hivyo katika mradi huu Kamati ilibaini baadhi ya changamoto ikiwemo mwamko mdogo wa walengwa ambao ni wachimbaji wadogo katika kutumia kituo hicho kwa shughuli za uchenjuaji wa dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa ujenzi wa jengo la Afisa Madini Mkazi, mkoa wa Geita. Mradi huu unatekelezwa na Wizara ya Madini na unahusu ujenzi wa wa jengo la Ofisi za Afisa Madini Mkazi Mkoa wa Geita. Ujenzi wa jengo hili unagharimu shilingi bilioni 6.2, pamoja na kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)*, ambazo ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kwa kuibua mradi kama huu ambao utasaidia kuboresha utoaji huduma kwa wachimbaji waliopo katika Mkoa wa Geita na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Fungu 100, Wizara ya Madini inalenga kutekeleza vipaumbele mbalimbali vya kibajeti vikiwemo vifuatavyo: -

(a) Ukusanyaji wa maduhuli; Wizara itatekeleza kipaumbele hiki kwa kufanya ukaguzi na usimamizi wa uchimbaji madini na masoko ya vituo vya ununuzi wa madini ili kusaidia na kukomesha vitendo vya utoroshwaji wa madini kwenda nje ya nchi na hivyo nchi kuweza kukusanya mapato kupitia sekta ya madini.

(b) Kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa; Wizara itaendelea kutekeleza hili kwa kuhamasisha na kuwahusisha wachimbaji na wauzaji wa migodi mipya na kuisimamia kwa misingi ya sheria. Aidha, Wizara itasimamia migodi yote nchini kutengeneza ajira kwa wazawa kupitia mnyororo wa uchumi madini *(Local content)* na huduma kwa jamii *(CSR)*.

(c) Taasisi zilizo chini ya Wizara; Wizara itatekeleza kipaumbele hiki kwa kuimarisha utendaji kazi wa taasisi hizo kwa kuzipatia rasilimali fedha, vifaa na watu. Aidha, Wizara itahakikisha Taasisi yake ya *STAMICO* inashiriki kikamilifu kwenye shughuli za madini; *GST* kufanya utafiti mkubwa wa madini ili kubaini maeneo mapya yenye mashapo ya madini; *TGC* kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini; na *TEITI* kupata rasilimali mbalimbali ikiwemo vifaa na vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake.

(d) Wachimbaji wadogo wa madini; kuhamasisha taasisi za fedha kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo, kutoa huduma za mafunzo kupitia vituo vya mfano, kutoa maeneo ambayo yana taarifa za kijiolojia na kuwahamasisha wachimbaji wadogo kushiriki kwenye maonesho ya madini ya vito nchini ili kukuza wigo wa biashara zao.

(e) Uwekezaji kwenye sekta ya madini; itafanya tafiti za majaribio kwa kurusha ndege ili kupata taarifa za jiofizikia na kuzitunza taarifa hizo za jiosayansi kutokana na matokeo ya tafiti hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu muundo wa bajeti, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Madini, Fungu Na. 100 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 174,983,580,000. Kati ya fedha hizo zilizoombwa shilingi bilioni 103.4 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi bilioni 71.5 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha iliyoombwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imepungua kwa wastani wa asilimia 28.57 ikilinganishwa na bajeti ya shilingi 224,984,150,000 iliyotengwa kwa mwaka wa fedha unaoisha. Kielelezo namba nane kinafafanua

kwa muhtsari ulinganisho kati ya bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027, kieleleza namba nane cha taarifa hii kinafafanua.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa bajeti ya Fungu 100 kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni kutokana na kupungua kwa shilingi bilioni 53.097 iliyokuwa ni fedha ya mkopo kutoka Serikali ya Hispania ambayo ilipangwa kutekeleza miradi ya maendeleo. Fedha hizo zilitengewa kutoka kwa wahisani kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 zilipaswa kutumiwa na Taasisi ya *GST* katika kufanya tafiti za madini nchini. Hata hivyo, kama ambavyo kielelezo namba tano kimeonesha, bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imeongezeka kwa shilingi bilioni 24.2 sawa na wastani wa asilimia saba nukta tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya makusanyo, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Madini pamoja na taasisi zake inaidhinishiwa kukusanya maduhuli ya trilioni 1.6, ambayo yatatokana na vyanzo mbalimbali kama ambavyo imeelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uchambuzi, Kamati imebaini kuongezeka kwa makadirio ya ukusanyaji wa Maduhuli ambayo yatakusanywa na kuwasilishwa Hazina. Makadirio hayo yameongezeka kwa shilingi bilioni 206 sawa na 17.6% ikilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha hasa za ndani katika kutekeleza majukumu ya Fungu 100, Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia uongozi wake taasisi imeingia katika ramani ya dunia kama mshindani mkuuwa Soko la Dunia. Hali hii imesaidia kuleta mageuzi katika sekta ya madini na hivyo kuifanya sekta hii kuwa ya pili katika kuchangia pPato la Taifa *(GDP).* Vilevile kupitia uongozi wake, amewezesha nchi yetu kushika nafasi nne kwenye kuvutia uwekezaji wa sekta ya madini Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua na kuthamini mchango wa sekta ya madini nchini, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

(a) Kamati inaishauri Serikali kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa migodi nchini. Serikali itenge fedha za kutosha ili kujenga mifumo thabiti ya kisasa ya *TEHAMA* itakayowezesha usimamizi, ufuatiliaji na ukaguzi wa shughuli za uchimbaji madini. Sambamba na hilo, ihakikishe kwamba inapambana na uchimbaji haramu.

(b) Kuongeza ushirikiano na wadau; Kamati inaushauri Serikali kuendelea kuimarisha ushirikiano na Serikali za Mitaa, sekta binafsi, taasisi za utafiti na jamii zinazozunguka migodi ili kuhakikisha kwamba sekta ya madini inaleta manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi.

(c) Kukamilisha na kupanga utekelezaji wa miradi ya kimkakati. Kamati inashauri kwamba Serikali kupitia Wizara ya Madini na taasisi zake, iendelee kutenga bajeti ya kuanzisha miradi mikubwa ya kimkakati na itakayokuwa na uwezo wa kuchenjua madini kwa njia za kisasa. Sambamba na hilo Serikali isimamie kikamilifu utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati na kwa viwango bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuwa na usimamizi wa kina kwa taasisi zake kwa ukaribu ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yake yote kwa ufanisi. Kamati ina imani kwamba usimamizi madhubuti utawezesha kutoa huduma yenye tija kwa wananchi na wadau wote wa sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni Mahsusi, kuhusu *STAMICO*. Kamati inatambua mchango wa Wizara na taasisi yake ya *STAMICO* katika kuchangia pato la Taifa letu hadi kufikia 10.1% kwa mwaka 2024. Mchango huo una umuhimu kwa wanachi wote wa Tanzania na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuwepo kwa mafanikio hayo, Kamati ina ushauri ufuatao kwa *STAMICO* ili iweze kuendelea kusaidia uchumi wa Taifa letu.

(a) *STAMICO* iendelee na kuzalisha nishati safi ya kuipikia ya kiwanda kilichoko Tabora.

(b) Serikali kupitia *STAMICO* itazame uwezekano wa kujenga kiwanda kama hicho katika maeneo mengine ya Mkoa wa Tabora ili kutimiza lengo la kuwasaidia wakulima wa tumbaku Mkoani Tabora. Sambamba na hilo, *STAMICO* itumie wakandarasi wazawa katika kutekeleza miradi mingine inayofanana na huo hapa nchini.

(c) Serikali ihakikishe kwamba kiwanda kinaongeza uzalishaji wa mkaa mbadala unaotokana na makaa ya mawe, ili kuweza kufikia lengo lililokusudiwa ambalo ni kuwezesha wakulima wa tumbaku kutumia nishati katika kukausha zao hilo.

(d) Serikali kupitia *STAMICO* ifanye tathmini ili kubaini maeneo yenye uhitaji wa viwanda vya kuzalisha mkaa wa nishati safi mbadala (mkaa wa mawe) katika maeneo mengine.

(e) Kuhusu kuongeza ushiriki wa *STAMICO* katika uchimbaji mkubwa, Kamati inaishauri Serikali iongeze mtaji wa *STAMICO* ili liweze kushiriki kikamilifu katika miradi mikubwa ya kimkakati. Hali hiyo itasaidia kuongeza mapato ya Serikali na kujenga uzoefu wa Kitaifa katika uendeshaji wa miradi mikubwa ya madini.

(f) Kuhusu kuendeleza migodi ya mfano kwa wachimbaji wadogo, tunatambua na kupongeza kuwepo kwa vituo vya migodi ya mfano kwa ajili ya kusaidia wachimbaji wadogo. Licha ya juhudi hizo Kamati inashauri Serikali kuendelea na uanzishwaji wa vituo vya mfano kama hivyo maeneo tofauti nchini huku ikiangalia na uhitaji wa kila eneo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti kwa sababu taarifa hii tunayo kwenye vishikwambi ninaomba uhitimishe tu.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa namna ya kipekee, ninaendelea kumshukuru Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu kwa maelekezo yake ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninakushukuru wewe Mheshimiwa Daniel Baran Sillo kwa namna unavyokusaidia unavyomsaidia Mheshimiwa Spika kutekeleza majukumu yake, pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kumsaidia kuendesha Vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ikiongozwa na Mwenyekiti wetu makini sana Mheshimiwa Subira Mgalu, ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Madini pamoja na taasisi zilizo chini yake. Maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Ninaomba niyatambue majina yao ili yote yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza Waziri wa Madini, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde kwa kazi nzuri anayofanya kwenye sekta ya madini, na kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Madini Mheshimiwa Steven Kiruswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Madini pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Mhandisi Yahya Samamba, na msaidizi wake Naibu Katibu Mkuu Dkt. Msafiri Mbibo. Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya Sekta ya Madini na inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Wakili Baraka Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu Namba 100, Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na kama yalivyoombwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA FUNGU 100 – WIZARA YA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuturuzuku uhai na afya njema na kutuwezesha Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya nchi kwa kutoa ushauri kwa Wizara ya Madini na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Kipekee nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya **FUNGU 100 Wizara ya Madini** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya **Kanuni ya 121 (4)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025 na imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

a) **Sehemu ya Kwanza** ni Utangulizi na inaeleza kuhusu Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeza majukumu yake;
b) **Sehemu ya Pili** inaeleza kuhusu Uchambuzi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

c) **Sehemu ya Tatu** ni Uchambuzi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

d) **Sehemu ya Nne** ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati; na

e) **Sehemu ya Tano** ni Hitimisho.

## 1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Majukumu yake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Kamati ilifanya yafuatayo:

a) Kupokea na kufanya uchambuzi wa Randama ya Wizara (Kanuni ya 118 (1));
b) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Kanuni ya 120 (1));

c) Kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

d) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA FUNGU 100 - WIZARA YA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 2.1 Msingi na Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inalipa Bunge madaraka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti. Kwa muktadha huo, Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti kwa Kamati za Kisekta kufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi za Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia msingi wa uchambuzi, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa **Fungu 100** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na kufanya ulinganisho na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (2).

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

a) Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli

b) Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

c) Utekelezaji wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

## 2.2 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, **Fungu 100 – Wizara ya Madini** ilitengewa bajeti ya jumla ya **Sh. 224,984,150,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 100,379,362,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 124,604,788,000.00** zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilikuwa imepokea **Sh. 74,371,336,463.38** sawa na **asilimia 33.06** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Sh. 64,168,235,615.07** sawa na **asilimia 63.9** wa bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa na **Sh. 10,203,100,848.31** sawa na **asilimia 8.18** wa bajeti ya maendeleo kama ambavyo **Kielelezo Na. 1** kinafafanua.

***KIELELEZO NA: 1Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha wa Fungu 100 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026***

| MAPOKEZI | BAJETI YA MWAKA 2026/2027 (TZS) | MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2026 (TZS) | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | 100,379,362,000.00 | 64,168,235,615.07 | 63.9 % |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | 124,604,788,000.00 | 10,203,100,848.31 | 8.18% |
| **JUMLA** | **224,984,150,000.00** | **74,371,336,463.38** | **33.06%** |

***Chanzo**:Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na mwenendo wa upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo ambayo hadi kufikia Februari 2026 Wizara ilikua imepokea asilimia 8.18 tu ya bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa.Upungufu huo wa Bajeti unaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji na ukamilishaji wa miradi ya maendeleo ambayo ilipangwa kutekelezwa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika**,Kamati ilielezwa kwamba mapokezi hafifu ya Fedha za Maendeleo yanatokana na kutokupatikana kwa Mkopo wa Sh. 53,097,080,000.00 ambao ulikuwa unatoka Serikali ya Spain.Mkopo huo ulilengwa kutumiwa na taasisi ya GST ili kutekeleza mradi wa utafiti wa madini nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Ni ushauri wa Kamati kwa Serikali kuhakikisha kwamba inaweka kipaumbele kutenga fedha za Ndani katika utekelezaji wa Miradi ya maendeleo ya Wizara hii na Taasisi zake.Hali hii itasaidia bajeti za maendeleo kutoathiriwa na changamoto ya kukosekana au kuchelewa kwa fedha za washirika wa maendeleo.

### 2.3 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Madini liidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. 1,405,537,268,735.00** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni mapato mengineyo,ada za mwaka,ada za ukaguzi wa madini,mirabaha,ada za kijiolojia, Adhabu na Faini za Malimbikizo ya Ada, Malipo ya Huduma za Maabara, HIIV levy na pamoja na makusanyo ya Maduhuli kutoka kwenye taasisi zake ambazo ni **STAMICO, GST** na **TGC**. Aidha katika makadirio hayo ya makusanyo ya maduhuli kiasi cha **Sh. 1,200,000,000,000.00** kilipangwa kuwasilishwa Hazina na kilichobaki ambacho ni **Sh. 205,537,268,735.00** zilipangwa kutumiwa na Taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika.** Hadi kufikia Februari, 2026, makusanyo yalikuwa ni **Sh. 880,711,819,180.05** sawa na **asilimia 109.5** ya malengo waliyojiwekea kwa miezi 8(Julai 2025 hadi Feb 2026) Mchanganuo wa mwenendo wa makusanyo unafafanuliwa katika Kielelezo Na. 2

**KIELELEZO NA: 2 Makusanyo kutoka vyonzo mbalimbali vya mapato yanayowasilishwa Hazina kuanzia Julai 2925 hadi Februari, 2026**

| Na. | Chanzo cha Mapato | Bajeti ya Mwaka 2025/2026 | Lengo la Miezi 8 | Makusanyo Julai 2025Februari 2026 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapato mengineyo | 2,000,000.00 | | 0.00 | 0.00 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. | Ada ya Mwaka | 65,180,847,813.00 | 39,587,231,888.67 | 37,307,228,112.78 | 94.24 |
| 3. | Ada ya Ukaguzi wa Madini | 164,263,722,901.00 | 109,509,148,600.67 | 104,293,022,025.81 | 95.24 |
| 4. | Mrabaha | 950,262,641,687.00 | 633,508,427,791.33 | 713,086,308,731.88 | 112.56 |
| 5. | Adhabu na Faini za Malimbikizo ya Ada | 2,534,180,411.00 | 2,356,120,274.00 | 2,998,110,551.42 | 127.25 |
| 6. | Ada za Kijiolojia | 17,131,607,188.00 | 10,329,745,625.79 | 10,242,015,164.67 | 99.15 |
| 7. | Malipo ya Huduma za Maabara | 625,000,000.00 | 416,666,666.67 | 375,326,828.71 | 90.08 |
| 8. | HIV Levy | 0.00 | 12,291,325,832.87 | 12,409,807,764.78 | 100.96 |
| | **Jumla** | **1,200,000,000,000.00** | **807,998,666,680.00** | **880,711,819,180.05** | **109.00** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Usanifu wa Kamati*

**KIELELEZO NA: 3 Mchanganuo wa Maduhuli yaliyokusanywa na kutumiwa na Taasisi**

| Taasisi | Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka | Lengo la Miezi 8 | Makusanyo Halisi | Ufanisi (%) kwa Miezi nane (8) |
|---|---|---|---|---|
| STAMICO | 201,538,768,735.00 | 134,588,679,156.67 | 53,902,045,515.00 | 40.05 |
| GST | 3,600,000,000.00 | 2,400,000,000.00 | 1,200,790,377.75 | 50.03 |
| TGC | 398,500,000.00 | 265,666,666.67 | 195,845,596.21 | 73.72 |
| **JUMLA** | **205,537,268,735.00** | 137,254,345,823.34 | 55,298,681,488.96 | 40.29 |

**Chanzo:** *Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, kwa wastani, mwenendo wa makusanyo ya **Fungu 100– Wizara ya Madini** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni wa kuridhisha. Kwakuwa hadi kufikia Februari 2026 ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa umevuka lengo lililokusudiwa.Kamati ilielezwa kwamba kuvuka kwa lengo kunatokana na kuongezeka

kwa ukusanyaji kunakotokana na vyanzo vyake ambavyo vimeanishwa katika **Kielelezo Na. 2** cha taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata ufafanuzi kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara kutofikia lengo la ukusanyaji kuwa kunatokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuchelewa kufungwa kwa mitambo ya *coal briquettes* Dodoma, Tabora na Kiwira; kushuka kwa bei ya makaa ya mawe kwenye soko la dunia na kuchelewa kuanza kwa mikataba ya huduma ya uchorongaji ambayo iliathiri ukusanyaji wa maduhuli kwa upande wa **STAMICO**, kuharibika kwa baadhi ya mashine/vifaa vya maabara ikiwemo tanuru (kiln) la kuchomea vyungu vya kuyeyushia sampuli za dhahabu (crucibles) na mashine za XRF na kupanda kwa bei ushauri elekezi baada ya taasisi ya **GST** kuingia kwenye kodi ya ongezeko la thamani **(VAT).**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa pongezi kwa Wizara kwa kuvuka lengo la ukusanyaji wa maduhuli hadi kufikia Februari 2026, Aidha ni ushauri wa Kamati kwa Serikali kuhakikisha kwamba Taasisi zilizo chini ya Wizara zinafikia lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kwakuwa sababu zilizochangia kutofikia malengo kwa kiasi kikubwa zimeshatatuliwa ikiwemo ujenzi wa kiwanda cha Rafiki coal briquette mkoani Tabora kukamilika na kufungwa mitambo ya *coal briquettes* jijini Dodoma kufika asilimia 80.

## 2.4 Utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Madinii ilitengewa jumla ya **Sh. 100,379,362,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizo zinajumuisha **Sh. 24,268,585,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi (PE) wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake na **Sh. 76,110,777,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari 2026, jumla ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizokuwa zimetolewa ni **Sh. 64,168,235,615.07** sawa na **asilimia 64** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo**, Sh. 15,438,637,241.12** zilkuwa ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi (P.E.) na **Sh.**

**48,729,598,373.95** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C.) kama ambavyo Kielelezo Na. 4 kinafafanua.

**KIELELEZO NA: 4 Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kufikia Februari, 2026**

| Na. | Matumizi | Bajeti ya Mwaka 2025/26 | Fedha zilizopokelewa hadi Februari, 2026 | Asilimia ya Fedha Zilipokelewa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Matumizi Mengineyo (OC) | 76,110,777,000.00 | 48,729,598,373.95 | 64.02b% |
| 2. | Mishahara (PE) | 24,268,585,000.00 | 15,438,637,241.12 | 63.62% |
| **Jumla Ndogo** | | **100,379,362,000.00** | **64,168,235,615.07** | **64.27** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2025/26 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa mapokezi ya fedha za Matumizi ya kawaida kwa Fungu 100 Wizara ya Madini na Pongezi kwa Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Daktari Samia Suluhu Hassan kuendelea kutoa fedha ambazo zinasaidia Wizara na watendaji wake kutekeleza majukumu yake.

## 2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Madini ilitengewa jumla ya **Sh. 124,604,788,000.00** ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 71,507,798,000.00** zilikuwa ni fedha za ndani, na **Sh. 53,097,080,000.00** zilikuwa ni fedha za nje. Mwenendo wa Mapokezi ya Fedha za Maendeleo unafafanuliwa katika Kielelezo Na. 5 kwa muhtasari.

**KIELELEZO NA: 5 Mwenendo wa Mapokezi ya Fedha za Maendeleo Bajeti ya 2026/2027**

| CHANZO | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 (TZS) | MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2026 (TZS) | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA NDANI** | **71,507,798,000.00** | **10,203,100,848.31** | 14.26% |
| **FEDHA ZA NJE** | **53,097,080,000.00** | 0 | 0% |
| **JUMLA** | **124,604,788,000.00** | **10,203,100,848.31** | **8.18%** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2025/26 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na mapokezi ya fedha za maendeleo kwa **Fungu 100**, Hadi Kufikia Februari mwaka 2026 jumla ya Fedha iliyopokelewa ni sawa na **asilimia 8.18** tu ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa.Mapokezi ya Fedha za ndani ni wastani wa **asilimia 14.26** na upande wa fedha za nje hakuna fedha iliyopokelewa. Hali hii inaleta mashaka kwenye utendaji wa Wizara hii ambayo kupitia Taasisi zake imekuwa ni kinara katika ukusanyaji wa maduhuli na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**,Ni ushauri wa Kamati kwa Serikali kuhakikisha kwamba inakuwa na vyanzo vya ndani ambavyo ni vya uhakika vitakavyowezesha Wizara kutekeleza miradi ya maendeleo iliyokusudiwa.Kutokupatiakana kwa fedha za maendeleo kunaweza kuathiri mpango kazi na utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara ukizingatia mchango wa sekta ya Madini katika kuongeza pato la Serikali na kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa letu.

## 2.6 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (1), Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kati ya tarehe 12 – 18 Machi, 2026 katika

mikoa ya, Tabora, Shinyanga, na Geita . Katika ziara hiyo, Kamati ilifanya tathmini ya baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.Tathmini iliyofanyika ilijumuisha uchambuzi wa mapokezi ya fedha, hali ya utekelezaji wa miradi husika na changamoto za utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

**2.6.1 Mradi Na 1119: Mradi wa Ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza mkaa mbadala wa kupikia (coal breiquette) Tabora.**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa na Shirika la Madini la Taifa(STAMICO) ya kutanua wigo wa matumizi ya makaa ya mawe kama nishati safi ya kupikia ijulikanayo kama Rafiki Briquettes. Gharama za mradi huu ni takribani **Shilingi 3,039,217,680** ikihusisha gharama za ununuzi wa mtambo wenye uwezo wa kuzalisha Rafiki Briquettes tani 20 kwa saa,usafirishaji,ujenzi na ukarabati wa jengo ambalo lilitolewa na Chama cha Ushirika cha Wakulima wa Tumbaku(WTCU).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kwamba malengo ya kuanzishwa kwa mradi huu kwa Mkoa wa Tabora ni kutoa suluhusho la kudumu la ukaushaji wa tumbaku ambao kwa kiasi kikubwa umeathiri na kukaribu mazingira ya mkoa wa Tabora.Aidha matarajio ya mradi huu ni kuongeza pato la Serikali kupitia kodi na tozo mbalimbali na pia kutoa ajira kwa vijana na wanawake katika mnyororo wa usambazaji na uuzaji wa Nishati hii safi.Kamati inatoa pongezi kwa juhudi znazofanywa na STAMICO katika kuunga mkono juhudi za **Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwenye matumizi ya nishati safi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo Kamati inaishauri Serikali kuendelea na uzalishaji na usambazaji wa bidhaa hiyo ili iweze kuwafikia wahusikaambao ni wakulima wa Tumbaku kwa haraka na hivyo kutimiza lengo lililokusudiwa.

## 2.6.2 Mradi Na. 1119 Upanuzi wa Kituo cha Mfano (Demonstration Centre) cha Madini Katente,Bukombe

**Mheshimiwa Spika**, Kituo hiki cha mfano cha Katente kimeanzishwa katika eneo la leseni ya uchimbaji mdogo namba PML**04548MBG** inayomilikiwa na **STAMICO**.
Aidha Leseni hiyo awali ilikuwa inamilikiwa na Ushirika wa wachimbaji Madini Katente **PML000194.**

**Mheshimiwa Spika,**Gharama za mradi huu ni takribani **Shilingi 1,743,103,346.41** ikihusisha gharama za usimikaji wa mitambo ya uchenjuaji dhahabu kwa kutumia teknolojia ya ***Carbon-In-Pulp*****(CIP),**ujenzi wa jengo la ofisi ya mafunzo,karakana ndogo,maliwato,jengo la maabara na uandaaji wa sampuli za madini,jengo la stoo kwa ajili ya kuhifadhia kemikali,uchimbaji wa kisima cha maji na pampu zake za kuvuta maji na jengo la elusion.Vilevile gharama hiyo ilitumika katika ununuzi na usimikaji wa mashine ya upimaji sampuli na usimikaji wa mitambo mbalimbali inayotumika katika uchenjuaji wa dhahabu.
Sambamba na hayo gharama nyingine zilitumika kununua jenereta kubwa la kuzalisha umeme pamoja na kuunganisha kituo hiko kwenye gridi ya Taifa

**Mheshimiwa Spika,**lengo la kuanzishwa kituo hiki ni kuwawezesha wachimbaji wadogo kuchenjua dhahabu kwa njia ya CIP ambayo ina ufanisi mkubwa zaidi ukilinganisha na uchenjuaji wa kutumia VAT leaching.Pia kituo hiki kimeanzishwa ili kutoa elimu na mafunzo kwa vitendo kwa wachimbaji wadogo juu ya namna ya kutumia njia za kisasa za uchenjuaji zenye tija kubwa katika uzalishaji wa dhahabu.

**Mheshimiwa Spika** toka kituo hiki kuzinduliwa Aprili 2020 hadi kufikia Januari 2026 kimeweza kuchenjua ya dhahabu wenye jumla ya **tani 6,786.01**, uchomaji wa caboni kwa awamu 399 ambazo zimeweza kuzalisha dhahabu gramu **281.200.64** zenye thamani ya Shilingi **45,005,023,169.6.**

**Mheshimiwa Spika,** kupitia kituo hiki Serikali imeweza kukusanya jumla ya **Shilingi 3,946,432,992.35** ambayo inajumuisha

mrabaha.ada ya ukaguzi,tozo za Halmashauri na TRA Kama inavyooneshwa kwenye kilelezo Namba 6 cha Taarifa hii.

**KIELELEZO NA: 6 Muhtsari wa uzalishaji na Kodi katika kituo cha Katente kwa Kipindi cha Aprili 2020 hadi Januari, 2026**

| Na. | Chanzo cha Mapato | Mapato |
|---|---|---|
| 1. | **UCHENJUAJI MBALE** | |
| a) | Tani zilizochakatwa CIP | 6,786,01 |
| | Jumla ya tani zilizochenjuliwa | 6,786,01 |
| 2. | **UZALISHAJI DHAHABU** | |
| i. | Dhahabu iliyozalishwa CIP.g | 59,098.99 |
| ii. | Dhahabu iliyozalishwa Elution,g | 222,101.65 |
| | **Jumla ya Uzalishaji** | **281,200.64** |
| 3. | **THAMANI YA DHAHABU** | |
| i. | Thamani ya Dhahabu CIP,TZS | 9,719,069,048.10 |
| ii | Thamani ya Dhahabu Elution.TZS | 35,285,954,121.51 |
| | **Jumla ya Thamani ya Dhahabu** | **45,005,023,169.61** |
| 4. | **MALIPO YA KODI** | |
| i. | Mrabaha | 2,700,301,390.18 |
| ii. | Tozo za ukaguzi wa madini,TZ | 450,050,231.70 |
| iii. | Tozo ya Halmashauri,TZS | 136,519,086.72 |
| iv. | TRA | 659,562,283.76 |
| | **Jumla ya Malipo, TZS** | **3,946,432.992.35** |

***Chanzo**:Taarifa ya Wizara kuhusu Utekelezaji wa mradi vituo vya wachimbaji wadogo cha Lwamgasa na Katente na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa mradi ambao unaendelea kuleta tija katika uchenjuaji dhahabu kwa wachimbaji wadogo.Ni rai ya Kamati kwa Serikali kupitia **STAMICO** kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wa maeneo ya Bukombe ndio wanakuwa wanufaika zaidi wa mradi huu.

### 2.6.3 Mradi Na. 1119 Upanuzi wa Kituo cha Mfano (Demonstration Centre) cha Madini Lwamgasa,Geita

**Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Lwamgasa kimeanzishwa kwenye eneo la uchimbaji mdogo lenye leseni PML 0013603 na PML 0013604 ambazo zinamilikiwa na Serikali ya Kijiji cha Lwamgasa kupitia Ushirika wa Wachimbaji wadogo wa Madini Lwamgasa.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa kituo cha Lwamgasa umegharimu jumla ya **Shilingi 1,519,721,034.44** ikihusisha kufanyika tafiti za jiojolojia,uchimbaji wa mitaro na mashimo ya utafiti,ujenzi wa mgodi wa mfano wa chini ya ardhi**(Underground model mine)** na Nishati,ujenzi wa karakana,jengo la mafunzo kwa wachimbaji na wageni,stoo ya kuhifadhia karakana,ujenzi wa bwawa la visusu na ujenzi wa maliwato.Vilevile gharama hiyo ilihusisha Usimikaji wa mitambo ya usagaji na ukamatishaji dhahabu kwa njia ya uzito**(Gravitation)** na ununuzi wa vifaa mbalimbali vikiwemo pampu za kuvuta maji na mitambo ya uchorongaji miamba.Aidha kituo hiki kama ilivyo kituo cha Katente kimeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika** Mwaka 2023 Kituo kilitumia **Shilingi 529,470,800** kufanya upanuzi wa kituo hic,o.Upanuzi huo ulihusisha kuongeza matanki mawili (leaching tanks)yenye ujazo wa lita 30,000 ,kusimika mtambo wa uchomaji kaboni yenye uwezo wa kubeba kilo 500 za kaboni kila mmoja.

**Mheshimiwa Spika** Mradi huu umekuwa na mafanikio kadhaa yanayoendana na lengo la kuanzishwa kwake ikiwemo kusaidia wachimbaji wachache kujenga CIP,kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo wapatao 3,028 juu ya namna bora ya uchimbaji na uchenjuaji miamba kutumia mitambo ya CIP,kutoa huduma ya umeme na maji na ushauri wa kitaaluma kuhusu uchimbaji ambao utakuwa na tija katika uzalishaji wa dhahabu.

**Mheshimiwa Spika** toka kuanzishwa mradi huu umeweza kuzalisha dhahabu zenye **gramu 210,824.34** zenye thamani ya jumla ya **Shilingi 44,979.086,296.33** na pia umewezesha Serikali kukusanya mapato ya **Shilingi 3,889,337,666.87** ambayo yanajumuisha

mrabaha,ada ya ukaguzi,tozo ya Halmashauri na TRA kama inavyoonekana katika kielelezo namba 7 la taarifa hii.

**KIELELEZO NA: 7Muhtsari wa Uzalishaji na Kodi katika kituo cha Lwamgasa kwa kipindi cha Aprili 2020 hadi Januari, 2026**

| Na. | Chanzo cha Mapato | Mapato |
|---|---|---|
| 1. | **UCHENJUAJI MBALE** | |
| i | **Mgodi wa mfano,t** | 677.00 |
| ii | Tani zilizochakatwa CIP | 7,078.30 |
| iii | Jumla ya tani zilizochenjuliwa | 7,755.30 |
| iv | Awamu za uchomaji wa Kaboni Elution | 70.00 |
| 2. | **UZALISHAJI DHAHABU** | |
| i. | Mgodi wa mfano,g | 995.30 |
| ii | Dhahabu iliyozalishwa CIP.g | 69,703.81 |
| iii | Dhahabu iliyozalishwa Elution,g | 140,125.23 |
| | **Jumla ya Uzalishaji wa dhahabu** | **210,824.34** |
| 3. | **THAMANI YA DHAHABU** | |
| i. | Thamani ya dhahabu mgodi wa mfano,TZS | 228,354,932.62 |
| ii | Thamani ya Dhahabu CIP,TZS | 10,618,851,599.24 |
| iii | Thamani ya Dhahabu Elution.TZS | 34,131,879,764.47 |
| | **Jumla ya Thamani ya Dhahabu** | **44,979,086,296.33** |
| 4. | **MALIPO YA KODI** | |
| v. | Mrabaha | 2,699,678,186.31 |
| vi. | Tozo za ukaguzi wa madini,TZ | 449,779,677.37 |
| vii. | Tozo ya Halmashauri,TZS | 134,933,905.98 |
| viii. | TRA | 818,183,155.34 |
| | **Jumla ya Malipo, TZS** | **3,889,337,666.87** |

*Chanzo:Taarifa ya Wizara kuhusu Utekelezaji wa mradi vituo vya wachimbaji wadogo cha Lwamgasa na Katente na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Palipo na mafanikio hapakosi changamoto,Hivyo pia katika mradi huu Kamati ilibaini baadhi ya changamoto ikiwemo mwamko mdogo wa walengwa ambao ni wachimbaji wadogo katika kutumia kituo hicho kwa shughuli za uchenjuaji wa dhahabu.

**Mradi Na. 1119 – Mradi wa ujenzi wa jengo la Afisa Madini Mkazi, Mkoa wa Geita**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wizara ya Madini na unahusu ujenzi wa wa jengo la Ofisi za Afisa madini Mkazi mkoa wa Geita.Ujenzi wa jengo hili unagharimu jumla ya **Shilingi 6,273,808,093.37** pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT),ambazo ni fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika,**Lengo la kuanzishwa mradi huu ni kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi wa Tume ya Madini walioko katika ofisi ya Afisa Madini mkazi wa mkoa wa Geita**.** Mkoa wa Geita ukiwa ni  miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa kuwa na wachimbaji wa madini wenye leseni mbalimbali,Hivyo ujenzi wa jengo hili utasaidia Wizara na Tume kuwafikia na kutatua changamoto kwa  wahusika ambao ni wachimbaji wa madini wa mkoa wa Geita.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati ilibaini changamoto ya kuchelewa kwa malipo ya mkandarasi ambayo yamechangia kuchelewa kukamilika kwa mradi huo.Aidha Serikali ilitoa ufafanuzi namna ambavyo wanakabiliana na kutafuta suluhisho la changamoto hiyo.Hivyo Kamati inatoa msisitizo kwa Serikali kutoa pesa kwa wakati ili kumuwezesha mkandarasi kumaliza ujenzi kwa mujibu wa mkataba wa  nyongeza.

**Mheshimiwa Spika**, diKamati inapongeza jitihada za Serikali kwa kuibua Mradi kama huu ambao utasaidia kuboresha utoaji huduma kwa wachimbaji waliopo katika Mkoa wa Geita na maeneo ya jirani.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FUNGU 100 - WIZARA YA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### 3.1 Vipaumbele vya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, FUNGU 100 – Wizara ya Madini inalenga kutekeleza vipaumbele mbalimbali vya kibajeti vikiwemo vifuatavyo: -

a) **Ukusanyaji wa maduhuli:**
Wizara itatekeleza kipaumbele hiki kwa kufanya ukaguzi na usimamizi wa uchimbaji madini na masoko ya vituo vya ununuzi wa madini, ili kusaidia na kukomesha vitendo vya utoroshwaji wa madini kwenda nje ya nchi na Hivyo nchi kuweza kukusanya mapato kupitia sekta ya madini.

b) **Kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa**:
Wizara itaendelea kutekeleza hili kwa kwa kuhamasisha uanzishaji wa migodi mipya na kuisimamia kwa misingi ya sheria.Aidha Wizara itasimamia migodi yote nchini kutengeneza ajira kwa wazawa kupitia mnyororo wa uchumi wadini(Local content) na huduma kwa jamii(CSR)

c) **Taasisi zilizo chini ya Wizara**:
Wizara itatekeleza kipaumbele hiki kwa kuimarisha utendaji kazi wa taasisi hizo kwa kuzipatia rasilimali fedha,vifaa na watu.Aidha Wizara itahakiisha Taasisi yake ya STAMICO inashiriki kikamilifu kwenye Shughuli za Madini,GST kufanya utafiti mkubwa wa madini ili kubaini maeneo mapya yenye mashapo ya madini,TGC kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini na TEITI kupata rasilimali mbalimbali ikiwemo vifaa na vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake

d) **Wachimbaji wadogo wa Madini**:
Kuhamasisha taasisi za fedha kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo,kutoa huduma za mafunzo kupitia vituo vya mfano, kutoa maeneo ambayo yana taarifa za kijiolojia na

kuwahamasisha wachimbaji wadogo kushiriki kwenye maonesho ya madini ya vito nchini ili kukuza wigo wa biashara zao.

e) **Uwekezaji kwenye Sekta ya Madini**:
Itafanya tafiti za majaribio kwa kurusha ndege ili kupata taarifa za jiofizikia na kuzitunza taarifa hizo za jiosayansi kutokana na matokeo ya tafiti hizo.

### 3.2 Muundo wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Madini (FUNGU 100) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 174,983,580,000.00.** ambapo kati ya fedha inayoombwa, **Sh. 103,475,872,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Sh. 71,507,708,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, fedha inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imeopungua kwa wastani wa **asilimia 28.57** ukilinganisha na Bajeti ya **Sh. 224,984,150,000.00** iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. Kielelezo Na. 8 kinafafanua kwa muhtsari ulinganisho kati ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**KIELELEZO NA: 8 Ulinganisho wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027**

| MAELEZO | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 | BAJETI YA MWAKA 2026/2027 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | 79,232,226,000 | 103,475,872,000.00 | +24,243,646,000 | 7.65 % |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | 124,604,788,000.00 | 71,507,708,000.00 | -53,097,080,000 | +76.5% |
| **JUMLA** | **224,984,150,000.00** | **174,983,580,000.00** | **53,097,080,000** | **-57.38 %** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 100 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Upungufu wa Bajeti ya Fungu 100 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni kutokana na kupungua kwa **Sh. 53,097,080,000** iliyokuwa ni fedha ya mkopo kutoka Serikali ya Hispania ambayo iliyopangwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Fedha hizo zilitegemewa kutoka kwa wahisani kwa mwaka wa fedha 2025/2026 zilipaswa kutumiwa na Taasisi ya GST katika kufanya tafiti za madini nchini.Hata hivyo, kama ambavyo Kielelezo Na. 5 kinavyoonesha, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imeongezeka kwa **Sh. 24,243,646,000** sawa na wastani wa **asilimia 7.65 %** ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha.

### 3.3 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Madini pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Sh. 1,611,543,299,735.00** ambayo yatatokana na vyanzo vyake mbalimbali. Kielelezo Na. 9.

**KIELELEZO NA: 9 Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yatakayokusanywa na kuwasilishwa Hazina katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Mwaka wa Fedha 2026/2027**

| Na. | Chanzo cha Mapato | Bajeti ya Mwaka 2025/2026 | Bajeti 2026/2027 | Tofauti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapato mengineyo | 2,000,000.00 | 0 | 0.00 | 0.00 |
| 2. | Ada ya Mwaka | 65,180,847,813.00 | 69,743,507,180.79 | 4,562,659,367.79 | 7.0 |
| 3. | Ada ya Ukaguzi wa Madini | 164,263,722,901.00 | 192,905,922,216.17 | 28,642,199,315.17 | 17.4 |
| 4. | Mrabaha | 950,262,641,687.00 | 1,119,643,458,872.69 | 169,380,817,185.69 | 17.8 |
| 5. | Adhabu na Faini za Malimbikizo ya Ada | 2,534,180,411.00 | 4,711,573,039.32 | 2,177,392,628 | 85.9 |
| 6. | Ada za Kijiolojia | 17,131,607,188.00 | 18,330,819,691.03 | 1,199,212,503 | 6.9 |
| 7. | Malipo ya Huduma za Maabara | 625,000,000.00 | 668,750,000.00 | 43,750,000 | 7 |
| 8. | HIV Levy | 0.00 | 0.00 | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **1,200,000,000,000.00** | **1,406,006,031,000.00** | **206,006,032,000** | 17.16 |

***Chanzo***: *Randama ya Wizara ya Madini Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na Usanifu wa Kamati*

**KIELELEZO NA: 10 Mchanganuo wa Maduhuli yaliyokusanywa na kutumiwa na Taasisi**

| Taasisi | Bajeti 2025/2026 | Bajeti 2026/2027 | Tofauti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| STAMICO | 201,538,768,735.00 | 201,538,768,735.00 | 0 | 0 |
| GST | 3,600,000,000.00 | 3,600,000,000.00 | 0 | 0 |
| TGC | 398,500,000.00 | 398,500,000.00 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **205,537,268,735.00** | **205,537,268,735.00** | | 0 |

***Chanzo***: *Randama ya Wizara ya Madini Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi Kamati imebaini kuongezeka kwa makadirio ya ukusanyaji wa Maduhuli ambayo yatakusanywa na kuwasilishwa Hazina.Makadirio hayo ymeongezeka kwa **Sh. 206,006,032,000** sawa na asilimia 17.6 ukilimganisha na Bajeti ya mwaka fedha unaoisha tarehe 30 Juni 2026 Aidha makadirio ya ukusanyaji wa Maduhuli yakakayokusanywa na kutumiwa na Taasisi chini ya Wizara hayajabadilika

**Mheshimiwa Spika**,Kutokana na mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa maduhuli, ni matarajio ya Kamati kuwa hadi kumalizika kwa robo ya nne ya mwaka wa fedha 2025/2026 kuna uwezekano kiwango cha makusanyo kikaongezeka zaidi. Hivyo ni ushauri wa Kamati kwa Wizara kuongeza kiwango cha makadirio ya maduhuli.

**Mheshimiwa Spika** katika kuongezeka ukusanyaji wa maduhuli,Kamati inashauri Wizara ifanye jitihada zitakazoibua vyanzo zaidi vya mapato na hivyo kuongeza wigo wa mapato yatokanayo na ukusanyaji wa maduhuli.

### 3.4 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2207, **FUNGU 100 – Wizara ya Madini** inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 103,475,872,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya

fedha hizo, **Sh. 27,365,095,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 76,110,777,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 imeongezeka kwa **Sh. 2,491,722,000,000** sawa **asilimia 2,46** ukilinganisha na **Sh. 100,984,150,000.00** iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 kamaambavyo Kielelezo Na. 11 kinaonesha.

**KIELELEZO NA: 11Ulinganishi wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kati ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Mwaka wa Fedha 2026/2027**

| MATUMIZI YA KAWAIDA | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 | BAJETI YA MWAKA 2026/2027 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| MISHAHARA (P.E.) | 24,268,585,000.00 | 27,365,095,000.00 | +3,096,510,000 | +12.7% |
| MATUMIZI MENGINEYO (O.C.) | 76,110,777,000.00 | 76,110,777,000.00 | 0 | 0% |
| **JUMLA** | **100,984,150,000.00** | **103,475,872,000.00** | **+2,491,722,000,000** | **2.46%** |

***Chanzo:*** *Randama ya FUNGU 100 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kwamba ongezeko hilo linatokana na kuajiri watumishi wapya na baadhi ya watumishi kupanda vyeo.Aidha bajeti ya matumizi Mengineyo haijabadilika ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha wa 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Wizara kwa kutoongeza Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2026/2027.Hali hii inaonesha kwa kiasi gani Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imedhamiria kupunguza matumizi ya Serikali.

### 3.5 Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, FUNGU 100– Wizara ya Madini inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh.**

**71,507,708,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Bajeti hii ni sawa na wastani wa **asilimia 40.07 ya jumla ya bajeti iliyoidhinishwa.**Bajeti hii inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inatokana na vyanzo vya ndani pekee.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepungua kwa **asilimia 57.3** ukilinganisha na Bajeti ya **Sh. 124,604,788,000** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Upungufu huo unaonekana katika
Kielelezo Na. 12

**KIELELEZO NA: 12 Ulinganisho wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo Kati ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Mwaka wa Fedha 2026/2027**

| MIRADI YA MAENDELEO | BAJETI YA 2026/2027MWAKA | BAJETI YA MWAKA 2026/2027 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA NDANI** | 71,507,708,000.00 | 71,507,708,000.00 | 0 | 0% |
| **FEDHA ZA NJE** | 53,097,708,000.00 | 0 | 0 | 0% |
| **JUMLA** | **124,604,788,000** | **71,507,708,000.00** | **53,097,708,000.00** | **57.3%** |

***Chanzo:*** *Randama ya FUNGU 100 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba upungufu wa Bajeti ya Maendeleo umetokana na kuondolewa kwa vyanzo vya nje katika makadirio ya Bajeti ya mwaka wa Fedha 2026/2027. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kubajeti utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutenga fedha za ndani pekee.

**Mheshimiwa Spika**, Ni ushauri wa kamati kwa Wizara na Serikali kufikiria na kubuni vyanzo vya fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya maendeleo. Licha ya kutenga kiasi hiko cha fedha kutoka vyanzo za ndani bado Kamati inaona kuna umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Utekelezaji kwakuwa Sekta ya Madini ni miongni mwa sekta ambayo inaoongoza kwa kuingiza mapato ya Serikali.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI
### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kamati inaipongeza Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na **Dkt Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kutoa fedha hasa za ndani katika kutekeleza majukumu ya **FUNGU 100 – Wizara ya Madini**.

**Mheshimiwa Spika,**Kupitia uongozi wake Tanzania imeingia katika ramani ya Dunia kama mshindani mkuuwa Soko la Dunia.Hali hii imesadia kuleta mageuzi katika sekta ya madini na hivyo kuifanya sekta hii kuwa ya pili katika kuchangia pato la Taifa **(GDP).** Vilevile Kupitia uongozi wake amewezesha Nchi yetu kushika nafasi nne kwenye kuvutia uwekezaji wa Sekta ya Madini barani Afrika

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kutambua na Kuthamini mchango wa Sekta ya Madini nchini, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

a) Kamati inaishauri Serikali kuimarisha usimamizi na ufatiliaji wa migodi nchini.Serikali itenge fedha za kutosha ili kujenga mifumo thabiti ya kisasa ya TEHAMA itakayowezesha usimamizi,ufuatiliaji na ukaguzi wa shughuli za uchimbaji madini.Sambamba na hilo ihakikishe kwamba inapambana na uchimbaji haramu.

b) Kuongeza Ushirikiano na wadau.Kamati inaushauri Serikali kuendelea kuimarisha ushirikiano na serikali za mitaa,sekta binafsi,taasisi za utafiti na jamii zinazozunguka migodi ili kuhakikisha kwamba sekta ya Madini inaleta manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi.

c) Kukamilisha na kupanga utekelezaji wa miradi ya Kimkakati,Kamati inashauri kwamba Serikali kupitia Wizara ya Madini na Taasisi zake iendelee kutenga bajeti ya kuanzisha miradi mikubwa ya kimkakati na itakayokuwa na uwezo wa kuchenjua madini kwa njia za kisasa.

Sambamba na hilo Serikali isimamie kikamilifu utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati na kwa viwango bora.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuwa na usimamizi wa kina kwa taasisi zake kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yake yote kwa ufanisi. Kamati ina amini kwamba usimamizi madhubuti utawezesha kutoa huduma yenye tija kwa wananchi na wadau wote wa Sekta ya madini.

**4.2 Maoni Mahsusi**

**4.2.1 STAMICO**

**Mheshimiwa Spika** Kamati inatambua mchango wa Wizara na taasisi yake ya STAMICO katika kuchangia pato la Taifa letu hadi kufikia asilimia 10.1 kwa mwaka 2024. Mchango huo una umuhimu kwa wanachi wote wa Tanzania na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**Licha ya kuwepo kwa mafanikio hayo Kamati ina ushauri ufuatao kwa STAMICO ili iweze kuendelea kusaidia uchumi wa Taifa letu.

**a) STAMICO-Kiwanda cha kuzalisha nishati safi ya kuipikia (Rafiki Briquettes) Tabora.**

(i) Serikali kupitia STAMICO itazame uwezekano wa kujenga kiwanda kama hicho katika maeneo mengine ya Mkoa wa Tabora ili kutimiza lengo la kuwasaidia wakulima wa tumbaku wa mkoa huo. Sambamba na hilo STAMICO itumie wakandarasi wazawa katika kutekeleza miradi mingine inayofanana na huo.

(ii) Serikali ihakikishe kwamba kiwanda kinaongeza uzalishaji wa mkaa mbadala unaotokana na makaa ya mawe, ili kuweza kufikia lengo lililokusudiwa ambalo ni kuwezesha wakulima wa tumbaku kutumia Nishati katika kukausha zao hilo.

(iii) Serikali kupitia STAMICO ifanye tathmini ili kubaini maeneo yenye uhitaji wa viwanda vya kuzalisha coal briquette katika maeneo mengine.

**b) Kuongeza Ushiriki wa STAMICO katika Uchimbaji Mkubwa**

**Mheshimiwa Spika**,Kamati inaishauri Serikali iongeze mtaji wa STAMICO ili liweze kushiriki kikamilifu katika miradi mikubwa ya kimkakati. Hali hiyo itasaidia kuongeza mapato ya Serikali na kujenga uzoefu wa kitaifa katika uendeshaji wa miradi mikubwa ya madini.

**c) Kuendeleza Migodi ya Mfano kwa wachimbaji wadogo**

**Mheshimiwa Spika**, Tunatambua na kupongeza kuwepo kwa vituo vya migodi ya mfano kwa ajili ya kusaidia wachimbaji wadogo.Licha ya juhudi hizo Kamati inashauri Serikali kuendelea na uanzishwaji wa Vituo vya mfano kama hivyo maeneo tofauti nchini huku ikiangalia na uhitaji wa kila eneo.

**d) Kuimarisha Huduma za Kitaalamu na Ushauri**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kupitia STAMICO kuongeza huduma zake za ushauri wa kitaalamu (consultancy services) kwa wachimbaji wadogo na wa kati, hususan katika maeneo ya utafiti, usalama migodini, na uongezaji thamani wa madini.

**Mheshimiwa Spika**,sambamba na hilo Kamati bado inashauri Serikali kuongeza matumizi ya teknolojia za kisasa za uchimbaji na uchakataji madini ili kuongeza ufanisi, kupunguza gharama na kulinda mazingira.

**e) Kuimarisha Huduma za Kitaalamu na Ushauri**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri STAMICO kushirikiana na REA kuwa na mkakati wa pamoja katika kuhamisha matumizi ya nishati safi.Kamati inasisitiza kwamba utoaji wa majiko kuende sambamba na usambazaji wa mkaa mbadala

**4.2.2 Tume ya Madini.**

**Mheshimiwa Spika**, tunatambua mchango mkubwa wa Tume ya Madini katika kuisimami sekta hii Muhimu nchini.Kutokana na

utendaji wake Kamati ina shauri yafuatayo katika bajeti ya Wizara;

a) Ihakikishe inafanya ukaguzi ya mara kwa mara kwenye migodi mikubwa,ya kati na ya wachimbaji wadogo ili kuimarisha usalama wa wachimbaji nchini

b) Tume iwawezeshe maafisa wakaguzi kwa kuwekea mazingira wezeshi ambayo yatasaidia kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

c) Kudhibiti mwenendo wa watu kushikilia leseni za maeneo makubwa ya uchimbaji kwa muda mrefu bila kuyaendeleza.

d) Kuwa na mifumo ya kidigitali itakayowezesha kufuta leseni ambazo hazifanyiwi kazi na kuzirejesha kwenye kanzidata ya Tume.

**4.2.3 Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST).**

**Mheshimiwa Spika**,Kamati inatambua mchango wa taasisi ya GST iliyopo chini ya Wizara hii,Hivyo katika utekelezaji wa Bajeti ijayo Kamati inaishauri Serikali ,Kuwekeza nguvu katika kufanya tafiti za kina kuhusu maeneo yenye rasilimali ya madini kote nchini.
Sambamba na hilo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatenga Bajeti ya kutosha ili kuiwezesha taasisi kutimiza wajibu wake wa msingi ambao ni kufanya tafiti za madini nchini.
Tafiti hizo zitawawezesha wachimbaji wa madini wakubwa na wadogo kufanya shughuli zao kwa ufanisi na kwa uhakika.
Vilevile Serikali kupitia GST Serikali itafute vyanzo vya mapato vya uhakika ili kuwezesha shughuli za utendaji kazi pamoja na kuboresha maslahi ya watumishi wa ofisi hiyo.

**4.2.4 Taasisi ya uhamishaji uwazi na uwajibikaji katika Rasilimali,madini,mafuta na Gesi Asilia.(TEITI)**

**Mheshimiwa Spika,** Kuimarisha bajeti ya TEITI ni hatua muhimu katika kuhakikisha rasilimali za taifa zinasimamiwa kwa uwazi, zinachangia kikamilifu uchumi, na kunufaisha wananchi wote.

Serikali inapaswa kuipa taasisi hii kipaumbele cha kifedha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi

**Mheshimiwa Spika** kwa muktadha huo Kamati inaishauri Serikali kupitia TEITI kutenga  fedha za kutosha kuendeleza mifumo ya kidijitali ya ukusanyaji na uchakataji wa data ili kuhakikisha taarifa zinapatikana kwa wakati na kwa usahihi zaidi

**SEHEMU YA TANO**

**5.0 HITIMISHO**

**5.1 Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati. Aidha, namshukuru Naibu Spika, Mhe. Daniel Barran Sirro (Mb.) kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha Vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini  ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Madini  pamoja na taasisi zilizo chini yake. Maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe hao ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge  *(Hansard)* kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Simon Songe Lusengekile Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Agustino Philipo Mulugo, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Joseph Kasheku Msukuma, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Aisha Msantu Mduyah, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Mariam Anzuruni Mungula, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Abuu Jumaa Hamoud, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Nassor Said Nassor, Mb – Mjumbe

10. Mhe. Lulu Guyo Mwacha, Mb – Mjumbe
11. Mhe. Kija Limbu Ntemi, Mb – Mjumbe
12. Mhe. Esther Lukago Midimu, Mb – Mjumbe
13. Mhe. Sandali Chilombe Fadhili, Mb – Mjumbe
14. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb – Mjumbe
15. Mhe. Paul Kapalata Neto, Mb – Mjumbe
16. Mhe. Ali Khalil Mirza, Mb – Mjumbe
17. Mhe. Jacqueline Chrisant Mzindakaya, Mb – Mjumbe
18. Mhe. Eng. Amos William Maganga, Mb – Mjumbe
19. Mhe. Eng. Chacha Mwita Wambura, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Dotto Jasson Bahemu, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb - Mjumbe
23. Mhe.Godwin Oloyce Mollel,Mb - Mjumbe
24. Mhe. Samira Khalfan Amour, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Waziri wa Madini, Mhe. Anthony Peter Mavunde , (Mb)kwa kazi nzuri anayofanya kwenye sekta ya madini na kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Nishati , Mhe. Steven Lemomo Kiruswa (Mb). Aidha niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Madini pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu mkuu wa Wizara ya Madini Mhandisi Yahya Samamba ,na msaidizi wake Naibu Katibu Mkuu Dkt. Msafiri L. Mbibo. Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya Sekta ya Madini, na inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidii.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Wakili Baraka Leornard Idelphonce kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

### 5.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi

ya FUNGU 100 – Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Subira Kamis Mgalu, Mb.
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**
**NISHATI NA MADINI**
27 Aprili, 2026

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti kwa kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati yetu ya Nishati na Madini.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea taarifa zote hizo mbili ya mtoa hoja na taarifa ya Kamati, sasa hapa ninayo orodha ya wachangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa *Engineer* Chacha Mwita Wambura, atafuatiwa na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka na Mheshimiwa Festo Sanga ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti hii ya Madini. Awali ya yote, ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jinsi ambavyo ameendelea kutupa afya na tumeendelea kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii pia, kumshukuru na kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi ambavyo ameendelea kuisimamia Serikali na hasa katika Wizara yetu hii ya Madini ambapo tunaona kwamba kila kunapokucha pato lake limeendelea kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu, nitajielekeza katika masuala kama manne hivi. Suala la kwanza ambalo nilitamani kuchangia ni katika eneo la utafiti. Wizara inayo mkakati mzuri ambao inauita *Vision 2030*, ambapo mpango huu unamaanisha kwamba tunapofika mwaka 2030 tuwe

tumeweza kufanya utafiti kufikia 50% na sasa hivi tumeshafanya utafiti kwa 16% tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ombi langu kwa Wizara na Serikali kwamba jambo hili tumaanishe na ili tumaanishe ni lazima tutenge fedha kwa ajili ya jambo hili. Ukiangalia katika taarifa ambayo imesomwa mwaka jana katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, ni shilingi bilioni 10 tu ya maendeleo ndiyo ambayo imeshatoka ambayo hiyo ndiyo inaenda kufanya suala zima la utafiti, lakini ukiangalia hata hiyo shilingi 10,000,000,000 ambayo ni asilimia nane imeenda kwenye majukumu ambayo siyo *direct* kwenye utafiti, yameenda kujenga ofisi na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwendo huu ni kweli kabisa kwamba tunavyofika 2030 bado lengo hili hatutakuwa tumelifikia. Ninaiomba Wizara, lakini ninaiomba Serikali iweze kuona kwamba kuna haja kuanzia sasa hivi kutenga fedha za ndani kwa ajili ya utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tulikuwa tunategemea fedha za nje na hazikuja na hakuna kilichofanyika. Kwa hiyo, ninaomba sana tunapofika hitimisho la bajeti hii, Mheshimiwa Waziri basi ahakikishe kwamba wanaangalia utaratibu mwingine wa kupata fedha kwa ajili ya utafiti. Tunaamini kama tutafanya utafiti tukafika 50% na kama sasa hivi pato la Taifa kwenye Sekta ya Madini linachangia 11.9%, basi litaenda ku-*double* na tuki-*double* Serikali yetu itaenda kupata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo ninataka kuchangia ni sehemu ambayo tumekuwa na wageni wengi sana Tanzania wakichukua leseni za wachimbaji kwa kigezo cha *technical support*. Sasa hivi ukiangalia Tanzania nzima kuna wageni wengi wapo lakini kigezo kikubwa wanachokitumia ni kwamba wamekuja kutoa *technical support* na ukiangalia kazi wanazozifanya ni zile zile ambazo Watanzania wanazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mikataba hii inayoingiwa na Watanzania kwenye leseni na hao wageni imekuwa ni kiini macho kiasi kwamba kile kinachoandikwa kwenye makaratasi sicho kinachotekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sana Wizara, ninajua kwamba ina namna nyingi za kufanya *auditing*, tufanye *auditing* kwenye hii mikataba yote ya *technical support* iliyopo, tuone kwanza ni aina gani ya *technical support* inayotolewa na hao wageni kwa Watanzania. Pia, tuone huu mkataba ulioandikwa kwamba huyu Mtanzania, huyu mwenye leseni atapata asilimia kadhaa, je wanaipata kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba sana Wizara tunapomaliza Bunge hili la Bajeti basi twende tukahakikishe tunaangalia, tuna-*review*, tunaangalia hii *technical support*. Kweli Watanzania hatuna uwezo hapa? Wizara kama wizara, hizo *technical support* zinazotolewa na hao wageni hatuwezi kuzitoa hapa ndani tukaacha kuuza maeneo na leseni zote kuzitoa kwa wageni kwa kigezo cha *technical support*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuzungumzia eneo lingine la *CSR*. *CSR* kweli ninaipongeza migodi imekuwa ikitoa *CSR* ambayo imesaidia maendeleo katika maeneo ambayo yanazunguka migodi. Hata hivyo, *CSR* hii imekuwa na changamoto kubwa sana. Ninachukulia mfano pale Geita Mjini katika Mgodi wetu wa *GGM* pale. Toka mwaka 2018 na kule nyuma *CSR* ilikuwa inatolewa na Mgodi wa *GGM* kwa jinsi watakavyoona inafaa, lakini mwaka 2018 baada ya kukaa vikao na majadiliano wakakubali kutoa kwa mwaka shilingi bilioni 5.02. Mpaka leo tunavyozungumza 2026 mgodi wa *GGM* unatoa *CSR* shilingi bilioni 5.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuangalia 2018 dhahabu ilikuwa inauzwa shilingi 100,000 kwa gramu lakini sasa hivi dhahabu inauzwa shilingi 390,000 kwa gramu. Mgodi wa *GGM* umeongeza uzalishaji. Mwaka ule ulikuwa unatoa *CSR*, tukiangalia kwenye *CSR*, ulikuwa unatoa *service levy* kama shilingi 800,000,000 lakini sasa hivi inatoa shilingi bilioni 7.5 kiasi kwamba uzalishaji umeongezeka, mapato yameongezeka *almost* mara 10, lakini

*CSR* imebaki kutolewa ile ile ambayo ilikuwa inatolewa 2018 mpaka leo 2026 tunapata *CSR* ile ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara na ofisi yako, tunapomaliza Bunge hili tubadilishe hizi taratibu twende tuka-*discuss* tukubaliane. Hoja yangu sasa ni kwamba tuangalie kiasi hiki kinachotolewa. Kweli kama kipindi kile tulikuwa tunazalisha *almost* sasa hivi tume-*triple* karibu mara 10 ya uzalishaji wa kipindi kile. Mapato yameongezeka karibia mara 10 lakini *CSR* imeendelea kutolewa ile ile ambayo ilitolewa miaka 10 iliyopita kuna haja ya kubadilisha na kutafuta mfumo mpya wa kutoa hii *CSR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, *CSR* hii inayotolewa hata hiyo ndogo inayotolewa, hata hiyo ndogo inayopatikana, utaratibu wake wa manunuzi wa kutekeleza miradi umekuwa mgumu sana. Sasa hivi unakuta kwamba kuanzia zabuni inatangazwa, inasimamiwa na mradi unasimamiwa na Mgodi wa GGM lakini halmashauri au manispaa inaenda tu kukagua au kukabidhiwa mradi. Ninaomba tubadilishe utaratibu, manunuzi yafanyike Halmashauri, Mgodi wa GGM ubaki na fedha kwa ajili ya kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itapunguza gharama kubwa ambayo tunaingia ya kutekeleza miradi kwa kiwango kile kile ambacho Serikali inaweza kutekeleza kwa gharama ndogo, lakini tunapotekeleza kwa kutumia mgodi tunatekeleza kwa kutumia gharama kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ila siyo kwa umuhimu, ninaomba kanuni zibadilishwe kwa sababu mwisho wa siku baada ya uchimbaji huu kuendelea kuna siku moja madini yataisha na yakiisha hii migodi itaondoka. Tuwe na utaratibu kulingana na hizi pesa tunazozipata tuzibadilishie kanuni na sheria ili basi iweze kutengeneza miradi ya uchumi ambayo itaendelea kudumu kwa miaka mingi na itaendelea kutoa ajira na kutengeneza mzunguko wa fedha ili hata pale itakapoondoka tusiendelee kutekeleza tu miradi ambayo Serikali inaweza kutekeleza kwa fedha zake za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ninaomba nizungumzie *double taxation* ambayo inafanyika katika Wizara hii ya Madini. Kule kule kwenye uchimbaji tunao wachimbaji ambao kiukweli ninaipongeza Wizara imewapa leseni za kutosha na kwa kweli wana leseni nyingi ambazo wanachimba sasa hivi lakini tumekuwa na *double taxation*. Tumekuwa tukichaji mrabaha mpaka mara tatu kwa wachimbaji hawa wa wadogo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, muda wako umekwisha. Tunashukuru sana kwa mchango wako.

**MHE. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana, Wizara yetu ya Madini. Kwanza, ninaanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, hotuba ambayo imesheheni kila kona. Ninampongeza Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri lakini na wasaidizi wake wengine wote wakiongozwa na Katibu Mkuu. Kwa kweli wanatutendea haki Watanzania hasa ambao wapo Sekta ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kuipongeza pia Wizara kwa kuendelea kuongeza mapato. Tumeona hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri namna ambavyo tumeweza kwenda kuyafikia malengo ya mapato kutoka makusanyo ya Mfuko Mkuu asilimia tisa mwaka 2023 mpaka leo tumefikia 11%. Haya ni mafanikio makubwa sana na hii yote inaakisi malengo ya Rais, mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna maono yake aliyokuwa nayo Wizara kweli wameenda kuyatekeleza kwa vitendo na sisi tunaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona pia mapato yao kwa kadri ambavyo waliwekewa malengo kwa mwaka huu ambapo ilikuwa wakusanye shilingi trilioni 1.4, lakini mpaka kufikia Machi ambapo ilikuwa wakusanye shilingi bilioni 900, lakini wamefikia shilingi trilioni 1.03. Haya ni mafanikio wameweza kuvuka lengo kwa zaidi ya 114%, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba wanaweza kwenda kuvuka malengo haya ambayo wamewekewa na haya ambayo sisi tunaendelea kuwashauri, tunaomba sana waendelee kuilinda hii sekta ya uchimbaji vizuri ili wachimbaji wetu waweze kufanya kazi zao kwa uhuru, waweze kuchimba vizuri na malengo yao na malengo ya Serikali yaweze kwenda kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nimpongeza Mheshimiwa Waziri, aliweza kutekeleza yale maono ya Mheshimiwa Rais kwenda kuzifuta zile leseni za utafiti, leseni ambazo kwa muda mrefu zimeshikiliwa na watu na zilikuwa hazijaendelezwa; wamezifuta na kuzirudisha Serikalini. Hili ni jambo kubwa na kilio cha wananchi na wachimbaji wetu wengi kilikuwa ni hizi leseni nyingi za utafiti kwenye maeneo yetu ambazo zimeshikiliwa na watu na hazifanyiwi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuzifuta na kuzirudisha Serikalini, nina ushauri mdogo wa nini cha kwenda kufanya. Mheshimiwa Waziri, pamoja na kuzifuta na kuzirudisha Serikalini, tunaomba cha kwanza leseni hizi ziweze kutambuliwa ili wananchi wetu na wachimbaji wetu waweze kuzifahamu. Hii itaturahisishia kwenye utaratibu wa kwenda kuzigawa kwenye leseni ndogondogo kwa maana ya *PML*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale watakapokwenda kuzigawa, wao itawawia rahisi kwenda kuyatembelea maeneo hayo na mtu anapokwenda kuomba leseni hizi kwenye maeneo husika anajua eneo gani ambalo yeye ataweza kwenda kulipata na hii itaturahisishia yale manung'uniko ya wachimbaji wetu wadogo kukosa maeneo ya kufanya kazi, haya yataenda kupunguza kupitia mfumo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba twende tukayagawe kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo lakini muhimu kupitia taasisi yetu ya utafiti *GST* twende tukayafanyie utafiti maeneo haya ili tunapokwenda kuwagawia wachimbaji wetu wadogo kupitia *PML* twende tukawagawie maeneo ambayo wao wakienda kuyafanyia kazi wataenda kupata tija, uzalishaji utakuwa mzuri, lakini pia wao wapate na Serikali iweze kupata kupitia kodi mbalimbali ambazo watakuwa wanazilipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kwenye hotuba ya Waziri amezungumza hapa mpango mzuri wa *MBT*. Kupitia hizi leseni ambazo wamezifuta kupitia leseni kubwa za utafiti tuone namna bora na nzuri kwenye zile leseni ndogondogo watakazozigawa na zenyewe waendelee kutenga maeneo ya vijana wetu kwa ajili ya *MBT* ili wayafanyie utafiti na vijana hawa waweze kugawiwa maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile fedha shilingi bilioni 200 ambazo Mheshimiwa Rais alizitoa na Wizara ya Madini ilizipata, vijana wawezeshwe ili kuyapata maeneo kupitia *RASHIA,* ndipo ambapo tutakuwa tumewasaidia vijana wetu. Tutakuwa tumewasaidia kwenye utafiti kwenye maeneo haya ya *MBT* lakini pia maono ya Wizara na maono ya Mheshimiwa Rais tutakuwa tumeweza kuyafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri haya kuna baadhi ya maeneo ambayo ninataka kuyachangia. Jambo la kwanza ni jambo la utafiti. Tumeona kwenye hotuba hapa bado nchi yetu eneo la utafiti lililofanyika ni kidogo sana na maeneo mengi ya utafiti yaliyofanyika bado tija yake wananchi hawajaiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza hapa Mikoa ya Lindi, Geita na mingineyo kwamba yalifanyiwa utafiti na baadhi ya maeneo ambayo yalienda kufanyiwa utafiti wakishirikiana na Barrick ikiwemo Nyang'hwale, Nzega, Igunga na mengineyo. Tunaomba Serikali iwekeze kwa nguvu kubwa katika maeneo ya utafiti ndiyo itakuwa ukombozi kwenye Sekta ya Madini, lakini pia

tutaenda kuzalisha zaidi kuliko hiki ambacho tunazalisha sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano kwenye Wilaya yangu ya Chunya. Leo maeneo mengi ambayo wachimbaji wetu wanaendelea kufanya uchimbaji hayajafanyiwa utafiti. Wanafanya uchimbaji wa kawaida, lakini tunaweza kuzalisha kwa wastani sasa hivi ni *almost* kilo 400 kwa mwezi, ndiyo tunayozalisha sasa hivi, ni fedha nyingi. Hizi kilo 400 kwa mwezi ukipiga wastani kwa bei ya shilingi 360,000, kwa bei ya leo, tunapata zaidi ya shilingi bilioni 142 ambayo tukilipa kodi ya moja kwa moja zaidi ya shilingi bilioni 12 tunalipa kwa mwezi Serikalini, ni fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kuyafanyia utafiti maeneo mengi ndani ya Wilaya ya Chunya tutatoka uzalishaji wa kilo 400 kwa mwezi tutakwenda kukimbilia kwenye kilo 500 kwa mwezi. Ndivyo ambavyo Serikali itapata, wachimbaji wetu watapata lakini na uchumi wa nchi yetu utazidi kukua na kwenda mbele zaidi. Ndege nyuki zinaruka lakini sisi kule kwetu Chunya hatujaziona. Mheshimiwa Waziri, ninaomba na sisi Chunya tunahitaji ndege nyuki ili ziweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la msingi na muhimu ni suala la umeme kwa wachimbaji wadogo. Tunafahamu Serikali chini ya mama yetu Samia Suluhu Hassan imeendelea kufanya vizuri kwenye upande wa umeme, imepeleka vijiji vyote na sasa tunakwenda kupeleka kwenye maeneo ya vitongoji vyote kufikia 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Wizara ije na mpango kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, kama hatanieleza jambo la msingi kwa namna ambavyo atapeleka nishati ya umeme kwa wachimbaji wangu wadogo Wilaya ya Chunya, leo ninashika shilingi hapa simwachii kwenye mshahara wake ili kuhakikisha kwamba umeme unaenda kwenye maeneo ya wachimbaji wangu wilaya yangu ya Chunya na wao waweze kunufaika, wapunguze gharama ya uzalishaji kutumia mafuta. Hivi ndivyo tutakavyoweza kwenda kuwasaidia wachimbaji wetu wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kubwa na la kimsingi ni hili jambo la *technical support*. Tumeona namna ambavyo leo tumekuwa na raia wa kigeni wengi sana kutoka Bara letu la Asia, wale wenye macho madogo madogo, wamezagaa wengi kwenye maeneo yetu ya uchimbaji. Hakika huko tunakokwenda tunaenda kutengeneza janga lingine kubwa zaidi. Wameingia kwa kuleta utaalam kwenye maeneo ya uchimbaji, lakini ukienda *ground* kule na vibali vyao vinavyoeleza kitu wanachokwenda kukifanya kule ni tofauti na malengo ambayo yamekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaona raia hao wanafanya uchimbaji mdogo mdogo ambao Watanzania na wachimbaji wetu wadogo wangeweza kufanya. Wanaendesha mitambo, wanaendesha mpaka maguta mpaka boda boda ambazo ndiyo ajira za vijana wetu, lakini wao leo ndiyo wanazozifanya hizo. Kuendesha ma-*excavator* ni ajira ambazo siyo za kitaalam, vijana wetu wanaweza wakafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuone namna nzuri na bora za kuweza kusimamia vibali vyao na wao waweze kufanya kazi iliyowaleta na siyo tu kufanya kazi iliyowaleta, tunataka waje walete *technical support*, waambukize Watanzania ili Watanzania wapate ule utaalam tuweze kujiendesha wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi tukawa tunaendelea kuwatumia wao miaka hadi miaka. Wamefika hatua sasa hivi wanaingia mikataba na wachimbaji wetu wadogo hawa, mikataba kandamizi, mikataba ya kuchimba kwenye maeneo yao, maeneo ambayo ni hatarishi sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wako.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa John Stephano Luhende.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nichangie kwenye Wizara ya Madini, Wizara ya kaka yangu Mheshimiwa Athony Mavunde.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa bajeti yake nzuri ambayo ameisoma. Pili, kwa jinsi ambavyo Wizara hii ameituliza kwa sababu ukifuatilia Mabunge yaliyopita nyuma huko, Bunge la Tisa, la Kumi, migogoro ya wachimbaji wadogo ilikuwa ni mikubwa sana, lakini kwa sasa kumetulia. Tunampongeza sana Waziri, lakini tunaipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo inafanya kazi na kwa jinsi ambavyo wanaratibu majukumu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Rais, *political will,* utayari wa Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba *investment* na uwekezaji mkubwa unafanyika kwenye Sekta ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache ya kuchangia. Jambo la kwanza ninalotaka kuchangia, ni kwenye kitu kimoja kinaitwa *local contents: local contents* kwanza ninamshukuru na ninampongeza Mheshimiwa Waziri. Akiwa kama kijana ameonesha nia ya dhati, thabiti ya kuwatetea vijana wa Kitanzania kuhakikisha kwamba *local content* ya nchi yetu inalindwa, inasimamiwa na inabaki kuwa sehemu ya Watanzania. Moja kati ya kauli zake ameongea kwenye mimbari hapa ni kwamba, atadhibiti bidhaa zote ambazo zinatoka nje. Ambazo zinaweza kutolewa na Watanzania, zitolewe na Watanzania kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo kubwa, kama vijana tuna-*appreciate*, kama vijana tunatambua kwamba kama Wizara wameamua kabisa kuunga mkono. Kwenye *local content* Mheshimiwa Waziri ni jambo kubwa kama nchi kwa sababu tuna rasilimali kubwa ya madini. Ukisoma kwenye Ilani ya CCM, inasema kwenye kitabu kidogo, inasema hivi "CCM inatambua

kuwa Sekta ya Madini ina nafasi ya kipekee katika kuchangia ukuaji wa pato la Taifa, ukuaji wa fedha za kigeni na ukuaji wa uchumi kwa ujumla".

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri yake anakwenda chini anasema wataongeza kufanya utafiti, lakini pia kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Hii yote ambayo wanaifanya kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo, ni kwamba wanaisimamia Ilani ya CCM na wanatekeleza kile ambacho pia Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake alisema:

*"Katika jitihada zetu za kuendeleza Sekta ya Madini, tutapitia upya leseni zilizotolewa ili kubaini ambazo hazijaendelezwa na kuchukua hatua na kuzitoa kwa wachimbaji wenye nia ya dhati ya kufanya uendelezaji wa maeneo husika. Wachimbaji wadogo wamekuwa nguzo ya kutegemewa katika Sekta ya Madini nchini". (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri anafanya lile ambalo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alilihutubia ndani ya Bunge, lakini pia Watanzania wamekuwa wakitegemea kutoka kwao. Kwa hiyo, ninampongeza sana kwa jinsi ambavyo wanalinda *local content*. Moja, ameweka katika ukurasa wake wa 87 wa hotuba anasema: *"Tutarasimisha wachimbaji wadogo ili wawe na sehemu ya mnyororo wa thamani'*. Hili ni jambo kubwa kwamba wachimbaji wadogo wamekuwa wakifanya kazi za uchimbaji kiholela, kama Wizara wanachukua hatua ya kwenda kurasimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na uzuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha leo yuko hapa na hili ni jambo kubwa. Hii bajeti ambayo tunaipitisha hapa, ni bajeti ambayo walitengewa kukusanya shilingi bilioni 124, lakini Serikali imewapatia asilimia nane tu ya bajeti. Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko hapa, wizara hii ndani ya miezi nane imekusanya shilingi bilioni 880 licha ya kwamba tumewapa asilimia nane tu ya bajeti yao, lakini wamekusanya shilingi bilioni 880. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri yake tukiwapa fedha Wizara ya Madini, tutakusanya fedha nyingi sana za kigeni kwenye nchi

yetu, tutakusanya fedha nyingi sana katika maendeleo yetu. Asilimia nane Mheshimiwa Waziri ni fedha ambayo ni ndogo, waiangalie kwa jicho la karibu Wizara ya Madini, kuiwezesha kwa kuipatia fedha kwa sababu bila fedha, hatutawezesha utafiti, bila fedha hatutawezesha kuendeleza hiki ambacho Mheshimiwa Waziri anakifanya kuhakikisha kwamba, tunapata maeneo mengi ambayo ni ya uchimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sana kama wameweza kukusanya shilingi bilioni 880 ndani ya muda mfupi wa miezi minane tu, basi tuiombe Wizara ya Fedha iwaongezee fedha iwapatie fedha kwa wakati ili watuletee fedha nyingi za kigeni kwenye nchi yetu na ili waweze kutusaidia kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kama kijana tunamtegemea Mheshimiwa Waziri wa Madini kwenye suala la *CSR*, hii *mandatory*, *CSR* ni *mandatory*, *CSR* siyo mtu anajifanyia kwa anavyojitakia. Ninampa tu utaratibu mmoja wa Nchi ya Zambia, waliamua kwamba *CSR* yao wanaielekeza kwenye kujenga viwanja vya nchi yao na wakawa wameisimamia ikafanya hivyo. Waziri kwenye *CSR* kwenye sheria ambayo tumeipitisha mwaka 2023 Mheshimiwa Waziri, sehemu moja amezungumza hapa chini amesema hivi, ninaomba ninukuu alichokisema, anasema hivi; *"Mmiliki wa leseni ya madini atakayeshindwa kutekeleza masharti yaliyoainishwa chini ya kanuni hizi za CSR atakuwa ametenda kosa chini ya sheria na atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Kifungu cha 63 cha Sheria"* na amesaini tarehe 15 Juni, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri yake ni nini? Ni kwamba, kuna watu wanafanya kazi hawatoi *CSR*, wanafanya vile wanavyojisikia wao, malalamiko ya *CSR* ni makubwa, *CSR* itatupunguzia kwenye changamoto mbalimbali za shule, kwenye vituo vya afya, kwenye maeneo mbalimbali. *CSR* siyo hisani, ni sheria. Watengeneze utaratibu kupitia Tume ya Madini kuhakikisha kwamba wanaisimamia *CSR* ili iweze kuwasaidia Watanzania na iweze kufanya kazi ile ambayo imekusudiwa. Tofauti na hapo tutafanya watu wachimbe madini, waondoke, lakini hawako *concerned* na jamii yetu ambayo inakaa na madini hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunatamani Wizara hii isimamie *CSR*, isimamie *CSR* ili maneno yote ambayo yanatoa, yanahusika na uchimbaji wa madini tuweze kupata. Sisi kama Makete tumepata fedha ya *BARRICK*, walifanya vizuri sehemu fulani kwenye *CSR*. Tunatamani na migodi mingine iweze kuacha hiyo fedha kwa sababu ni sheria na wameitunga wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninaweza kuipongeza Wizara kwenye *gold reserve*. Tanzania kihistoria na Watanzania lazima wafahamu tumekwama kwa mara nyingi sana kuwa na *gold reserve*, ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pekee mwaka 2024 ndiye aliyeweza kuwa na *gold reserve* kwenye nchi yetu. Toka mwaka 1997 ambapo tulikuwa na *Mineral Policy* ya mwaka 1997 lakini na *Mineral Act* ya mwaka 1998, tulijaribu kuwa na *gold reserve* tukashindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuwekea *reserve* ambayo hadi sasa tunaelekea karibu tani 23 tunaenda kuzifikia ambapo kihistoria tunaenda kuwa wa sita au wa tano barani Afrika kwa kuwa na *gold reserve* kwenye nchi yetu. Ukiwa na *gold reserve* tafsiri yake ni nini, unalinda shilingi yako, unalinda uchumi wako lakini muda wowote jambo likitokea mnaweza mkauza *gold reserve* na mkafanya jambo lingine. Hili ni jambo kubwa katika nchi kuwa na *gold reserve*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi alivyoamua yeye mwenyewe kwa makusudi ya dhati wamepita Waheshimiwa Marais wangapi, tumeshindwa kuwa na *gold reserve*. Kuwa na *gold reserve* ni ulinzi wa nchi yetu, kuwa na *gold reserve* ni heshima kwa Taifa letu, kuwa na *gold reserve* inatupelekea kwenye taswira kubwa katika uchumi na ukuaji wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Kubwa wanawahakikishia *assurance* wachimbaji wadogo kwamba kuna soko la kuuza wanapopata changamoto ya wanunuaji, *BoT* inahusika kwenda kununua. Hii

wanawapa *assurance* ya soko, ni kitu kikubwa kwa vijana wetu kwenye nchi yetu, ni jambo kubwa ambalo nilitamani kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kijana mwenzake ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuiunge mkono Wizara hii, tuwapitishie bajeti yao, tuwape fedha wakafanye hiki ambacho wamekifanya, kama ndani ya miezi nane wamekusanya shilingi bilioni 880 kwa fedha ambayo wamepewa asilimia nane tu ya fedha waliyoiomba, ni vyema nikawashawishi Wabunge wenzangu tuwaunge mkono na tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuko tayari kum-*support* na tunasema wazi kwamba kazi anayoifanya Waziri tunaiunga mkono, hizo leseni ambazo zimefutwa azisimamie ili Watanzania wapate haki na watendewe haki. Zaidi wana utaratibu wanakwenda kuufanya kwenye suala la ubia, ninashukuru kwamba wana mkakati kwa wale Watanzania ambao wanaingia ubia na watu wa nje katika uchimbaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wameona changamoto ambayo inajitokeza, Watanzania wanapigwa na wanaumizwa, wameunda mkakati ambao unaenda kuwa-*support* ikiwa ni kuhakikisha kwamba kunakuwepo na kanuni ambazo zinamlinda zaidi Mtanzania kuliko mazingira ambayo anakutana nayo kwa sasa. Hili ni jambo kubwa kwetu na sisi kama Watanzania tunafurahi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Richard Sanga. Nilimtaja Mheshimiwa John Stefano Luhende, atakuwa mchangaji wetu wa mwisho mchana huu.

**MHE. JOHN S. LUHENDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii uliyonipa ili niweze kutoa mchango wangu katika Sekta ya Madini. Kwanza ninaanza kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mchango mkubwa sana alioonesha katika Sekta ya Madini kwa kuendelea kulisaidia Shirika la *STAMICO* kuendelea kununua mitambo ya kuchoronga na kusaidia wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri wa Madini, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Madini kwa kuendelea kufanya kazi ya kusaidia Watanzania kujiendeleza kupitia Sekta ya Madini. Pongezi za mwisho ninamalizia kwa kumpongeza Rais wa Wachimbaji Wadogo, Ndugu John Wambura Bina, leo yuko hapa kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwaunganisha wachimbaji wadogo na kuwasaidia kupata *exposure* ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa ninapitia mitandao ya kijamii, nimeona baadhi ya wachimbaji wadogo wameelekea Canada kwa ajili ya kujifunza uchimbaji wa madini ili waweze kuleta tija ndani ya Taifa letu. Hongera sana ndugu Rais wa Wachimbaji Wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku ya leo nitachangia jambo moja tu kuhusiana na Sekta ya Madini na jambo hili linahusu shughuli za utafiti katika Sekta ya Madini. Shughuli za utafiti katika Sekta ya Madini ni sawa na kupanda mbegu kwa wale wakulima. Kadri unavyoongeza utafiti, ndivyo tunavyopanda mbegu ya uvunaji wa madini na kuleta maendeleo yenye tija ndani ya Taifa letu. Hata hivyo, Sekta ya Utafiti ina changamoto kubwa. Sekta ya Utafiti inakabiliwa na ukosefu wa Bodi ya Wajiolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi hii tumeanza kuipigania tangu 2017, Waheshimiwa Mawaziri wengi tumewaalika kwenye *TGS*, Mheshimiwa Waziri Mkuu pia amefika na kila Mheshimiwa Waziri aliyefika pale aliahidi kwamba jambo hili la msingi kwa maslahi mapana ya Taifa na watahakikisha linasajiliwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami Januari mwaka huu swali langu mojawapo la kwanza kuuliza ndani ya Bunge hili, lilikuwa ni lini Serikali itaweza kusajili Bodi hii ya Wajiolojia. Majibu yaliyotoka ni kwamba Bodi hii inatarajiwa kusajiliwa na bado Wizara inaendelea kukusanya maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hivi, Wizara tunawaomba sana muda wa kukusanya maoni umekwisha na maoni waliyonayo

yanatosha, huko mtaani hali si shwari. Sasa hivi huwezi kutofautisha Mjiolojia na vishoka walioko huko, wananchi wanatapeliwa sana. Wapo watu wanaojiita wao ni wataalam wa utafiti wa madini, wananchi wanatumia fedha kubwa kuwalipa, wanaandaa ripoti feki, wanakula fedha ya utafiti na wananchi wale wanawekeza fedha nyingi kwenye maeneo ambayo yamefanyiwa utafiti feki, hivyo wanakula hasara kubwa sana na kupelekea kufilisika kwa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mifano hai ya watu wengi ambao wameandikiwa taarifa feki za kiutafiti na wakawekeza fedha nyingi na wengine wamekopa. Ukitembelea kwa mfano Mkoa wa Geita maeneo ya Nyarugusu, kuna mradi mkubwa sana ulianzishwa na mchimbaji mdogo, lakini ulikufa kwa sababu wataalam walimwandalia taarifa feki za kiutafiti. Ukienda maeneo mengine ya Bukombe kule, kuna mradi ulikufa kwa sababu wataalam walimwandalia taarifa feki ya kiutafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, taaluma hii ya Wanajiolojia inasaidia sana katika nyanja zifuatazo:- Utafiti wa maji; sasa hivi ukiangalia kwenye majimbo yetu, tunachimba visima vingi vya kuchoronga lakini visima vingi pia tunapata maji na vingine hatupati maji. Hii ni kutokana na kwamba taarifa za kijiolojia zinazofanyika pale zinakuwa hazina uhalisia. Hivyo Serikali inaingia gharama kubwa ya kuchoronga visima visivyotoa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo takwimu mbalimbali za uwepo wa mafuta, gesi na kadhalika. Kazi hizo zinafanywa na hawa Wajiolojia, lakini bahati mbaya sasa ukosefu wa hii Bodi umepelekea wale Wajiolojia ambao ni halisi wanaojua kazi, wanakuwa siyo waadilifu, kuna wakati wanafoji *data*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Sekta ya Utafiti pia kuna *fraud* kubwa sana huwa inaendelea. Kwa mfano, ili uweze kupata taarifa sahihi, kuna namna ambayo unatakiwa ufanye katika kupata taarifa hizo iwe *geophysics*, iwe kwenye ku-*drill* na kadhalika. Kwa hiyo, kuna wakati mtu anakuja anakuletea ripoti amechoronga mashimo 20, lakini kiuhalisia mtu yule amechoronga mashimo 10. Mashimo 10 mengine ameandika *data* feki na bado analipwa fedha ya mashimo 20. Madhara

yake ni kwamba utakapoenda kutekeleza mradi huo, lazima utafeli kwa sababu utakuwa ni mradi ambao hauna taarifa za kujitosheleza kuweza kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, uwepo wa hii Bodi ambayo Wizara ya Madini wakiweza kuisajili, itahakikisha kwamba Wajiolojia wote ama wataalam wa Sekta ya Utafiti ndani ya Sekta ya Madini wanakuwa waadilifu. Wale ambao hawatakuwa waadilifu, bodi hii itawajibika kuhakikisha kwamba inawafutia leseni za utafiti kwa sababu tutakapokuwa na hii Bodi, ili uweze kutafiti katika nchi hii tutaweka utaratibu wa kwamba mradi wowote lazima usajiliwe na ukisajiliwa mradi ule, ni lazima utalipiwa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ile itatumika katika uendeshaji wa Bodi hii lakini kuna baadhi ya fedha itaingia Serikalini kama vyanzo vya mapato, ili mteja aliyefanyiwa utafiti atakapoleta malalamiko ya kwamba utafiti ule aliambiwa hapa kuna dhahabu kilo 10 akachimba shimo lake pale akakuta hakuna dhahabu mfano, anayo fursa sasa ya kulalamika kwenye hiyo Bodi na yule mtu aliyemfanyia utafiti wa kumdanganya akachukuliwa hatua za kisheria na kulipa gharama alizotumia mchimbaji huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchangia katika Fungu la Utafiti wa Madini kupitia *GST*, *STAMICO* na *TPDC*. Ninashauri Serikali kupitia Wizara ya Madini, waweke utaratibu kama ambavyo tumeweka utaratibu kwenye Mifuko mingine kama *Road Fund* kwamba kila lita ya mafuta yanayoingia hapa nchini kuna shilingi 100 kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, waweke pia utaratibu kwamba kila gramu moja inayouzwa ya dhahabu ama ya madini yoyote yale, kiasi fulani cha fedha kiingie kwenye Mfuko wa Utafiti wa Madini ndani ya Taifa letu. Kwa kufanya hivyo tutahakikisha kwamba tunapata fungu la kutosha wakati wote wa uzalishaji wa madini yetu ambalo fungu hilo litatumika sasa katika kuziwezesha taasisi zinazohusika na masuala ya utafiti ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kuchangia suala la *CSR*, kumekuwa na changamoto kubwa katika jamii yetu. Unakuta eneo hilo linazalisha madini mengi sana, hata hivyo, mazingira ya eneo hilo ikiwemo barabara, shule, hospitali zinatia huruma sana na wawekezaji hawawajibiki kusaidia maendeleo ndani ya Taifa letu. Kwa hiyo, ninapendekeza Wizara ya Madini ije na mkakati, waje na sheria na sisi Waheshimiwa Wabunge tutaunga mkono sheria hiyo, waweke kwamba, *CSR* kuanzia sasa tuanze kulipa kwa asilimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujue kwamba kwa kila kiwango fulani cha madini unachozalisha, kuna asilimia fulani ya *CSR* ambayo italipwa moja kwa moja kwenye masoko yetu ya madini na fedha ile itaweza kuingia kwenye Mfuko huo ili iweze kusaidia wananchi wetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JOHN S. LUHENDE** Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo mengine, lakini kutokana na uchache wa muda, nitayachangia kwa njia ya maandishi. Hata hivyo, ninakushukuru sana na niwapongeze Wizara ya Madini kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa wabunge, huyu alikuwa mchangaji wetu wa mwisho kwa wachangiaji wa mchana huu.

Tunayo matangazo machache. Kwanza, tangazo la wageni waliopo Bungeni muda huu:-

Wageni wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Waziri wa Madini; tunaye Mhandisi Filbert Rweyemamu ambaye ni Mwenyekiti wa *Chamber of Mining*; Mhandisi Benjamin Mchwampaka, Katibu Chemba ya Migodi; na Ndugu Sara Masasi, Mkurugenzi Mkuu wa *Geita Gold Refining*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Ndugu Osman Tharia, Mwenyekiti *Tanzania Minerals Dealers Association (TAMIDA)*; Ndugu Baraka Ezekiel, Mwenyekiti wa *Busolwa Mining Limited;* Dkt. Mary Mwanjelwa, Mkurugenzi wa *Kudu Graphite Limited;* Ndugu Onesmo Mbise, Mkurugenzi wa *Franon Limited;* Shekhe Salim Msami, Mwakilishi wa Shekhe wa Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mavunde, Waziri wa Madini ni Mwenyekiti wa Shirikisho la Wachimba Makaa ya Mawe Tanzania, Ndugu Daniel Mikenze; tunao wawakilishi wa vyama vinavyoshughulika na kazi za madini; tunao wawakilishi wa Shirikisho la Vyombo vya Wachimbaji Madini Tanzania *(FEMATA)* ambao tuna *TAWOMA*, *TWIMI*, WIMO, *TAMIDA*, *TAMISA*, CHAMATA, *TASPA* na *WIMA*. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ambao ni viongozi wa CCM kutoka Jiji la Dodoma; tunayo Jumuiya ya Wazazi Wilaya na Mkoa wa Dodoma; Ndugu na marafiki wa Mheshimiwa Waziri. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ambao ni Makampuni ya Madini yenye ubia na Serikali. Tunao *Twiga Minerals Corporation Limited, Tembo Nickel Corporation Limited, Faru Graphite Corporation Limited*, *Nyani Minerals Sands Limited*, *Mamba Minerals Corporation Limited, Sotter Mining Corporation Limited, Duma Graphite Limited, Williamson Diamond Limited* na *Shanta Goldmine Limited*. Ahsante na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mchana tutaendelea na mjadala tutaanza na Mheshimiwa Agnes Matthew Marwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi, Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda, Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu na orodha itendelea kutajwa kadri tunavyoendelea kuchangia.

Baada ya matangazo haya, ninaahirisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 6.59 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tunaanza na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii adhimu ya kuchangia siku ya leo, lakini nimshukuru sana *Allah Subhanahu Wataala* kwa siku nzuri kama ya leo, siku yangu ya kwanza kuchangia hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Wizara kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuandaa bajeti nzuri na hongera sana Mheshimiwa Waziri kwa bajeti nzuri aliyoileta Mezani. Katika bajeti hii Mheshimiwa Waziri ameonesha kwamba kuna maeneo yaliyorudishwa Serikalini ambayo walipewa wachimbaji wadogo wakati huo wakashindwa kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inavyoonekana kwa kuwa yamerudishwa Serikalini pia watarudishiwa wale wachimbaji ambao sasa wanaweza kuyafanyia kazi vizuri. Ninaishauri Serikali maeneo hayo watakapopewa hao wachimbaji wadogo wadogo, ni vema sasa wakasaidiwa kufanya uchunguzi, lakini pia

wakasaidiwa kuangalia maeneo hayo ambayo yana madini ili wapewe maeneo ambayo yako tayari wakijua madini yanapatikana sehemu gani ili kuwa-*empower* lakini pia kuwapunguzia gharama zisizokuwa na sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimpongeze sana mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini kwa upendo mkubwa anaotuonesha Watanzania. Mama yetu Samia Suluhu Hassan ameweka jicho lake kwenye sekta ya madini kupitia Mpango wa *MBT* wa kuwawezesha akina mama, vijana na walemavu na wao pia kuonekana kwenye sekta ya madini wanashiriki vilivyo ni jambo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza sana Rais wetu kwa jambo zuri hili alilolifanya kwa kweli anaonesha ni jinsi gani anavyotaka kuwasogeza Watanzania wa hali ya chini kwenye uchumi wa kati. Ushauri wangu kwa Serikali, ninaishauri Serikali kuweka mikopo isiyokuwa na mazingira magumu ili kuwasaidia wachimbaji hawa wadogo ili na wao waweze kujimudu yaani mikopo ya bei nafuu, lakini pia wapewe mafunzo kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapopata mafunzo kwa vitendo na wao inawasaidia kuwafanyia kazi zao kuwa nyepesi. Niendelee kumpongeza sana Waziri wetu kwa juhudi kubwa anazozifanya, lakini pia kuwawezesha wananchi wetu hususan akina mama kwa kweli Mheshimiwa Rais hakukosea kumchagua, kazi zake tunaziona kaka yetu aendelee yuko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe pia tuweke juhudi kubwa kuhakikisha tunawawezesha wananchi wetu hususan akina mama kupata ujuzi wa kuongeza thamani ya madini yetu hasa kwenye madini ya vito. Tunapofanya jambo hili kwa sababu Watanzania wengi hususan wachimbaji wadogo wanakuwa hawana ujuzi huu, tunapowapa ujuzi huu inasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mkoani kwangu Mara pale Musoma Mjini tuna soko kubwa sana la madini, lakini wanawake wa pale Musoma Mjini hawana ujuzi wowote wa vito, wanaona tu watu wanakuja wananunua madini wanaondoka.

Pia, pale wapo vijana ambao wangefanya kazi hizo. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, mafunzo hayo sasa yawe ya haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuiona fursa hiyo. Mama yetu Samia Suluhu Hassan alivyoitangaza kupitia Wizara yetu ya Madini basi na mimi moja kwa moja nikaongea na vijana, akina mama na watu wenye ulemavu na hivi wako tayari. Nimekwishaandaa watu 5,000 ambao sasa wanasubiri mafunzo hayo ili na wao moja kwa moja watakapowezeshwa waingie kwenye biashara hiyo ya vito vya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakavyo-*wind up* hapa, nitamshukuru sana kama atanikubalia kuja pale Musoma katika Jimbo langu la Musoma Mjini kuja kuangalia wale wanawake wa Musoma Mjini ambao wanahitaji mafunzo hayo na vijana pamoja na walemavu. Niendelee kuipongeza Serikali kwa mipango yake mizuri inayoendelea nayo ya kuwawezesha Watanzania na hasa Mkoani kwangu Mara, ninashukuru wanaendelea vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Mheshimiwa Rais wa kutunza akiba ya dhahabu ni jambo zuri sana na ni jambo la uzalendo, nimpongeze sana Rais wetu, mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya za kuendelea kujali rasilimali ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niishauri Serikali pamoja na kutunza dhahabu, ninashauri Serikali sasa ielekeze jicho kwenye utunzaji wa akiba ya madini ya *Tanzanite* ambayo ni madini pekee kote duniani yanapatikana Tanzania peke yake. Madini hayo yanaweza kutusaidia kwa sababu hakuna mtu mwingine duniani kote mwenye madini hayo wala nchi yoyote inayoweza kupata madini hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo na sisi ni kitu cha kwetu ambacho tunajivunia ni kitu cha kipekee ni sawa na *muse*, sisi madini yetu ya *Tanzanite* ndiyo *muse* yetu ya Tanzania. Yanapoweza kutokea majanga kama yaliyotokea majanga ya mapigano, majanga mbalimbali, kwa mfano kipindi cha majanga

yalitokea ya kimataifa mafuta yamepanda bei yalipotokea majanga haya ya kimataifa, gharama za maisha zimekuwa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza sasa na sisi wakati huo wao wakipandisha bei mafuta na sisi tunapandisha madini yetu ya *Tanzanite* bei kwa maana ya kwamba kama kuna mtu anataka kupandisha chake bei basi na sisi cha kwetu tunakipandisha bei ili tubadilishane hiyo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi na Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa ninaomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa uzima na uhai hatimaye leo tarehe 27 tupo humu ndani. Ninaomba nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia sekta ya madini, ameitendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze sana Waziri wetu ambaye anafanya kazi nzuri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Makamishna wote wa Wizara, wanafanya kazi vizuri sana wanastahili pongezi kupitia sekta ya madini, tunaona tumepata faida kubwa, mafanikio makubwa yamepatikana kupitia sekta ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu nina kata tatu ambazo kuna wachimbaji wawekezaji. Kwa sababu katika maeneo ya kata hizo tatu tuna wawekezaji, lakini kuna wawekezaji wengine na wao ni wachimbaji wadogo wadogo,

ninaomba kutengewa maeneo *blocks* kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo kwa sababu wachimbaji wadogo wadogo ndiyo nguvu kazi ya Taifa letu, pia ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unakuta katika maeneo yetu, unakuta mtu mmoja ana leseni 100 au zaidi ya 100, tuna vijana, tuna wanawake ambao ni wachimbaji ambapo wakipata fursa kubwa wanaweza kuwasaidia wanawake wenzao, lakini sasa kumekuwa kuna wawekezaji ambao sasa na wao wamekuja kuwa wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo yetu. Matokeo yake sasa wale wachimbaji wadogo wadogo wa kwetu wa Tanzania wanakosa fursa ya kuchimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimshauri Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa sababu kuna leseni ambazo wamefanya utafiti zimeonekana zile leseni hazifanyi kazi. Mheshimiwa Waziri alishaahidi kuwa zile leseni ambazo hazifanyi kazi, atakwenda kufanya utaratibu ili vijana wetu waweze kupata sehemu ya kuchimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wanawake vilevile ambao wana uwezo mkubwa tunawaona ambao wanafanya kazi nzuri ya kimataifa, wanajulikana tuendelee kuwapa uwezo ili na wenyewe waweze kuwainua akina mama wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya wawekezaji ifuatiliwe, kuna ujanja ujanja kwa wawekezaji. Serikali inapoteza mapato mengi sana kwa sababu mwekezaji anakuja anakwenda kule kijijini moja kwa moja hapitii kwenye Wizara anakwenda kufanya *lobbying* kwa mwananchi ambaye hana uelewa wowote anamdanganya, anaingia naye ubia, akishaingia naye ubia anaanza kuchimba matokeo yake yule Mtanzania anakuja kupata hasara. Tunaomba hili jambo muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika ofisi za Mikoa wasimamizi wale wa mikoa, Ofisi za Madini wapitie mikataba upya ya wawekezaji. Kwa sababu kuna wawekezaji wengine wameingia kiujanja ujanja wanakimbia hata kutoa mapato ya uhalisia. Sasa kwa sisi Watanzania tunazidi kuathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali iliweka 30%. Serikali imesema 30% kwa ajili ya wawekezaji wa ndani, lakini unakuta katika ile mikataba inakuwa tofauti. Vilevile, mikataba ya Serikali kupitia wawekezaji walishawapa miaka mitatu lakini kuna wawekezaji wengine wanafanya ujanja ujanja hawafuati sheria wanakwenda mpaka miaka mitano au zaidi, sasa hiyo inaendelea kutunyonya sisi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali isimamie kwa ukamilifu kwa sababu tumeona mafanikio makubwa kupitia sekta ya madini. Sasa kuna watu ambao wameingia katika nchi yetu, wanaitwa wawekezaji ambapo hawa wawekezaji wanakimbia hata kutoa katika maeneo husika, wanatakiwa watoe *percentage* katika halmashauri zetu, lakini hawatoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wamekaa kwenye vijiji vyetu wanatakiwa watoe huduma katika maeneo ya vijiji vyetu kwenye zahanati, kwenye vituo vya afya, kwenye shule za msingi na sekondari, lakini hawatoi wanajificha. Hivi hao ni wawekezaji au wawekezaji bandia? Mwekezaji kama mwekezaji, tunamjua mwekezaji anatoa misaada katika maeneo ya vijijini katika maeneo yale husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana, hitimisha muda wako umekwisha…

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikushukuru sana, lakini ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri. Ninajua Mheshimiwa Waziri ana ahadi na mimi, atakwenda kuangalia nguvu kazi, atahakikisha wananchi wangu wa kata zile tatu Ibindi, Sitalike na Machimboni wamepata maeneo ya kuchimba. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa idadi yetu bado ni kubwa sana na hoja hii inahitimishwa leo, kwa hiyo tutatumia dakika saba kila atakayepata nafasi. Tunaendelea na Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda na Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru sana kwa nafasi hii kwa ajili ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Madini. Kwanza nimpongeze Waziri wa Madini, kaka yangu Anthony Mavunde kwa kazi anayofanya, anafanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Mavunde sifa zake zimevuma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu moja nimpongeze kwa kutoa leseni katika eneo la Kigosi, alifanya kazi kubwa sana, alikuwa na malengo ya kutoa leseni 6,000 ila akapitiliza akatoa leseni 9,000. Ni 146% zaidi ya kiwango ambacho alikuwa amejipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mavunde amekuwa mtu mwema sana wa kutoa maeneo kwa wachimbaji wadogo. Tumeona alitoa eneo lile la Sengerema – Igalula juzi juzi hapa leseni zimeshatoka, watu wamepata ili wakafanye kazi, kwa sababu Waziri anajitahidi kuwasaidia watu ili waweze kufanikiwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze katika eneo ambalo ninataka nizungumzie kidogo kiujumla Wizara ya Madini wanafanya vizuri. Asubuhi ma-*RMO* wa Mikoa yote hapa nchini walikuwepo, tulitamani kuwapongeza kwa kazi wanayoifanya kumsaidia Waziri wa Madini kutekeleza majukumu katika kila eneo wale ma-*RMO* wakiongozwa na *RMO* wangu wa Geita kaka yangu Samwel Shoo, wanafanya kazi kubwa sana kutekeleza majukumu yao na kusimamia sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie tu mambo machache. Kwanza niipongeze *STAMICO* kwa kazi inayofanya nzuri kwa sababu uhalisia Mheshimiwa Waziri wa Madini *STAMICO* ilikuwa inaelekea kufa, lakini baada ya kuingia wameisimamia

wakiwa na Balozi Kamanda Sirro, sasa inasimama inafanya kazi vizuri sana. Mimi niwaombe waende wakaongeze nguvu kwa *STAMICO* ili iweze kuwasaidia wachimbaji wadogo waweze kufanikiwa zaidi katika utafiti na katika mambo yote ili waweze kufanikiwa kupata mali nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie jambo moja ambalo linaonekana kama lina changamoto kidogo. Mheshimiwa Waziri kuna kitu kinaitwa *VAT leaching plant.* Jambo hili ambalo leo linatuletea changamoto kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri baada ya bajeti yake akatusaidie basi. Mfano watu wanaotokea Chato wanalipa ushuru na *Service Levy,* watu wale wenye *VAT Leaching*, lakini kuna sehemu nyingine hawalipi, kuna sehemu nyingine wanalipa fedha nyingi. Tunaomba basi, kama alivyoweka kwenye madini na akatuwekea wazi kabisa, kwa mfano, kama sisi Geita ametuwekea mpaka na *TV,* ukienda kupima asilimia zako unaziona, hamna wizi; ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri anafanya vizuri. Maana, kama ameweza kutuwekea uwazi huo, tulikuwa tunapoteza, wakati mwingine unapimiwa tu hovyo hovyo, sasa hivi ukifika unapimiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa *VAT Leaching* tunaomba basi tuwe na kodi moja. Kama tunalipa shilingi laki tano, yaani nchi nzima tulipe shilingi laki tano, kama vile tunavyolipa *royalty* 8.7% au 9%. Hii *double standard* inawaumiza wachimbaji na kuongeza malalamiko makubwa. Ninaamini kwa sababu, Mheshimiwa Waziri ni msikivu, mtendaji na mtu anayeshughulika na mambo mengi, tunaamini atatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumza jambo lingine la mwisho. Sisi wachimbaji wadogo ni wavumbuzi, lakini pia, kuna msemo unasema kwamba, ni wavamizi. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, wale waliochukua leseni, kwa ajili ya uchimbaji wao, sisi Watanzania wote hatuwezi kupata leseni kwa pamoja, lakini wengine tuna mitaji kununua mawe tu; baada ya bajeti yake kupita, ninaamini tutampitishia maana tunamwamini, ataenda kufanya na tutaenda vizuri, akatusaidie wachimbaji

wetu wadogo wadogo ambao leo wanaondolewa kila maeneo kwa sababu ya wenye leseni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba, hawa wachimbaji wadogo, wanapokwenda kuvumbua madini, kama mwenye leseni hataki wachimbaji wadogo wafanye kwenye eneo lake, kwenye leseni yake, basi muda mchache waondolewe, ili wasije wakachimba kwa muda mrefu halafu mwisho wa siku wanakuja kuambiwa ondokeni kwenye eneo hili nyie siyo wenye leseni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli usiopingika ma-*RMO* wanasimamia sheria na wanafanya vizuri. Wakisema kwamba, jamani hili eneo siyo la kwenu ni la mtu amekata leseni, inatuletea changamoto kwa wachimbaji. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, maana anajua na anafuatilia, basi alibebe hili akalifuatilie. Hawa wachimbaji wadogo wanapoanza kuchimba kwenye leseni zao, watu wanaokuja kuchimba kwenye leseni zao, wale wavumbuzi siyo wavamizi. Mtu mwenye leseni awahi kutuambia kwamba, jamani ondokeni hamtakiwi, lakini akichelewa akatuacha wiki mbili, mwezi mzima, tumeingia na gharama, anakuja kutuambia, inatupa changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, yapo mambo mengi ya kuzungumzia, ninaomba, Mheshimwa Rais juzi amezungumza, hatuwezi kupeleka hela kwenye Mfuko wa Vijana wote. Sisi, Mheshimiwa Waziri wa Madini, kuna vijana ambao hawawezi kufanya kazi ya kilimo, hawezi kufanya kazi nyingine, kazi yao ni madini. Tumemshuhudia juzi akiwasaidia wachimbaji kupata fedha kutoka Benki ya *CRDB*. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri amefanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu na watu wengine wana leseni ikiwezekana atuletee mpango mkakati atakaosimamia wachimbaji wote waweze kupata fedha katika benki ili wachimbaji wetu waweze kuchimba vizuri. Tunaamini kwa sababu ameanza na kwa sababu atapitishiwa bajeti hii, ninaomba tumwombe aendelee kuzungumza na benki zote, siyo *CRDB* tu, zipo benki nyingine zinazoweza kutusaidia sisi wachimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho. Kuna jambo ambalo linatupa shida sana, la *CSR*. Waziri amesimamia vizuri sana, pamoja na kwamba, zipo changamoto kwenye *CSR*, lakini kazi yake inaonekana, anaifanya, *CSR* zinatoka japo changamoto zipo. Ninamwomba basi, ikiwezekana Mheshimiwa Waziri ... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge. Muda wako umekwisha.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi ninamwombea baraka Mheshimiwa Waziri wa Madini. Mungu amsaidie akayatekeleze haya yote. Tunamwamini akayatende kwa uhakika, maana sisi wachimbaji na mimi ni mchimbaji, tunamwamini sana kwamba atatekeleza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge tukumbushane tu kwamba, unapochangia zungumza na Kiti, Waziri atasikia.

Tunaendelea na Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, ujiandae.

**MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami ninaipongeza Wizara kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwa kweli, hakuna ambaye atapinga kwamba, wachimbaji wadogo nchi hii wamesaidiwa sana. Ni ukweli usiopingika kwamba, wachimbaji wadogo hawa Wizara hii imewabeba sana kupitia *STAMICO*, lakini pia, ndiyo wamekuwa nguzo kubwa ya uzalishaji mkubwa wa madini ambao uko ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kwenye bajeti yake mauzo ya dhahabu nje ya nchi yameongezeka na yameweza kuchangia zaidi ya 52.5%. Mchango huu wa mauzo ya nje

unachangiwa na wachimbaji wadogo nchini. Tuwapigie makofi na tuwapongeze sana wachimbaji wadogo wote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, wachimbaji wadogo baada ya kuwa wametengewa maeneo yao, wamefanya kazi nzuri sana, ambayo inaonekana. Wamechangia ndani ya nchi yetu, lakini pia, kwenye halmashauri zetu wamechangia sana. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kutenga maeneo. Juzi tumeona kuna leseni zimekuwa *surrendered*, basi leseni hizi pia, zigawiwe kwa wachimbaji wadogo ili waendelee kuongeza tija na inachangia pia upatikanaji wa ajira kwa vijana pamoja na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii pamoja na mambo mengine yote, imekumbwa na changamoto nyingi sana toka ilipofanyiwa marekebisho mwaka 2017, lakini pia, toka walivyotambuliwa wachimbaji wadogo bado wameendelea kukumbana na changamoto mbalimbali kwenye maeneo yao wanayofanyia kazi. Kwa mfano, kwenye maeneo yaliyorasimishwa ya wachimbaji wadogo bado ziko tozo za halmashauri ambazo ni chechefu, ambazo zimeendelea kuwasumbua wachimbaji wadogo na kuua mitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji mdogo ni sawasawa na wajasiriamali wengine wote ambao wamekuwa wakipewa mikopo ya 10% kwenye maeneo yetu ya halmashauri. Wamekuwa pia, hawapati usimamizi mzuri, hasa wanapopata changamoto za tozo, za ushuru, kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mchimbaji mdogo huyu amepewa leseni ameanza kuchimba, lakini amepewa leseni hii bila hata kufanyiwa *just a basic simple geological, geophysics*. Ameanza kuchimba kwa mtaji wake, anamaliza kuchimba, aende sasa kufanya uchenjuaji anakutana na tozo ya mawe; hili Mheshimiwa Waziri liko pale kwenye Mgodi wetu wa Mwakitolyo. Kila mfuko mmoja wa mawe anaotoa mchimbaji mdogo anatozwa 1,000 mpaka 2,500, lakini tozo hizi, Mheshimiwa Waziri, zinakinzana na Sheria Mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa mfano, ili aweze kuzalisha kilo moja ya dhahabu, mchimbaji mdogo huyu, anahitaji kuwa na mawe zaidi ya tani 12,000. Kwa hiyo, ina maana hata kabla hajaanza uzalishaji anapaswa kulipa halmashauri shilingi milioni 12, tozo ambayo ni kinyume kabisa na Sheria ya Madini. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri, ninajua halmashauri pia zinakusanya mapato, wakakae chini wafanye *harmonization,* ili waweze kujua ni tozo zipi basi halmashauri wanatoza kwa sababu, mwisho wa siku ametozwa mawe anakwenda, akichenjua kwa kukamatisha na *mercury* anatengeneza rundo, anakuja tena kutozwa rundo hilo, wakati analisafirisha kwenda kwenye uchenjuaji wa *CIP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mzigo huo huo pia, akimaliza uchenjuaji akienda kwenye *elution,* anakwenda sasa kulipa zile tozo ambazo zinatakiwa kwa mujibu wa kanuni, sheria na taratibu. Ana *Service Levy* halmashauri, ana mrabaha na tozo nyingine nyingi ambazo zipo kwenye Sheria ya Madini. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, awasaidie wachimbaji wadogo, hela zao wakichimba, wakizalisha, tunaziona nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ambayo wachimbaji wadogo wamechimba, uzalishaji wake na faida tumeiona ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, tunaomba sana wasaidiwe kwenye maeneo hayo, ili kupunguza *double taxation* kwa wachimbaji wadogo. Hiki kimekuwa ni kilio chao na hasa wachimbaji wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni tumeona na ninawapongeza pia, Wizara baada ya kuanzisha hii Kanuni ya Msaada wa Kiufundi. Kanuni hii ya ilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali mwaka jana tarehe 25 Aprili, 2025. Ni sheria nzuri ukiipitia, lakini kanuni hizi zimekuwa kichaka cha kuwanyonya wachimbaji wadogo. Ni sawasawa tumemgeuza mchimbaji mwenye leseni anatakiwa apate 30% na yule anayekuja kutoa *technical support* anatakiwa apate 70%.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa jicho lingine unaiona kama ni *free carried interest,* 70%, anachukua huyu. Huyu anayetoa *technical support* wengi kwa kweli, ni Wachina; miaka

10 ijayo, miaka 20 ijayo, nchi hii leseni zote za wachimbaji wadogo kwa kisingizio cha kutoa *technical support* zitakuwa zinafanywa na wageni kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ile *essence* na maana ya kuwapa ajira wachimbaji wadogo na hasa wanawake na vijana, inapotea kwa sababu, ukiangalia kabisa kwa lile jicho la tatu, 30 kwa 70 ni sawa sawa tunampa *free carried interest* ya 70%. Tujiulize, hivi hii *technical support* ni ipi? *What is the definition?* Nini maana ya *technical support*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *definition* ya *technical support* ni utafiti ambao Wizara, kwa kupitia *GST,* wangefanya *basic geophysics.* Wachimbaji wadogo wakajua tu umbali wa mwamba wa mali ulipo, wakaacha kuchimba kiholela na kupiga ramli ambazo ni chonganishi, wala tusingehitaji *technical support*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamekuja pia haka kamtambo kanakoitwa *CIP*, wanakujanako sana hawa wanaokuja kutoa *technical support*. Tuna vyuo vyetu humu ndani, tuna chuo chetu, tuna wataalam wetu, wako humu ndani, kutoka *UD* na kutoka maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati anakuja kuhitimisha hoja yake Mheshimiwa Waziri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA:** ...atupe maana ya hii *technical support,* ili kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Sitaunga mkono hoja mpaka atakaponijibu jambo hili. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko na Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma ajiandae.

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, ninaomba niungane na Mwenyekiti wetu, kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama kijana nimejua kwamba, vijana wote wanafarijika pale ambapo vijana wenzetu wanapata nafasi, wanazitumia vizuri na wanazitendea haki. Mheshimiwa Waziri Anthony Mavunde anaitendea haki sana nafasi yake, ambayo Mheshimiwa Rais amemwamini. Tunampongeza, sisi vijana wenzake na anazidi kutu-*inspire* katika maeneo mengine na tunamtakia kila la heri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tunajua kwamba, hakuna kijiji kisicho na wazee, kaka yetu pia, Naibu Waziri, tunampongeza sana kwa msaada mkubwa anaoutoa kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Menejimenti nzima ya Wizara. Baada ya pongezi hizo, sisi katika Jimbo letu la Ngara tuna Mradi wa Kabanga Nickel; kama ambavyo maeneo mengine yana dhahabu, mengine yana almasi, sisi katika Jimbo la Ngara na Wilaya ya Ngara Mwenyezi Mungu ametujalia tumepata *nickel,* lakini imekuwa ni *story* ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu ama kumbukumbu inaonesha kwamba, utafiti wa kwanza ulianza kufanyika mwaka 1976 pale *Kabanga Nickel*. Hii ni kwa mujibu wa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano wakati wakisaini mkataba na kampuni ambayo inatakiwa kuendesha huu mradi, alisema yeye mwenyewe kwamba, utafiti wa kwanza ulianza mwaka 1976.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi chote hicho ambacho sisi watu wa Ngara tumekuwa tunasubiri kwa muda mrefu kuweza kunufaika na ile rasilimali ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia, mpaka leo hakuna namna ambavyo tunaweza tukasema kwamba, tupo tumenufaika au tunaona dalili za kunufaika. Kwa bahati mbaya ni kwamba, hata jitihada zote ambazo zinafanywa na Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais kwa sasa hivi, mimi Bahati nzuri nimekuwa ninazungumza na

Mheshimiwa Waziri mara kwa mara, ameniambia jinsi ukweli ulivyo na ninauona mwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku ya leo ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kwa mdomo wake, aongee na watu wa Ngara atuambie Mradi wa *Kabanga Nickel* ni lini unaanza? Kauli moja tu! Atuambie Mradi wa *Kabanga Nickel* ni lini unaanza? Hilo tu litakuwa limetosha; sisi hatuna kitu kingine ambacho tunataka kusikia kwa siku ya leo kutoka kwa Waziri zaidi ya kwamba, Mradi wa *Kabanga Nickel* unaanza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, siyo kwamba hatuamini, tunaamini kwamba ni kitu kinakuja kutokea, lakini kwa bahati mbaya sisi watu wa Ngara tulishang'atwa na nyoka huko nyuma, sasa hivi tukiona majani tunakuwa na wasiwasi. Kuanzia mwaka 1976 mpaka leo ambavyo tunaendelea, tumekuwa tunaona zinakuja kampuni; inakuja kampuni hii inatoka, inakuja kampuni nyingine inatoka, inakuja kampuni inatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi uelewa wetu, wananchi wa kawaida, ni tunajua kwamba, tayari pale shughuli zinaendelea. Hayo mambo ya kitaalam wanayajua wao kwamba, sijui ni utafiti! Sijui ni nini, lakini sisi wananchi wa kawaida ambao tumezunguka eneo lile, ambao tunategemea tuwe tunanufaika na eneo lile, tunajua kwamba shughuli zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mwaka 2021 tunakumbuka ndipo mkataba ulisainiwa, kwa ajili ya kuanza huu mradi rasmi, miaka mitano iliyopita. Ninakumbuka kwenye ile hafla ya kusaini ule mkataba iliyofanyika Bukoba, mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano na miongoni mwa watu ambao walitufanya sisi watu wa Ngara tukapata faraja kwamba sasa tunaenda kunufaika ni Mheshimiwa Profesa Kabudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Kabudi wakati anaelezea manufaa ya ule mradi, *item* Namba 7 aliyoitaja, ninaomba niinukuu alisema: "*Miongoni mwa faida za huo mradi ni kuendeleza biashara, uchumi na maisha bora kwa Wilaya ya Ngara na Wilaya ya Kahama na wananchi wake kwa ujumla*". Akamalizia kusema, "*Ngara Oyee!*", akamalizia kusema

*"Kahama Oyee!"*. Sasa, leo ni miaka mitano imepita tangu kauli zile za kututia matumaini za Mheshimiwa Profesa Kabudi, ambazo alizitoa jinsi ambavyo tunaenda kunufaika na *Tembo Nickel*, lakini mpaka sasa hivi watu wa Ngara wanaamini kwamba, ni *story* zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu, tumepita katika vipindi mbalimbali vya kuambiwa hiki kitaenda hivi, hiki kitaenda vile, mpaka leo, hata angekuja nani leo akatuambia, mimi ninajua kwa sababu, pengine angalau nimepata nafasi ya kuwa kwenye Kamati ya Nishati na Madini, ninajua kwamba, kuna kitu kinakuja, lakini watu wa Ngara wanaamini ni *story* kwa sababu, *story* za hivyo wameambiwa kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, leo inawezekana ikawa ni siku ambayo wananchi wa Ngara watafurahi sana watakapomsikia Waziri. Kwa kipindi chote ambacho kimepita Mheshimiwa Waziri, tunaomba basi leo awafurahishe watu wa Ngara, awape matumaini, awaambie Mradi wa *Kabanga Nickel* utaanza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijana wengi wa kule Ngara wameomba kazi katika huu mradi ambao wanaamini kwamba, unakwenda kuanza, sasa hata akipata kazi sehemu nyingine anaogopa kwenda kwa sababu, anategemea hapa kwa hiyo, kuna vitu vingi sana vime-*stuck*. Kuna watu wengine wameanza kutengeneza biashara zao, wameanza kubuni mawazo ya biashara, lakini kila siku kitakuja hiki, kesho kitakuja kitu kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ilitokea huko nyuma tukawa tunaamini kwamba hiki kitu kinaenda kutokea na kwa sababu hakijawahi kutokea, Mheshimiwa tunaomba atushangaze watu wa Ngara, basi tunaomba itokee. Sisi Ngara mambo ambayo huwa tunayaomba kwa Serikali, ni mengi. Wakati huu ambao tumekuja tumesema vitu vingine, wakitupa vitaenda kupunguza shida nyingine hata hawatapigiwa kelele.

Mheshimiwa Naibu Spika, watakapotupa *Tembo Nickel* kuna mambo mengine *automatically* yataanza kujipeleka. Sisi watu wa Ngara hatutalalamika kwa sababu, tunaamini tutapata ajira,

tutapata uchumi kama ambao alisema Mheshimiwa Profesa Kabudi, lakini kama itaendelea kuwa *story,* kama miaka yote, sisi watu wa Ngara tutaendelea kuwa *disappointed*. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, mimi ninamjua vizuri sana, ninajua jinsi gani ambavyo yuko *committed* na mara kwa mara amekuwa akiniambia nenda kaa vizuri na *Tembo Nickel*, kitu kinaenda kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba, watu wa Ngara nimewaambia vitu vingi sana, vingine vinatokea vingine vitakuja kutokea, lakini vingine havitatokea. Hili wakilisikia kutoka mdomoni mwa Waziri leo, atapokuwa anahitimisha hapa, atuambie *Tembo Nickel* inaanza lini na *Kabanga Nickel* inaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Ngara watamshukuru na sisi tunamwombea kila la heri, tunamtakia utekelezaji mwema wa bajeti yake, ili kuwa na mengi, lakini ninaomba nisichanganye hili la *Tembo Nickel* na na kitu kingine. Ninaomba leo libaki hilo hilo la *Tembo Nickel* peke yake, ili kama ananijibu, anijibu hilo peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma na Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Madini, Wizara ambayo ni muhimu kabisa katika utekelezaji wa Dira yetu ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 – 2050 kwa sababu, inabeba uchumi wa Taifa letu na inaajiri Watanzania wengi ambao wako katika sekta hii. Tunajua tumeweka *70%* ya *Private Sector* kuhakikisha kwamba, tunafikia Dira yetu ya *2050.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita pamoja na Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote, kwa kuhakikisha kwamba, wamewekeza na kuhakikisha wanawavutia wawekezaji. Tumeona hata katika

hotuba yake ameainisha kabisa kwamba, tumeweza kuchangia 11.9% kwenye pato la Taifa kupitia madini haya. Ni kwa sababu, wameongeza uwekezaji na mapato ya Serikali yameweza ku-*double* mpaka *about a trillion* na mauzo nje yamefikia *almost 14 trillion* kwa mwaka, lakini pia, kwenye *export earning* wametuainishia kwamba, ni 52.7%.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo ukienda kwenye Ibara ya 46 umeainisha hapa kwamba, alitoa vibali takribani 8,635 vya kusafirisha madini ghafi kwenda nje, dhahabu, almasi, ameainisha madini ya bati, madini ya shaba, pamoja na makaa ya mawe. Hili ongezeko ambalo tunaliona ni kwa sababu ya madini ghafi. Sasa, umefika wakati pamoja na mikakati yote ambayo Waziri ameiweka, aone kuna umuhimu wa kuongeza thamani kwenye madini, tuweze ku-*process* hapa nchini ambapo tutatoa ajira za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ongezeko ambalo tunaliona ni kwa sababu ya madini ghafi, sasa imefika wakati pamoja na mikakati yote ambayo Waziri ameiweka haoni kwamba kuna umuhimu wa kuongeza thamani kwenye madini, tuweze ku-*process* hapa nchini ambapo tutatoa ajira za kutosha. Katika tafiti ambayo nimepitia kama tungeweza kuchakata hapa nchini na kuongeza thamani kwenye haya madini tu ambayo amesafirisha, hivi vibali alivyovitoa, tungeweza kutoka kwenye trilioni 14 ambazo tumepeleka kama mauzo nje ika-*range* kati ya trilioni 18 mpaka trilioni 30. Kwa hiyo, tuone kwamba ni wajibu sasa hivi tuweze kufanya hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipitia ukiangalia alivyoeleza kwenye Ibara yake ni dhahiri kabisa kwamba *critical minerals* na *strategic minerals* hazijaweza kuhusika kuhakikisha zinachangia kwenye mapato ya Taifa letu. Tanzania ni takribani katika nchi 10 tajiri zenye madini haya, ambayo madini haya tukiyatumia kimkakati yatatusaidia sana kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna hiyo *strategic gap*, kwa kuhakikisha kwamba tunawekeza zaidi, hapo umeainisha tu kwamba umetoa leseni 454 za madini haya lakini hizi leseni sasa kwa sababu tunaanza, tunatakiwa tuwe na mpango mkakati.

Ninampongeza kwenye ile *mining vision* yake ya 2030, tuwe na mpango mkakati wa kuweka *road map* hata ya *ten years*. Sasa hivi katika nishati safi nchi nyingi *by 2040* zinaondokana kabisa na magari ya petroli, zinawekeza kwenye magari ya umeme *and the like*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia huu mpango, haya madini Tanzania ya *graphite*, *nickel*, *cobalt* na hizi *rare earth elements* tunazo nyingi sana Tanzania, ambazo ni madini, *they call geopolitical minerals,* ni madini ya kimkakati, tukiyatumia tunaweza kuwa na usalama wa uchumi wetu, tukawa na nguvu ya kishawishi kimataifa, lakini pia yakasaidia kuhakikisha tuna-*win* masoko pale ambapo tutayageuza kuweza kuchakata nchini, tuite wawekezaji wa ndani na wa nje, waweze kuchakata nchini na kubadilisha kuwa bidhaa katika teknolojia ya kisasa ambapo yanatengeneza simu, *computer*, runinga, *magnetic* hizi na mambo mengine, pia mpaka umeme wa upepo na magari kama nilivyosema. Kwa hiyo, tuziangalie sana kuhakikisha kwamba tunawekeza katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine kuhakikisha kwa kweli tunapovutia wawekezaji wanakuja, kama hizo leseni 454 umezitoa lazima tuweke masharti ambatanizi. Unavyompa leseni ahakikishe kwamba anakuja pia kuhakikisha kwamba anakuwa na kiwanda au anakuwa na *chain* kuhakikisha kwamba anachakata na kutengeneza hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, nilikuwa najaribu kulinganisha hii *rare mineral elements* na nchi nyingine za kimataifa kwa mfano China, wenyewe wanazalisha *almost* 70% ya hii *rare earth elements,* wanazalisha lakini wanachakata 85% ya hizi *rare* zote za dunia. *That means*, karibia asilimia 20 mpaka 25 ambazo wanachukua malighafi kutoka nchi nyingine ikiwepo kwetu Tanzania wanaenda wanachakata kule na baadaye wanatuuzia bidhaa zenye thamani kubwa. Kwa hiyo, *we are just exporting jobs* halafu tunanunua bidhaa teknolojia kwa bidhaa kubwa sana, wakati Mwenyezi Mungu ametubariki haya tuweze kuyafanya hapahapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda na kengele imelia nilikuwa nataka tu kushauri nini tufanye. Kama nilivyosema awali, kuwepo na *mandate value addition* kwa wawekezaji wote wanaokuja hapa Tanzania, kuhakikisha kwamba wanaweka thamani kwenye madini yetu. Pia tuanzishe *special economic zones* za *barite minerals* na tunajua tunatakiwa tuhame kwenye nishati, nilichangia juzi *graphite*, *nickel*, *lithium* tuweze kuhakikisha tunatengeneza, tukishakuwa na hii *industrial zone* tutavutia wawekezaji lakini tutatengeneza bidhaa kama nilivyosema na kuongeza thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuvutie *strategic partnership*, wasiwe tu *just* wawekezaji kuja kuchukua vitalu na kuchimba na kupeleka. Waje watuletee ujuzi, waje wahakikishe kwamba walete teknolojia hapa Tanzania ili tuweze ku-*benefit* kama Taifa. Pia katika hizi *natural critical minerals* na *strategic minerals* tuhakikishe tunaziainisha kama ambavyo Waziri amesema mapema kabisa, ili tujue zipo ngapi ili tuweze kuwekeza kwa uthabiti, lakini pia tuziwekee sasa kwa mpango mkakati, *if it is five years* kama alivyosema kwenye *vision* yake au *it's ten years* ili sasa kuhakikisha kwamba tunakamata soko la kimataifa na tunanufaika nazo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho tuhakikishe sasa, ninaona sasa *it's high time* kwa sababu ya haya madini ya kimkakati na madini muhimu, Serikali iangalie uwezekano wa kuunda kamisheni ambayo itakuwa ina-*deal* na haya madini muhimu, yaani ikiwepo kamisheni kabisa muhimu ambayo ita-*deal* na haya, iweze kuratibu, uweze kuvutia wawekezaji na iweze kuona ni vipi tunakwenda. Maana yake haya madini tukiyaweka, sasa hivi hivyo tu nimesema madini jadi ndiyo yanatuletea hizi fedha zote, dhahabu, almasi, *tanzanite*, rubi *and the like*. Tukiwekeza huku kwingine kwenye madini muhimu na madini ya kimkakati, tutaenda mbali na tutafikia uchumi wa dola trilioni moja kama ambavyo tumejiwekea kwenye Dira ya 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutahakikisha *per capital income* ya Mtanzania inakuwa *seven thousand dollars* kwa mwaka na tutahakikisha tunakuza *GDP* yetu kama ambavyo tumeweka kwenye mpango wetu kwa Dira ya Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni hayo ambayo nilikuwa ninataka nishauri leo, kwa sababu ya muda mengine nitaandika kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko.

Nimemtaja Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kusimama siku ya leo kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa ninapenda kumpa pongezi kaka yangu Mavunde na timu yake yote, Naibu Waziri, Katibu kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Tunapoongelea madini maana yake tunaongelea uchumi wa Tanzania na tunaongelea ukuaji wa uchumi wa Tanzania. Kwa hiyo, kaka yangu Mavunde, kiatu alichokivaa kimemtosha sawasawa, akaze mwendo na ashikilie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninafarijika sana. Nikiangalia jinsi tulikotoka na tunapoelekea. Ukiangalia takwimu zinaonesha mwaka wa fedha 2023/2024 tilipata maduhuli zaidi ya bilioni 750 na kadhaa, lakini mwaka unaofuata tulipata zaidi ya trilioni moja na mwaka 2026 hatujamaliza mwaka wa fedha, ndani ya miezi tisa tumeshazidi zaidi ya 114% katika ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inamaanisha nini? Hii ina maana kwamba mikakati ambayo Waziri amejiwekea kama Wizara ya Madini, inaenda sawasawa siyo mikakati ya kwenye makaratasi. Kwa hiyo, ninaomba nimpongeze kwa sababu sisi ni *Tomaso,* tunataka kitu ambacho Waziri anakizungumza tukione. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitajikita moja kwa moja katika madini ambayo mchangiaji dada yangu Mheshimiwa Esther ametoka kuyasemea. Nimetoka Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Morogoro kila mtu anafahamu jinsi tulivyobahatika kuwa na madini ya kila aina, lakini sasa shida inayokuja ni kwamba haya madini hayajapewa thamani ambayo yanatakiwa kupewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Morogoro tu pale tuna madini kama *limestone*, tuna marble, tuna *golden shine*, *amethyst*, *sand stone*, kitenge, *feldspar*, *just name it*! Ninaweza nikataja mpaka asubuhi, lakini ukiangalia kwa takwimu mwaka 2023 mpaka mwaka 2025 tumefanikiwa kukusanya maduhuli ambayo ni kama bilioni 16 siyo kweli! Hii ni kwa sababu ninaona kama nguvu kubwa tumeiweka kwenye baadhi ya madini ambayo ni *gold* na *Tanzanite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni wakati wa kuyapa haya madini thamani na nini sasa kifanyike? Mimi binafsi ni mchimbaji mdogo na kumekuwa kuna shida ambayo wachimbaji wengi wa madini haya ambayo either siyo ya vito wanapitia, mojawapo ni kukosa masoko. Mfano, ninachukulia sasa hivi mtu anachimba *sandstone*, leo hii ukichimba *sandstone* ukimpelekea Mchina anakwambia shilingi laki tatu kwa kilo, kesho ukipeleka anakwambia shilingi laki tatu kwa kilo, baada ya wiki ukimpelekea anakwambia hii jiwe leo leta mbaya sana, mimi nitanunua kwa shilingi elfu nane, kwa sababu hakuna soko, *I mean* hakuna bei elekezi ambayo ipo *manageable*, unakuwa huna cha kufanya inabidi uuze.

Mheshimiwa Naibu Spika, *imagine* nimetoka na mzigo kutoka kwa baba yangu kule Profesa Kabudi, Kilosa mpaka Dar es Salaam, mzigo ambao ninaenda kuuza kwa kilo shilingi laki na hamsini, nikifika Dar es Salaam ananiambia shilingi elfu nane. Siwezi kurudi nao ule mzigo Kilosa! Kwa sababu nilipokwenda mara ya kwanza alinunua kwa kilo shilingi laki na hamsini nilivyorudi nimeenda kukopa na kufanya kila kitu ili niongeze kilo nyingi kwa sababu ninajua nikipeleka Dar es Salaam nitauza kwa shilingi laki na hamsini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikifika Dar es Salaam akisema kwa shilingi elfu nane na tena ukienda muda mbaya anakwambia fanya haraka mimi nataka funga ofisi. Kwa hiyo, ukiangalia sasa mimi ninafanyeje, inabidi uuze kwa bei hiyo hiyo. Sasa hii hatukuzi Uchumi. Haya madini ni kweli yanauhitaji ndiyo maana hawa ndugu zetu zamani walikuwa wanakaa Dar es Salaam lakini sasa hivi ukienda Gairo, ukienda Dutumi, ukienda Kisaki wamejenga mpaka na nyumba. Wanachosema wenyewe wanatupa *technical assistance* lakini *technical assistance* kwetu kule Morogoro hawa majamaa wanatupa *digger* na jenereta ndiyo *technical assistance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, anatupa *digger* na jenereta, lakini yeye anachukua 85%, anakupa 15%, anaondoka nayo. Kilichobakia kwamba vijana wetu wengi wamekuwa na *stress* na hawaoni thamani, mbaya zaidi haya madini wakiyauza wanaona kabisa hawa wanunuzi wanafaidika. Imefika sehemu sasa hivi unamwona Mchina anakuja kununua madini kijijini kule Kilosa amejenga na nyumba, lakini pesa anayonipa mimi siwezi hata kuezeka bati. Kwa hiyo, sasa hii kipekee kwa uchumi ambao tunataka kwenda nao kwa kweli, ni ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali hii *technical support* ambayo hawa wawekezaji wanakuja nayo kama kofia ya kuwekeza si kweli, hii *technical support* wanayoisema si kweli! Sisi ambao tupo chini tunajua, wanachokifanya wanachimba na likibaki shimo ambalo wanajua halina mwamba, halina mwendelezo anaondoka anaenda sehemu nyingine. Mbaya zaidi aina hizi za madini mchakato wake haufanyiki Tanzania, haya yanaondoka makinikia kama yalivyo, yanaenda kufanyika huko China.

Mheshimiwa Naibu Spika, *at least* hata tungekuwa tunachimba Tanzania, tunasema usafishaji wake labda kama dhahabu unafanyika Tanzania, watu wapate ajira, *processing* zingine zinafanyika Tanzania tungesema kweli *at least* hata kama unanunua kwa bei ndogo lakini *some processes* zinafanyika Tanzania na vijana wetu na ndugu zetu wanapata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, akinunua *sand stone* na vumbi lake vilevile analibeba kupeleka China, akienda China anatengeneza ananiletea mimi *tiles* hapa, ananiletea vyoo, ananiletea taa. Kwa hiyo, ukiangalia kabisa ni kwamba thamani haipo, sisi wanatuachia mashimo, hawatuachii kitu na hizo *CSR* wanazosema hazipo. Kwa sababu, mtu anaahidi hizo *CSR* kama walivyotangulia wachangiaji wengine, ninaona sasa ni wakati ambao inabidi zifanyike kwa *percentage*. Kwa sababu mtu hawezi kuchimba madini, akapata thamani ya milioni 500 akajenga tundu moja la choo, hakuna kitu kama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hizi sehemu za uwekezaji wa madini, kaka yangu Mavunde anapoteza pesa nyingi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, unga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja, mengine kaka yangu nitakuja tuyaongee. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu ajiandae.

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Madini. Niendelee kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kahama Mjini kwa kuendelea kuchapa kazi na kusadifu ile kaulimbiu ya Mheshimiwa Rais ya kazi iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Wizara ya Madini na kaka yangu Anthony Mavunde, kwa kazi nzuri ambayo

wameifanya. Tumeona katika taarifa yao, uzalishaji wa madini katika nchi yetu umeongezeka na mchango wake katika pato la Taifa umeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kutokea mwaka 2023 mchango wa sekta ya madini umechangia kwa asilimia 9.1, mwaka 2024 umechangia kwa 10.1% na mwaka 2025 umechangia kwa 11.9%. Hii tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba tukiwa na utashi wa kusema kwamba tufanye *exploration* nzuri katika sekta hii ya madini itaenda kufikia hata kuchangia kwa 50% ya pato la Taifa na twende tumpunguzie mzigo mwananchi wa kawaida kwa kumtoza kodi nyingi wakati tuna *resources* nyingi sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia hadi kufikia mwezi Machi, 2026, kati ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 1.4 Wizara ya Madini imekusanya shilingi trilioni 1.03, hii ni tafsiri nzuri na ni mwendelezo mzuri sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona mpango mkakati wa Wizara ya Madini katika kuongeza tija na thamani ya madini katika nchi yetu. Tumeona kwamba wanataka kuiwezesha *STAMICO,* lakini pamoja na kuiwezesha *GST* katika kufanya *survey* kwa kurusha hizi ndege nyuki kwa maana ya *drones* ili ziweze kufanya utafiti ulio mzuri na kuweza kuwapatia wananchi wetu na wawekezaji wengine maeneo mbalimbali ya kufanya uchimbaji wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hadi kufikia Machi, 2026, Wizara ya Madini imegawa karibu leseni 11,674. Hapa ninaomba niweke wazi suala moja kwamba ugawaji wa leseni uendane na kuendeleza vitalu hivi au leseni hizi za madini, kwa sababu gani? Kwa sababu hawa watu wanaochukua hivi vitalu na leseni za madini wanazichukua na wanaanza kuwa wanalipia zile kodi za kila mwaka, lakini hawafanyi mwendelezo. Sheria ya Madini ya Mwaka 2023 inasema, unapopata leseni ya kuchimba madini uanze kuifanyia kazi miezi mitatu tangu tarehe ya kupewa leseni hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wanachukua, wanalipia tu kodi halafu wachimbaji wadogo wakienda wakipata

madini wanafukuzwa, wanaambiwa hapa tunataka ibaki miti na ndege. Hii siyo haki na nimwombe Waziri wa Madini, nimemsikia juzi hapa amefuta baadhi ya leseni. Ninaomba hapa hata ile Tume ya Madini, isiwe kazi yake kugawa leseni tu, izifuatilie na kuona kwamba zinaendelezwa, kama haziendelezwi zichukuliwe zirudishwe chini ya Serikali au wapewe vyama vya ushirika kule katika kata na vijiji vyetu ili wananchi wetu wapate mahali pa kwenda kufanya shughuli za kuchimba madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa katika Wilaya yangu na Jimbo langu la Kahama wananchi wameenda wamevumbua sehemu madini, lakini baadaye wakaambiwa hapa ni kwa mwekezaji. Ni kweli kuna mwekezaji lakini tuwaangalie hawa wananchi nao kuwapatia maeneo ya Serikali ambayo wanaweza wakaenda wakachimba na kuendeleza kipato chao. Kwa sababu sekta ya madini hii kule Kahama na kanda ya kule ndiyo uchumi wa kule wa kwetu, sasa wananchi wanapokosa maeneo ya kuchimba kwa kweli tunakuwa hatuwatendei haki wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wenye leseni wanapozipata hizo leseni na madini yakapatikana pale wanaingia *joint venture*, mikataba na wawezeshaji. Kwenye Sheria ya Madini ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, imesema ni wawezeshaji siyo wawekezaji. Kwa hiyo, wanakuja hawa ndugu zetu kutoka Bara la Asia, Wachina wanakuja hapa na teknolojia yao, pale Kamati ya Madini imesema wanaenda kuboresha teknolojia ya *Vat leaching* na *CIP*. Hata hivyo, ninataka nikwambie kuna teknolojia inaitwa *heap leaching*, hii inafanywa na wawezeshaji hawa wa Kichina, wanakuja na teknolojia hii ambayo hawakubali kuipeleka na kuifundisha kwa wazawa ili na wao waweze kupata tija katika uchenjuaji wa madini ya dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sielewi Tume ya Madini na hawa wenzetu wa *NEMC* wanaijua hiyo teknolojia na hizo zote *chemicals* zinazotumika katika kuchenjua dhahabu au hawajui? *Environmental conservation* inafanyikaje? Ninaomba sana teknolojia *transfer* kwa mujibu wa *local content* katika Sheria yetu ya Madini, iende ikasimamiwe, tusilete Wachina wanatuachia

mabonanza, yale madude ya kwenda wanaweka kwenye baa, watu wetu wanaanza kucheza kamari zile za kuweka shilingi mia mbili, mia mbili, anakuja jioni anakusanya, anapata mtaji, anafanya madini, hana mtaji, hana chochote, twende tukaliangalie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii mikeka tunayo-*bet* ya Wahindi, tunatandika mikeka inatutosha, haya mabonanza, kwanza hata mapato yake sijui yanasimamiwaje katika Halmashauri zetu kule, kwa sababu sijaona sehemu yoyote wameweka kama chanzo cha mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sekta ya madini kwetu kama nilivyosema ndiyo uchumi wa maeneo yetu na Majimbo yetu ya kule. Ninamwomba sana Waziri Mavunde, hizi leseni ambazo haziendelezwi zichukuliwe zirudishwe Serikalini, wapewe wachimbaji wetu wadogo, waweze kufanya shughuli za uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna Vyama vya Ushirika, kwa mfano kuna hiki chama cha ushirika kinaitwa Tanzania *National Miners…*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, tunashukuru kwa mchango wako muda wako umekwisha.

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, sitaunga mkono hoja mpaka nipate maelezo hayo kwa mujibu wa maelezo ya wananchi wangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilimtaja Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu na Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga ajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi mchana wa leo ili kuchangia bajeti hii ya Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninaomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi wametoa sifa nyingi sana kwa sekta hii au Wizara hii ya madini na ninaomba niungane nao, ninamshukuru sana Waziri, Watendaji wote kwa kazi nzuri waliyoifanya katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi katika ripoti ya Mheshimiwa Waziri ameeleza kwa kina jinsi gani sekta hii inavyochangia uchumi wa nchi yetu. Imeelezwa kwamba ni sekta ya pili katika uchangiaji wa pato la Taifa; na kwa *figure* ambazo amezieleza kila mwaka kutoka mwaka wa fedha 2023/2024 na mwaka wa fedha 2025/2026 hadi mwezi Machi sekta hii inaendelea kukua na kukua; na inaonekana kwamba karibu 11.9% imeongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kufurahisha zaidi ni ukusanyaji wa maduhuli ambao unakwenda moja kwa moja Hazina. Sekta hii ukiangalia kila mwaka nayo inafanya maendeleo makubwa sana. Ukiangalia mwaka jana mwaka wa fedha 2023/2024 sekta hii ilikusanya shilingi milioni kama 900 hivi ambazo zilikwenda Hazina. Mwaka wa fedha 2024/2025 fedha zimeongezeka na kufika karibu bilioni moja pointi *something*. Kwa hiyo utaona kabisa kwamba ongezeko la takriban 49% kwenye sekta katika ukusanyaji wa maduhuli limefanyika katika Wizara hii ya Madini, hongera sana kwa ndugu zangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni udhibiti na usimamiaji wa utoroshaji wa madini. Wameonesha jinsi gani sekta ya madini kwa kushirikiana na Serikali wameweza kudhibiti watoroshaji wa madini. Tumeweza kuona bilioni 3.3 zimeweza kudhibitiwa, madini yenye thamani hiyo hayakuweza kuondoshwa na yamezuiliwa. Ninawapa hongera sana kwa kufanya kazi nzuri sana kwa kuzuia madini haya ambayo yalitakiwa kutoroshwa nje ya utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana Tume ya Madini, taasisi ambayo iko chini ya Wizara ya Madini, pamoja na

*STAMICO*. Zimefanya kazi nzuri sana kwa kutoa leseni. Kwa upande wa Tume ya Madini takriban leseni 8,000 zimetolewa; na *STAMICO* imefanya majukumu yake kikamilifu kwa kufanya utafiti, kutoa mafunzo jinsi gani ya kuchimba, kuchenjua, kuangalia hifadhi ya mazingira na kadhalika. Kwa hiyo hongera sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, ninawapongeza sana Wizara, wameeleza pale kwamba hadi sasa hivi tunazo kampuni sita ambazo zinashughulika na *refining* ya dhahabu. Kwa kweli hili jambo ni la kujipongeza sana. Ni kampuni za Kitanzania; na moja ya kampuni hizi kuna kampuni ambayo inaongozwa na mwanamama inafanya kazi vizuri sana. Hongereni sana Wizara kwa kuhakikisha kwamba sekta hizi za watu binafsi, za wazalendo zinashiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri, hizi sekta binafsi ambazo zimeshughulika katika kuanzisha *refining* za dhahabu zetu je, zinazo ithibati? kama zinazo au hazina, Wizara ihakikishe kwamba zinapata ithibati ili ziweze kutambulika kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaomba pia nichangie katika changamoto ambazo zipo, hususan katika jimbo langu. Ndani ya Jimbo la Nanyumbu tunayo pia madini ya dhahabu. Wananchi wa kule wanakumbana na changamoto zifuatazo; ninaomba Mheshimiwa Waziri anisaidie jinsi gani ya kukabiliana na changamoto hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumezungukwa na Hifadhi ya Lukwika Lumesule; na ndani ya hifadhi ile kuna madini ya dhahabu. Ule ni ukanda kutoka Msumbiji ambao unaingia hadi katika nchi yetu; tunayo madini ya dhahabu lakini madini yale yanashindwa kuchimbwa kwa sababu watu wa *TFS* na watu wa *TAWA* ni vizingiti vikubwa, hawaruhusu vijana wetu kwenda kuchimba. Sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atueleze; je, sisi watu wa Nanyumbu tuwe waangalizi tu wa yale madini au kuna utaratibu ambao unatakiwa ufanywe ili wananchi wale waweze kunufaika na madini hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda Ushirombo kuna utaratibu mzuri sana umeandaliwa; wananchi wameweza kwenda katika hifadhi, wamechimba madini na hifadhi ya mazingira inaendelea kulindwa. Kwa hiyo ninaomba utaratibu ule nao ukatumike kwa wananchi wa Jimbo langu la Nanyumbu ili vijana waweze kunufaika na madini hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi watu wa Nanyumbu tulikuwa na kituo cha uuzaji wa dhahabu; tukafanya sherehe kubwa kwenye ufunguaji wa kituo kile, lakini leo kituo kimefungwa bila taarifa yoyote. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze ni lini kituo kile kinafunguliwa? Vijana wanahangaika wanakwenda kilomita 54 kwenda kuuza dhahabu zao ilhali tulikuwa na kituo ndani ya jimbo letu. Ninaona kwamba hii si sawa kile kituo kufungwa. Ninaomba kile kituo kifunguliwe ili vijana wetu waweze kunufaika na madini hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningeomba sana, watu wetu wa *STAMICO* waje kule watoe mafunzo kwa vijana wetu. Vijana wanahitaji mafunzo. Inaonekana kama suala la madini kuna ukanda fulani ambao ndiyo unatiliwa maanani; sisi watu wa huku ndiyo tunaojikokota; hebu na sisi watunyanyue, watu wa *STAMICO*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya.

**MHE. YAHYA A. MHATA** …waje kusini kutuletea elimu na vijana wetu waweze kuchimba madini hayo na kupata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, utafuatiwa na Asia Abdukarim Halamga na Mheshimiwa Regina Henry Mikenze ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo ili nichangie katika

Wizara hii ambayo tunaisimamia kwa niaba ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Taarifa yetu tumeiwasilisha na maoni yetu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ya kuiletea mapinduzi sekta hii ya madini. Hakika takwimu zilizowasilishwa leo, taarifa iliyowasilishwa kwa kina, mafanikio katika kila aina ya kidunia, ngazi ya Afrika na hapa nchini yanatafsiri uthubutu, ujasiri na uchapakazi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi Waziri, Mheshimiwa Mavunde pamoja na Naibu Waziri, Wakuu wa Taasisi zote chini ya Wizara hii, Wenyeviti wa Bodi wote, watumishi wote wa taasisi zote; lakini pia kubwa Maafisa Madini wote wa Mikoa lakini na wadau wote wa sekta hii ya madini ambao wako leo hapa kushuhudia bajeti hii; na kwa kweli kila ukiongea na wadau hao wanamshukuru kwa ushirikiano, kwa usikivu wake. Kuelekea bajeti tumeona namna alivyokutana na makundi mbalimbali ili kuwasikiliza mafanikio yao na changamoto zao. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa mfupi. Kwanza, Mheshimiwa Waziri katika taarifa hii ametuelezea mwenendo wa biashara ya madini duniani. Katika mwenendo huo pia amegusia kuhusu mwenendo wa biashara ya *Tanzanite* yetu, madini maalum ambayo yanapatikana hapa nchini kwetu Tanzania na kwamba hakuna soko la uhakika na pia thamani yake imeshuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sababu hizo nimwombe Mheshimiwa Waziri, kama ambavyo amekuwa akiwasikiliza wadau; yeye pamoja na Naibu Waziri wake, zipo changamoto ndani ya mfumo wetu wa ndani ya nchi, ikiwemo utaratibu wa kuhakikisha kwamba madini yale hayauzwi nje ya eneo ambalo yanapatikana; jambo ambalo limeonyesha kusababisha kushuka kwa thamani na pia kukosekana kwa ajira. Vilevile limesababisha baadhi ya mashine za kuongeza thamani

ya madini hayo nyingi hazitumiki na zimesababisha kuwepo kwa gharama kubwa kwa wachimbaji na wanunuzi wa madini hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hili ni la kikanuni na sheria na amekuwa hodari; hata kwenye bajeti hii ameainisha namna walivyofanya maboresho ya Sheria ya Madini Kifungu Namba 123; sisi Kamati kwa niaba ya Bunge tuko tayari kushirikiana naye kufanya mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali ambazo zitaleta mchango mkubwa wa madini tuliyokuwa nayo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema, kwamba kazi nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia na kwa usaidizi wa karibu wa Mheshimiwa Mavunde na Naibu Waziri inaonekana kupitia takwimu; makusanyo ya trilioni 1.43. Tangu Mheshimiwa Mavunde amekabidhiwa Wizara hii na msaidizi wake yeye ni kukusanya trilioni moja na kuendelea, ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Wizara ya Fedha kuendelea kuipatia fedha Wizara hii ya Madini; hususan za maendeleo. Bilioni 10 iliyoipatia hata mpaka Machi mafanikio yake ni trilioni moja na pointi tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ni kama ng'ombe aliyenona; ili umkamue vizuri mwezeshe kupitia *GST*, Tume ya Madini, *STAMICO* na *TEITI* kwa kuwapelekea fedha zao za maendeleo. Tume ya Madini inahitaji magari 24 na tunahitaji ndege. Mchakato umeanza, nchi hii inakwenda kupima 18%, tulipo sasa ni 16% ambazo ni tangu tumepata uhuru; lakini Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kuweka rekodi mpya ya kutaka kuipima hadi kufikia 18%. Ufanyike utafiti wa kina, tuainishe madini mengine ya kimkakati na muhimu kama ambavyo mahitaji yameongezeka duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini Waziri wa Fedha hatashindwa kuipatia Wizara hii; kama ambavyo Kamati ya Uongozi kupitia Kamati ya Bajeti iliamua bilioni 28 tu. Wao wamekusanya trilioni moja, wamewapatia bilioni 82; maana yake wamepeleka fedha nyingi zaidi; niiombe sana Wizara ya Fedha, hiki ni chanzo cha uhakika; kisaidie kufanya utafiti wa kina

tubainishe madini yako wapi, tuendelee kuwavutia wawekezaji zaidi kama kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimalizie kwa kumpongeza kwa dhati kwa namna ambavyo kwa mara ya kwanza Serikali hii ya Awamu ya Sita imejenga kiwanda kwenye sekta ya chumvi kule Kilwa. Ameifanya sekta ya chumvi kutulia. Pia sisi Bagamoyo maeneo ya Kitame tunao wadau wa chumvi wamempongeza sana. Sisi Bagamoyo tunayo madini ya ujenzi kupitia Halmashauri za Chalinze na Bagamoyo. Ombi langu, ashirikiane na sekta nyingine ikiwemo miundombinu ya barabara ili maeneo yapitike na madini yaendelee kutoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mchango huu ninaunga mkono hoja na hongera sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Subira Mgalu. Nilimtaja Mheshimiwa Asia Halamga atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Henry Mikenze, Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka 2026/2027. Nianze kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuhakikisha anakuwa kinara wa kuhakikisha kwamba anazibeba sekta zote ili ziendelee kutoa nafasi ya uchumi na kutoa nafasi ya ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuendelea kumpongeza kwa moyo wa dhati kabisa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Naibu wake, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Madini. Ameendelea kuwa kielelezo kwa sisi vijana wa Kitanzania. Akipewa nafasi anaweza kuwasaidia Watanzania wenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea kuhakikisha kwamba anaendelea kuilinda na kufanikisha dhamira njema ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuendelea kutoa ajira na kuleta tabasamu kwa

Watanzania. Mheshimiwa Waziri amekuwa ni kielelezo katika Wizara zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Wizara hii ya Madini, kwa sababu ukiingia katika Afrika leo Tanzania tunaweka historia kuwa wa nne katika uwekezaji wa sekta ya madini kutokana na mazingira bora. Mazingira haya bora ya kiuwekezaji hayajaja kwa bahati mbaya, yamekuja kwa sababu tuna nchi iliyotulia, tuna Rais ambaye anavutia wawekezaji, nchi ipo salama; na ndiyo maana leo tunajivunia kuwa nafasi ya nne ukiachana na Botswana ya kwanza, Morocco ya pili na Zambia ya tatu. Tunaiweka historia ya Tanzania kushika namba nne katika Bara la Afrika. Hii ni kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza Wizara hii. Tumemwona Mheshimiwa Waziri hivi karibuni. Ameendelea kuwaona akina mama na vijana. Akina mama wa Tahoma ni hivi karibuni tumemshuhudia ametoa mashine za pampu zaidi ya 10 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanawake wanaendelea kuinuka katika sekta hii ya madini. Bado haitoshi, kuna watu ambao walikuwa wanazichezeachezea leseni *(PL)* Mheshimiwa Waziri amezichukua; zaidi ya leseni 40; amezirejesha Serikalini kwenye Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuzichukua leseni hizi hakwenda kuziweka Wizarani zikae kama mzigo, bali azipeleka huko kwa vijana wa Kitanzania na kwenda kutoa ajira kwa vijana, akina mama pamoja na Watanzania wa kawaida. Hongera sana kwa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Waziri wa Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna ng'ombe anayeweza kutoa maziwa bila majani. Tunapoongelea Wizara ya Madini ni Wizara ya pili ya kimkakati kwa Nchi yetu ya Tanzania inayoingiza fedha za ndani pamoja na fedha za kigeni. Hakuna namna yoyote; hapa tunaongea na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni lazima tuwekeze katika sekta ya madini, tuwape fedha za kutosha ili twende sasa kwenye utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivi kwa sababu tulichokiona na kukigundua, ardhi ya Tanzania karibu kila sehemu

kuna rasilimali za madini. Tuna madini ya kila aina. Kwa hiyo ni lazima sasa tujikite kutoa fedha ili kuweza kufanyika utafiti wa madini yaliyopo na pia kugundua madini mapya kwa sababu ardhi yetu ina madini ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Waziri; kwenye *Tanzanite* tunaomba atusaidie. Tunajua hali ya kidunia, lakini tutafute namna ya kulinda *Tanzanite* kwa sababu ni kitu cha kidunia na kimeporomoka bei na pale kuna Watanzania ambao ni biashara yao ya kila siku. Sasa ajira zimeanza kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumpongeza kwa kuendelea kutoa leseni kwa zaidi ya vikundi 21 pale Mji wa Mererani, Wilaya ya Simanjiro.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi watu wa Mkoa wa Manyara tuendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri. Nje ya *Tanzanite* ameendelea kumulika kwa jicho la kipekee kuona na maeneo mengine ikiwemo Hanang', Mbulu na Babati Vijijini yanakuwa ni fursa kubwa ambazo zitakuja kuwasaidia vijana wa Kitanzania. Jimbo la Hanang tunayo chumvi ya kutosha. Rasilimali ile ni rasilimali ya Watanzania. Nimekwishaiongelea hapa toka nikiwa Mbunge wa Viti Maalum; lakini sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri alibebe hili na hatimaye ile chumvi ya Hanang iweze kutoa ajira kwa vijana wa Hanang pia vijana wa Kitanzania na kuleta fedha za ndani pamoja na fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuchukua nafasi hii kusisitiza wawekezaji wote kuendelea kutoa *CSR* zinazostahili. Wanatuachia mashimo, fedha wanazozichangia ni chache sana. Tuombe sana Mheshimiwa Waziri asimamie kwenye hili ili fursa hii adimu na adhimu katika Taifa letu la kupewa madini, Mwenyezi Mungu ametubariki, lazima tuone sasa tunaingiza pato, lakini watu hawa wanapoondoka na manufaa, basi waweze pia kutuachia manufaa na sisi, kwa maana ya kupata huduma za afya, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuendelea kusisitiza hasa kwenye suala la utafiti.  Ni lazima tuongeze utafiti

kwa nguvu zetu zote ili tuendelee kuona kwamba sekta hii inaendelea kutoa pato la Taifa kupitia fedha za kigeni pamoja na fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imeendelea kutoa mazingira mazuri; na hapa niendelee kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan; zamani ilikuwa mtu ukisikia unaenda kwenye madini inaonekana moja kwa moja unaenda kutapeliwa na inawezekana ukakaliwa kikao cha ukoo; lakini kwa sasa sekta ya madini unaona kila mtu anaikimbilia. Inaweza kuwa na tija kwa mwananchi mmoja mmoja na itakuwa na tija kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya kwa vijana na akina mama wa Kitanzania. Niendelee kuomba, suala la utafiti ni suala muhimu ili tuweze kuwasaidia vijana, akina mama na wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Asia Halamga. Nimtaje Mheshimiwa Regina Henry Mikenze, atafuatiwa na Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila na Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula ajiandae.

**MHE. REGINA H. MIKENZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara muhimu kabisa ya Madini, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambazo anazifanya na kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika sekta ya madini; ninampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja ambalo nisipolisema nitaona sijaendelea haki, ambalo ninapenda kumpongeza, ni jambo la uwekezaji wa Mfuko kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa akihutubia Bunge hili Tukufu alisema kwamba katika uongozi wake atahakikisha katika sekta ya madini ataweka Mfuko kwa ajili ya vizazi vijavyo. Alisema kuwa madini siyo mahindi kwamba tukivuna tutapata mbegu tena ya kupanda upya; kwa hiyo vizazi vijavyo visije vikakuta mashimo tu na visipate faida yoyote. Kwa hiyo katika hili ninampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandiko matakatifu katika Kitabu cha Mithali, Sura ya 13 mstari wa 22 unasema: "Mtu mwema huacha urithi kwa wana wa wanaye." Rais Samia Suluhu Hassan ni Rais mwema, ni Rais anayejali kizazi kijacho ndiyo maana anawekeza kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Madini, kaka yangu Anthony Mavunde kwa hotuba nzuri aliyoitoa siku ya leo. Kimsingi nilikuwa na maswali mengi na mambo mengi najiuliza, lakini kwa hotuba yake amejibu mambo mengi, amenifilisi kwa kina. Kwa hiyo ninawapongeza sana yeye pamoja na Naibu wake na wasaidizi wake ambao wanamsaidia katika Wizara hii ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nijielekeze sasa katika mchango wangu. Mimi ni Mbunge kutoka katika Mkoa wa Geita ambako tunachimba madini. Siku ya leo ningependa kuwasemea wanawake wa Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili tena sitasita kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia amefanya jambo kubwa la kukumbukwa. Katika miaka yake minne, ametoa leseni zaidi ya 80 kwa wanawake wa Mkoa wa Geita pamoja na vikundi mbalimbali vya wanawake. Tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo sasa kuna changamoto ambazo zimejitokeza. Wanawake hawa wamelipokea hili kwa mikono miwili na wamenituma nije nimshukuru. Pamoja na shukrani zao, wanaomba wasaidiwe mitaji kwa ajili ya uchimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa wakweli kuna mikopo mingi ambayo inatolewa kwa ajili ya wanawake. Kuna mikopo ya 10% kwa wanawake, lakini ni mikopo ambayo haiwezi kuwa na tija katika sekta ya uchimbaji. Sekta ya uchimbaji inahitaji mikopo mikubwa sana, inahitaji kununua mashine kubwa, mitambo mikubwa na mashine za kuchenjua. Kwa hiyo, kwa mikopo hii midogo midogo ambayo inatolewa haiwezi kuleta tija katika uchimbaji na haiwezi kumkomboa mwanamke mchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili tumsaidie mwanamke ili tuweke *legacy* ya Mama Samia ambaye amekwenda kuwasaidia wanawake waingie katika uchimbaji wa madini katika Mkoa wa Geita; niombe kuishauri Serikali na Wizara hii ya Madini. Niombe tuige *model* kama ile ya sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya kilimo nilisoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba, Serikali iliweka vituo 79 na ikanunua matrekta 360 na ikasambaza matrekta hayo katika vituo mbalimbali ili kuwawezesha wakulima walioko katika maeneo mbalimbali waweze kupata vifaa kwa gharama ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba *model* kama hii itumike katika migodi midogo midogo ili kuwasaidia wanawake wachimbaji na wachimbaji wadogo wadogo wakiwemo na vijana. Inunuliwe mitambo na mitambo hiyo iwekwe katika vituo mbalimbali au migodi hii midogo midogo ambayo wanashiriki kuchimba hao wanawake, vijana na wachimbaji wengine wadogo wadogo nao wapewe ikiwezekana kwa gharama ndogo kama ambavyo inafanyika katika kilimo, iwasaidie kushiriki na kupata uchimbaji wenye tija. Ninaamini kwa kufanya hivyo, tunakwenda kupata mabilionea wengi katika Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Geita ni mkoa wa matajiri. Katika wilaya zote za Geita kote kuna migodi na wanawake pamoja na vijana wamehamasika katika uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tunahitaji pia kusaidiwa, au wanawake wanahitaji kusaidiwa, wanawake

wachimbaji ni katika utafiti. Ni ngumu sana kwenda kuchimba uchimbaji wa madini katika karne hii ya sayansi na teknolojia uchimbaji wa kubahatisha…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Malizia muda wako umekwisha.

**MHE. REGINA H. MIKENZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaomba wanawake wasaidiwe gharama za utafiti ili waweze kuchimba uchimbaji wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula na Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga ajiandae.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Niungane na wenzangu kuwapongeza sana Wizara ya Madini, Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Kiruswa. Kwa kweli hotuba hii ya leo ni nzuri sana na kwa kweli inatoa matumaini makubwa sana kwa wachimbaji wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kahama ambapo kwa madini ni mkoa wa kimadini, katika leseni 1,640 leseni 840 zinapatikana Jimbo la Msalala za wachimbaji wadogo. Katika leseni 70 za utafiti, leseni 32 zinapatikana Jimbo la Msalala, lakini Jimbo la Msalala lina kata 18, kata 12 ni za wachimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Msalala ukizungumzia kwenye uzalishaji wa madini katika mkoa wa kimadini wa Kahama, tunazalisha mpaka kuanzia mwezi wa saba mpaka mwezi wa tatu tani 1.7 zimezalishwa katika mkoa wa kimadini wa Kahama, tani 1.3 zimetoka Msalala. Kwa upande wa makusanyo Serikalini, Serikali imekusanya shilingi 135,000,000,000

katika Mkoa wa Kimadini wa Kahama, shilingi 110,000,000,000 zimetoka Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia adha wanazopitia wachimbaji katika Jimbo la Msalala, endapo zikitatuliwa wanaweza kuzalisha mara mbili ya hiki ambacho tumekusanya. Katika Jimbo la Msalala tunazalisha miezi minne kwa nusu uzalishaji hasa katika msimu wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake barabara zetu kule hazipitiki, ukiangalia tunazo barabara kama saba ambazo hizi peke yake ndizo zinazochangia haya mapato yote ambayo tumeyaleta hapa. Barabara hizo ni Segese - Jomu, Lunguya namba tisa, Nyambula - Chela na Masavi – Chela. Hizi barabara zikiweza kupitika misimu yote tunakwenda ku-*double* huu uzalishaji ambao tunaufanya kwenye Jimbo la Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto ambazo zimeibuka. Tunaishukuru sana Wizara ya Madini kwa kuendelea kusimamia sekta hii, lakini tuna changamoto za wenye mashamba, wachimbaji wadogo wenye maduara, lakini wenye leseni. Tayari suluhisho limekwishapatikana kwa wachimbaji wenye maduara pamoja na wenye leseni, lakini tunaomba sasa sheria yetu iende ikawatambue wenye mashamba, ili mtu anapoomba leseni kwenye mfumo ikiwezekana apewe kwa 80%, 20% ibaki kwa wenye mashamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sisi hapa kwa wachimbaji wakubwa, tuna 16% inabaki kwa ajili ya Taifa letu. Kwa nini kwa wachimbaji wadogo tusiweke angalau 20% au hiyo hiyo 16% ibaki kwa wenye mashamba? Ili mtu anavyokwenda kuwekeza, *either* lile eneo liwe la kwake amelinunua ama aende akaingie ubia na wenye mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwezekana wenye mashamba waunde vikundi ili wamiliki pamoja leseni ili kuondoa migogoro. Sasa hivi tunayo migogoro kwenye maeneo yetu. Tunao mgogoro Mheshimiwa Waziri anaufahamu, mgogoro wa Busulwangili unaendana na hizi hizi changamoto. Mgogoro wa Mwakata unaendana na hizi hizi changamoto, kwamba unakuta

anayeomba leseni, anaomba leseni akiwa Dar es Salaam hajui leseni anayokwenda kupatiwa tayari kule walishaanza kuchimba miaka miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akija kupewa leseni huku yeye anakwenda pale, anavyoanza kuwafukuza; mtu alikuwa anapata mgao kama mmiliki mwenye shamba, anapata mgao wa shilingi 200,000,000 au shilingi 300,000,000 kila mgao unapofanyika, wanauza mawe, kila mgao unapofanyika anapata mgao, leo unakwenda kumkadiria heka moja shilingi 800,000 kwa sheria ya ardhi. Lazima mgogoro utaibuka tu kwa namna yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumza Jimbo la Msalala lina kata 18, kata 12 ni za wachimbaji. Hizo kata zote zikiwa na migogoro hilo jimbo litakuwaje? Tutakaa kila siku tunatatua migogoro kwenye hilo eneo. Niombe tuwatambue wenye mashamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine, Mheshimiwa Waziri ninaomba sasa leseni hizo ambazo tumezifuta, tukawagawie vijana wetu na akina mama ili waweze kuendeleza leseni hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Amosy William Maganga na Mheshimiwa Mhandisi Ramadhani Hamza Singano ajiandae.

Mheshimiwa Amosy William Maganga.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kutupa uzima na afya, hatimaye umefika muda na mimi niweze kutoa mchango wangu katika sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Madini pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote ambao kwa kweli tumeona kazi kubwa wanayoifanya na kimsingi hakika wanaitendea haki hii Wizara ya Madini. Niseme tu wazi wazi kabisa kwamba Watanzania wanaona kazi wanayoifanya na macho ya Watanzania ndiyo macho ya Mungu. Kwa hiyo, Mungu anawaona jinsi wanavyofanya, waendelee kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri, kwa kweli hotuba yak ni nzuri, ameeleza mambo mengi sana. Niombe tu Serikali iendelee kuwaunga mkono ili kusudi haya mambo mazuri tuliyoyaona, basi tuweze kuyaona kwa vitendo na hawa wachimbaji wetu wadogo basi wanaendelea kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema kwamba ametoa maelekezo kwamba, ifikapo mwaka 2034 angalau 80% ya Watanzania basi wawe wanatumia nishati safi ya kupikia. Kweli Wizara ya Madini hawajabaki nyuma, Wizara ya Madini wamelichukua hilo na leo hii tunaona kuna viwanda vinne vimejengwa vya kutengeneza mkaa unaotokana na makaa ya mawe. Viwanda hivi wamejenga Mbeya, Kisarawe, hapa Dodoma na vilevile kule Tabora. Sisi Wanatabora tumefarijika sana na ujenzi wa kiwanda hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wanatabora ni wakulima wa zao la tumbaku, tunakausha tumbaku yetu kwa moto. Tulikuwa na mashaka, Wanatabora walianza kuwa na mashaka kwamba je, miaka 10, 15 inayokuja itakuwaje? Tukizingatia kwamba miti iliyopo kule Tabora na hususan Sikonge, basi wana Sikonge ni kama *supplier* wa mkaa katika nchi hii, miti ilikuwa inakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kumbe yeye alishaliona tayari na akatoa maelekezo kwa Wizara ya Madini kwamba waende wakajenge kiwanda pale Tabora. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa juhudi hizi ambazo wamezifanya. Hata hivyo, kiwanda kimekamilika na tayari

kimeshazinduliwa, lakini mpaka hivi sasa bado hakijaanza kufanya kazi. Tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake, hebu kiwanda hiki kianze kufanya kazi basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu unaokuja tungependa kuona kwamba wakulima wa tumbaku katika Mkoa wa Tabora basi wanaanza kukausha tumbaku yao kwa kutumia haya makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, ninaona elimu bado haijafika. Hebu wafike kule waende wakatoe elimu. Bado kuna wakulima wana mashaka mashaka kwamba yawezekana makaa ya mawe labda yanaenda kuwaongezea gharama ya uzalishaji. Wafike kule watoe elimu, wawaelimishe wananchi waweze kufahamu, ili kusudi huo mkaa uweze kupokelewa na wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe tu, ninaamini kwamba wameshafanya *research* ya kutosha, wameshafanya utafiti wa kutosha na wameshajua gharama za wakulima wa tumbaku wanatumia kiasi gani katika kuni na je, sasa gharama zenu wanazokuja nazo zinakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe, suala la kutumia mkaa wa makaa ya mawe, ni suala la kimazingira. Niwaombe sana Wizara watumie lugha yoyote wanayoweza, ili kusudi wadau wa mazingira, wadau wa mazingira waweze kuingia pale na ikiwezekana basi kuwe na ruzuku ili kusudi gharama ya kutumia makaa ya mawe iwe ni chini zaidi ukilinganisha na gharama ya kuni wanazotumia. Hakika si kwamba tutasaidia mazingira, lakini vilevile kwa hawa wakulima wa tumbaku watakuwa wameongeza kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe sana ndugu zangu, hebu watufanyie hayo Wanatabora ili kusudi tuweze kuona kwamba kwa kweli Serikali ya Mama Samia imefanya kazi kubwa na imetusaidia sisi Wanatabora kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye upande wa madini, sisi watu wa Sikonge kweli hatuna madini mengi, lakini madini

tunayo. Ukienda katika Kata ya Kitunda, tunayo dhahabu, lakini ukija jirani yake hapa panaitwa Kururu, madini ya dhahabu yamegundulika mahali hapo, lakini changamoto aliyoipata msemaji aliyetangulia pale mbele kwamba bado kuna changamoto kati ya *TFS*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maganga muda wako umekwisha.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana *TFS* na *TAWA* wamalize changamoto zao ili kusudi tuweze kufaidika na hayo madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Mhandisi Ramadhani Hamza Singano, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Paschal Lutandula ajiandae.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kuniona wakati huu ili niweze kuchangia katika sekta hii iliyopo mbele yetu. Kwa dhati ya moyo wangu nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa wasaa wa wakati huu, lakini pia nimshukuru Mama yetu kipenzi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Wizara ya Madini kwa hotuba nzuri ya kisomi ya kisayansi, yenye kutupa matumaini kwa Tanzania ijayo. Nimshukuru ndugu yangu Waziri wa Madini Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde na Naibu wake, lakini na watendaji wote wa Wizara ya Madini, nimemsikia ndugu yangu Mhandisi Yahya Samamba, Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda niende moja kwa moja kwenye yale maeneo nyeti ambayo ninataka nishauri. Eneo la kwanza ni eneo la vibali kwenye maeneo ya migodi. Eneo hili lina changamoto kidogo, lakini kwa sababu ni Wizara yenye weledi, ninaamini inaenda kukaa na kuweka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ya mgodi kuna kitu kinaitwa bwawa la tope sumu. Kwa lugha nyepesi hiki ndiyo choo cha mgodi, kwa sababu uchafu wote huhifadhiwa hapa. Sasa Wizara ya Maji inatoa vibali vya ujenzi lakini na Wizara ya Madini inatoa vibali vya ujenzi. Kufika mahali tukawachanganya wale wawekezaji; nani atoe kibali?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji yeye ndiye anapitisha michoro na kuona usahihi wa michoro hiyo na kutoa kibali cha ujenzi. Wizara ya Madini naye anatoa kibali cha ujenzi. Kwa hiyo, hili likaliwe sawa ili kutowachanganya wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini wanayo Sheria ya 2010 ambayo ni utekelezaji wa Sera ya Madini ya 2009 lakini imekuwa ikipitiwa 2017 na 2024. Wizara ya Maji wanayo Sheria namba 11 ya 2009 ambayo imepata marekebisho pia 2022. Sasa hizi zote ni sheria zinahitaji kukaa ili kuona jibu la pamoja, kusiwe na vibali zaidi ya kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni eneo la *bond*. Sheria ya Madini ya 2010 ilikuja na kitu kinaitwa kanuni ya *rehabilitation bond (Bond* ya ukarabati*)* kwa maana kila kampuni yenye mradi mkubwa inapaswa isukume, ipeleke dhamana yake ya kulinda mazingira ambayo ndiyo hiyo *bond,* lakini leo *NEMC* nao wamekuja na kanuni inayoitwa *environmental performance bond*. Sasa hapa pia tunawachanganya wawekezaji. Ipelekwe wapi; *NEMC* au Madini? Au *NEMC* kwa sababu ndiye mwenye mazingira yake? Hapa pia panahitaji kuwekwa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni wakati wa kufunga mgodi, mabwawa ya tope sumu haya ni hatari sana. Sasa ile *layer* ya juu inayowekwa kwa kufunika maana yake lazima iangaliwe kwa jicho la kihandisi. Nishauri taasisi zote za maji, mazingira na madini zikae pamoja kuona kuhitimisha hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ni kufunga mashimo ya mgodi, inaitwa *(pit)* namna ya kuzifunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mwongozo sahihi unaojitosheleza haujapatikana. Watu watajiuliza je, tufukie kwa

vifusi, je, tuache maji yajae iwe ni maziwa, ni *pit lake*. Lakini kabla hilo halijafikiriwa kuna mambo ya kitaalam ya kuweza kufanya. Je, kemia ya huo mwamba inafahamika? Kama kuna *element* za *Sulphur* huoni kwamba tunaenda kwenye mambo ya *acid mines drainage*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuna mambo mengine ya ki-*geology,* mwamba unatiririsha maji, yana mwelekeo kuelekea wapi. Kuna wakati *pit lake* iko juu, *level* ya maji ya chini ya ardhi iko juu kwa hiyo inalisha, lakini kuna wakati ni kinyume chake, haya yasiposimamiwa vizuri yataleta hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni usimamizi wa mazingira katika eneo zima la mgodi. Haya ni maeneo muhimu ambayo nayo yanahitaji wataalam wakae chini watoe miongozo ili tusije tukatengeneza bomu la miaka ya baadaye. Pia ni lazima watu waangalie zile kuta za lile shimo kabla hatujaamua liwe *pit lake*. Je, ni *stable*? Na kama siyo *stable* ikitokea mmomonyoko au *landslide* tutakuwa wageni wa nani?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, ninaunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwita Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Pascal Lutandula na Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Kiruswa ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hii Wizara muhimu kwa sababu watu wangu wa Jimbo la Tarime Vijijini wanahusika sana katika madini. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri amefika Nyamongo yeye na Naibu Waziri wake, lakini ametusaidia sana kutoa leseni kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri ile kasi ambayo alianza nayo iendelee vijana, wapate matokeo ili waweze ku-*encourage* wengine. Inasaidia kupunguza ugomvi kati ya vijana wa Tarime na mwekezaji wa Barrick *Plus* Mara. Kwa sababu hawawezi kushuhudia dhahabu inatoka tu halafu wao hawapati chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba tuna mgogoro wa *CRS*. Ninaumia sana mpaka hapo kwamba mvua imenyesha kule Tarime Vijijini tulikuwa na miradi kwenye kata zote 26, sasa maeneo hayapitiki ukienda Bumera hakuna mawasiliano, Susuni hakuna mawasiliano, Itiryo hakuna mawasiliano, Nyarokuba hakuna mawasiliano barabara zimekatika. Hata hivyo, fedha iko pale mgodini tangu Januari zaidi ya shilingi bilioni nne, mgogoro ule ukiisha watu wafanye kazi za maendeleo wapate huduma kama ambavyo Mheshimiwa Rais anatamani tupate huduma wote, watusaidie sana kumaliza mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwenye *CSR*. Ukienda kuangalia namna ambavyo *CSR* inavyofanyika kule Geita na inavyofanyika Kahama na Tarime ni tofauti. Kwa mfano pale Kahama, *Barrick* wenyewe wamekubali kujenga Barabara ya lami kilomita 96, ninadhani kutoka Kahama mpaka pale Msalala. Vile vile kuna Barabara kutoka Komaswa kwenda mpaka Nyamungo wanatumia mitambo yao, wanapita vumbi, wanaogopa mifugo ya watu hawajengi lami katika lile eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika hizi kanuni zilizopo ambazo zina mgogoro sasa, miradi ile inatekelezwa na halmashauri, wanatangaza tenda wanalipa wenyewe. Darasa la shilingi milioni 20 mpaka 25, leo mkandarasi wa mgodini analipwa shilingi milioni 37, zahanati ya kujenga kwa shilingi milioni 50 mpaka milioni 100, sasa hivi wanaenda mpaka milioni 160. Fedha nyingi imeenda kwenye miradi ambayo wanatoa utaratibu kwa *local fund* kupitia TAMISEMI, gharama inakuwa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tungeomba kanuni hii ibadilike. Mgodi *core function* yao ni uchimbaji na kutafuta dhahabu, siyo kazi ya kujenga madarasa, kazi ya kuchimba vyoo,

kazi ya kutengeneza makalavati, unaongeza kazi ambayo ni ya ziada kwao. Wao wabaki na fedha ile ya mgodini, utaratibu wa manunuzi ufanyike na halmashauri, wakishakamilisha mgodi ulipe kwa viwango vya kawaida. Ule Mgodi wa *Barrick* ukisimama leo hakuna mtu wa kawaida atafanya tenda pale Tarime, kwa sababu kama analipwa milioni 37, kwa nini afanye mradi wa milioni 20 au 25, hiyo kazi ni ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ambayo wenzangu wamezungumza sana hapa ya *technical support*. Hili jambo ni *very serious* tuna shida ya ajira katika hii nchi, vijana wetu wanahangaika mtaani wamesoma hawana kazi, hii sekta ya madini ni sekta ya kuwatoa vijana wengi mtaani wakopeshwe wakachimbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wageni ambao wanakuja hapa kwamba wanatoa *support,* wanatudanganya kama danganyatoto halafu kule wanafanya shughuli nyingine. Mheshimiwa Waziri alete sheria hapa tubadilishe, yeye ametembea, ukienda China, India zipo kazi ambazo mgeni hawezi kupewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tena mikataba inasema kama una utaalamu ambao hatuna, tunakupatia leseni miaka miwili, mitatu ni lazima uwa-*company* Watanzania, ukikaa miaka miwili utaalam wako utuachie, rudi kwenu ili vijana wapate ajira hapa. Kwa namna ilivyo... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, ahsante sana, malizia.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ilivyo, mwisho wa siku tutaanza kama mambo ya Afrika Kusini, watu kuanza kupigana. Utaratibu huo uwekwe wazi. Mkataba uoneshe anaomba kufanya kazi gani, ni utaalam gani haupo, simamia leseni watu wafanye kazi. Wabunge wamesema tumezungumza, tumemshauri Waziri, asije kulalamika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Madini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pascal Lutandula, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kiruswa ambaye ni Naibu Waziri na Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. PASCAL L. LUTANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ambayo ninaipenda. Maisha yangu, suti yangu hata tai niliyoivaa ni kwa sababu ninachimba madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimshukuru sana Waziri wa Madini, kaka yangu Mheshimiwa Mavunde (Wakili Msomi) kwa kazi nzuri ambayo ameifanya tangu aingie kwenye hii Wizara na Katibu wake ndugu yangu, kaka yangu Samamba na wasaidizi wao wote mikoani huko *RMOs* kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Kwa niaba ya wachimbaji wenzangu ambao walinituma niwe sauti yao humu ndani, ninamshukuru sana Waziri na wasaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ninataka niseme neno moja katika Mithali 31 lile fungu la 29, Selemani alisema neno hili: *"Binti za watu wengi wamefanya mema mengi, lakini wewe umewapita wote."* Kwa nini nimetumia hili fungu, kama leo Biblia ingeliandikwa, inawezekana ingeandika hivi *"Marais wengi wamefanya kazi nzuri, lakini wewe Mheshimiwa Dkt. Samia umefanya vizuri zaidi."* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuamini Mheshimiwa Dkt. Samia, huwa ninataka tu niulize sijui ni Mungu tu alituletea, ninapopiga picha Waheshimiwa Wabunge alipoingia Awamu ya Tano akiwa Makamu, Mheshimiwa Dkt. John Magufuli, akiwa Rais alikuja kutusikiliza sisi wachimbaji. Rais Bina wa wachimbaji alikuwepo, tuliitwa tukaenda Dar es Salaam ndiyo mara ya kwanza sisi wachimbaji kwenda kukaa ukumbi mzuri pale unaitwa Nyerere nini, mtamalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wote walifurahi. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu, Rais alimpa jukumu la kutusikiliza wachimbaji ambao tulikuwa tumeenda tukiwa na kero 31. Zote alizipokea pamoja na Rais wa Awamu ya Tano wakasema hizi kero zote tunazimaliza. Kwa kweli hakuna Rais kama huyu mama mwenye huruma kwa wachimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niwaombe Wabunge wenzangu hata wasipokubali leo ipo siku kwa sababu maneno yangu yanaingia kwenye *Hansard,* watakubali kwamba Rais wa Awamu ya Sita amefanya mengi kuwapita wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Waheshimiwa Wabunge niwape picha tu, mama huyu ndiyo ametoa leseni nyingi kuliko Marais wote. Waziri huyu Mheshimiwa Mavunde (Wakili Msomi) ndiyo ametoa leseni nyingi kwa wachimbaji kupita Mawaziri wote. Hilo halitoshi, Rais huyu ndiyo ameanzisha Benki ya Tanzania kuwa na dhahabu. Tuna subiri jambo likwame tumalizane nalo, ni Rais Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mama huyu nimtaje vipi? Niseme huyu Rais msikivu na mnyenyekevu. Watu wamekuwa wakihangaika juu ya utafiti, wachimbaji wanakata kuku, wengine wanakwambia nimeoteshwa hapa kuna dhahabu, unakuta na wewe unamwambia ana moko na koleo nimeoteshwa, anaenda kuchimba hajui anaenda kuchimba nini. Huyu mama amekuja na suluhusho, Waziri na wataalam wamekuja na suluhisho, wanakwenda kufanya utafiti nchi nzima ili sisi wachimbaji tuendelee kuwa mabilionea. Nani kama Samia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pascal, ahsante sana muda umekwisha.

**MHE. PASCAL L. LUTANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kwa dakika moja.

**NAIBU SPIKA:** Malizia sekunde 30.

**MHE. PASCAL L. LUTANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja tu. Ndugu zangu ninataka kusema mazuri yaliyofanywa tusiyafumbe kwa mabaya. Nimwombe Waziri, kule Geita bado tuna changamoto ya mrabaha wa mawe, umebaki mkoa mmoja ninaomba aondoe haraka. Hii *technical support* Wabunge wote huku wamesema, sisi kwa niaba ya hawa wachimbaji tunasema hatuitaki, ninaomba akalimalize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Kiruswa na Mtoa Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii iliyopo mezani ya bajeti yetu ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kuwa hapa leo kwa mara nyingine katika bajeti hii ya kwanza tangu tuingie katika Awamu hii ya Muhula wa Pili wa Serikali ya Mama Samia, Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru yeye mwenyewe kwa kuendelea kuniamini kuwa Naibu Waziri wa Madini nikimsaidia Waziri mahiri, kijana mwenye hekima na busara na mwenye kipaji cha uongozi, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ambaye chini ya uongozi wake tumeona matokeo kama yalivyowasilishwa kwenye hotuba yake leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya uongozi wake na timu kubwa tunayofanya nayo kazi inayoongozwa na Katibu Mkuu Mheshimiwa Samamba pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Kamishna wa Madini, Viongozi na Wakurugenzi wa Taasisi mbalimbali na Bodi zinazosimamia hizo Taasisi za Wizara kazi mnayoiona ni matokeo ya kazi ya timu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya ufinyu wa muda nijikite kujibu baadhi ya hoja za wajumbe wa Kamati yetu, lakini

pia nimwachie Waziri nafasi aweze kujibu hoja za wajumbe walioongea hapa ambao ni Wabunge. Hata hivyo, nisianze kabla sijaishukuru Kamati tuliyonayo. Kamati hii ya Wizara ya Madini ni Kamati mahiri, yenye wataalam wa madini, ni Kamati yenye watu wenye maono na ambao wamejitoa kwa hali na mali katika kusaidia uendeshaji wa Wizara hii kwa ushauri na maoni mbalimbali ambayo sisi tumeyapokea na kila wakati tumekuwa tukiyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa yao ya leo kuna baadhi ya hoja ambazo wamezileta. Kwa mfano wamesema wanaishauri Serikali iendelee kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa migodi nchini. Sisi katika kuliitikia hili ambalo tumepokea huu ushauri tumetenga shilingi 4,750,000,000 kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya TEHAMA ambayo itakwenda kutusaidia kurahisisha ufuatiliaji wa ukaguzi wa shughuli za uchimbaji madini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia imeishauri Serikali iendelee kuimarisha ushirikiano wa Serikali katika Wizara yetu na Serikali za Mitaa, watu binafsi, sekta binafsi na taasisi za utafiti. Katika hili ninapenda kuijulisha Kamati yangu Tukufu kwamba, Serikali imeendelea kushirikiana kwa karibu sana na hizi taasisi. Kwa mfano, kuna ushirikiano wa karibu sana katika suala la ufungaji migodi, suala la ukaguzi wa migodi, suala la ukaguzi wa madini yanavyochimbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana kuna wataalam kutoka TAKUKURU, kuna watu kutoka Ofisi ya *DC*, kuna wataalam mbalimbali ambao hushiriki shughuli hizo na hata katika shughuli za *CSR* ambazo Wabunge wameliongelea sana hilo suala hapa na ninajua Waziri atalitolea ufafanuzi, kwamba kwenye *CSR* siku zote ni Kamati inayoundwa yenye mwekezaji na wajumbe kutoka halmashauri, ndiyo wanaofanya hizi kazi, kwa hiyo ushirikiano huo utaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati iliishauri Serikali kupitia Wizara ya Madini kwamba waongeze usimamizi wa kina kwa taasisi zake. Tuwaongezee uwezo taasisi zetu, tuwape vitendea kazi, tuwape magari, tuwape vifaa, tuwaongezee mafunzo na ofisi na haya yote tumeendelea kutekeleza, kila

mwaka wa fedha tumetenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya utendaji kazi kwenye taasisi zetu zote tano zinazosimamiwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuliongelea Shirika letu maarufu la *STAMICO* (Shirika la Taifa la Madini). Kamati imependekeza kwamba baada ya kuona kile kiwanda cha Tabora ambacho Mheshimiwa Mbunge wa Sikonge ameliongelea sana hapa kwamba huo mtambo haujaanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kusema kwamba tulipokwenda kutembelea kwenye *commission* tuliwapa siku 30 waanze kufanya kazi. Tunafuatilia kwanza tujue kama kweli bado haujaanza kazi, lakini *Rafiki Briquettes* ambayo ni nishati safi inayotokana na makaa ya mawe licha ya kwamba imewekezwa hapo Tabora, Kamati iliomba tutafute maeneo mengine ya kuongeza kwa sababu ya wakulima wa tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu hii kwa maelekezo yao imetupatia kazi ya kuendelea kufanya tathmini tuone ni wapi tunaweza kuongeza mitambo ya *Rafiki Briquettes* ili kuondoa changamoto ya watu wanaotumia kuni katika kuchoma tumbaku. Tumewekeza hii mitambo Kiwira, tumewekeza Pwani, tuna mitambo inakuja Dodoma, kuna mengine itaenda Geita na *STAMICO* wataendelea kupanua wigo wa kutekeleza azma ya kusambaza nishati safi mbadala inayotokana na makaa ya mawe ambayo tunayo kwa wingi katika nchi yetu katika kupunguza tatizo la uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia imeendelea kuishauri kupitia Wizara yetu kwamba *STAMICO* ishiriki kikamilifu katika uwekezaji wa uchimbaji wa migodi mikubwa. Pia ninapenda kuwaambia Wajumbe wa Kamati na Bunge lako Tukufu kwamba tumewatengea *STAMICO* shilingi 4,100,000,000 katika bajeti ya mwaka huu ili wazidishe utafiti katika kugundua maeneo yenye uchimbaji mkubwa ambao unaweza ukawa na tija na wao wafanane na *Barrick*, *GGML* na *Ashanti Gold Mine*. Huo ndiyo mwelekeo na siri ya mafanikio kwenye uchimbaji, ni utafiti na ndiyo maana Wizara inaendelea kuwaongezea fedha katika bajeti yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Kamati imeelekeza kwamba kuna vituo vya mfano walivyovitembelea wakashauri tuendelee kuweka vituo vya mfano vya kuwajengea uwezo wachimbaji wadogo. Walienda cha Katente, Lwamgasa, walitembelea vyote lakini sasa wanataka tuongeze hivyo vituo na sisi kama Wizara tumeitikia wito huo. Tuna vituo vingine viwili vinakwenda kujengwa katika mwaka huu wa fedha katika maeneo ya Buhemba na katika maeneo ya Mwakitolyo katika Mkoa wa Shinyanga, Buhemba ipo katika Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kituo kingine cha umahiri katika Sekta ya Uchakataji Chumvi ambayo imekamilika ipo kule Lindi na inaweza ikaanza kazi wakati wowote ndani ya kipindi cha miezi miwili au mitatu ijayo. Kwa hiyo, *STAMICO* itaendelea kupanua wigo katika kuwajengea wachimbaji wadogo uwezo kwa kuweka vituo mahiri vya utoaji mafunzo na uongezaji wa thamani madini yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia iliendelea kuhamasisha katika Sekta ya *STAMICO* kwamba Serikali ijikite zaidi katika kuongeza hii fani ya ukaguzi. Kwa sababu suala la ukaguzi ni nyeti sana katika masuala ya usalama wa watu migodini, mazingira na kadhalika, lakini sisi kama Wizara tumeendelea kupanua wigo katika ukaguzi. Mwaka huu wa fedha unaoishia tulikagua migodi mikubwa sita, tukakagua ya kati 31 na migodi ya wachimbaji wadogo wadogo 9,621.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Kamati imeendelea kuishauri Serikali kwamba Maafisa wetu wa Ukaguzi wajengewe uwezo. Kila mwaka wa fedha tumetenga fedha kwa ajili ya mafunzo na tunaendana na teknolojia ya kisasa, kila teknolojia mpya inapotoka sisi hatupo nyuma katika kuinunua kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalam wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitushauri kwamba tuangalie namna ya ku-*deal* na suala zima la watu wanashikilia leseni, watu wanahodhi leseni. Suala hili ninajua Waziri atalitolea ufafanuzi kwa kina. Hata hivyo, itoshe kusema kwamba Serikali imepokea huu ushauri na tutaendelea kufuta leseni zinazokuwa hazifanyiwi kazi.  Hili ni zoezi endelevu na baada ya kufuta Waziri

atazitangaza na wachimbaji wadogo ndiyo watapewa vipaumbele katika leseni zinazokwenda kufutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu pia imeendelea kushauri Wizara kwamba mifumo ya kidijiti iendelee kuimarishwa ili kurahisisha utendaji kazi na ufanisi wa kazi zetu kama Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu katika suala hili, Serikali inalifanyia kazi kwa umakini sana. Sasa hivi tupo katika hatua za kuboresha mfumo tulionao wa utoaji leseni, ufutaji leseni, ulipiwaji leseni. Kwa hiyo, tunategemea siku siyo nyingi zijazo mtu atatumiwa tu ankara yake aweze kulipia leseni yake na ndani ya muda ambao utakuwa umebainishwa na kanuni zitakazorekebishwa, asipofanya hivyo leseni yake inapotea *automatically*. Kwa hiyo, ninadhani teknolojia inaenda kutupeleka ndani sana katika usimamizi wenye ufanisi katika sekta yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilishindilia sana katika kutuhimiza tusimamie suala la tafiti za kina. Katika hili wanaitakia *GST* iongezewe uwezo wa kufanya utafiti kwa kina zaidi. Katika kipindi hiki tulichoko Serikali kwa kushirikiana na wadau wametenga bilioni 53 kwa ajili ya kusaidia *GST* waweze kufanya tafiti za ki-*geophysical* kwa kutumia ndege na fedha hizi zitatusaidia kuongeza hii 16% ambayo imeeongelewa kwa muda mrefu kwa kuongeza 18% nyingine katika eneo ambalo limefanyiwa utafiti wa kina juu ya ardhi ya nchi yetu, hivyo kufikisha 34% ndani ya muda wa kipindi cha mwaka huu wa fedha mpaka mwaka ujao ili tufikapo mwaka 2030 walau ile 50% ya *Vision 2030* iwe imefikiwa katika utafiti wa kina wa madini yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii ambayo tunaenda kuwaomba Waheshimiwa watupitishie, *GST* wametengewa zaidi ya shilingi 92,200,000,000 kwa ajili ya kuongeza tija katika utafiti wao. Tunakwenda kununua ndege, tunakwenda kutumia *drone* pia tutakuwa na ya kwetu kwa ajili ya utafiti wa kina na kununua vifaa mbalimbali vya kisasa sambamba na kujenga maabara ya kisasa ambayo inaendelea kujengwa hapa Dodoma na zingine za kikanda ambazo zinajengwa katika Mikoa ya Geita na pia katika Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ninasikia kama hiyo ndiyo kengele ya mwisho, itoshe tu kusema kwamba sisi kama Wizara tumepokea maoni ya Kamati yetu, tunayafanyia kazi, tuko tayari pia kuwasilisha kwa maandishi na haya yote ambayo Wabunge zaidi ya 20 waliyochangia leo hapa ndani tumenukuu na tunakwenda kutumia mawazo yao, ushauri wao na maoni kuendelea kuboresha utendaji wa sekta yetu hii ambayo ni tegemeo la uchumi wetu katika kutupatia fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Mheshimiwa Rais siku ile alipokuwa anazindua hili Bunge, alisema kwamba katika nyakati hizi za kuyumbishwa na yale mambo yaliyotokea Oktoba, sekta ambayo tunaitegemea itaibeba nchi hii ni sekta ya madini. Kweli wameona matokeo yake jinsi mapato yanavyopanda. Tunategemea kwamba tafiti hizi zitapokwenda kufanyika, sekta hii itakuja kuwa kinara katika kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru kwa nafasi uliyonipa na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa nimwite Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Waziri wa Madini ambaye ni mtoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana kwa nafasi uliyonipatia ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Ninaomba uniruhusu kwanza nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa miongozo na maelekezo yao ambayo yameendelea kuimarisha sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa ninaomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini kwa ushirikiano mkubwa anaonipa na msaada mkubwa ambao ananipatia kuendesha sekta hii. Pia, nimshukuru Katibu Mkuu na timu nzima ya wataalam

wa Wizara ya Madini ambao wote kwa pamoja wamekuwa msaada mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda ninaomba uniruhusu niende kujibu hoja za Wabunge 20. Hoja moja baada ya nyingine, lakini pia kwa sababu kuna hoja zimesemwa sana nitazipa muda kidogo niweze kueleweka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nianze na jambo hili, ni bahati mbaya sana watu wengi huwa wanachukulia vitu kwa kawaida na nabii huwa hakubaliki kwao. Leo ninataka niliambie Bunge lako Tukufu, kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye sekta hii ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwanza, Sera ya Madini ya Mwaka 2009, Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Mpango wa Maendeleo uliiwekea sekta ya madini *target* ya kufikia 10% ya uchangiaji wake kwenye pato la Taifa. Mwaka wa fedha 2023/2024, sekta ya madini ilikuwa inachangia kwenye pato la Taifa kwa asilimia 9.1 na malengo yalikuwa ifikapo mwaka 2025 tuwe tumefikisha 10%. Kwa mujibu wa taarifa za takwimu, Shirika la Takwimu la Taifa *(NBS)* mwaka 2024, mwaka mmoja kabla ya mwaka wa kimalengo, sekta ya madini hivi sasa inachangia kwenye pato la Taifa kwa 10.1% kwa maana ya *double digits*. Hii ni kazi nzuri ya maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa, Pato letu la Taifa ni dola bilioni 91 sawa na shilingi trilioni 220. Ndugu zangu Wabunge, waende katika nchi zote za Bara la Afrika wanitafutie nchi 10 ambazo zinachangia 10% kwenye pato la Taifa kupitia sekta ya madini. Haitokei popote, siyo jambo la kawaida, ni kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Tanzania ni moja kati ya nchi kubwa na wazalishaji wakubwa wa madini ya dhahabu, lakini kwa muda wote nchi yetu haikuwemo kwenye orodha ya nchi zenye akiba ya dhahabu kupitia Benki Kuu. Kwa mujibu wa takwimu, nchi inayoongoza katika Bara la Afrika kwa kuwa na

akiba kubwa ya dhahabu kupitia Benki Kuu ni Algeria, ina tani 174 na kwenye 10 bora ya mwisho ni Msumbiji ina tani 3.682 ya akiba ya dhahabu kupitia Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwa sekta ya madini, tufanye mabadiliko ya sheria, Kifungu cha 59(1) na (2) cha Sheria ya Madini, Sura ya 123 tumekifanyia marekebisho na hivi sasa kinasomeka ifuatavyo; "Mtu yeyote ambaye ana leseni ya uchimbaji na ambaye anasafirisha madini nje ya nchi, lazima atenge asilimia isiyopungua 20 ya madini yote kwa ajili ya kuongezwa thamani, kusafishwa, kuchenjuliwa na biashara ya ndani."

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutunga Sheria hiyo Benki Kuu ya Tanzania imeanza kununua dhahabu tarehe Mosi Oktoba, 2024. Leo miezi 18 Benki Kuu ya Tanzania imeweka historia ina tani 23.8 ya dhahabu na hivi sasa Tanzania ndani ya miezi 18 ipo kwenye 10 bora ya nchi zenye akiba ya dhahabu, hii ni kazi kubwa sana imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo lazima tumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mwaka wa Fedha 2015/2016 sekta hii ya madini iliingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 161 kwa mwaka mzima. Baada ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2017, tukaanzisha vituo vya ununuzi na masoko ya madini na kudhibiti biashara haramu na utoroshaji. Leo sekta ya madini inachangia kuingiza fedha nyingi zaidi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha uliopita tuliwekewa malengo ya kuingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi trilioni moja, mpaka tarehe 30 Juni, 2025, mwaka wa fedha ulipokuwa unaishia tuliingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi 1,071,000,000,000, sawa na 113%. Mwaka huu tumewekewa lengo la kuingiza shilingi trilioni 1.2 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Ninavyosimama hapa leo mbele yako mpaka siku hii ya leo, sekta ya madini imeingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi 1,156,000,000,000, tumebakiza bilioni 44 kuvunja rekodi yetu ya mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kazi nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Waheshimiwa Wabunge makofi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan hayatoshi, tuongeze makofi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yalikuwa ni maneno ya utangulizi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, sasa ninaanza kujibu hoja za Wabunge. Ninaanza na hoja ya kwanza, hoja ya kwanza ni ya kuhusu utafiti. Waheshimiwa Wabunge, ninakubaliana nanyi, hatuwezi kuendeleza sekta ya madini pasipo utafiti. Utafiti ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ya Tanzania tumefanya kitu kinaitwa *Low Resolution Airborne Geophysical Survey* kwa 100% ambayo ilifanyika miaka kati ya 1978 mpaka 1979. Maana yake ni kwamba, tunairusha ndege ambayo inakuwa katika uso wa dunia kwa meta 120 na katika upana wa kilometa moja, lakini tumefanya utafiti wa jiokemia kwa 24% katika Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa dunia inafanya kitu kinaitwa *High Resolution Airborne Geophysical Survey*. Huu ndiyo utafiti wa kina ambao una uwezo wa kupiga picha chini ya ardhi mpaka kilometa moja ikakuonesha *anomalies* za *magnetic point* kwa maana ya viashiria vya mipasuko ya madini ili tuwaongoze vizuri wachimbaji wetu wadogo wasichimbe kwa kubahatisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili tumelifanya kwa 16% tu kwa nchi yetu ya Tanzania. Nchi yetu ya Tanzania ina ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 945,000 ambayo ni sawasawa na ekari 233. Tumeigawa Nchi yetu ya Tanzania katika vitu vinaitwa *QDS (Quarter Degree Sheets)* zipo 322. Kila *QDS* moja ina urefu wa kilometa 54 na upana wa kilometa 54 na hivyo inatengeneza eneo la kilometa za mraba 2,916 sawasawa na ekari 726,696, maeneo haya tunayo 322 tunayofanyia utafiti wa kina ni 16% tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niliambie leo Bunge lako, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kuweka *record* katika Nchi yetu ya Tanzania katika eneo hili la utafiti.

Tunao mradi ambao tuko hatua za mwisho kuukamilisha na wenzetu wa Hispania, tukiusaini mradi huu tutarusha ndege katika *blocks* mbili. *Blocks* hizi mbili zina eneo la ukubwa kilometa za mraba 176,676 sawasawa na 18% ya Nchi yetu ya Tanzania. Ndugu zangu hivi sasa tuna 16% ukiongeza hizi 18 ambazo tutazianza muda siyo mrefu tutafika 34%, ninataka niwaondoe hofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Geita Mjini ndugu yangu Chacha alikuwa anapata wasiwasi, tutafika 2030 kwa 50%? Kama leo 2026 tunakaribia 34%, tunao mdau mwingine kaonesha *interest* mkataba uko Wizara ya Fedha atapima *block* ya kuanzia Dodoma, Singida, Tabora, mpaka Shinyanga, ambayo itakuwa ni 18% na yenyewe pia. Kwa hiyo, tutafika zaidi ya 50% ndani ya muda mfupi huu katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge tumpe imani Mheshimiwa Rais, dhamira ni njema tutaifikia kuipima nchi yetu katika kiwango hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, *local content*, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, migodi yote nchi nzima inatumia shilingi trilioni 5.1 kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa na huduma. Tumetunga sheria hivi sasa, Kanuni ya 13A ya *Local Content Regulation*, inasema: bidhaa ambazo tutaziainisha ziko 20, hazipaswi kufanywa na mgeni isipokuwa Mtanzania, ili hela hii trilioni tano ibaki Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue fursa hii, kurudia tena ni marufuku kwa mgeni yeyote ambaye ana kampuni hapa Tanzania kufanya kazi zile 20 ambazo zimeainisha kwa mujibu wa *regulation* yetu hizi ni kwa ajili ya Watanzania, tuujenge uchumi wetu na hii ni kazi kubwa ambayo imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kuhusu leseni. Nitaendelea kufuta leseni, ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, nitaendelea kufuta leseni. Leseni siyo za upangishaji, leseni ni za kuchimba au kufanya utafiti. Hivi sasa wapo Watanzania na wapo wageni wanamiliki

maeneo makubwa ya leseni na hawayafanyi kazi, wachimbaji wetu wadogo wanakosa maeneo ya kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuta leseni 40 wiki iliyopita, lakini bado nina mtiririko wa leseni nyingi sana na nitaendelea kuzifuta. Wapo wenzetu 38, wanamiliki eneo lenye ukubwa sawasawa na halmashauri za manispaa za Moshi uziunganishe 10. Watu 38 ndiyo wanazimiliki, watu hao hatuwezi kuwaacha na hawafanyi chochote katika leseni hizo, nitafuta leo, kesho na kesho kutwa hatutaacha wachimbaji wetu wanakosa maeneo ya kuchimba kwa sababu ya watu wachache kuzuia leseni hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo limegusa hisia ya Wabunge wengi sana ni eneo la *technical support agreement* na hapa nitapunguza sauti yangu. Sheria ya Madini, Sura 123, Kifungu cha 9 kimetamka hivi: "Ni marufuku kwa mgeni yeyote kuingia kwenye leseni ndogo ya uchimbaji, ni marufuku." Leseni hizi ni maalum kwa ajili ya Watanzania, lakini tukaenda mbali zaidi, sheria ikatambua kwamba kuna wakati Watanzania wanaweza wakachimba, lakini wakafikia sehemu wakakosa baadhi ya vitu vichache na usaidizi wa kuweza kumfikia ili aweze kuchimba kwa tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 9 cha Sheria ya Madini kimeweka ruhusa ya kuwepo kwa mikataba ya msaada wa kiufundi. Ninataka nikiri, Waheshimiwa Wabunge mmezungumza kwa hisia na ninakubaliana nao, katika kipindi fulani kifungu hiki kilikuwa *abused* na kiasi kwamba kikapelekea wageni wengi sana wakaingia kwenye leseni ndogo za uchimbaji pasipo kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilichukua maamuzi gani? Hapa ninaomba niliseme na nieleweke vizuri. Hatua ya kwanza ambayo tuliichukua katika kuhakikisha kwamba tunaweka masharti magumu ya mgeni kuingia kwenye leseni ndogo ya uchimbaji, cha kwanza tulitunga kanuni. Tulitunga kanuni ya msaada wa kiufundi ambapo hapo awali haikuwepo, lakini pamoja na hiyo tukasema mambo yafuatayo. Nitaomba hapa,

wachimbaji wadogo ninajua wapo hapo juu wanielewe vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nirudie tena leo, ni marufuku mtu yoyote mwenye leseni ya uchimbaji kuingiza wachimbaji wadogo katika leseni yake, ni marufuku. Leseni ni ya uchimbaji siyo ya kuwapangisha watu kuweka maduara. Ukikubali watu waingie kwenye leseni yako mambo yafuatayo lazima yafanyike:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ilikuwa haiwatambui watu wenye maduara na Wizara ya Madini hatujatengeneza haki madini mpya ya watu wenye maduara isipokuwa tumeweka utaratibu. Hivi sasa kwenye leseni yoyote ambapo kuna maduara yamechimbwa, sharti la kwanza ukikubali kuingiza wachimbaji wadogo hakikisha mmesaini mkataba na mkataba umesajiliwa Tume ya Madini, kati ya kwako wewe na mchimbaji mdogo aliyeweka duara lake, ili siku ukipata mwekezaji, kwanza *right of first refusal* apewe aliyeweka nguvu yake maduara, kwa sababu wewe ndiye umemkaribisha mwenye leseni. Akishindwa yeye ndiyo uende kwa mtu wa pili, hivyo ndivyo Kanuni yetu inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 18A ya *Mineral Rights* inazungumza hivyo, kwamba hilo ni sharti. Ikitokea hivi sasa ni kwamba wamekwenda wageni wengi sana katika maeneo yetu, na kwa kusaini mikataba ambayo muda mwingine imekuwa na mapungufu makubwa sana, nimeelewa kilio cha Wabunge. Waheshimiwa Wabunge, ninaomba waniamini kijana wao, nimesimama hapa mbele ya Bunge hili, nina hofu ya Mungu, siko hapa kuzungumza jambo la uongo, ninataka niwaambie ukweli kabisa. Kanuni yetu tumeitunga ikiwa ina mwaka mmoja, ninaomba waniruhusu nifanye yafuatayo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayasema hapa Bungeni kuanzia sasa ni marufuku kwa Afisa Madini yeyote kusaini mkataba wa kiufundi (*Technical Support Agreement)* mpaka mambo yafuatayo awe amejiridhisha nayo: *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, eneo ambalo mkataba wa kiufundi unaingiwa kama kuna wachimbaji wadogo, hakikisha wale wachimbaji wadogo wamepewa haki ya msingi ya kwanza ya kuwekeza, kama hilo halijatokea, basi na kama hawana nguvu ya kuwekeza hapo lazima wafidiwe gharama ya kile ambacho wamekiweka pale katika yale maduara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ndiyo kuanzia hapo sasa unaweza kwenda katika hatua ya kumtafuta mwekezaji mwingine ambaye anaweza akaweka nguvu, lakini hatuwezi kuweka nguvu katika maduara ambayo Watanzania wameweka nguvu zao na utaratibu haukufuatwa, hicho ndicho ambacho kanuni inasema. Sasa Waheshimiwa Wabunge ninaomba nitoe maelekezo kwa Maafisa Madini wote wakazi hapa, kuanzia leo ninatoa wiki mbili Maafisa Madini wakazi wote wapitie upya Mikataba yote ya *Technical Support Agreement* na kuifanyia *audit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua wako Watanzania wenzetu ambao wametoa taarifa za uongo, mikataba iliyoletwa tume ni tofauti na ile ambayo wanaitekeleza kule. Kama Mheshimiwa Chacha alivyosema, akibainika mtu wa namna hiyo amevunja sheria kwa mujibu wa Sheria ya Madini na hatua ambayo itafuata ni nitafuta leseni yake. Waheshimiwa Wabunge, katika *span* hii ninawapa kazi timu yangu kupitia na kufanya *audit* ya kutosha katika eneo hili, *then* baada ya hapo, Waheshimiwa Wabunge kwa mapendekezo ambayo wameyaleta, katika haki ya siri kuna nafasi pia, ya kuweza kusikiliza upande mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, waniruhusu kwa leo badala ya kutamka hapa kwamba, ninaiondoa moja kwa moja, kwanza nikafanye ukaguzi kupitia timu yangu *then* tutakuwa tunaendelea ku-*monitor situation,* ikiendelea kuwa *worse* tutaifuta hii *technical support.* Ninaomba kwa leo wanikubalie hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwanahamisi ameniambia kwamba, leo haungi hoja hii mkono mpaka nifafanue *technical support* maana yake ni nini. Kwa mujibu wa Kanuni ya 3 ya Kanuni ya Utoaji Msaada wa Kiufundi, inafafanua kwamba, msaada wa kiufundi ni ule msaada ambao una

utaalam wa uchimbaji na uongezaji thamani madini, pamoja na uendeshaji wa mitambo ambao haupatikani kirahisi ndani ya nchi; kwa hiyo, tuna *underline* hapa haupatikani kirahisi ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, timu yangu ikienda kwenye *audit* ikayabaini haya, kilichosemwa kwenye mkataba na hali halisi ni tofauti, Mheshimiwa Mwanahamisi, ndiyo hapo anakwenda kufuta hizo leseni na hicho kitu kinakuwa kimeishia hapo. Sasa arudishe shilingi yangu Mheshimiwa Mwanahamisi, katika hoja hiyo ninafikiri tumeelewana vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine Waheshimiwa Wabunge wameisema kwa sauti kubwa sana ni ya *CSR*. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, miaka 10 iliyopita uwajibikaji kwa jamii ilikuwa ni hisani, haikuwa kwa jamii, haikuwa kwa mujibu wa sheria. Mwekezaji alikuwa anaamua awajengee choo au darasa ile *host community*. Waheshimiwa Wabunge tufanye marekebisho ya kanuni, hivisasa kwa mujibu wa Kifungu cha Sheria cha 133, kimeweka sharti la lazima kwa kila *license holder* ahakikishe anatimiza wajibu wake kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Waheshimiwa Wabunge utaratibu ni kwamba, kijiji au eneo husika ndiyo wao wanabuni mradi, wakibuni mradi unapita kwenye Kamati ya Kata, baadaye unaletwa kwenye Kamati ya Fedha, Kamati ya Fedha inapeleka kwenye Baraza la Madiwani. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hii mipango wanaipitisha wenyewe. Ninawaomba hivi sasa waanze kushiriki, wale ambao katika maeneo yao kuna migodi inapitia huku kwenu katika utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo ninakwenda kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa TAMISEMI, kwa ajili ya kupitishwa. Sasa hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge hapa wamesema ni kwamba, kuna wasiwasi wa kwamba, gharama inayotumika ya ujenzi wa kupitia *CSR* ni kubwa kuliko ile ya Serikali. Kabla haijafika mbali kamati ile ipo katika Kamati ya Fedha na Baraza la Madiwani, ni njia ya kwanza ya kumwambia mwekezaji na Kamati ile ya Wataalam kwamba, gharama hii siyo gharama ambayo inakubalika na waipitie upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wajibu wetu kuanzia ngazi ya chini kabisa. Nawaomba sana Waheshimiwa katika eneo hili tuhakikishe tunasimamia ipasavyo, lakini wameenda mbali zaidi, wamesema kwa nini fedha hizi zisiende halmashauri, wao ndiyo wasimamie suala la utoaji wa hizi fedha. Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwapitishe Kifungu cha 3 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma. Kinasema fedha gani ni fedha ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CSR,* siyo fedha ya umma. Haiwezi kuingizwa kwenye mchakato wa *procurement process* ya kikawaida kwa sababu, haiingilii huko. Hata ukisoma Kifungu cha 2 cha *Public Finance Act* kimeiweka pale bayana, zipi ni fedha za umma; Waheshimiwa, *CSR* haimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni ngumu sana kui-*subject* katika utaratibu wa kuipitisha katika halmashauri; hili nimelisema na nimetoa ufafanuzi sana. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, zipo hoja ambazo Mheshimiwa Chacha amezisema, ninaomba nizipokee kama ushauri. Pia, ninafahamu changamoto ambazo zimetokea kwa Mheshimiwa Mwita Getere, wanipe muda mchache. Baada ya wasilisho hili, nilisema nitawaita, tutakaa kwa pamoja tuweke mkakati, ili *CSR* hizi ziweze kuwanufaisha wananchi wao kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa hoja ya *double taxation.* Hili ninaomba wanikubalie kwamba, ziko changamoto zinazojitekeza ambazo zinasababisha baadhi ya maeneo kutozwa mgawanyo wa mawe zaidi ya mara moja au mara mbili. Tumeongea ndani ya Wizara, nitaitisha wadau, wakiwemo wachimbaji wadogo na wadau wengine wote, pamoja na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI nitamwomba tushiriki naye kwa pamoja kwa sababu, pia, halmashauri huwa zinaingia katika eneo hili, tujadili kwa pamoja namna bora ya kulifanya jambo hili, liwe suluhisho la kwanza, ili mchimbaji mdogo asichajiwe mawe mara mbili, kwa maana ya tozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho la kwanza, wachimbaji wadogo wapo pale juu jukwaani, niliwaambia hivi; sheria inataka mtu yoyote aliyepewa leseni ya uchimbaji ukitaka kuchakata,

ukichimba, lazima uchakate ndani ya leseni yako. Ukiyatoa *monitoring* yake ndiyo inaleta changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tukikubaliana kwamba, leo wananiruhusu niweke katazo, hakuna mchimbaji yoyote mdogo Tanzania kutoa mawe nje ya leseni yake hakutakuwepo na tozo ya mara mbili, haitakuwepo. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge waniruhusu, tutakaa kwa pamoja kulijadili hili jambo tutengeneze njia nzuri zaidi, ambayo Serikali haitaumia, lakini vilevile tutamsaidia mchimbaji mdogo aweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limesemwa hapa ni la uongezaji thamani katika madini ya dhahabu. Tumepiga hatua, tuna viwanda sita hivi sasa vya kusafisha dhahabu mpaka kufikia 99.99%. Sasa tunawasaidia waweze kufikia ithibati ya *LBMA,* ambayo inataka uwe na uwezo wa kuchakata tani 10 ya dhahabu kwa mwaka na uwe na fedha kiasi cha *euro* milioni 15, kwa maana ya kuweza kufanya biashara hiyo. Ndiyo sehemu ambayo tunawasaidia hivi sasa hawa wenzetu kuongeza thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna wakati tumeongeza viwanda vingi vya kuongeza thamani ni wakati huu wa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Dodoma peke yake ina viwanda tisa vya kuongeza thamani ya madini, kikiwemo kiwanda kikubwa cha *Zingzong* kilichoko Zamahelo, ambacho hivi sasa kimeanza kuyeyusha madini ya *nickel,* lakini ukienda Nala kuna kiwanda cha kubadilisha jiwe lile la shaba, kutoka kwenye kuwa jiwe kwenda kuwa *copper cathode*.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mabadiliko makubwa sana ambayo yamefanyika hapa, lakini tunategemea kuwa na kiwanda kikubwa cha kuyeyusha *ferro niobium* pale *Panda Hill,* Mbeya, ambayo itakuwa ni *smelter* ya nne kwa ukubwa duniani, ukiacha mbili ambazo, moja iko Canada na moja Brazil. Kwenye eneo hili pia, tumefanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Madini ya *Tanzanite,* ni kweli imekuwepo changamoto ya kuporomoka kwa bei, lakini tumekuja na mkakati hivi sasa. Mkakati wa kwanza ni kuhakikisha

kwamba, tunarejesha minada ya madini haya ya vito ya *Tanzanite*, lakini la pili ni kuendelea kufanya maonesho makubwa ya Kimataifa kuitangaza *Tanzanite* yetu Kimataifa, ili kuweza kuiletea soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ya vito ni madini ya *luxury,* tunashindana na sehemu nyingine zote duniani. Sisi pia, tumeandaa mkakati wa kuhakikisha tunaiweka mbele *Tanzanite* yetu, inarudisha heshima yake na kuchangia kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na hasa wachimbaji wadogo. Tumeweka utaratibu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hitimisha.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka utaratibu hivi sasa, kupitia Benki Kuu ya Tanzania ambako imekwenda kutengenezwa taasisi ya kuwapa dhamana wachimbaji wadogo, inaitwa *Credit Guarantee Corporation,* ambayo itaanza na mtaji wa shilingi bilioni 300 mpaka trilioni sita, kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wazawa wa Nchi yetu ya Tanzania. Haya yote ninaamini yakifanyika tutakuza sana uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni la ndugu yangu Mheshimiwa Doto Bahemu, ananiangalia sana pale, anataka kusikia kuhusu *nickel* Kabanga. Mheshimiwa ninataka nimhakikishie kwamba, sisi, kama Wizara ya Madini, mwekezaji siwezi kusema hapa leo anatakiwa lini aanze. Alipaswa kuanza muda mrefu kwa mujibu wa Mkataba wa Msingi wa Mwaka 2021; tumempelekea barua na ameleta *commitment,* ambayo sasa timu yangu inaifuatilia kuona kile ambacho kimetimizwa, ili kazi hii ianze mara moja kwa mujibu wa mkataba aliousaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu mradi huu ni mkubwa. Mimi nitafika, kwa ajili ya kutoa ufafanuzi mzuri kwa wananchi wake, ili niweze kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 100 – Wizara ya Madini**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*……………..Sh. 8,025,916,889
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………..Sh. 1,719,191,861
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*……….Sh. 2,173,222,411
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*.......……………….........Sh. 771,598,494
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*….....………………Sh. 2,305,890,585
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*..Sh. 1,250,021,086
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*…….Sh. 921,368,390

Kifungu 1009–*Management Information Systems Unit*…………………………………………Sh. 789,120,000
Kifungu 2001 – *Minerals Division*……..…..…………....Sh. 84,631,928,249

Kifungu 1008 – *Monitoring and Evaluation Unit*……...Sh. 887,614,035

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 100 – Wizara ya Madini**

Kifungu 2001 – *Minerals Division*…….……….....……Sh. 71,507,708,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yako imekamilisha kazi.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 126 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kutoa Taarifa kwamba, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu kukubali na kupitisha hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Ninaamini walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri wetu wa Madini, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii. Tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Niwapongeza Waheshimiwa Wabunge kuanzia Kamati yetu ya Nishati na Madini chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Subira Mgalu; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Simon; pamoja na Wajumbe wa Kamati hii wote pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote mliopata nafasi ya kuchangia katika Wizara yetu, nawapongeza wote.

Baada ya kusema hayo, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho, saa tatu 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.38 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 28 Aprili, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*